Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 28 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 138

### Kujenga Barabara ya Mchepuo Uyole hadi Mbalizi Songwe 40 km *(Bypass Road)*

**MHE.DKT. MARY M. MWAJELWA** aliuliza:-

Jiji la Mbeya linakuwa kwa kasi sana na hivyo kuongeza idadi ya watu na magari, na ndio *"Gate way Corridor"* ya Kusini mwa Afrika hali inayosababisha msongamano na ajali za mara kwa mara zinazopelekea wananchi kupoteza maisha:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kurekebisha hali hiyo kwa kuchepusha barabara kutoka Uyole hadi Songwe baada ya Uwanja wa Ndege kwa ajili ya magari yetu makubwa?

(b) Je, ni lini mpango huo utatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti maalum, Swali lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli hivi sasa katika Jiji la Mbeya upo msongamano mkubwa wa magari hali ambayo husababisha usumbufu kwa wafanyabiashara katika soko la Mwanjelwa na wananchi kwa ujumla.

Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali inakubaliana na pendekezo la kujenga barabara ya mchepuo kutoka Uyole hadi Songwe (Mbalizi) ili magari hasa ya mizigo yanayoenda nchi jirani yaweze kupita katika barabara hiyo bila kulazima kuingia katikati ya Jiji. Barabara hiyo inakadiriwa kuwa na urefu wa kilometa 40 kuanzia Mlima Nyoka, kupitia katika Kata za Ilomba, Mwakibete, Iyela, Nzovwe, Iyunga, Iwambi na kuunganishwa na barabara kuu ya eneo la Mbozi.

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo, Serikali itafanyia upembuzi yakinifu *(feasibility study)* ambao utasaidia kujua gharama halisi za kutekeleza mradi huo wa barabara inayokadiriwa kuwa na urefu wa km 40.

Aidha, hatua hiyo itawezesha Serikali kubaini wananchi watakaoathirika kutokana na utekelezaji wa maradi na kuhitaji kulipwa fidia. Hata hivyo utekelezaji wa mpango huu utategemea upatikanaji wa fedha. Kwa mantiki hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati Serikali inakamilisha taratibu za awali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWAJELWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama nilivyoulizwa kwenye Swali langu kwamba, Mbeya ni *Gate way Corridor* za nchi nyingi za Kusini mwa Afrika. Hili suala limekuwa ni tatizo la muda mrefu sana, tumelijadili mpaka kwenye vikao vyetu vya *Road Board* bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa anaponiambia upembuzi yakinifu mpaka pesa zitakapopatikana tukumbuke kwamba barabara hii imesababisha ajali na vifo vingi sana licha ya kwamba barabara yenyewe pia inaharika. Sasa hili jibu kwa kweli mimi namba niseme haliridhishi. Naomba atupatia jibu la uhakika. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme kitu kimoja, Mheshimiwa Mbunge anasema jambo la maana sana hapa. Jambo kubwa tu zuri.Yaani kule kuna Songwe *International Airport*. Kule kuna watu wanakwamba barabarani, kuna ajali zinatokea, wamelileta hili jambo limekuja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mstahiki Meya ndiye amelileta hili jambo kwa Waziri Mkuu. Wamezungumza habari hii Mheshimiwa Waziri Mkuu amemwandikia amemwandikia barua Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi/Kicheko)*

Hela zinazotakiwa hapa kwa kifupi niwaambie ili tuweze kuelewana vizuri. Barabara kilomita moja unahitaji shilingi bilioni moja pamoja na madaraja

yalikuwepo pale zipo kilomita pale 40, jumla ni shilingi bilioni 42. Halmashauri ya Jiji la Mbeya pale, imetengewa katika Bajeti hii tunayopitisha hapa bilioni moja na milioni 42 (1,420,000,000/=).

Mheshimiwa Spika, nikisema hapa leo nikamwambia dada yangu Mwanjelwa, sawa! Ofisi ya Waziri Mkuu inaahidi mwaka huu tutamaliza *feasibility study* na kila kitu tutaweka barabara pale. Wataniuliza hivi bwana wewe ulikuwa umekunywa pombe asubuhi ukajibu vitu hivi?Mimi naomba niseme kitu kimoja hapa. Mheshimiwa huyu anasema jambo kubwa na la msingi. Tutakachofanya sisi barua hizi zimekwenda ninazo nakala zote kama anataka nimwonyeshe, ninazo *correspondence* zote. *(Makofi)*

Leo asubuhi nimezungumza pale na *Engineer* Killian Haule ameniambia kwamba wao Halmashauri ya Jiji, tukiwaachia hawataweza. Mimi nataka nimuahidi ninazo barua zote, ninazo *correspondence* zote.

Moja tunaiomba Wizara ya Ujenzi, Serikali itusaidie jambo hili na yapo maelekezo ya mapelekwa kule, amepeleka rai kuomba barabara hii na barua hiyo ya Waziri Mkuu ninayo hapa na *file* lote ninalo hapa. Ninataka nimwahidi kwamba sisi tutashughulikia jambo hili ili hicho anachokisema kiweze kufanyika. Ni kwa ajili ya taifa zima, barabara inayokwenda mpaka Johannesburg kule Afrika Kusini.

**SPIKA:** Samahani. Umeahidi vyote hivi lakini hata hivyo tunaendelea, Mheshimiwa Aliko Kibona. Wamemalizia muda wangu.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pia nimeshukuru kwa majibu ya Waziri lakini nina Swali moja la nyongeza.

Kwa sababu mchakato unaendelea kama alivyotuahidi hapa na hali kule ni mbaya wananchi wanapata ajali wanachelewa kufika makazini na kurudi majumbani.

Je, Serikali inaweza kuchukua hatua gani za dharura wakati pesa hizo nyingi bilioni 42 zikisubiriwa ili wananchi waweze kuishi maisha kama walio huru katika nchi yao?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba unijibu kwa kifupi sana maana yake jibu lenyewe ushajibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nitajibu kwa kifupi sana. Mheshimiwa Kibona anakuja tena na *angle* nyingine.

Sasa mkishaanza nyinyi mtarudisha hii halafu tutawaambia twende tukatengeneze barabara ya moramu pale halafu utarudisha hili jambo litarudi nyuma litaanguka hili.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tufanye hivi hii mambo ya watu wanagongwa na nini, ni suala la sisi, trafiki na watu wa mambo ya ndani tuzungumze nao vizuri tuweze kuweka pale kama ni matuta ama tutaweka utaratibu wa kusimamia watoto wasigongwe na magari na vitu vingine. Hilo tutafanya.

Kama kuna wazo hapa kwamba sasa kwamba ebu nenda ukaweke hata barabara ya moramu watu wawe wanapitia huko! Sisi tutakwenda kuliangalia hili jumla lakini *at the end of the day*, Halmashauri ya Jiji la Mbeya ndio linatakiwa liseme hivyo. Liseme kwamba sasa achana na barabara ya lami hebu twende tukaweke moramu pale tuone kama itawezekana.

Mimi nawaomba tusimame hapa tusiwe kama kina Tomaso msirudi nyuma tena mnaanza kusema kwamba tuanze kuangalia na nini mtalirudisha hili jambo nyuma, sisi tutasimama nalo, tutamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tuweze kuzungumza na wenzetu wa Ujenzi.

Na. 139

**Maombi ya Kupatiwa Leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini**

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED (K.n.y. MHE. AHMED ALI SALUM)** aliuliza:-

Kikundi cha wachimbaji wadogo cha Nyaligongo *Gold Mine Group* Kata ya Mwakitolyo kiliomba leseni ya uchimbaji tangu tarehe 18 Januari, 2013 katika Ofisi ya Madini Shinyanga.

Je, leseni hiyo itatolewa lini kwa kuwa hadi sasa hakuna majibu yoyote yaliyotolewa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini,, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa ufafanuzi kuwa, Kikundi cha Wachimbaji Wadogo cha Nyaligongo *Gold Mine Group* Kata ya Mwakitolyo hakijawahi kuwasilisha rasmi ombi la kupewa leseni ya uchimbaji mdogo wa Madini katika eneo la Mwakitolyo kama Sheria ya Madini (2010) na Kanuni zake zinavyoelekeza.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 3(2) ya Kanuni za Madini za mwaka 2010, utaratibu wa kuomba leseni za Uchimbaji Mdogo *(Primary Mining License)* ni pamoja na kujaza Fomu *MPF 5* inayotumika kuombea leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini. Fomu hiyo huambatishwa na mchoro unaoonesha eneo husika na baada ya kukamilika huwasilishwa kwa Afisa Madini wa Kanda inayohusika na usimamizi wa eneo hilo ikiambatana na malipo ya ada ya ombi ambayo hivi sasa ni shilingi 50,000/= kwa kila leseni inayoombwa.

Mheshimiwa Spika, Kikundi cha wachimbaji wadogo cha Nyaligongo *Gold mine Group* kiliwasilisha maombi yao ya leseni kwa njia ya barua bila kufuata utaratibu nilioutaja. Barua hiyo ya kuomba leseni ililetwa kwa mkono na wahusika kwa Afisa Madini Kanda ya Kati Magharibi tarehe 22 Januari, 2013. Baada ya kupokelewa, mwakilishi wa Kikundi hicho alielekezwa kufuata utaratibu wa kisheria kuwasilisha ombi hilo, lakini hadi sasa kikundi hicho hakijawahi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya Madini Kanda ya Kati Magharibi (Shinyanga), imebainika kuwa eneo ambalo Nyaligongo *Gold Mine Group* wanaomba kupewa leseni ya *PML* tayari lina leseni ya *PL No. 5044/2008* inayomilikiwa na kampuni ya *Pangea Minerals Ltd*. Hivyo, haitawezekana kuwapatia Nyaligongo *Gold mine Group*eneo hilo kwa sasa hata wakiwasilisha maombi yao kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy maswali ya nyongeza.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, imekuwa tatizo kubwa, wachimbaji wadogo wadogo hawapati ardhi ya kuchimbia migodi yao kwa sababu wachimbaji wakubwa wamechukua maeneo makubwa, wamehodhi na hawalipii *license,* wameweka tu alama ya ajabu ajabu na moja wapo katika Mkoa wa Katavi, mapori makubwa yamechukuliwa na baadhi ya wachimbaji lakini hata kulipia hawalipii na mchimbaji akitaka kwenda kule anafukuzwa.

Je, Wizara yako inachukua hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, leseni za Madini zinamilikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini (2010) na katika leseni za utafiti mkubwa, zina umri ambao miaka minne ya mwanzo, mchimbaji anamiliki, anapo *renew* anaachia eneo hilo nusu na *renew* tena kwa miaka mitatu baada ya miaka mitatu anaachia tena eneo nusu ana *renew* tena miaka miwili. Hiyo ndio kwa mujibu wa sheria.

Wizara imekuwa ikifanya kazi ya kupitia leseni kubwa nyingi na zile ambazo hazi-*perform,* tumekuwa tukichukua hatua ya kuzifuta na kuzirudisha Serikalini. Hivi tunavyozungumza ni zaidi ya leseni mia moja, tumeweza kuzifuta na zipo katika taratibu ya kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa maeneo mbalimbali ya nchi, ikiwemo eneo la Mpanda ambapo Mheshimiwa Keissy anatoka na maeneo mengine katika nchi yetu ambayo yanahodhiwa na wachimbaji wakubwa lakini wameshindwa kuyaendeleza, tunayarudisha na kuwapa wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Arfi swali la nyongeza.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza Swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa watafiti wa awali huwa ni wachimbaji wadogo wadogo, ndio huwa wenye kugundua maeneo ambayo yana rasilimali na kuanza kufanya kazi za uchimbaji na wamekuwa wanatapakaa katika nchi nzima. Matokea yake maeneo ambayo yamegunduliwa na hawa wachimbaji wadogowadogo yanahodhiwa na watu wenye nguvu kubwa ya kifedha na uwezo wa kununua leseni. Tatizo hilo kama alivyosema mwulizaji aliyetangulia ni kubwa mno.

Sasa nilikuwa nataka kujua ni lini mnamaliza tatizo hilo kwa wachimbaji wadogo wadogo walioko Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo mengi ya uchimbaji yamekuwa yakichimbwa na wachimbaji wadogo wadogo kwa miaka mingi na Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa wachimbaji wadogo kwamba kumiliki ardhi kwa Hati za kimila haitoshi kukupa haki ya kuchimba madini. Hivyo tumekuwa tukihamasisha wachimbaji wadogo kuomba leseni ili waweze kupata haki ya kuchimba madini.

Sasa kwa Sheria zetu, mwombaji wa leseni anapokuja kuomba na eneo likakutwa halina leseni yoyote, basi mwombaji yule hupewa leseni hiyo. Sasa eneo ambalo anapewa unakuta tayari kuna wachimbaji wadogo ambao wanaendelea na uchimbaji bila ya kuwa na leseni ama kuwasilisha maombi na hapo ndipo panapotokea migogoro ya umiliki.

Tumeendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo nchini kote, umuhimu wa kukata leseni na kuwasisitiza wachimbaji wakubwa kwamba maeneo ambayo yana wachimbaji wengi wadogo waweze kutenga pia maeneo hayo kwa wachimbaji wadogo.

Tumefanya hivyo Singida hivi karibuni kwenye mgodi wa Shanta, tumeweza kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo pia tumeweza kufanya hivyo Geita kwa wachimbaji wa Mgusu na tunaendelea kutoa na maeneo mengine ikiwemo eneo la Bilyanhulu kule kule kwa wachimbaji wa Nyangalata.

Sasa kwa kesi ya Mpanda ni kweli kwamba eneo kubwa la Mpanda limeshikiliwa na wachimbaji wachache na kuacha wachimbaji wadogo wengi wakiwa hawana leseni. Zoezi hili ni endelevu hatuwezi kulimaliza kwa siku moja lakini Mheshimiwa Mbunge anafahamu jitihada tunazozifanya za kuhakikisha kwamba wale wote bila ya kuangalia ni nani ambaye anamiliki eneo ambalo haliendelezi, tunawanyang'anya na tutayagawa kwa wachimbaji wadogo kwa mujibu wa taratibu na sheria zilivyo na naomba tu Bunge lako Tukufu liweze kuunga mkono jitihada hizi za Wizara kuhakikisha tunatoa usawa kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Na. 140

**Mpango wa Kufua Umeme wa MW600 Ngaka-Mbinga**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kampuni ya *TANCOAL* wanao mpango wa kufua umeme wa MW 600 pale Ngaka-Mbinga.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga njia ya umeme toka Ngaka mpaka Songea?

(b) Je, Kampuni ina mpango gani wa kusambaza umeme unaopatikana katika Vijiji vya Ntunduwaro, Ruanda, Namsweya, Paradiso, Litumbandyosi na Amani Makoro?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imejipanga kujenga njia ya umeme toka Ngaka mpaka Songea mapema mwaka 2015. Mpango huo utafanyika sambamba na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa awali wa *MW 200.* Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2016.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TANCOAL* ina mpango wa kusambaza umeme kwenye maeneo ya Ntunduwaro, Ruanda, Paradiso na Amani Makoro kupitia mradi wa Gridi ya Taifa wa Makambako- Songea. Hatua iliyofikiwa sasa ni kwamba tayari Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya upimaji inayofanywa kwa ushirikiano wa wataalamu wa *TANESCO* na Mhandisi Mshauri (*M/s SWECO International*) kutoka Sweden.

Ujenzi wa mradi huu utatekelezwa na Kampuni ya *ISOLUX INGENIERIA S.A.* kutoka Spain, na unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2015 na kukamilika mwezi Oktoba, 2015. Katika mradi huu, wateja wa awali wapatao 13,000 wataunganishiwa umeme. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 153.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Namswee na Litumbandyosi havikuwekwa kwenye mradi wa Gridi ya Taifa wa Makambako- Songea. Hata hivyo, tayari Vijiji hivi vimefanyiwa tathmini na kujumuishwa kwenye Mpango kabambe wa Umeme Vijijini awamu ya Pili kama nyongeza, na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015.

**SPIKA:** Kijiji kile ni Namsweya siyo Nanswea. Mheshimiwa Kayombo swali la nyongeza.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Nchi yetu imekuwa ikitegemea maji kama chanzo kikubwa cha umeme na hivyo tumeingia kwenye matatizo makubwa sana ya umeme mpaka hivi juzi lilipokuja suala la gesi na kule Mkoani Ruvuma sisi tuna makaa yamawe. Kampuni ya *TANCOAL,* lengo lake kubwa ni kuzalisha umeme lakini imekuwa ikiuza makaa muda wote huu kwa sababu majadiliano yao na *TANESCO* yamechukua karibu muda wa miaka minne sasa. Tukizingatia hasara ambayo *TANESCO* inaipata ya shilingi bilioni 4.5 kila siku, ni lini mazungumzo ya *TANESCO* na *TANCOAL* yataisha ili tuweze kupata umeme unaotokana na makaa ya mawe?

Huu mradi upo katika kijiji cha Ntunduwaro na matumaini ya wananchi wale hata mwanzo waliambiwa kwamba kutajengwa mtambo wa kufua umeme, ni lini mtambo huu utajengwa?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati na Madini naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, majadiliano kati ya *TANESCO* na kampuni ya *TANCOAL* yamechelewa kwa sababu kubwa moja. *TANESCO* inatambua kwamba umeme ulio nafuu zaidi ni wa maji, unaofuatia ni umeme wa makaa ya mawe, unaofuatia ni wa gesi.

Lakini wenzetu wa *TANCOAL* wameng'ang'ania kuiuzia *TANESCO* senti 12 za dola, lakini *TANESCO* wanasema kwamba ni lazima utuuzie kati ya senti tano na senti sita ili tuweze kuingia. Hivyo, majadiliano yalipokwama ni hapo katika kuhakikisha kwamba *TANESCO* wanauziwa umeme kwa bei nafuu ili Watanzania waweze kupewa umeme kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa mtambo ni kama nilivyoeleza katika jibu la kwanza kwamba mara tu upembuzi utakapokamilika na makubaliano yatakapokuwa yamefikiwa ujenzi utaanza mara moja na tunatarajia kwamba wataanza ujenzi mwaka kesho. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Ningependa kumwuliza Waziri kwamba katika kijiji cha Wenda na kijiji cha Wenda katika Kata ya Mseke na Kijiji cha Kiwere katika Kiwele vimekuwa vina

matatizo ya umeme kwa muda mrefu sana ambapo umeme umekuwa ukipita juu ya hivyo vijiji viwili, wanakijiji wamekuwa wakipiga kelele kwa muda mrefu, ningependa kufahamu ni lini Serikali itaenda kuliangalia suala hili na kuweza kuwatatulia matatizo haya ya umeme wanakijiji wangu ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Naibu Waziri, umeme unapita juu ya vijiji hivyo lakini wenyewe hawana umeme.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, natambua kabisa Mheshimiwa Mgimwa tumekaa tumeongea na nimemwonesha kwamba vijiji hivi viko katika mpango kabambe wa *REA Na. 2* na sasa hivi Mkandarasi yupo *site* akipima na hapo atakapokuwa amekamilisha uwekaji wa umeme katika vijiji vya Wenda na Kiwere utawekwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMAD:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *TANCOAL* na kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe umekwama kwa sababu ya shirika la *TANESCO* kutokutoa *tariffs* zinazokubalika na Kamati yako ya Bajeti iliagiza Wizara na *TANESCO* waje na *tariffs* ili wawekezaji wote wajue kama mimi nikiwekeza kwa *coal rate* yangu ni hii, nikiwekeza kwa maji *rate* yangu ni hii mpaka leo Serikali haijatoa. Lakini Serikali hii inanunua senti hamsini kwa *Symbion* badala ya senti 12 wanazozikataa kwenye kampuni nyingine kwa sababu hakuna *uniformity* katika maombi ya Umeme.

Je, ni lini Serikali itakuja *tariffs* ili kila mwekezaji ajue ni *tariffs* za aina gani, ni umeme wa aina gani nitauza bei gani Tanzania ili kuondokana na huo usumbufu wa mazungumzo yasiyokwisha kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika maswali yaliyotangulia ni kwamba gharama za umeme sasa hivi zinaanza kuwa katika hali inayoeleweka. Kama nilivyosema ni kwamba umeme utokanao na maji ndiyo umeme nafuu zaidi ukifuatiwa na umeme utokanao na makaa ya mawe, ukifuatiwa na umeme utokanao na gesi.

Mpaka sasa hivi tumeweza kutambua gharama zinaooneshwa kimataifa, lakini inategemea na mwekezaji anawekeza katika eneo gani.

Mwekezaji mwingine anaweza kuwekeza sehemu ambayo miundombinu yake ni mibovu sana inabidi yeye mwenyewe aongeze gharama ya kutengeneza miundombinu ili kuhakikisha kwamba anafika sehemu hiyo.

Hivyo, *TANESCO* wanapojadiliana na Mwekezaji wanahakikisha kwamba wanaangalia na kuwa *fair* kwa Mwekezaji huyo ili tuweze kuhakikisha kwamba *tariffs* zinazotolewa zinakuwa katika kiwango fulani. Ndiyo sababu ninasema kuanzia kiasi fulani mpaka kiasi fulani, haiwezi kuwa *very specific*. Lakini tuna uhakika kabisa viwango vinaeleweka na mtu yeyote ambaye anataka kuwekeza katika umeme aonane na *TANESCO* watamweleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, wengine mtasubiri Wizara itakapokuja, tunaenda Wizara ya Maji Mheshimiwa Cecilia Paresso, anauliza swali hilo.

Na. 141

**Mradi wa Maji Wilaya ya Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Serikali inatekeleza mradi wa maji katika Wilaya ya Karatu ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Arusha *(AWUSA)*:-

(a) Je, mradi huo umegharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, mradi umetekelezwa kwa kiwango gani mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa maji katika Mji wa Karatu ikiwa ni mpango wa dharura wa kukabiliana na upungufu mkubwa wa maji uliokuwepo Karatu. Mradi huo ulikadiriwa kugharimu shilingi milioni 930 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi milioni 620 zimetumika kukamilisha kazi zifuatazo;

Ujenzi wa tanki moja linalopeleka maji kwenye tanki, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu kwa kilomita 11.3, ujenzi wa njia kuu ya umeme

yeneye urefu wa kilomita 1.2 na kufunga *transfoma,* ufungaji wa pampu na ujenzi wa vituo 12 vya kuchotea maji.

Utekelezaji wa awamu hii ya mradi umefikia asilimia 80 na umeanza kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Karatu ambapo tayari mradi umezinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 22 Aprili, 2014.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya mradi itaanza mwaka wa fedha 2014/2015 shilingi milioni 250 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi wa mradi ili kupeleka maji maeneo mengine hasa Karatu Magharibi.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matanki mawili ya mita za ujazo 225 kila moja, ujenzi wa mtandao wa bomba urefu wa kilomita 20, ufungaji wa umeme, ujenzi wa vioski vya maji, ujenzi wa nyumba ya pampu na ufungaji wa pampu. Kukamilika kwa awamu zote za mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 850,000 hadi lita 3,000,000 kwa siku na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 20 hadi kufikia asilimia 70. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, mradi huu ulikadiriwa kugharimu shilingi milioni 930 na mpaka sasa imetumika shilingi milioni 620, kwa kuwa siku ya uzinduzi Mheshimiwa Rais na Waziri husika waliahidi kwamba fedha zilizosalia zitaletwa haraka iwezekanavyo kiasi cha shilingi milioni 310. Je, ni lini fedha hizo zitapelekwa?

Kwa kuwa mradi huu mpya utakuwa chini ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka itakayoanzishwa na itahitaji kuwa na watumishi, na kwa kuwa katika Halmashauri yetu tuna upungufu wa Watumishi.

Je, Wizara iko tayari kuwaleta watumishi watakaoendesha Mamlaka hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliji-*commit* kwamba itakamilisha mradi huu kwa awamu na kupeleka fedha. Lakini ahadi yetu ipo pale pale kwamba fedha hizi ni katika Bajeti inayoishia mwezi wa sita. Kwa hiyo, awe na subira na niwape matumaini wananchi wa Karatu kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba mradi huu

unatekelezwa. Fedha hizo zitatoka katika mwaka huu wa fedha unaoishia mwezi wa sita, 2014.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, kweli utaanzisha mamlaka na mamlaka hizi zipo daraja (a), (b) na (c). Kwa hiyo, hii itakuwa ni daraja c ambalo Serikali itagharamia mishahara ya Watumishi na malipo ya umeme. Lakini pia watumishi wengine watatoka Serikalini na wengine katika Halmashauri husika ya Karatu. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maji anajua mradi huu wa maji Karatu ambao ulikuwa wa dharura, ulikuwa chini ya *AWUSA* na baadaye ikaleta mgogoro kukabidhi Halmashauri ya Karatu, na thamani ya mradi milioni 930 mpaka sasa milioni 620 zimeshatumika.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri wa Maji, ndani ya mradi huu kuna harufu ya ufisadi naomba ukaguzi maalum uweze kufanyika ili kujua thamani ya mradi na hasa ukilinganisha kwamba kisima kilichokuwepo ambacho kinatoa maji sasa kilichimbwa na KAVIWASU wao walikuja kudandia tu. Nitaomba mradi huu ufanyiwe ukaguzi maalum ili kupata thamani ya mradi halisi?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pili, ningependa nimshukuru sana mwuliza swali ambaye amekuwa anafuatilia kwa makini sana utekelezaji wa mradi huu na kushiriki katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa maji katika Mji Karatu na katika Miji mingine ambayo ina matatizo makubwa sana ya maji, imefanywa kwa dharura ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji haraka iwezekanavyo. Nataka nimhakikishie Mchungaji Natse pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba hamna ufisadi katika utekelezaji wa mradi huu. Wizara yangu haina tatizo kabisa na ufanyaji wa ukaguzi maalum katika miradi hii ikiwa ni pamoja na Karatu, Ngudu na miradi ambayo hivi sasa tunahakikisha kwamba wanapata maji haraka iwezekanavyo.

Meshimiwa Spika, ni kweli kwamba bado sehemu ya mradi huu umebaki na kama Naibu Waziri alivyosema matarajio yetu ni kutekeleza mwaka huu kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hakuna kutofautiana kokote kati ya Serikali na Halmashauri ya Karatu, hivi tunachongojea ni Halmashauri ya Karatu iteue Bodi kwa ajili ya uendeshaji wa mradi huo. Tayari Meneja wa Mradi ameshateuliwa na wafanyakazi wachache wa Halmashauri ya Karatu wameteuliwa.

Aidha, kisima kilichokuwepo Karatu ambacho kimetumika kwa awamu ya kwanza ya mradi huu hakikuchimbwa na KAVIWASU, kimechimbwa na fedha za *Water Sector Development Program.*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, naomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 142

**Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 Waziri wa Maji aliahidi ndani ya Bunge kuwa ifikapo Mei, 2013 wananchi wa Kata ya Selembala na Mkulazi Wilayani Morogoro wanaotakiwa kuhama na kupisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda watakuwa wamelipwa fidia zao, lakini hadi leo hakuna hata mwananchi mmoja aliyelipwa:-

(a) Je, ni lini Wananchi hao wa Wilaya vya Kidunda, kiburumo, Bwila Juu na Bwila chini watapatiwa fidia hiyo ambayo wameisubiri kwa muda mrefu?

(b) Je, ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro itapewa fedha na *DAWASA* au Wizara kwa ajili ya kuandaa viwanja, miundombinu ya barabara, shule zahanati na maji ili Wananchi hao wakilipwa fidia zao wapewe viwanja na wakute miundombinu iliyokamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango maalum wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kazi mojawapo katika mpango huo ni ujenzi wa Bwawa la Kidunda litakalohakikisha upatikanaji wa

maji ya kutosha kwa muda wote katika mto Ruvu kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha maji Ruvu Juu Mlandizi na Ruvu Chini Bagamoyo. Katika mradi wa Bwawa la Kidunda ipo miradi mingine ya kujenga barabara na mradi wa kuzalisha umeme. Maeneo yatakayojengwa Bwawa, njia a kupitisha nguzo za umeme na barabara yanahitaji kulipwa fidia kwa wananchi. Tathmini ya maeneo hayo imefanyika na gharama ya fidia iliyopatikana ya shilingi bilioni 7.9.

Kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha kwa sasa Serikali inakamilisha mapitio ya mahesabu ya ongezeko la thamani ya fidia, fedha hizi zitaanza kulipwa mara baada ya kukamilisha mapitio ya mahesabu hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imetuma kiasi cha shilingi milioni 241 Mwezi Oktoba, 2013 kwenda Halmashauri ya Morogoro kwa ajili ya kuanza upimaji wa viwanja vya makazi mapya vilivyopo eneo la Nzasa lililopo katika kijiji cha Bwila Chini. Kazi ya upimaji imechelewa kuanza kwa sababu ya mvua na mafuriko ambayo yamekata mawasiliano ya barabara. Kazi hii itaendelea mara baada ya mvua kwisha. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Waziri ni kielelezo tosha kwamba Wizara haijajipanga au Serikali haijajipanga katika kuendeleza mradi huu. Dhamira ya dhati inayoonekana kwa Serikali ni kutaka kuendelea kuwatesa wananchi wa vijiji vya Bwila Juu, Kiburumo, Bwila Chini na Kijiji cha Kidunda kukamwisha kuwaletea maendeleo.

Je, ni lini sasa Serikali itawalipa wananchi hawa fidia yao hasa ukizingatia Waziri anayenipa majibu alikuja tukafanya mkutano na wananchi hao na aliahidi kwamba ipo bilioni tatu ambayo tuliona ilitengwa katika Bajeti ya mwaka uliokwisha na aliahidi siku 14 wananchi hawa watapata hela. Lakini mpaka leo ni zaidi ya miezi mitatu hakuna na leo naambiwa kwamba inatafutwa bilioni saba.

Je, ikiwa imeshindikana wananchi hawa wa vijiji hivi, wana haki ya kuukataa huu mradi ili waendelee na maendeleo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali haina nia ya kuwatesa wananchi wa Jimbo lake na hasa ambapo tutajenga mradi huu. Pia Serikali inayo dhamira ya kweli na iko katika mipango imeanza michakato na harakati za kuhakikisha kwamba bwawa la Kidunda linajengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli mimi na yeye na Mheshimiwa Nkya tulikwenda na tulifanya mkutano pale Bwila na wananchi sasa wananisikia. Katika Mkutano huo niliagiza kwamba wananchi wale kwanza walikuwa hawaelewi hata ni nini watakacholipwa, nilielekeza Halmashauri na *DAWASA* wawaelewe wananchi wale kila mmoja anadai nini. Lakini lilizuka jambo la kuongezeka kwa fidia kwa sababu imekaa muda mrefu hivyo thamani ya fedha inabadilika hivyo hilo nalo likawa jambo jipya japo bilioni tatu zipo na wangeweza kuzipokea lakini ilionekana kwamba ni lazima ifanywe tathmini upya ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimeeleza wazi kwamba tathmini hii mpya karibia inakamilika ili tuweze kulipa fedha hizo kutokana na thamani ya sasa.

Pili, kwa kuwa Serikali inayo nia hiyo ya kujihakikishia maji katika Jiji la Dar es Salaam, ningewashawishi wananchi hawa wasiususie mradi huu na Serikali iendelee na mipango yake kuhakikisha inatekeleza mradi huu.

**SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila atauliza swali hilo.

Na. 143

**Wasimamizi wa Sheria Kupatiwa Mafunzo**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** alliuliza:-

Wasimamizi wa Sheria kama vile Polisi, Mahakama, Maafisa Magereza na Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji hutakiwa kupata mafunzo juu ya kuratibu na kutekeleza haki zinazohusu wanawake:-

(a) Je, ni lini Serikail*(Makofi)* imetoa mafunzo hayo?

(b) Je, Serikali imewawezeshaje wasimamizi hao katika Mkoa wa Rukwa ili kuwafikia wanawake waliopo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Fastine Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jionsia na Watoto katika kipindi cha mwaka 2006 – 2011 ilitoa mafunzo yanayohusu haki za wanawake na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa wasimamizi wa Sheria wakiwemo Askari Polisi 110, Askari Magereza 110,

Mahakimu 60 katika Mikoa 8. Vile vile Watendaji wa Kata 80 na viongozi wa kimila wa Wilaya za Tarime, Rorya na Serengeti waliopata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Watendaji hao walipata mafunzo ili kuhakikisha kwamba wanatimiza wajibu wao wa kuratibu na kuhakikisha kwamba haki zinazohusu wanawake zinazingatiwa. Mafunzo haya yalitolewa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Wanawake *(UNWOMEN)* na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani au *(UNFPA)*.
Vile vile Wizara yangu kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilitoa mafunzo ya uelewa wa haki za binadamu kwa Mahakimu Wakazi 35 wa Mkoa wa Dar es Salaam lakini pia ilitoa mafunzo kuhusu haki za binadamu ikiwemo haki za wanawake na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake kwa Watendaji wa Halmashauri za Manispaa, Miji, Wilaya, Kata, Mitaa na Vijiji katika Mikoa 18 ya Tanzania Bara na Mikoa mitano ya Tanzania Zanzibar.

Aidha, mafunzo kwa wasimamizi wa Sheria yamekuwa pia yakitolewa pia yakitolewa na Asasi za kiraia kama vile Shirika la Kimataifa la Sheria ya Wanawake *(WILDAF)*, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, *TAWLA, WLAC, AFNET* na mashirika mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wasimamizi wa Sheria wanawezeshwa ili iwafikie wananchi wakiwemo wanawake hususani walioko vijijini wakimemo wa Mkoa wa Rukwa.

Aidha, wasimamizi wa sheria wamekuwa wakiwezeshwa kuwafikia wananchi kwa kupatiwa vitendea kazi mbalimbali zikiwemo, Sheria, Shajala, vipeperushi vinavyohusu kupinga ukatili kwa wanawake na kompyuta kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa majibu mazuri ya Naibu waziri, na pia niipongeze Serikali na *NGO's* mbalimbali ambazo kumbe wamekuwa wakitoa mafunzo haya kwa Wasimamizi wa Sheria na Haki za Wanawake. Lakini pia nimpoze Mheshimiwa Waziri kwamba wana mpango kabambe wa kupeleka mafunzo haya kwa Wasimamizi kule Mkoani Rukwa, mafunzo ambayo pia yatawafikia wanawake hadi Vijijini. Nina maswali mawili kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri kufuatia mafunzo hayo ambayo yanatolewa kwa Wasimamizi.

Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kufanya ufuatiliaji ili kwamba mafunzo haya yaendelee kutolewa lakini mafunzo hayo yaendelee kutolewa kwa wanawake hadi vijijijni?

Kutokana na takwimu mbalimbali inaonekana kwamba wanawake wengi wanafanyiwa ukatili wa aina mbalimbali. Ikiwemo ukeketaji, ambao mara nyingi sana umepelekea vifo kwa wanawake wakati wa uzazi.

Je, Serikali inaharakisha au ina mpango gani wa kuharakisha upelelezi na usikilizwaji wa kesi ambazo zinahusu ukatili kwa wanawake, kesi ambazo ziko Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana muuguzi huyu mstaafu kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia haki mbalimbali za wanawake hususani wanawake wa Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Katika swali lake la kwanza kwamba tuna mpango gani kama Serikali wa kuhakikisha kwamba tunafanya ufuatiliaji wa mafunzo ambayo Serikali imekuwa ikitoa kwa Wasimamizi wa Sheria. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunayo miongozo mbalimbali. Lakini vile vile tunazo *Standard Operating Procedures* mbalimbali ambazo Polisi wameandaa.

Lakini vile vile iko miongozo ambayo imeandaliwa pia na Wizara ya Afya. Iko miongozo ambayo imeandaliwa na Wizara Wanawake. Iko miongozo ambayo imeandaliwa na Mahakama lakini vile vile Wizara ya Katiba na Sheria katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufuatiliaji.

Lakini si hiyo tu Mheshimiwa Spika, yako Madawati mbalimbali takribani 417 ya jinsia na watoto ambayo yameanzishwa katika vituo mbalimbali vya Polisi ambavyo vinafungua majalada ya kesi mbalimbali.

Lakini vile kupitia madawati haya tumekuwa tukiwawezesha na wanao mwongozo wa utendaji kazi.

Lakini vile vile katika ngazi ile ile pale chini ya Kituo hicho dawati lile basi viongozi wao wamekuwa wakifuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba mafunzo haya yanatolewa. Lakini si hilo tu tumekuwa tukifanya ukaguzi sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba madawati haya au Wasimamizi hawa wa Sheria wamekuwa wakitoa huduma kwa kadiri miongozo ilivyo.

Katika swali lake la pili, ni kwa namna gani Serikali inaharakisha upelelezi na usikilizwaji wa mashauri mbalimbali. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba liko tamko la Nchi za Maziwa Makuu la Mwaka 2012 mwezi Julai, ambapo Waheshimiwa Marasi wa nchi za Maziwa Makuu walikubaliana kuhakikisha kwamba kunakuwa na Vikao Maluum vya Mahakama kwa ajili ya kusikiliza mashauri yanayohusu ukatili wa kijinsia. Lakini si hilo tu tuko katika taratibu za kukamilisha utaratibu wa kuharakisha na kuyapatia masuala ya ukatili kipaumbele katika ngazi ya upelelezi.

Lakini vile vile kuhakikisha kwamba yanapewa kipaumbele katika hatua ya usikilizaji wa mashauri haya na kuyatolea hukumu. Lakini kimsingi tu nipende kumweleza kwamba katika tamko hili la nchi ya Maziwa Makuu ilikubalika kwamba mashauri haya yasipelelezwe kwa zaidi ya miezi mitatu. Lakini vile vile yanapofika Mahakamani basi yaendeshwe kwa chini ya miezi mitatu ili kwa ujumla wake basi isizidi miezi sita ili wahanga wa masuala haya yaweze kupatiwa haki kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa haya matukio yanazidi kuendelea tunashuhudia vyombo vya habari watoto wanabakwa, wakina mama nao pia wanabakwa na haki zinakuwa hazipatikaniki.

Je, Mheshimiwa Waziri utahakikisha hawa akina mama wanavyofika kwenye mambo ya Sheria wanapata haki zao pamoja na watoto?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kwamba nitaweza kuhakikisha kwamba wanawake wanavyofanyiwa vitendo hivi vya ukali wa kijinsia au watoto wanapata haki zao. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba milango ya Wizara yetu iko wazi, lakini milango ya Taasisi zingine za Serikali.

Lakini endapo kuna mtu yoyote atapata ugumu katika kuharakishiwa masuala mbalimbali amefanyiwa ukatili basi Ofisi yangu iko wazi. Napenda kumhakikishia kupitia yeye Mbunge. Lakini vile vile kupitia Wizara ya Sheria na mara nyingi nimekuwa nikigawa namba yangu ya simu na wengi wengi wamekuwa wakinipigia. *(Makofi)*

**Utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake**

**MHE. CHRISOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Mwaka 1985 Tanzania ilisaini mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake *(CEDAW)* wa mwaka 1979 hivyo kukubali kutoa taarifa ya utekelezaji wa matakwa ya mkataba huo:-

Je, Tanzania itatoa taarifa ya aina gani juu ya utekelezaji wa kipengele kinachotaka kuwepo kwa mipango thabiti itakayosaidia wasichana kuendelea na masomo ikiwa ni pamoja na wale wanaokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito usiotegemewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi *CEDAW* ulipitishwa tarehe18 Desemba 1979 na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Mkataba huu ulianza kutumika taerehe 3 Septemba, 1981. Tanzania ilisaini mkataba huo tarehe 17 Julai, 1980 na iliridhia mkataba huo mwaka 1985.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipengele kinachotaka kuwepo kwa mpango wa kuwasaidia wasichana wanaopata mimba kifungu Na. 10(f) *CEDAW* kinazitaka nchi wanachama kuweka mkakati wa kupunguza idadi ya wanafunzi wasichana wanaoshindwa kuendelea na masomo.

Aidha, nchi zilizoridhia mkataba huo zinapashwa kuanzisha *program* za kuwaendeleza wasichana wanaoshindwa kuendelea na masomo. *Program* zilizoanzishwa na Tanzania ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya stadi mbalimbali za maisha ambazo zitawasaidia katika kujiendeleza kiuchumi, kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi kwa kutumia ujuzi walioupata.

Mafunzo haya yanatolewa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Ulembwe, Njombe, Ilula, Ikwiriri, Bigwa, Mamtukuna na Mbinga. Mafunzo haya ya stadi za maisha yanatolewa pia na Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi kama vile UMATI na kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambapo vipo chini ya Wizara yangu. Aidha, kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa

waliokosa MEMKWA wanafunzi wasichana wanapata fursa ya kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Katika kuhakikisha kuwa wasichana wanamaliza masomo yao mkakati uliyopo kwa hivi sasa ni pamoja na kujenga mabweni ya wasichana katika shule za Sekondari za Kata. Aidha, upo umuhimu wa kuwaelimisha wanafunzi wa kike na kiume kuhusu elimu ya uzazi ili kuepukana na tatizo hili. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Spika, athari za mtoto wa kike kupata mimba akiwa mdogo ni nyingi. Mojawapo ikiwa ni kukosa elimu ya darasani.

Kwa hiyo, mtoto huyu hata maisha yake ya baadaye yanaathirika Mtoto huyu anapopata mimba akiwa mdogo anakosa pia elimu ya uzazi. Hivyo inapelekea kupata tena mimba nyingine na matokeo yake tunazalisha watoto wengi wa mitaani. Lakini kikubwa zaidi Mheshimiwa Spika, ni kunyanyapaliwa. Swali langu kwa sababu jibu la msingi la Waziri ni kwamba kuna vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa ajili ya watoto hao wanaopata mimba lakini ukizingatia kwamba umri wa watoto hao wengi ni mdogo, wengine ni wa shule za msingi, kati ya miaka 9 mpaka 16.

Hawa watoto watawezaje kwenda kusoma au kupata elimu katika vyuo vya maendeleo wakati umri wao bado ni mdogo na akili yao haijakomaa? Serikali ina mkakati gani mwingine wa kuwawezesha watoto hawa kupata elimu ya darasani ili waweze kuishi maisha mazuri pamoja na watoto watakaowazaa?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, nauliza kwa kifupi. Swali la pili Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu wengi wanaowapa ujauzito watoto hawa ni watu wenye umri mkubwa wana uwezo wa kifedha, pia wana ushawishi mkubwa kwa wanabinti hawa na matokeo yake wanaposikia watoto hao wamepata ujauzito wanawaruka. *(Makofi)*

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuja na sheria nyingine yenye meno kuwabana wanaume hawa waharibifu kuliko hii ya sasa hivi ambayo haina matunda? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kimsingi mkakati tuliokuwa nao kupitia Wizara ni kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Ellimu wanafunzi wanaweza wakapata elimu ya MEMKWA. Huu ni mpango wa Elimu ya Msingi kwa waliokosa. Lakini

mikakati mingine kama nilivyosema ni kuwaweka wanafunzi hawa karibia na Shule zao ikiwa ni pamoja na kujenga mabweni ili kusiwe na eneo refu la kute mbea wakati wanakwenda shule.

Lakini kama nilivyosema Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinatoa elimu hii kwa sababu kwenye vile vyuo vya Maendeleo ya Jamii kuna kozi inaitwa MAMAKOZI. Hiyo MAMAKOZI inasaidia mwanafunzi akitoka darasani anaenda kunyonyesha. Akisha nyonyesha anarudi. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu MEMKWA pia inawasaidia. Maana elimu ni haki ya kila mmoja. *(Makofi)*

Kuhusiana na wale wanaotenda makosa ikiwa ni pamoja na makosa ya kubaka, kuwapa mimba wanafunzi, Sheria ya Makosa ya kujamiana *Sexual Offense Act* inakataza kabisa wanafunzi kupata mimba wakati wakiwa shuleni. Kwa hiyo, Sheria hii tunayo, na kwa kweli inafanya kazi na hususani kupitia madawati yetu ya jinsia ambayo tunayo katika Vituo vyetu vya Polisi, makosa haya yamekuwa *reported.*

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata. Kwa sababu ni maswali mengi bado Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Deo Sanga atauliza swali linalofuata.

Na. 145

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Serikali ilitangaza nia ya kujenga soko la Kimataifa katika mji wa Makambako na eneo kwa ajili hiyo lilishatengwa ambapo baadhi ya wananchi walioguswa na eneo hilo waliahidiwa kulipwa fidia.

(a) Je, soko hilo litajengwa lini kama ilivyokusudiwa?

(b) Je, wananchi watakaohamishwa wataslipwa lini fidai yao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpe pongezi sana Mheshimiwa Sanga kwa jinsi ambavyo anamekuwa ni mfuatiliaji nzuri sana wa Maendeleo ya Jimbo lake hususani soko hili la Kimataifa la Makambako, ambalo kwa miaka mingi amekuwa akilifuatilia. Naomba sasa nijibu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza lengo la Serikali la kufanikisha ujenzi wa soko la Kimataifa la Makambako, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Mji wa Makambako, imekamilisha yafuatayo:-

Kwanza upembuzi yakinifu umeshakamilika, eneo la soko la ekari 62 katika eneo la Mji Mwema limeshaandaliwa. Mpango kabambe wa utekelezaji yaani *master plan* imeshakamilika. Tathmini ya athari ya mazingira imeshafanywa na sasa hivi kinachosubiriwa ni hati yake tu. Michoro imeshakamilika na kuwasilishwa Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kupatiwa Hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefanya mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Tanzania *TIB* kuhusu upatikanaji wa rasilimali za ujenzi wa soko hilo ambako mwanzoni mwa mwezi Mei, 2014 *TIB* wametembelea eneo la mradi na kufanya mazungumzo na uongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Mji wa Makambako kwa lengo la kuhimiza ukamilishwaji wa taratibu za muhimu ili waweze kutoa fedha.

Aidha, rasimu ya makubaliano yaani *MOU* ilishawasilishwa na *TIB* kwa Ofisi ya Mkurugenzi tangu mwezi Machi, 2014 na inasubiriwa ili kukamilisha taratibu za kutiliana saini.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwomba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Makambako kuridhia na kupitisha Rasimu hiyo haraka na kuiwakilisha *TIB* kwa ajili ya hatua zaidi kwani TIB wameshindwa kuendelea na taratibu nyingine wakisubiria *MOU* hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya malipo kwa wananchi 217 watakaohamishwa ilifanyika mwaka 2011/2012 ikionyesha zaidi ya shilingi bilioni 2.175 zitalipwa. Aidha, ili kufanikisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa soko hilo Halmashauri ya Mji wa Makambako imekubaliana na *TIB* kuwa ilipe fidia ili kuharakisha ujenzi wa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, fedha zitakazotumika kulipa fidia zitatoka *TIB* na zitakuwa kama sehemu ya gharama za gharama za mradi. Baada ya kukamilika kwa taratibu za malipo fidia italipwa pamoja na malimbikizo yake kwa walengwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 ambayo ndiyo inayotumika hivi sasa. Nashukuru.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Waziri kwa majibu mazuri sana. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi hawa wa eneo hilo la Mji Mwema tangu mwaka 2002 wamekuwa wakiishi kwa hofu sana, kwa sababu eneo tangu lichukuliwe na Serikali wamekatazwa nyumba zao kufanya ukarabati, kuendeleza kitu chochote.

Je, wananchi hawa ili sasa wasiishi kwa wasi wasi anawaambia nini wananchi wangu wa Makambako?

Swali la pili, je Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge hili la Bajeti ili haya aliyosema twende tukawaambie wananchi wale wa Makambako ili waishi bila wasi wasi juu ya kulipwa fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, mimi nataka kutoa rai kuwa wananchi wa Makambako ambao maeneo hayo yatachukuliwa kwa ajili ya soko hili la kimataifa, waondoe wasi wasi kwa sababu Serikali itawafidia kama ambavyo ilivyokubaliana na kwamba soko hili vile vile litawasaidia kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo ni kutu ambacho pia kina manufaa kwao.

Kuhusiana na kwenda kutembelea, Mheshimiwa Spika, nataka tu niwatangazie, Mheshimiwa Deo Sanga na Wabunge wengine wote ambao maeneo yana masoko ambayo yamelengwa kuwa mara tu baada ya Bunge hili mimi natarajia kuzungukia masoko yote ambao yameainishwa kwa ajili ya kwenda kuangalia.

Na. 146

**Uvamizi wa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza:-

Kumejitokeza hali ya uvamizi wa makazi ya wanafunzi hasa katika Vyuo Vikuu na kuwapora wanafunzi mali zao na hata kuwadhuru:-

(a) Je, ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha maeneo yote ya vyuo yenye wanafunzi yatapewa ulinzi wa uhakika?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza idadi ya wanafunzi walioshambuliwa na mali zilizoharibiwa kutika kwa wanafunzi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lwenye Sehemu (a) na (b), kama ifwatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama wa raia wa nchi hii, wakiwemo Wanafunzi wa Shule na Vyuo, ni sehemu muhimu ya mustakabali wa elimu ya vijana wa Taifa letu. Jukumu hili ni letu sote kama sehemu ya wajibu wetu wa Kikatiba na kijamii. Jeshi la Polisi kama chombo chenye dhamana ya kusimamia wajibu huo litaendelea kuchukua hatua za kupambana na vitendo vya uvamizi na uhalifu mwingineo unaotokea katika vyuo vyote nchini.

Tutaendelea kushirikiana na Mamlaka husika zikiwemo Uongozi wa Vyuo, Halmashauri za Miji na Serikali za Mitaa katika Vyuo hivyo, ili kuweka miundombinu ya ulinzi shirikishi utakaosaidia kukabili matukio ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini kutumia Askari Polisi Wasaidizi *(Auxiliary Police)*. Au kuanzisha Vituo vya Askari hao kwenye maeneo yao, ili kutoa huduma za Kipolisi pale ambapo huduma hizo hazipo karibu. Aidha, napenda kuwaasa wanafunzi wa vyuo kutojihusisha na shughuli za mazingira hatarishi kwa usalama wao na mali zao.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2012/2013 jumla ya matukio ya uvamizi yaliyoripotiwa kwenye vyuo hapa nchini, ambayo yalisababisha vifo vya wanafunzi wawili na mali, zikiwemo simu, *computer* mpakato na nguo zao.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla sijauliza swali la nyongeza, naomba uniruhusu nitoe shukrani kidogo. Mwaka jana Mwanafunzi wa Chuo Kikuu, Kitivo cha Sheria, Alex Mugabe, alivamiwa na wanafunzi wenzake, majambazi, yakampiga risasi na akatoboka matundu 36 katika utumbo wake; naishukuru Serikali, nawashukuru Madaktari, walioweza kuokoa maisha ya kijana huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa bahati nzuri mzazi wa mtoto huyo amekuja kushuhudia nauliza swali hilo. Mheshimiwa Mugabe yuko hapa, Diwani wa Kata ya Lwanga.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, ulinzi wa vijana hawa ni jukumu la Serikali. Na kwa kuwa, dunia sasa imeingiliwa mno

na watu wanaohatarisha usalama. Kwa nini, Serikali, isiweke masharti magumu ambapo kuna nyenzo kama hizi za kucheki watu tunazopewa sisi na kuhakikisha kwamba, mazingira ya wanafunzi yanakuwa na uangalizi mkali, ili kuwaondolea wazazi wasiwasi watoto wao wanapokuwa mbali na wao?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage, kama ifwatavyo.

Mheshimiwa Spika, awali naomba nizipokee shukrani za Wizara kwamba, hapa Polisi imefanya vizuri na tuwape moyo vijana kama huyu, ili waendelee kufanya vizuri kila mahali.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi katika maeneo ya watu wengi na hasa katika kipindi hiki ambacho na ugaidi unatajwa ni lazima tusilinde tena kama tulivyozowea; lazima tutumie *gadgets* ambazo zinahitajika.

Nitoe wito kwa vyuo ambapo kuna mkusanyiko wa watu mkubwa wa wanafunzi, lakini pia hata kwenye maeneo muhimu kama mahoteli, kuhakikisha kwamba, tunatumia ulinzi wa kuhakikisha kwamba, kila anayeingia anapekuliwa Kisheria na ikiwezekana tutumie *gadgets* za kiteknolojia, ili kuhakikisha kwamba, anayeingia hataweza kusababisha madhara kwa watu ambao wanatumia maeneo yale.

Na. 147

**Ucheleweshaji wa Fedha za Halmashauri**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Lipo tatizo sugu la ucheleweshaji wa fedha za Robo ya Mwaka toka Serikali Kuu kwenda Hlmashauri:-

Je, usugu huu unatokana na nini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mwanza, kama ifwatavyo.

Mheshimiwa Spika, ruzuku kutoka Serikalini kwenda Halmashauri zetu ni takribani 90% ya Bajeti nzima za Halmashauri zetu hapa nchini. Aidha, Serikali inatambua tatizo la ucheleweshwaji wa ruzuku unaosababisha kuwepo kwa athari hasi katika utekelezaji wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Kwa kawaida fedha za Matumizi Mengineyo hutolewa kila mwezi na fedha za maendeleo za ndani hutolewa katika kila robo ya mwaka, wakati ambapo fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo hutolewa baada ya kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ucheleweshaji wa fedha za robo ya mwaka kutoka Serikali Kuu kwenda Halmashauri linatokana na ukweli kwamba, mapato yetu hayatoshelezi mahitaji muhimu, hususan mahitaji ya miradi ya maendeleo. Mara baada ya Bajeti ya Serikali kuidhinishwa na Bunge, Wizara ya Fedha hutekeleza jukumu la kutoa fedha kwenda katika Mafungu mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje. Utaratibu huu unatokana na ukweli kwamba, tunatekeleza Bajeti kwa kutumia mfumo wa *Cash Budget*.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mhesimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ruksa ya pili. Nipende pia kumshukuru Naibu Waziri kwamba amekuwa mkweli kuizungumzia Serikali yake kwamba, Bajeti haitoshelezi, ukiendelea hivyo utakuwa Waziri mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali. Kama hali hii ya Serikali kwamba, mapato hayatoshelezi na hasa hasa katika miradi ya maendeleo. Sasa Serikali ina mpango gani sasa, baada ya kukiri hivyo, kuwa na vyanzo vya mapato vingine tukiacha hivi ambavyo ni *business as usual,* kuwa na mapato ambayo yataletwa hapa, ili tuwe na Bajeti iliyo na fedha? Tunapopitisha tukiwa tunajua tuna pesa, kulikoni kupitisha Bajeti hewa kama lilivyo jina langu hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Hata kama fedha hizi zinaweza kupatikana, Serikali huwa mnatumia vigezo gani kupeleka katika Halmashauri zetu kwa sababu, Halmashauri hizi zinapishana utajiri na umasikini wa Halmashauri hizi. Mnatumia vigezo gani, ili kuwa sawa katika mgao wa mapato haya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati mingi. Kama nilivyosema mara kdhaa hapa katika kujibu maswali mbalimbali, moja ya mkakati ambao tunategemea utaongeza fedha, tunategemea kuleta Sheria ya Mabadiliko kwenye mambo ya Kodi, ambayo tunategemea kufuta baadhi ya Misamaha ya Kodi na fedha zitakazopatikana ziweze kwenda kwenye shughuli za maendeleo ya wananchi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili; tunaendelea kuimarisha makusanyo kwa kuwabana wakwepa kodi. Hili ni jambo lingine ambalo tunategemea litaweza kuongeza fedha. Lakini pia timu ya Wataalamu imeendelea kufanya kazi na tunategemea vyanzo vingine vya mapato vitaibuliwa na vyenyewe vitaweza kujumuishwa kwenye Sheria, ili kuweza kuongeza wigo wa mapato ya Serikali na kuaondokana na hili.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu Bajeti ambayo huwa tunapitisha sio hewa, isipokuwa ni ufinyu wa Bajeti na ndio maana katika makusanyo ya kila mwaka, kadiri fedha zinzvyopatikana, zimekuwa zikipelekwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, lakini mkakati mwingine, huu ni mtambuka kwamba, tunaendelea kuimarisha utaratibu wa kuetekeleza miradi kwa *PPP*. Hii itasaidia kama miradi mikubwa itaweza kufanywa, kutekelezwa kwa utaratibu huo, maana yake fedha ambazo zitakuwa zimeokolewa zitaweza kwenda katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; bajeti yetu ya Serikali inatengenezwa kuanzia ngazi za Halmashauri kwa hiyo, ngazi za Halmashauri wanatengeneza bajeti zao, zinaenda ngazi za Mikoa, zikishapitishwa ndio zinakuja kuunganishwa katika Serikali Kuu.

Huwa utaratibu wa Serikali Kuu baada ya kuwa tumeshashirikisha bajeti zakutoka kila maeneo fedha zinaanza kugawiwa kufwatana na wao walivyoweka vipaumbele. Kwa hiyo, kila Wilaya inakuwa na kipaumbele chake na sisi Serikali kwa kushirikiana nao tunaenda kutekeleza baada ya kuwa fedha zimepatikana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tumekula muda wa ajenda nyingine. Naomba niwatambue Wageni tulionao hapa:-

Kuna Wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ambao ni Wanafunzi 15 kutoka Chuo cha Ardhi Tabora; naomba wasimame walipo? *(Makofi)*

Ahsante sana. Mmesikia matatizo ya kupima ardhi kwa hiyo someni kwa bidii, pengine nchi nzima itakuwa imepimwa baada ya nyie kukamilisha kusoma kwenu. *(Makofi*

Tuna Wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Simbachawene kutoka *Tourist Safari – Arusha,* wakiongozwa na Ndugu Ricky Thomson, yuko wapi? *Okay.*

Tuna Mgeni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes, ambaye ni Ndugu Alfred Athanas Rwebangira, Mwenyekiti wa Vijana *CCM,* Kata ya Igura; yuko wapi Mwenyekiti? Ahaa ahsante, na yeye kijana anaonekana. *(Makofi)*

Nina Wageni 10 wa Mheshimiwa Lolensia Bukwimba kutoka Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Mji wa Geita, wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo; Mheshimiwa Diwani Elisha Lupunga, Mheshimiwa Diwani Lupunga yuko wapi? Ndio Mwenyekiti na Madiwani wengine wapo, yupo Diwani Ahmed Mbaraka; ahsante karibuni na ninadhani mmetoka safari ndefu. *(Makofi)*

Tuna Wagni 6 wa Mheshimiwa Halima Mdee, ambao ni Wajasiriamali kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Musa Kajanja na Bi. Getrude Ndibalema; naomba hawa wasimame, Wajasiriamali wenyewe wako wapi? Na Wajasiriamali waliokujanao ni wawili tu? *Ok.* Asante sana, karibuni sana. Tuna Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, huyu ni Mwalimu kutoka Rudewa, Mbarali huko Mbeya, anaitwa Ndugu Gloria Mlay; ahsante sana Mwalimu. *(Makofi)*

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Augustino Masele ambao ni Ndugu Philip Mtalasi – Katibu Mwenezi *CCM* Kata ya Nyakafulu, yuko Ndugu Lulwa Mashenji – Katibu Mwenezi wa *CCM* Kata ya Lulembela na Ndugu Masele Kasigala. Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* naomba wasimame wanafunzi wote kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, tafadhali simameni *Okay,* ahsanteni sana, karibuni sana. Msome kwa bidii Wanafunzi wetu kwa sababu hii ndio Dunia ya Mapambano hii.

Tunao Wanachama wengine 6 kutoka *Tanzania Youth Vision Association;* naomba wasimame walipo. Asanteni sana, tunashukuru sana. Karibuni na Wageni wengine wote ambao hatukuwataja hapa, wote mnakaribishwa sana.

Tuna Matangazo ya Kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 8.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati, ambacho kitafanyika katika Ukumbi Namba 227, jengo la Utawala.

Halafu Mhesimiwa Hussein Mzee, yeye ni Naibu Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wote wa *CCM* na Makaimu Katibu Wabunge wote wa *CCM;* anaomba niwatangazie Wabunge wote wa *CCM* kuwa, leo saa 7.00 mchana, mara baada ya kumalizika kwa Kikao hiki, kutakuwa na Kikao cha *Caucus* katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Naomba wote wanaohusika wahudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, muda wetu tumekula.
Katibu tuendelee?

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi?

Kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Bulaya?

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijasoma naomba nimpe pole Mheshimiwa Naibu Waziri, George Simbachawene, Mbunge, kwa kufiwa na baba yake na maiti iko nyumbani kwake, lakini yuko kwa ajili kutekeleza majukumu. Nampa pole sana, kamati itaungana na wewe katika mazishi, huko katika Jimbo lako la Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, lakini...

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni Baba yangu Mdogo.

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ni Baba yake Mdogo, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru Wapiga Kura wangu vijana wa Tanzania kwa kunipa ushirikiano wakiongozwa na vijana wa Mkoa wa Mara kuhakikisha majukumu yangu nayatekeleza. Mimi nawaahidi utumishi uliotukuka na sitawaangusha pale yanapokuja maslahi ya vijana katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana Jijini Dar es salaam, kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Wakati wa kuchambua bajeti…

**SPIKA:** Naomba wanaotoka *silence* inatakiwa humu ndani.

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baadhi ya Ushauri umezingatiwa na kufanyiwa kazi na Ushauri huo ulikuwa ni pamoja na Serikali

ihakikishe kwamba Halmashauri za Wilaya na Manispaa zote Mjini zilizokopeshwa fedha za Wizara kwa ajili ya kupima na kukuza viwanja, zinarejesha fedha hizo haraka iwezekanavyo, ili fedha hizo zipelekwe katika maeneo mengine ya nchi ambako upimaji wa viwanja unahitajika. Jumla ya shilingi milioni 308 zilirejeshwa kutoka kutoka katika Halmashauri 12, Halmashauri 15 hazijarejesha.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo hazijarejesha ni kama ifuatavyo; Bunda Mkoani Mara milioni 36, Manyoni milioni 72, Sengerema milioni 20, Tungamalenga – Iringa milioni 16, Songea – Ruvuma milioni 3, Manispaa ya Songea milioni 20, Singida milioni 41, Tarime milioni 36, Manispaa ya Morogoro milioni 10, Manispaa ya Kibaha milioni 220, Manispaa ya Kinondoni milioni 150, Manispaa ya Ilala milioni 400, Magu laki 6, Mji Mdogo Makambako milioni 20, Chato – Kagera milioni 32. Jumla ya fedha ambazo hazijarejeshwa ni 77,891,000/=.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahitaji utulivu.

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono utaratibu wa Wizara wa kuzikopesha fedha Halmashauri kwa ajili ya kupima viwanja.

Hata hivyo baadhi ya Halmashauri za Miji kwa makusudi zimekataa kulipa fedha hizo na hivyo kuzorotesha jitihada za Wizara katika kutoa huduma kwa maeneo mengine nchini. Kamati inazitambua Halmashauri 12 zilizorejesha fedha walizokopeshwa na Wizara na kuzitaka Halmashauri nyingine 15 ambazo hazijarejesha zifanye hivyo mara moja.

Aidha Kamati inapendekeza kiasi cha fedha kiongezwe ili kuongeza kasi ya upimaji viwanja.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kuwa jengo la ghorofa 16 ambalo liko katika kiwanja namba 1662/75 mtaa wa Indira Ghandi jijini Dar es Salaam ambalo limejengwa kinyume na kifungu namba 62 na 63 cha sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288, Toleo la mwaka 2002 pamoja na Kanuni namba 139(1)(c) ambayo ni hatari kwa usalama wa wananchi, livunjwe mara moja na kuwachukulia hatua kali za kinidhamu viongozi na watendaji wote wanaoendelea kutoa vibali vya ujenzi wa maghorofa bila kuzingatia sheria ya Mazingira na nyinginezo zilizopo. Suala hili tuliliagiza katika bajeti iliyopita na tunazidi kusisitiza utekelezaji huu ufanyike mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba agizo hili halijatekelezwa. Kamati inaiagiza Serikali kufikisha suala hili kwa Rais haraka ili lipatiwe ufumbuzi kabla ya madhara kutokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kusitisha utoaji wa kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT* kwa nyumba za Shirika la Taifa zinazojengwa kwa ajili ya kuuzwa kwa gharama nafuu kwa wananchi. Agizo hili halijatekelezwa na hivyo kuwafanya wananchi wa kipato cha chini kushindwa kunufaika na nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhakikisha deni la shilingi 9,082,000,000/= linalipwa haraka iwezekanavyo na Wizara na Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Shirika la Nyumba la Taifa ili Shirika liweze kukamilisha azma yake ya kujenga nyumba 15,000 ifikapo mwaka 2015. Kiasi cha shilingi bilioni 4,855,000,000/= kililipwa hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2014, deni lililobaki ni 4,226,000,000/=.

Kamati inasisitiza Wizara na Taasisi ambazo hazijalipa, kulipa madeni yote mara moja.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 108. Kati ya fedha hizo shilingi 25,959,000,000/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 72,172,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mpaka kufikia mwezi Aprili 2014, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 47 tu kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23, zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, changamoto: Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa ucheleweshwaji wa fedha za miradi ya maendeleo na kiwango kidogo kuliko fedha zilizoidhinishwa. Mfano Mradi wa Ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni uliidhinishiwa shilingi bilioni 50 ambapo hadi kufikia Aprili, 2014 Wizara ilipokea shilingi bilioni 7 tu sawa na asilimia 14 tu ya fedha zote zilizoombwa.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali: Kwa mfano, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wawekezaji, wanavijiji, Serikali na wananchi inayotokana na ucheleweshwaji wa kulipa fidia nakadhalika, ufinyu wa pesa zinazotengwa kila mwaka kwa kitengo cha Mabaraza ya Nyumba, kutokana na ufinyu huu, kasi ya kufungua Mabaraza

katika Wilaya mbalimbali imekwama na hivyo kuendelea kusababisha kuwepo mlundikano wa mashauri kwenye Mabaraza machache yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa viwanja vilivyopimwa unasababisha kuongezeka kwa ujenzi holela mijini hasa katika miji mikubwa inayoendelea kukua kwa kasi, kutokuwepo kwa ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na ardhi ya akiba *(land bank)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, ukosefu wa Mfuko wa Fidia ya Ardhi *(Land Compensation Fund)* kwa ajili ya kupata ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na wawekezaji, rushwa katika vitengo mbalimbali vya Wizara, Nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba kuendelea kuwa ghali kutokana na kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kinyume na maelekezo ya Rais aliyoyatoa tarehe 12, Desemba, 2012 alipokuwa akizindua mradi wa nyumba za gharama nafuu Kigamboni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, endapo Wizara itaisimamia mikakati iliyojiwekea kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kupunguza urasimu katika zoezi zima la kutoa vibali vya kuajiri, Wizara itafanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta maendeleo kwa Taifa kwani ardhi ndiyo msingi wa maendeleo kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015 pamoja na kazi zilizopangwa kutekelezwa: Kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliomba Bunge lako Tukufu idhinishiwe makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 88,850,000,000/=, kati ya fedha hizo, shilingi 42,933,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 34,379,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi 34,379,000,000/= kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kinajumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 21 na shilingi 13,379,000,000/= kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Maoni na ushauri wa Kamati: Ardhi ni rasilimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu ya ardhi.

Kwa kuzingatia thamani na umuhimu wa ardhi, ni vyema Serikali ikasimamia sheria zake za ardhi kwa manufaa ya maendeleo ya kila Mtanzania na kuhakikisha ardhi ya nchi yetu haiuzwi, kumilikishwa ovyo kwa wawekezaji kutoka nje.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwa kuwa mara nyingi viongozi wa vijiji huingia mikataba mibovu na wawekezaji ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wawekezaji na kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji, wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika nchi yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi: Moja ya changamoto kubwa ya Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kwa mfano, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wawekezaji na wanavijiji, Serikali na wananchi. Migogoro hii inachangia kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokupimwa kwa maeneo mengi ya makazi ya wananchi, upatikanaji mgumu wa hatimiliki za kimila, ucheleweshwaji wa kulipa fidia pale ambapo wananchi wanatakiwa kuhama.

Mheshimiwa Spika, moja ya madhumuni ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Migogoro ya Matumizi ya Ardhi ilikuwa ni kupunguza matumizi ya ardhi ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Pamoja na kuwepo kwa Tume hii bado migogoro ya ardhi imeendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali nchini ikichangiwa na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inashauri Serikali iangalie upya utendaji wa majukumu ya Tume kwa lengo la kuiongezea nguvu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na ardhi ya akiba *(land bank)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kamati inaamini utaratibu huu utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Kamati inaishauri Serikali kutatua tatizo la migogoro kwa kuendelea kuelimisha umma kuhusu maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na shughuli nyingine na kusimamia yasivamiwe kwani gharama ya kuwahamisha wananchi huwa ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, mipango miji na maendeleo ya makazi: Miji mingi hapa nchini imeendelea kukua kwa kasi kubwa bila ya kuwa na uwiano na taratibu za mipango miji. Ukuaji huu umechangia kuwepo kwa makazi yasiyo rasmi ujenzi holela hasa katika maeneo ya miji ambayo yamekuwa na wahamiaji wengi kutoka vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2008 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zinasimamia ukuaji wa miji na majiji na zinatoa dira juu ya namna gani miji ipangwe kulingana na miundombinu ya eneo husika. Hata hivyo Halmashauri za Manispaa na Wilaya

zimekuwa zikishindwa kuwapatia wakazi wake huduma mbalimbali zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kupima viwanja kwa ajili ya makazi na kwa mpangilio unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge kituo cha kupokelea picha za *satellite* mjini Dodoma ili kuharakisha upimaji wa ardhi na hivyo kuharakisha umilikishaji ardhi na hivyo kupunguza na hatimaye kuondokana na tatizo la migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza Serikali kwamba uandaaji na utekelezaji wa mipango miji ufuate sheria za ardhi zilizopo ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Vijiji Namba 5 ya 1999 na ya Mipango Miji Namba 8 ya 2007 vifungu namba 15, 28 na 29. Hapa Serikali inatakiwa kuwa makini katika kipindi cha utekelezaji wa mipango inayoandaliwa na iliyopo ili kuhakikisha mipango hiyo baadaye haibadilishwi kiholela kwa maslai binafsi au watu wachache.

Mheshimiwa Spika, kusimamia upatikanaji wa ulipaji wa fidia stahiki kwa watu wote ambao ardhi zao zimewekwa katika mipango miji pale Serikali inapobadilisha umiliki wa ardhi kwa kutumia vigezo vya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004. Utaratibu huu uende sambamba na upatikanaji wa tathimini sawa kuhakikisha kodi ya ongezeko la thamani inalipwa Serikali wakati wa kubadilisha umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana Kamati iliagiza Serikali kuvunja jengo moja la ghorofa lililopo katika Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam ambalo linaonekana kuhatarisha usalama na maisha ya wananchi, agizo ambalo mpaka leo halijatekelezwa. Mbaya zaidi ni pale uongozi wa Wizara ulipotoa majibu kwa Kamati kwamba jengo la ghorofa tulilotaka livunjwe bado halijavunjwa kwa kuwa wamiliki wamepeleka suala hili mahakamani na Mahakama kuweka pingamizi hadi kesi itakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali inasubiri jengo hili lianguke lipoteze tena maisha ya watu ndiyo ichukue hatua? Kigugumizi kinasababishwa na nini? Kamati inaishauri Serikali kujali zaidi maslahi ya wananchi na maisha ya wananchi waliowaweka madarakani badala ya rushwa kusababisha Serikali kutojali mali na maisha ya wananchi. Kamati inasisitiza jengo livunjwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha jengo hilo ambalo ni hatari kwa usalama wa wananchi linavunjwa mara moja ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya watu, taasisi na idara za Serikali ama kwa bahati mbaya au kwa makusudi kupindisha Sheria ya Mipango Miji ni lazima

vidhibitiwe kwa nguvu zote. Matukio kama ya ujenzi holela mijini, ujenzi usiozingatia sheria mara nyingi umesababisha maafa makubwa ikiwa pamoja na kuporomoka kwa baadhi ya majengo na mafuriko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni: Mnamo mwezi Oktoba, 2008, Serikali ilitoa tamko kupitia *GN* Namba 229 kuhusu mpango wa kujenga mji wa kisasa eneo la Kigamboni ambao unatarajiwa kuwa sehemu ya kivutio cha huduma za kijamii, kiuchumi na teknolojia cha Jiji la Dar es Salaam. Aidha uendelezaji huo unatarajiwa kuuwezesha mji mpya wa Kigamboni kushindana na miji mingine duniani katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na mkakati wa uendelezaji wa mradi wa Kigamboni. Toka mchakato wa kuendeleza mji wa Kigamboni uanze kumekuwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na malalamiko ya wakazi wa eneo husika kwamba mchakato wa uandaaji wa mpango kabambe wa mji mpya haukuzingatia Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 na wananchi kuzuiwa kukarabati na kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi hivyo kukosa imani na mradi huo. Kamati inaiagiza Serikali yafuatayo:- Moja, kuanza mara moja kukamilisha maandalizi ya mpango kabambe na kuanza utekelezaji wa mradi. Ili hilo lifanikiwe, kuna haja ya Serikali kubadili mkakati wake wa utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaishauri serikali ijishughulishe na ujenzi wa Miundombinu na maendeleo mengine yaachiwe wawekezaji na wananchi wanaomiliki ardhi ya Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, pili, kuanzia sasa Serikali iwashirikishe wananchi wa Kigamboni katika kila hatua ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na suala la fidia. Tatu, Serikali ihakikishe kwamba, wataalamu wa Wizara ya Ardhi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Katiba na Sheria na wadau wengine wote wanaohusika katika ustawishaji wa mipango miji na makazi wahusishwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nne, mapendekezo yote yatakayotolewa na wadau wote wakati wa mchakato ni muhimu yaletwe kwenye Kamati ili kujiridhisha, lengo likiwa ni kuepuka kutokea tena kwa utata wa utekelezaji wa ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaiagiza Serikali, baada ya kuwepo kwa ucheleweshwaji mkubwa katika utekelezaji wa mradi wa Mji Mpya wa Kigamboni na kama tulivyoshauri hapo awali ni wakati muafaka sasa kubadili

mkakati wa utekelezaji kwa kushirikisha wabia wengine wakiwemo wananchi wa Kigamboni. Aidha, kwa kuwa tatizo kubwa lililosababsha kukwama kwa utekelezaji wa mradi limekuwa ni ufinyu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuachana na mambo mengine ya utekelezaji badala yake ijikite kwanza katika suala la miundombinu ya Mji Mpya wa Kigamboni. Aidha, Wizara ya Ujenzi irejeshe shilingi 2,354,000,000/= iliyokopa kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo la Ujenzi wa Daraja la Kigamboni, Kurasini.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Dar Es Salaam kama vile mgogoro wa Chasimba, Makongo na Mloganzila-Kwembe iliyohusisha Serikali na wananchi wa maeneo hayo.

Kamati inasikitika kuona kwamba mbali ya malalamiko ya migogoro hiyo kupitia vyombo vya habari, Serikali haijafanya jitihada za makusudi kunusuru hali ya amani na usalama katika maeneo hayo. Na cha kushangaza zaidi, Kamati haijashirikishwa wala haijui na kwa maana hiyo Bunge lako Tukufu halijui kinachoendelea. Kamati inaitaka Serikali pale inapoamua mambo makubwa yanayohusu Ardhi kuhakikisha inashirikisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambayo hufanya kazi kwa niaba ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu uliopatikana katika mradi wa Kigamboni, ili kuepusha matatizo katika mradi wa Kigamboni na kuepusha matatizo katika miradi mingine ya ujenzi wa miji mipya, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

Moja, ushirikishwaji wa dhati wa wananchi wanaomiliki maeneo ambayo yametengwa mahsusi kupanga upya na kuendelezwa na Sheria ya Mipango Miji. Ushirikishwaji huu uanze katika kipindi cha kuandaa *Master Plan,* na uendelezaji wake na kwa kuwa Bunge lilishapitisha Sheria ya *PPP,* ni vyema Serikali kwa maana ya Wizara ikatumia sheria hii kila iwezekanavyo kuleta maendeleo ya kweli.

Pili, ushirikishwaji wa wananchi uende sambamba na uwazi katika kuangalia na kusimamia maslahi halisi ya taifa na wadau. Hii itasaidia kuhakikisha wadau walio wengi kufahamu kinachoendelea hivyo kuondoa sintofahamu wanayokuwanayo wananchi na wasiwasi kwamba wajanja wachache wanatumia mali ya Serikali kuandaa na kutekeleza mipango miji ili kujilimbikizia ardhi na kuitumia baadaye kwa maslahi binafsi bila hata faida ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikizingatia na kutekeleza mapendekezo haya Kamati inaamini yafuatayo yanapatikana. Migogoro inayotokana na ardhi

itapungua na hasara inayopatikana kwa taifa hivi sasa pia itapungua kwa kiwango kikubwa. Kamati haioni sababu kwa nini Serikali inashindwa kudhibiti migogoro hii wakati uwezo wa kuepusha na hata kuzuia inao. Wamiliki wa Ardhi, wananchi na jamii kwa ujumla wataona umuhimu wa shughuli za Serikali ikiwemo mipango miji na faida zake, hivyo kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake kwa maslahi mapana ya umma. Kuondoa mianya inayotoa fursa na ushawishi mbovu kwa viongozi na watu wachache wasio na nia njema kwa maslahi ya Taifa bali kujilimbikizia mali kwa maana ya ardhi kwa kutumia mgongo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wengi wa ndani na nje ya nchi watavutiwa na mazingira hayo mazuri, lakini pia mazingira hayo yatajenga ushirikiano mwema na jumuiya za kimataifa kutokana na kuwapo kwa mazingira stahiki ya uwezeshaji yaani *conducive investment climate.* Taifa litafanikiwa katika mipango yake ya kujenga miji mipya ya kisasa na yenye miundo mbinu toshelezi na maeneo yenye kutunzwa vizuri kwa matumizi ya kijamii kama maeneo ya wazi, bustani za miti na maua, viwanja vya michezo na kadhalika kama ilivyoainishwa katika sheria. Kamati inaamini kwamba kuwapo kwa maendeleo haya katika miji mipya ni muhimu kwa afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati inaishauri Serikali kutaifisha maeneo yote makubwa yasiyoendelezwa na kugawa kwa wananchi kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejifunza katika ziara yake nchini Singapore na Uturuki kwamba jukumu la uendelezaji wa miji mipya yamepewa mashirika ya nyumba ya nchi husika. Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipatie shirika mamlaka ya kupanga miji katika maeneo yake ya miradi mikubwa ili kuweza kuongeza ufanisi na ubora wa utekelezaji wa kazi kwenye miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo: Kama ilivyoelezwa hapo awali, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi bilioni 72 kwa ajili ya miradi sita ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 56 zilikuwa fedha za ndani na bilioni 16 fedha za nje, ambapo shilingi bilioni 50 zilitengwa kwenye mradi wa *Land Management Project* kwa ajili ya kuendeleza miji mipya ukiwepo wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi tajwa zilikuwa shilingi 15,747,000,000/= tu sawa na asilimia 21.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za miradi, ni wazi kwamba miradi kwamba mingi haijatekelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa na hivyo kuchelewesha fidia ambazo nchi inatarajia kuzipata

baada ya kukamilisha miradi iliyopo. Kamati inaitaka Serikali kuongeza jitihada za makusudi katika kuhakikisha fedha zinazotengwa zinapatikana kwa wakati ili kutekeleza miradi kama hiyo yenye tija kwa Taifa. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuongeza jitihada za makusudi katika kuhakikisha fedha zinazotengwa zinapatikana kwa wakati ili kutekeleza miradi kama hiyo yenye tija kwa Taifa.

Aidha, Kamati inataitaka Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya mradi wa Kigamboni, shilingi bilioni 43 ili kuwezesha mradi huu uanze na kama Serikali haiwezi kutoa fedha hizo basi itoe tamko kwamba imeshindwa kuendeleza mradi huu na wananchi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 1999, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu la msingi la shirika hili ni kujenga na kuwezesha ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara kwa ajili ya matumizi ya wananchi na Serikali pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za wazi za Shirika katika kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza, bado nyumba hizo zinaonekana kuwa ghali kutokana na mnunuzi kulazimika kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kwa mfano, kwa sasa nyumba ya bei ya chini inayouzwa shilingi milioni 46.9 kujumuisha *VAT*, ambapo bila *VAT* mnunuzi angeweza kulipa shilingi 39.8 ikiwa ni tofauti ya shilingi milioni 7.1.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Shirika limeweka lengo la kujenga nyumba 15,000 ifikapo mwaka 2015 ili kuwawezesha wananchi wengi hasa wenye kipato cha chini na kati kumiliki nyumba zinazojengwa na Shirika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa nyumba za shirika zinazojengwa kwa ajili ya kuuza kwa wananchi wa kipato cha chini na kati. Sambamba na ushauri huo, Kamati inatambua hatua ya Serikali ya hivi karibuni ya kuondoa ushuru wa forodha pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa na hilo kutoka nje ya nchi, Kamati inaiagiza Serikali kuliondolea Shirika la Nyumba *VAT* kwa vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaendelea kushughulikia ukubwa wa bei ya nyumba za Shirika la Nyumba kutokana na kodi, Kamati inaendelea kuwahamasisha wananchi kununua nyumba zinazojengwa na shirika hivi sasa badala ya kung'ang'ania kununua nyumba za zamani ambazo zilitaifishwa na kukabidhiwa Shirika la Nyumba la Taifa. Na kwa vile sababu ya kutaifisha nyumba hizo bado ni hai, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha nyumba hizo haziuzwi. Nyumba hizo ni mali na urithi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kulisaidia Shirika la Nyumba kuweza kumiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa gharama nafuu au kwa kupewa bure.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia kupunguza gharama ya nyumba ambazo zinajengwa kwa ajili ya kuziuza kwa wananchi wa kawaida; na itaisaidia Serikali, kwa kuwa Shirika la Nyumba ndiyo chombo pekee cha Serikali ambacho kinaweza kutumika kwa ajili ya kutunza ardhi ya akiba kwa ajili ya mwananchi.

Mheshimwia Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa msamaha wa kodi ya ardhi kwa shirika *(land rent)*;

Mheshimiwa Spika, Madeni ya Serikali na Taasisi zake kwa Shirika la Nyumba la Taifa: Katika maoni yake kwa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba Na Maendelo ya Makazi kwa mwaka 2013/2014.

Kamati iliishauri Serikali kulipa madeni yake yote ya kodi za pango kwa Shirika la Nyumba la Taifa ili liendelee kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi yake ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha deni la shilingi 4,229,000,000/= lililobakia linalipwa. Wizara na taasisi zinazodaiwa ni hizi zifuatazo: Kwa sababu ya muda sitazisoma, lakini Wizara ya Uchukuzi inaongoza inadaiwa 1,160,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha deni hilo linalipwa haraka iwezekanavyo kama kweli inataka Shirika la Nyumba kukamilisha azma yake ya kujenga nyumba 15,000 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Uthamini wa Mali ni kitengo muhimu katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kitengo hiki ni nguzo mojawapo ya utawala na usimamizi bora wa ardhi kwa kuwezesha maamuzi ya maendeleo bora ya ardhi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kitengo hiki ndicho kinachohusika na uthamini wa mali na fidia kwa wananchi waliohamishwa katika ardhi na mali iliyomilikiwa na Serikali na wamiliki binafsi, na kutokana na kuongezeka kwa ushindani wa mahitaji ya ardhi kulinganisha na ardhi iliyopo, ni vema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukiwezesha kitengo hiki kuongezewa wataalam na vifaa ili kiweze kutimiza wajibu wake kwa umakini mkubwa kwa sababu kitengo hiki ndiyo roho ya upimaji ardhi, lakini hakipewi fedha za kutosha.

Kitengo kinahitaji zaidi ya billioni 16 kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, heshima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze wajumbe wote wa Kamati nikianza na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Charles Mloka…

*(Hapa kengele Ililia)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati naomba kuwasilisha. *(Makofi*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU**
**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana Jijini Dar es salaam, kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Prof. Anna K. Tibaijuka, (Mb) akiwa na Naibu Waziri wake Mhe. George Simbachawene, (Mb) pamoja na Watendaji wakuu wa Wizara hiyo aliwasilisha taarifa na maelezo yake mbele ya Kamati.

Pamoja na majukumu ya Wizara, Mheshimiwa Waziri alieleza Dira na Dhima ya Wizara na masuala yaliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Katika kikao hicho, Kamati ilipitia taarifa zifuatazo:-

i. Utekelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015;

ii. Utekelezaji wa kazi za Shirika la Nyumba la Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na Mpango wa kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015;

iii. Utekelezaji wa kazi za Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na Mpango wa kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015; na

iv. Utekelezaji wa kazi za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na Mpango wa kazi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Ushauri umezingatiwa na kufanyiwa kazi. Ushauri huo ulikuwa ni pamoja na:-

(i) Serikali ihakikishe kwamba Halmashauri za Wilaya na Manispaa zote za Miji zilizokopeshwa fedha na Wizara kwa ajili ya kupima na kuuza viwanja, zinarejesha fedha hizo haraka iwezekanavyo ili fedha hizo

zipelekwe katika maeneo mengine ya nchi ambako upimaji wa viwanja unahitajika;

Jumla ya shilingi milion 308,109,000/= zimerejeshwa kutoka Halmashauri 12. Halmashauri 11 hazijarejesha.

Halmashauri ambazo hazijarudisha fedha ni:-

1. Bunda (Mara) - 36,000,000/=
2. Manyoni - 72,000,000/=
3. Sengerema - 20,000,000/=
4. Tungamalenga (Iringa)- 16,000,000/=
5. Songea (Ruvuma) - 3,419,700/=
6. Manispaa ya Songea - 20,000,000/=
7. Singida - 41,474,300/=
8. Tarime - 36,000,000/=
9. Manispaa ya Morogoro- 10,000,000/=
10. Manispaa ya Kibaha - 220,388,463/=
11. Manispaa ya Kinondoni- 150,000,000/=
12. Manispaa ya Ilala - 400,000,000/=
13. Magu (Mwanza) - 600,000/=
14. Mji mdogo Makambako- 20,000,000/=
15. Chato (Kagera) - 32,000,000/=

Jumla - 1,077,891,351/=

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono utaratibu wa Wizara wa kuzikopesha fedha Halmashauri (revolving fund) kwa ajili ya kupima viwanja. Hata hivyo baadhi ya Halmashauri za Miji kwa makusudi zimekataa kulipa fedha hizo na hivyo kuzorotesha jitihada za Wizara katika kutoa huduma kwenye maeneo mengine ya nchi. Kamati inazitambua Halmashauri 12 zilizorejesha fedha walizokopeshwa na Wizara na kuzitaka Halmashauri nyingine 11 ambazo hazijarejesha zifanye hivyo mara moja. Aidha Kamati inapendekeza kiasi cha fedha za *Revolving Fund* ziongezwe ili kuongeza kasi ya upimaji viwanja.

(ii) Serikali ihakikishe kuwa jengo la ghorofa 16 ambalo liko katika kiwanja namba 1662/75 mtaa wa Indira Ghandi jijini Dar es Salaam ambalo limejengwa kinyume na kifungu namba 62 na 63 cha sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) sura ya 288,Toleo la 2002 pamoja na Kanuni Na 139(1)(c) ya *Government (Urban Authorities) Development Conditions Regulation, GN No 242/2008* ambalo ni hatari kwa usalama wa wananchi linavunjwa mara moja na kuwachukulia hatua kali za kinidhamu viongozi na watendaji wote wanaoendelea kutoa vibali vya ujenzi wa magorofa bila kuzingatia sheria ya Mazingira na nyingine zilizopo. Suala hili tuliliagiza katika

bajeti iliyopita na tunazidi kusisitiza utekelezaji huu ufanyike mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitikishwa kwamba agizo hili halijatekelezwa. Kamati inaiagiza Serikali kulifikisha suala hili kwa Rais haraka ili lipatiwe ufumbuzi kabla ya madhara kutokea.

(iii) Serikali kupitiaWizara ya Fedha ione umuhimu wa kusitisha utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa zinazojengwa kwa ajili ya kuuzwa kwa gharama nafuu kwa wananchi;

Agizo hili halijatekelezwa na hivyo kuwafanya wananchi wa kipato cha chini kushindwa kununua nyumba hizi. Serikali isipoondoa kodi ya ongezeko la thamani nyumba hizi zitanunuliwa na watu wenye kipato cha juu na kuwanyima fursa hii wananchi wa kipato cha chini. Kamati inasisitiza Serikali kuondoa VAT ili wananchi wengi zaidi waweze kununua nyumba hizi.

(iv) Serikali kuhakikisha deni la shilingi 9,082,673,738/= linalipwa haraka iwezekanavyo na Wizara na Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Shirika la Nyumba la Taifa ili Shirika liweze kukamilisha azma yake ya kujenga nyumba 15,000; ifikapo mwaka 2015.
Kiasi cha shilingi bilion 4,855,716,534.35 kililipwa hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2014. Deni lililobaki ni billion 4,226,957,203.65. Kamati inasisitiza Wizara na Taasisi ambazo hazijalipa kulipa madeni yao mara moja.

(v) Serikali itambue umuhimu wa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa kutengea bajeti ya kutosha ili kuiongezea uwezo Tume katika kupunguza tatizo la migogoro ya ardhi inayoendelea kukua kwa kasi nchini;

Kamati inatambua kwamba Serikali imeitengea Tume shilingi bilioni 1,900,000,000/= mwaka 2014/15 lakini fedha hizi hazitoshi.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi billion

108,330,273,040/=. Kati ya fedha hizo shilingi billion 25,959,443,000/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi billion 72,172,349,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwezi Aprili 2014, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi billion 47,940,512,196/=. Kati ya fedha hizo, shilingi billion 23,733,514,925/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi billion 15,747,125,171/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 3.1 CHANGAMOTO

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Changamoto hizo ni pamoja na:-

1) Kuwepo kwa ucheleweshwaji wa fedha za miradi ya maendeleo na kiwango kidogo kuliko fedha zilizoidhinishwa. Mfano Mradi wa ujenzi wa mji mpya kigamboni uliidhinishiwa shilingi 50,172,349,000/=ambapo hadi kufikia Aprili 2014 Wizara ilipokea shilingi bilioni 7 sawa na asilimia 14 tu ya shilingi bilioni 50,172,349,000/= zilizoidhinishwa na Bunge;

2) Uhaba wa watumishi wa sekta ya ardhi kwa ujumla katika ngazi zote kuanzia Wizara, Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Watumishi waliopo hivi sasa ni asilimia 24 tu ya mahitaji halisi, hali ambayo inachangia ufanisi hafifu wa Wizara.

3) Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Kwa mfano migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wawekezaji na wanavijiji, Serikali na wananchi inayotokana na ucheleweshwaji wa kulipa fidia n.k;

4) Ufinyu wa pesa zinazotengwa kila mwaka kwa kitengo cha Mabaraza ya Nyumba. Kutokana na ufinyu huu, kasi ya kufungua mabaraza katika Wilaya mbali mbali imekwama na hivyo kuendelea kusababisha kuwepo mlundikano wa mashauri kwenye mabaraza machache yaliyopo.

5) Upungufu wa viwanja vilivyopimwa unaosababisha kuongezeka kwa ujenzi holela mijini hasa katika miji mikubwa inayoendelea kukua kwa kasi;

6) Kutokuwepo kwa ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na ardhi ya akiba *(Land Bank)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;
7) Ukosefu wa Mfuko wa Fidia ya Ardhi *(Land Compensation Fund)* kwa ajili ya kupata ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali na wawekezaji

8) Rushwa katika vitengo mbalimbali vya Wizara;

9) Nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba kuendelea kuwa ghali kutokana na kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kinyume na maelezo ya Rais aliyotoa tarehe 11 Desemba, 2012 alipokuwa akizindua mradi wa nyumba za gharama nafuu Kigamboni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, endapo Wizara itaisimamia mikakati iliyojiwekea kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kupunguza urasimu katika zoezi zima la kutoa vibali vya kuajiri, Wizara itafanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta maendeleo kwa Taifa kwani ardhi ndiyo msingi wa maendeleo kwa watu wote.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015 PAMOJA NA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA:

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 88,850,730,480/=. Katika fedha hizo, shilingi 42,933,854,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 34,379,977,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Shilingi 34,379,977,000/= kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kinajumuisha fedha za ndani shilingi 21,000,000,000/= na shilingi 13,379,977,000/= kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, kitatumika kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara ikiwa ni pamoja na:-

- Kujenga Mfumo wa ki-elektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi;

- Kuboresha maabara na karakana za utafiti wa vifaa vya ujenzi;

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mji mpya wa Kigamboni kupitia Wakala wa Mji mpya wa Kigamboni; na

- Kuandaa Mpango wa matumizi ya ardhi wa Bonde la Msimbazi kama Bustani ya Jiji.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya msingi na ya muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni rasilimali adimu ambayo hushindaniwa na watu au shughuli mbalimbali na hivyo kuifanya iwe na thamani kubwa. Kwa sababu hiyo ardhi inatakiwa kumilikiwa Kiserikali na Kimila kwa Sheria, Kanuni na taratibu zinazokubalika.

Kwa kuzingatia thamani na umuhimu wa ardhi, ni vyema Serikali ikasimamia Sheria zake za ardhi kwa manufaa ya maendeleo ya kila Mtanzania, na kuhakikisha ardhi ya nchi yetu haiuzwi/kumilikishwa ovyo kwa wawekezaji kutoka nje.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwa kuwa mara nyingi viongozi wa vijiji huingia mikataba mibovu na wawekezaji, ni dhahiri kwamba Serikali isipokuwa makini katika suala la kumilikisha ardhi kwa wawekezaji na kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji, wananchi wataendelea kuwa maskini na watwana katika nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 kama ifuatavyo:-

### 5.1 MIGOGORO YA ARDHI

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa za Wizara hii ni kuongezeka kwa migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Kwa mfano migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wawekezaji na wanavijiji, Serikali na wananchi n.k. Migogoro hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokupimwa kwa maeneo mengi ya makazi ya wananchi, upatikanaji mgumu wa hati miliki za kimila, na ucheleweshwaji wa kulipa fidia pale ambapo wananchi wanatakiwa kuhama.

Mheshimiwa Spika, moja ya madhumuni ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikuwa ni kupanga matumizi ya ardhi ili kuondoa

migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Mipango hii ya matumizi ya ardhi huongoza utendaji wa sekta zingine kama vile kutenga maeneo ya uwekezaji, kilimo, makazi, wanyamapori, misitu, vyanzo vya maji, malisho ya wanyama na shughuli zote zinazotumia ardhi zisigongane.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Tume hii bado migogoro ya ardhi imeendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali nchini ikichangiwa na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inashauri Serikali iangalie upya utendaji wa majukumu ya Tume kwa lengo la kuiongezea nguvu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeshindwa kufanya tafiti kwa wingi kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro. Kwa mfano kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Tume ilitengewa shilingi 950,000,000/- kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kamati inatambua kwamba Serikali imeongeza bajeti ya Tume kutoka million 950 hadi billion 1.9 kwa mwaka 2014/15. Ni matumaini ya kamati kwamba sasa Tume ya Mipango na Matumizi ya Ardhi itaongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha utaratibu wa kuwa na ardhi huru kwa ajili ya matumizi ya Serikali, na ardhi ya akiba (Land Bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kamati inaamini utaratibu huu utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la migogoro ya ardhi nchini.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali pale inapotwaa maeneo ya wananchi kwa ajili ya kuyaendeleza ihakikishe inawalipa fidia stahiki wananchi wa eneo husika kulingana na bei ya soko ya wakati huo ili kuepusha malalamiko na migogoro inayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kutatua tatizo la migogoro kwa kuendelea kuelimisha umma kuhusu maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na shughuli nyingine na kusimamia yasivamiwe kwani gharama ya kuwahamisha wananchi huwa ni kubwa zaidi.

## 5.2 MIPANGO MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

### 5.2.1 MIPANGO MIJI

Mheshimiwa Spika, miji mingi hapa nchini imeendelea kukua kwa kasi kubwa bila ya kuwa na uwiano na taratibu za mipango miji. Ukuaji huu umechangia kuwepo kwa makazi yasiyo rasmi *(squatter settlements)* na ujenzi

holela, hasa katika maeneo ya mijini ambayo yamekuwa na wahamiaji wengi kutoka vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2008 na Sera ya Maendeleo ya Makazi (2000), zinasimamia ukuaji wa miji na majiji na zinatoa dira juu ya namna gani miji ipangwe kulingana na miundombinu ya eneo husika.

Hata hivyo, Halmashauri za Manispaa na Wilaya zimekuwa zikishindwa kuwapatia wakazi wake huduma mbalimbali zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kupima viwanja kwa ajili ya makazi na kwa mpangilio unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango Miji kwani mbali na changamoto ya ukuaji wa kasi ya miji, kumekuwepo pia na ukaidi wa makusudi wa wananchi kutotii sheria hiyo;

Aidha Serikali ijenge kituo cha kupokelea picha za satellite *(satellite receiving station)* mjini Dodoma ili kuharakisha upimaji wa ardhi na hivyo kurahisisha umilikishaji ardhi na hivyo kupunguza na hatimaye kuondokana na migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza Serikali kwamba uandaaji na utekelezaji wa mipango Miji ufuate Sheria za ardhi zilizopo ikiwa ni pamoja na sheria ya ardhi namba 4 ya 1999, Sheria ya vijiji Namba 5 ya 1999 na ya Mipango Miji Namba 8 ya 2007 vifungu namba 15, 28 na 29.

Hapa Serikali inatakiwa kuwa makini katika kipindi cha utekelezaji wa mipango inayoandaliwa na iliopo ili kuhakikisha mipango hiyo baadaye haibadilishwi kiholela kwa maslai binafsi au watu wachache.

Kusimamia upatikanaji na ulipaji wa fidia stahiki kwa watu wote ambao ardhi zao zimewekwa katika mipango Miji pale Serikali inapobadilisha umiliki wa ardhi kwa kutumia vigezo vya Sheria ya ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya kodi ya mapato ya 2004.

Utaratibu huu uende sambamba na upatikanaji wa tathimini sawa kuhakikisha kodi ya ongezeko la thamani inalipwa Serikiali wakati wa kubadilisha umiliki wa ardhi.

### 5.2.2 UENDELEZWAJI WA MAJENGO

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha karibuni tumeshuhudia maendeleo makubwa katika ujenzi wa majengo ya ghorofa nchini kwa ajili ya makazi na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, sura ya 191 inazitaka mamlaka zote zinazohusika na kutoa vibali vya ujenzi wa majengo ya ghorofa yatakayozidi ghorofa tano zihakikishe majengo hayo yanafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM).

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana Kamati iliagiza Serikali kuvunja jengo moja la ghorofa lililopo katika Manispaa ya Ilala, Dar Es Salaam ambalo lilionekana kuhatarisha usalama na maisha ya wananchi agizo ambalo mpaka leo halijatekelezwa.Mbaya zaidi ni pale uongozi wa wizara ulipotoa majibu kwa Kamati kwamba jengo la ghorofa tuliloelekeza livunjwe bado halijavunjwa kwa kuwa wamiliki wamepeleka suala hili mahakamani na mahakama kuweka pingamizi hadi kesi itakaposikilizwa na kutolewa uamuzi. Hivi Serikali inasubiri jengo hili lianguke lipoteze tena maisha ya watu ndio ichukue hatua? Kigugumizi kinasababishwa na nini? Kamati inaishauri Serikali kujali zaidi maslahi na maisha ya wananchi walioiweka madarakani badala ya RUSHWA kusababisha Serikali kutojali mali na maisha ya wananchi. Kamati inasisitiza jengo hilo livunjwe.

Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha jengo hilo ambalo ni hatari kwa usalama wa wananchi linavunjwa mara moja ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya watu, taasisi na Idara za Serikali ama kwa bahati mbaya au kwa makusudi kupindisha Sheria ya Mipango Miji ni lazima vidhibitiwe kwa nguvu zote. Matukio kama ya ujenzi holela mijini na ujenzi usiozingatia sheria mara nyingi umesababisha maafa makubwa ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa baadhi ya majengo na mafuriko yasiyo ya lazima.

### 5.2.3 UENDELEZAJI WA MJI MPYA WA KIGAMBONI

Mheshimiwa Spika, Mnamo mwezi Oktoba 2008, Serikali ilitoa tamko rasmi kupitia GN namba 229, kuhusu mpango wa kujenga mji wa kisasa eneo la Kigamboni ambao unatarajiwa kuwa sehemu ya kitovu cha huduma za kijamii, kiuchumi na teknolojia cha Jiji la Dar es Salaam.
Aidha uendelezaji huo unatarajiwa kuuwezesha mji mpya wa Kigamboni kushindana na miji mingine duniani katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na mkakati wa utekelezaji wa mradi wa Kigamboni. Toka mchakato wa kuendeleza mji wa Kigamboni uanze, kumekuwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na malalamiko ya wakazi wa eneo husika kwamba mchakato wa uandaaji wa mpango kabambe wa mji mpya haukuzingatia sheria ya mipango miji Namba 8 ya mwaka 2007, na

wananchi kuzuiwa kukarabati na kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi hivyo kukosa imani na mradi huo. Kamati inaiagiza Serikali yafuatayo:- Moja, kuanza mara moja kukamilisha maandalizi ya mpango kabambe na kuanza utekelezaji wa mradi. Lakini ili hilo lifanikiwe kuna haja ya Serikali kubadili mkakati wake wa utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaishauri serikali ijishughulishe na ujenzi wa Miundombinu na maendeleo mengine yaachiwe wawekezaji na wananchi wanaomiliki ardhi Kigamboni.

Pili, kuanzia sasa Serikali iwashirikishe wananchi wa Kigamboni katika kila hatua ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na suala la fidia.

Tatu, Serikali ihakikishe kwamba, wataalamu wa Wizara za Ardhi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Katiba na Sheria na wadau wengine wote wanaohusika katika ustawishaji wa mipango miji na makazi wahusishwe kikamilifu.

Nne, Mapendekezo yote yatakayo tolewa na wadau wote wakati wa mchakato ni muhimu yaletwe kwenye Kamati ili kujiridhisha, lengo likiwa ni kuepuka kutokea tena kwa utata wa utekelezaji wa ujenzi wa mji mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaiagiza serikali, baada ya kuwepo kwa ucheleweshaji mkubwa katika utekelezaji wa mradi wa Mji mpya wa Kigamboni na kama tulivyoshauri hapo awali - ni wakati mwafaka sasa kubadili mkakati wa utekelezaji kwa kushirikisha wabia wengine na wakiwemo wananchi wa Kigamboni.

- Aidha, kwa kuwa tatizo kubwa lililosababsha kukwama kwa utekelezaji wa mradi limekuwa ni ufinyu wa fedha, Kamati inaishauri serikali kuachana na mambo mengine ya utekelezaji badala yake ijikite kwanza katika suala la miundo Mbinu ya mji Mpya wa Kigamboni.

- Aidha, Wizara ya Ujenzi irejeshe shilingi bilion 2,354,459,500/= ilizokopa kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo la Ujenzi wa Daraja la Kigamboni eneo la Kurasini.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu migogoro ya ardhi katika mkoa wa Dar Es Salaam kama vile mgogoro wa Chasimba, Makongo na Mloganzila-kwembe inayohusisha Serikali na wananchi wa maeneo hayo.

Kamati inasikitika kuona kwamba mbali ya malalamiko ya migogoro hiyo kupitia vyombo vya habari, Serikali haijafanya jitihada za makusudi kunusuru hali ya amani na usalama katika maeneo hayo na cha kushangaza zaidi Kamati haijashirikishwa wala haijui na kwa maana hiyo Bunge lako pia halijui kinachoendelea.

Kamati inaitaka Serikali pale inapoamua mambo makubwa yanayohusu Ardhi kuhakikisha inashirikisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambayo hufanya kazi kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu uliopatikana katika mradi wa kigamboni na ili kuepusha matatizo katika mradi wa Kigamboni na kuepusha matatizo katika miradi mingine ya ujenzi wa Miji mipya kamati inashauri serikali yafuatayo.

Mosi - Ushirikishwaji wa dhati wa wananchi wanaomiliki maeneo ambayo yametengwa mahsusi kupanga upya na kuendelezwa na Sheria ya mipango Miji. Ushirikishwaji huu uanze katika kipindi cha kuandaa mastaplan, planning schemes na uendelezaji wake na kwa kuwa Bunge lilikwishapitisha sheria ya ppp ni vyema serikali kwa maana ya wizara ikatumia sheria hii kila inavyowezakana kuleta maendeleo ya kweli.

Pili - Ushirikishwaji wa wananchi uende sambamba na uwazi katika kuangalia na kusimamia maslahi halisi ya taifa na wadau. Hii itasaidia kuhakikisha wadau walio wengi kufahamu kinachoendelea hivyo kuondoa sintofahamu wanayokuwa nayo wananchi na wasiwasi kwamba wajanja wachache wanatumia mali ya serikali kuandaa na kutekeleza mipango Miji ili kujilimbikizia ardhi na kulitumia baadaye kwa maslahi binafsi bila hata ya faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikizingatia na kutekeleza mapendekezo haya, Kamati inaamini yafuatayo yanapatikana:- Migogoro inayotokana na ardhi itapungua na hasara inayopatikana kwa taifa hivi sasa pia itapungua kwa kiwango kikubwa.

Kamati haioni sababu kwa nini Serikali inashindwa kudhibiti migogoro hii wakati uwezo wa kuepusha na hata kuzuia inao. Wamiliki wa Ardhi, wananchi na jamii kwa ujumla wataona umuhimu wa shughuli za Serikali ikiwemo mipango miji na faida zake, hivyo kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake kwa maslahi mapana ya umma.

Kuondoa mianya inayotoa fursa na ushawishi mbovu kwa viongozi na watu wachache wasio na nia njema kwa maslahi ya Taifa bali kujilimbikizia mali kwa maana ya ardhi kwa kutumia mgongo wa serikali.

Wawekezaji wengi wa ndani na nje ya nchi watavutiwa na mazingira hayo mazuri lakini pia mazingira hayo yatajenga ushirikiano mwema na jumuiya za kimataifa kutokana na kuwapo kwa mazingira stahiki ya uwezekaji yaani conducive investment climate.

Taifa litafanikiwa katika mipango yake ya kujenga miji mipya ya kisasa na yenye miundo mbinu toshelezi na maeneo yenye kutunzwa vizuri kwa matumizi ya kijamii kama maeneo ya wazi, bustani za miti na maua viwanja vya michezo na kadhalika kama ilivyoainishwa katika Sheria.

Kamati inaamini kwamba kuwapo kwa maendeleo haya katika Miji mipya ni muhimu kwa afya ya akili.

Aidha Kamati inaishauri Serikali kutaifisha maeneo yote makubwa yasiyoendelezwa na kuyagawa kwa wananchi kwa matumizi mengine.

### 5.2.4 Uendelezaji wa Miji ya Viungani (Satelite Cities)

Mheshimiwa Spika; Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilipendekeza kwamba Serikali ianze mikakati ya kuendeleza mji mdogo wa Luguruni katika Mkakati wake wa kuendeleza miji mdogo (Satellite cities) pembezoni mwa Jiji la Dar Es Salaam ili huduma katika maeneo ya pembezoni ziongezeke na kupunguza tatizo la msongamano wa watu na majengo katikati ya Jiji.

Wizara imeeleza kwamba baada ya kukabidhi eneo la Luguruni kwa Shirika la Nyumba la Taifa imeendelea kushirikiana na Shirika kwa kuunda Kamati inayobuni namna ya kuondoa vikwazo na kuandaa Mkakati wa utekelezaji.

Mheshimwia Spika; Kamati inaiagiza Wizara na NHC ziharakishe utekelezaji wa uendelezaji wa mji huu. Vile vile Wizara na NHC ziweke wazi vikwazo vilivyopo na Mkakati wa utekelezaji ulioandaliwa kuondoa vikwazo hivyo.

Kamati inafahamu kwamba NHC imefanya mazungumzo na Kampuni ya Surbana kutoka Singapore kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Uendelezaji wa Eneo hilo. Kamati inasisitiza Wizara kushirikiana kwa karibu na NHC kuhakikisha

mpango wa uendelezaji wa eneo hilo unakamilishwa na kutekelezwa kwa wakati kwa kuzingatia kwamba muda mrefu umepita bila eneo hilo kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejifunza katika ziara yake nchini Singapore na Uturuki kwamba jukumu la uendelezaji wa miji mipya imepewa kwa mashirika ya Nyumba ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi ilipatie Shirika Mamlaka ya kupanga miji katika maeneo yake ya Miradi mikubwa (Stelite City), ilikuweza kuongeza ufanisi na ubora wa utekelezaji wa kazi kwenye miradi mikubwa.

## 5.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi bilioni 72 kwa ajili ya miradi 6 ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 56 zilikuwa fedha za ndani na bilioni 16 fedha za nje. Ambapo shilingi bilioni 50 zilitengwa kwenye mradi wa *Land Management Project* kwa ajili ya kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Aprili 2014, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi tajwa zilikuwa shilingi bilioni 15,747,125,171/= tu sawa na asilimia 21.7 ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za miradi, ni wazi kwamba miradi mingi haitaendelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa na hivyo kuchelewesha faida ambazo nchi inatarajia kuzipata baada ya kukamilisha miradi inayopangwa.

Kamati inaitaka Serikali kuongeza jitihada za makusudi katika kuhakikisha fedha zinazotengwa zinapatikana kwa wakati ili kutekeleza miradi kama hii yenye tija kwa taifa.Aidha Kamati inaitaka Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya mradi wa Kigamboni shilingi billion 43 ili kuwezesha mradi huu uanze.

Kama Serikali haiwezi kutoa fedha hizo basi itoe tamko kwamba imeshindwa kuendeleza mradi huu na wananchi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao.

## 5.4 SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na 2. ya mwaka 1990, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu la msingi la Shirika hili ni kujenga na kuwezesha ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara kwa ajili ya matumizi ya wananchi na Serikali pia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la msingi, Shirika la Nyumba limeendelea na ujenzi wa miradi 7 yenye jumla ya nyumba 737 na kuanza matayarisho ya ujenzi wa miradi 38 yenye nyumba 4,114 za gharama nafuu, ya kati na ya juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za wazi za Shirika katika kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza, bado nyumba hizo zinaonekana kuwa ghali kutokana na mnunuzi kulazimika kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kwa mfano, kwa sasa nyumba za bei ya chini zinauzwa Tsh. Mil 46.9 kujumuisha VAT, ambapo bila VAT mnunuzi angelipa Tsh. Mil 39.8 ikiwa ni tofauti ya shilingi Milion 7.1.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Shirika limeweka lengo la kujenga nyumba 15,000 ifikapo Mwaka 2015 ili kuwawezesha wananchi wengi hasa wenye kipato cha chini na kati kumiliki nyumba zinazojengwa na Shirika. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Nyumba za Shirika zinazojengwa kwa ajili ya kuuza kwa wananchi wa kipato cha chini na kati.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ushauri huo,Kamati inatambua hatua ya Serikali hivi karibuni ya kuondoa ushuru wa Forodha pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa na Shirika la Nyumba la Taifa kutoka nje ya nchi. Kamati inaiagiza Serikali kuliondolea Shirika la Nyumba VAT kwa vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaendelea kushughulikia ukubwa wa bei ya nyumba za Shirika la Nyumba kutokana na kodi, Kamati inaendelea kuwahamasisha wananchi kununua nyumba zinazojengwa na Shirika hivi sasa badala ya kung'ang'ania kununua nyumba za zamani ambazo zilitaifishwa na kukabidhiwa Shirika la Nyumba. Na kwa vile sababu ya kutaifisha nyumba hizo bado ni hai, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha nyumba hizo haziuzwi. Nyumba hizo ni mali na urithi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kutungwa upya kwa Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa. Kwa kuwa sheria iliyopo sasa hailisaidii shirika kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika mazingira ya sasa na pia haiendani na mpango mkakati wa Shirika ambao upo katika utekelezaji. Na pia Serikali ikamilishe rasimu ya sheria (reguraltions) ambayo haijawahi kuandikwa tokea shirika lilipoanzishwa mwaka 1962;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kulisaidia Shirika la Nyumba kuweza kumiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa gharama nafuu au kwa kupewa bure. Kwa kufanya hivyo;

- Itasaidia kupunguza gharama ya nyumba ambazo zinajengwa kwa ajili ya kuziuza kwa wananchi wa kawaida; na

- Itaisaidia Serikali, kwa kuwa Shirika la Nyumba ndiyo chombo pekee cha serikali ambacho kinaweza kutumika kwa ajili ya kutunza ardhi ya akiba kwa ajili ya kila mwananchi.

Mheshimwia Spika, Kamati inaishauri serikal kutoa msamaha wa kodi ya ardhi kwa Shirika (land rent);

### 5.4.1 MADENI YA SERIKALI NA TAASISI ZAKE KWA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Mheshimiwa Spika, katika maoni yake Kwa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba Na Maendelo ya Makazi Kwa mwaka 2013/2014, Kamati iliishauri Serikali kulipa madeni yake yote ya kodi za pango kwa Shirika la Nyumba la Taifa ili liendelee kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi yake ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha deni la shilingi 4,226,957,203.65 lililobakia linalipwa. Wizara/Taasisi na Idara zinazodaiwa ni hizi zifuatazo:-

1. Wizara ya Uchukuzi - 1,160,389,916.76
2. Wizara ya Ujenzi - 629,570,166.45
3. Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo - 558,561,735.70
4. Wizara ya Afya - 552,758,522.83
5. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa 551,808,661.82
6. Muhimbili National Hospital - 136,857,924.00
7. Jeshi la Wananchi Tanzania TPDF - 116,416,193.04
8. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - 87,248,010.19
9. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - 83,051,671.49
10. Wizara ya Elimu - 65,524,081.44

11. Wizara ya Kilimo - 63,602,582.52
12. Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania - 50,146,448.62
13. Wizara ya Fedha - 43,362,376.93
14. Tume ya Utumishi wa Umma - 37,301,618.41
15. Mkurugenzi Taasisi ya Utangazaji - 24,766,376.73
16. Deputy Attorney General Shinyanga - 10,587,702.35
17. National Environmental Management Council - 9,615,535.22
18. Msajili wa Mahakama Kuu Tanga - 9,412,463.25
19. Mkurugenzi wa Uhamiaji - 9,094,754.74
20. Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi Moshi - 7,638,844.66
21. Bodi ya Ukaguzi wa Filamu - 5,649,950.89
22. Mbeya Referal Hospital- 5,364,373.40
23. Baraza la Kiswahili la Taifa- 4,508,810.56
24. Ustawi wa Jamii Tanga - 3,939,419.10
25. Atorney General Mbeya- 2,839,515.91
26. Ofisi ya Takwimu ya Taifa- 2,557,349.10
27. Uhamiaj Singida - 1,680,000.00
28. Kamishna wa Magereza- 925,822.46
29. Ukaguzi wa Elimu Bukoba- 639,215.00

J umla shilingi - 4,226,957,203

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha deni hili linalipwa haraka iwezekanavyo kama kweli inataka Shirika la Nyumba kukamilisha azma yake ya kujenga nyumba 15,000 ifikapo mwaka 2015.

**5.5 WAKALA WA TAIFA WA UTAFITI WA NYUMBA NA VIFAA VYA UJENZI**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) ulizinduliwa rasmi mwaka 2001 na kuchukua nafasi ya kilichokuwa Kituo cha Utafiti wa Ujenzi (NHBRU). Jukumu kubwa la Wakala huu ni kufanya utafiti, kukuza, kushauri na kushawishi ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia ubunifu, ili kuinua na kuboresha viwango vya nyumba kwa gharama nafuu pamoja na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba Serikali imeitengea Wakala shilingi 500,000,000/= katika mwaka wa Fedha 2014/15 ikilinganishwa na shilingi 400,000,000/= zilizotengwa mwaka jana. Fedha hizo zitatumika kuboresha maabara na karakana za utafiti wa vifaa vya ujenzi, na kukamilisha ukarabati wa jengo la Wakala.

Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Wakala ambao una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa, iongeze tengeo la fedha kwa Wakala huyu ili kuwezesha uwakilishaji bora wa teknolojia rahisi ya nyumba bora.

**5.6 KITENGO CHA UTHAMINI WA MALI**

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha uthamini wa mali ni kitengo muhimu katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kitengo hiki ni nguzo mojawapo ya utawala na usimamizi bora wa ardhi kwa kuwezesha maamuzi ya maendeleo bora ya ardhi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kitengo hiki ndicho kinachohusika na uthamini wa mali na fidia kwa wananchi waliohamishwa katika ardhi na mali inayomilikiwa na Serikali na wamiliki binafsi, na kutokana na kuongezeka kwa ushindani wa mahitaji ya ardhi kulinganisha na ardhi iliyopo, ni vema Serikali ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukiwezesha kitengo hiki kuongezewa wataalam na vifaa ili kiweze kutimiza wajibu wake kwa umakini mkubwa kwa sababu kitengo hiki ndiyo roho ya upimaji ardhi lakini hakipewi fedha za kutosha.Kitengo kinahitaji billion 16 kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**5.7 MASUALA MENGINEYO**

- Kamati inashauri kuwa; Serikali ianzishe mchakato wa kuhamisha ajira za wapimaji ardhi katika Halmashauri zote nchini kuwa chini ya Serikali kuu; Utaratibu wa sasa umeshindwa kuwahudumia wananchi. Maafisa wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri, Manispaa na Majiji badala ya kuwahudumia wananchi wengi wamejikita katika kudai rushwa na kufanya biashara zao binafsi.

- Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi ikamilishe maandalizi ya mpango kabambe wa jiji la Dar es Salaam na Arusha.

- Kamati inaishauri Serikali iitambue sekta ya Nyumba na kuipa hadhi kama sekta kiongozi na sekta ya msingi katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu (Declare housing as a top priority).

- Serikali iangalie upya utaratibu wa makusanyo ya maduhuli ili Wizara ibaki na makusanyo yake (retention at source) kwani mara nyingi fedha zinazopelekwa HAZINA huchukua muda mrefu kurudishwa katika

Halmashauri na hivyo kukwamisha shughuli muhimu za Halmashauri zihusuzo masuala ya ardhi;

- Serikali iwekeze kwenye miundombinu katika maeneo yanayojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa ili kupunguza gharama za ujenzi na hivyo kuleta unafuu kwa wapangaji na wanunuzi wa nyumba;
- Serikali ilete Bungeni taarifa ya migogoro yote ya ardhi nchini ikiainisha aina za migogoro hiyo. Aidha Serikali ilete orodha ya watu wote wanaostahili kulipwa fidia katika mradi wa Kigamboni na kiasi kinacholipwa.

## 6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. James Daudi Lembeli, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe.Abdulkarim E.Hassan. Shah, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi Mb - Mjumbe
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mb- Mjumbe
7. Mhe. Muhamad Amour Chomboh, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Michael Lekule Laizer, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Amina Andrew Clement, Mb - Mjumbe
12. Mhe. John John Mnyika, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Salim Hassan Turky, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Abuu Hamoud Jumaa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Kisyeri Werema Chambiri, Mb - Mjumbe
16. Mhe. AL-Shaymaa Kwegyir, Mb- Mjumbe
17. Mhe. Benedict Ole Nangoro, Mb - Mjumbe
18. Mhe. MwanaKhamis Kassim Said, Mb -Mjumbe

19. Mhe. Waride Bakar Jabu, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Clara Diana Mwatuka, Mb- Mjumbe
21. Mhe. Dkt Henry Daffa Shekifu, Mb- Mjumbe
22. Mhe. Haji Khatibu Kai, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Charles Mloka, Katibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili akisaidiwa na Ndugu Lukindo Choholo, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

James Daudi Lembeli, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA
27 Mei, 2013

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPITIO YA UTEKEZAJI WA BAJETI 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWENYE WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA 2014/2015 KAMA YALIVYOSOMWA BUNGENI.**

**MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningeomba *Hansard* ichukue kumbukumbu zote kama ambavyo nimeziwasilisha kwa sababu hotuba yangu inakurasa 78 na *summary* ina kurasa 25.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni ninaomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio ya utekezaji wa bajeti 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utangulizi: Norman Brown alisema kwamba. *"I am what is mine. Personality is the original personal property"*. Hii ina maanisha kwamba msingi wa haiba, heshima au utu wa mtu uko katika rasilimali halisi anayomiliki binafsi. Hivyo mtu anayepora ardhi ambayo ndiyo rasilimali halali tunayomiliki, anachezea haiba, heshima na utu wetu na kamwe hatuwezi kumvumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni: Katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, 2012/2013, 2013/2014 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliainisha matatizo makubwa ya ardhi nyumba na maendeleo ya makazi na kuitaka Serikali kutafuta ufumbuzi kwa kuchukua hatua za haraka. Matatizo hayo yalikuwa kama ifuatavyo kwa ufupi.

(i) Uporaji wa ardhi ya Tanzania unaofanywa chini ya usimamizi wa Serikali kwa mbinu au hila ya uwekezarikaji.

(ii) Ufisadi wa ardhi unaofanywa na viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi kwa kupora ardhi ya wananchi huku Serikali ya CCM ikiangalia pasipo kuchukua hatua. Mmoja wa viongozi hao akiwa kigogo wa Chama cha Mapinduzi aliyepora ardhi ya wananchi Kijiji cha Loiborsoit A, Jimbo la Simanjiro, mhusika mkuu katika mgogoro huu ni Bwana Brown Matthew Oleseya, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, ambaye amejimilikisha kiujanja-ujanja hekta za kijiji 3,425. *(Makofi)*

(iii) Migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ambayo kwa nyakati tofauti imepelekea umwagaji wa damu miongoni mwa wananchi. Wakati migogoro hii inachochewa na uhaba wa ardhi, kuna genge la watu wachache wanahodhi maeneo makubwa ya ardhi, ambayo hayajaendelezwa huku Serikali ikiwa haina ujasiri wa kuyarejesha ili yatumike kwa manufaa ya Watanzania walio wengi.

(iv) Matatizo katika tathmini ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuondoka katika maeneo yao kupisha matumizi mapya ya ardhi ikiwemo Luguruni, Kwembe, Kurasini na *North* Mara.

(v) Kuyarejesha kwa wananchi mashamba yote yaliyobinafsishwa ambayo wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza,

(vi) Serikali kuwanyang'anya ardhi watu wote Watanzania na wageni ambao wamemilikishwa ardhi za vijiji kinyume na Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 ya mwaka 1999.

(vii) Utekelezaji wa Kauli ya Waziri Mkuu juu ya ukomo wa ardhi ya kilimo kwa wawekezaji.

(viii) Ukaguzi kufanyika kwenye majengo yote yaliyojengwa na *Radha Construction Limited* aliyehusika na ujenzi wa Indira Gandhi lililoanguka na kuua watu wasiopungua 21. Kutokana na ukweli kwamba taarifa zilizopo ni kwamba mbia amekuwa na mahusiano ya kikazi na muda mrefu na Shirika la Nyumba na kuna nyumba alizozijenga ambazo kuna wapangaji ndani yake na ziko kwenye mazingira hatarishi.
Hali kadhalika taarifa juu ya jengo pacha lililotakiwa kuvunjwa kwa maelekezo ya Waziri wa Ardhi, lakini mpaka sasa halijavunjwa, licha ya taarifa juu ya uhatarishi wake. *(Makofi)*

Taarifa za kina za ufisadi wa CCM na suala la *Radha Construction* na nyumba zilizodondoka nimeambatanisha kama kielelezo.

Mheshimiwa Spika, Uporaji wa Ardhi: Huu ni mwaka wa nne mfululizo tumekuwa tukizungumzia dhana ya uporaji wa ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inalichukulia suala la ardhi kwa upana wake kutokanana ukweli kwamba dunia tunayoishi inakabiliana na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa gharama za chakula, kuongezeka kwa idadi ya watu duniani, kuongezeka kwa mahitaji ya chakula, nishati ya mimea na malighafi na mbao.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa ni taifa la ajabu na lisiloona mbele tusipoyajadili haya kwa kina na kuchukua hatua haraka sana hasa ikizingatiwa kwamba inatarajiwa itakapofika mwaka 2050 mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa 70%, idadi ya watu diniani itaongezeka kutoka bilioni 7.2 mpaka bil 9.6, halikadhalika idadi ya Watanzania itaongezeka kutoka watu milioni 44.9 kufikia milioni 82. Na ikumbukwe kwamba kati ya mwaka 2002 - 2012, Watanzania tumeongezeka kwa 30%.

Mheshimiwa Spika, Kwa kina kabisa tulizungumzia juu ya uporaji wa ardhi wa aina mbili:- Uporaji wa ndani, huu ukiwahusisha vigogo wa Serikalini na wafanyabiashara wakubwa na Serikali kwa kutumia nafasi zao kupora mapande makubwa ya ardhi huku wananchi walio wengi wakiachwa bila hata kiwanja.

Pili, tulizungumzia juu ya uporaji wa nje unaowahusisha wageni, wanaokuja kwa jina la uwekezaji wengi wao wakiwa hawana mitaji wakitegemea kutumia ardhi yetu kukopea pesa na katika mazingira mengine kutokuweka kabisa pesa walizokopa katika ardhi husika.

Utafiti uliofanywa hivi karibuni na taasisi za kimataifa unaonyesha kwamba kuna mikataba mikubwa zaidi ya 1217 ya utoaji ardhi kwa masuala ya kilimo ambayo ni sawa na hekta milioni 83.2 imeridhiwa au iko katika mchakato wa kuridhiwa kati ya mwaka 2007 - 2012. Bara la Afrika ambalo ndilo mlengwa mkuu wa mkakati huu ni kinara likiongoza kwa  kuwa na mikataba 754 inayojumuisha eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 56.6, ikifuatiwa na Asia yenye hekta milioni 17.7, huku Bara la Amerika ya Kusini likishika nafasi ya tatu kwa kuhusisha ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni 7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watafiti wanabainisha kwamba licha ya mataifa ya nje ama makampuni ya kimataifa kulenga nchi 84 duniani, ni nchi 11 ambazo zinaongoza kwa kupokea maombi mengi zaidi ya wawekezaji. Nchi hizo ni Sudan, Ethiopia, Mozambique, Tanzania, Madagascar, Zambia and DR Congo, Philippines, Indonesia na Laos  kwa Bara la Asia.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa hapo awali, Tanzania inatajwa kuwa miongoni mwa nchi 11 duniani zinazoongoza kwa kupokea maombi mengi ya ardhi toka kwa wawekezaji, hii kwa kiwango kikubwa inachochewa na kauli za viongozi wakuu wa nchi hii, hususan Rais na Waziri Mkuu ambao wamekuwa mstari wa mbele kuitangazia dunia na makampuni ya kibeberu kuja kuwekeza katika ardhi, katika mtizamo ambao unaonyesha kwamba Tanzania kuna ardhi kubwa sana isiyo na kazi wala mwenyewe. Kwa lugha nyingine viongozi hawa wamegeuka madalali wa ardhi ya nchi hii katika nchi za ughaibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitoa tahadhari kwa Serikali, kuwa makini na mtazamo huu kwani unahatarisha amani na ustawi wa Taifa letu hasa ikizingatiwa kwamba ardhi ndiyo mtaji mkuu wa uhai na maendeleo ya Afrika na Tanzania. Tumekuwa tukijiuliza, kama Tanzania tuna kiwango kikubwa hivyo cha ardhi, kiasi cha kuitiwa watu kutoka nje kununua, kama ndiyo hivi ni kwa nini kila kukicha migogoro  imekuwa ikiota sugu na kuongezeka kwa kiwango kikubwa?

Mheshimiwa Spika, Uhalisia kuhusu Ardhi iliyopo: Sera ya Taifa ya Ardhi inaonyesha kwamba 75% ya ardhi ya Tanzania ni ngumu kuisimamia  kutokana na uwepo wa wadudu aina ya mbung'o, mvua isiyotabirika, hifadhi za taifa, mapori ya hifadhi na milima. Wakati ardhi inayofaa kwa kilimo  ni hekta milioni 48.8. Taarifa za hivi karibuni zinaonyesha kwamba kilimo kinatumia 14%  ya ardhi ambayo ni hekta milioni 12.8, mapori na misitu 62%, uwanda wa majani ni 16%,

maeneo oevu ni 7% eneo la makazi na eneo la wazi linafikia 0.16% na 0.15%. *(Makofi)*

Kwa takwimu hizi, tafsiri yake ni kwamba zaidi ya 86% ya ardhi yote inayosemekana inafaa kwa kilimo ama *arable land* haitumiki kwa shughuli za kilimo na inawezekana ni sehemu ya maeneo ambayo siyo rafiki kama ilivyoainisha hapo juu, hivyo haifai kwa kilimo au haipo.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya upya tathmini ya ardhi kwa kina ili kuliwezesha Taifa letu kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa tija na manufaa ya kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Mji wa Kigamboni: Mpango wa Ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni umekuwa ukilalamikiwa sana na kutiliwa shaka na wadau mbalimbali wakiwemo wananchi waishio eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli huo unathibitika kutokana na mvutano uliopo kati ya wananchi wakiongozwa na Mbunge wao na Waziri Mwenye dhamana ya ardhi kuhusu kukiukwa kwa sheria katika uandaaji wa mpango huo. Ni miaka saba sasa imepita wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao hali kadhalika kufanya shughuli zozote za uchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kifungo cha miaka saba na mateso makubwa kwa wananchi, Kambi ya Upinzani inataka ipate kauli ya Serikali nini kinachoendelea katika mradi huu mfu. Kwa nini Serikali inaona aibu kukiri kwamba haina uwezo wa kuendeleza mradi husika? Nini kauli ya Serikali juu ya tuhuma za ufisadi zinazohusu fidia za Kigamboni kwamba watu wawili kati ya watu 228 waliofanyiwa tathmini kuandaliwa malipo ya shilingi bilioni 22 kati ya bilioni 32 za fidia zilizotengwa kama ilivyoripotiwa na gazeti la Tanzania Daima tarehe 26 Mei, 2014. *(Makofi)*

Waziri ana maelezo gani juu ya kutuhumiwa kutoa agizo la usitishwaji wa mradi wa nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa lenye hekari 200 kwa kile kinachoelezwa shirika hilo likifanikiwa katika mradi wake kutakuwa na uwezekano wa kuvuruga mipango ya baadhi ya kujineemesha kupitia fidia zitakazolipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa Chasimba, kiwanda cha saruji, na harufu ya uwizi na ufisadi wa bilioni 69: Eneo la Chasimba lina kaya 4096, kwa wastani wa watu watano kila kaya, eneo hili lina jumla ya

watu 20,480. Kwa muda mrefu sana wananchi hawa wamekuwa wakiitwa na Serikali yao kwamba ni wavamizi.

Lakini ukweli unabaki kwamba kuna siri kubwa sana iliyojificha na namna ya kiwanda kwa kutumia viongozi wa kijiji wa kipindi hicho kiunjanja waliuza ardhi ya wananchi wakiwa ndani kisha kubadilisha mipaka, hatimaye kiwanda kupewa hati kinyemela.

Mheshimiwa Spika, Mahakama iliamua wananchi wahame, lakini pia iliagiza Serikali kwamba wajibu wake katika mgogoro huu ni kuwapatia makazi mbadala. Katika vikao na wananchi, Serikali ikiwakilishwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ambaye sasa hivi ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Mayunga, Mthamini Mkuu wa Serikali na watendaji wa Wizara, wananchi waliahidiwa kulipwa shilingi 15,000 kwa *square* mita pamoja na viwanja mbadala.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kile kilichoonekana kuna harufu ya wizi na rushwa, katika kikao kilichofanyika *bar* kikiwahusisha Waziri wa Ardhi, Diwani wa Kata ya Bunju, Mwenyekiti wa Mtaa wa Basihaya pamoja na inayoitwa kamati ya wananchi, Waziri alisema wananchi hawatalipwa shilingi 15,000/= kwa *square meter*, bali watapewa 5000 ya kifuta jasho. Dalili za wizi!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Waziri, sababu za kubadilisha ghafla kiwango cha fidia ni ukosefu wa fedha na kwamba ardhi siyo ya wananchi. Anasahau kwamba hukumu hiyo hiyo anayoisimamia iliitaka Serikali kutoa makazi mbadala. Kwa mujibu wa nyaraka ambazo Kambi ya Upinzani inazo, kwa kaya 4096 zilizofanyiwa tathmini, kwa kiwango cha shilingi 15,000/= *square meter*, fedha iliyotakiwa kulipwa ni shilingi bilioni 47.3. Hii inathibitishwa kwa barua ya tarehe 8/11/2013, yenye Kumb. Na. *CBA* 171/312/01 kutoka kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *Prof*. Anna Tibaijuka kwenda kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, yenye kichwa cha habari Mgogoro wa Ardhi baina ya Wananchi wa Mtaa wa Chasimba na kiwanda cha Saruji Wazo. Mapendekezo ya Utaratibu wa Kupata Bajeti Kulipia Fidia kuwahamisha kwenda Mabwepande.

Mheshimiwa Spika, katika barua husika, Waziri anamtaarifu Waziri Mkuu juu ya uhitaji wa shilingi bilioni 69 kwa matumizi ya kulipa fidia, kutwaa eneo la makazi mbadala, kulipanga eneo jipya kimipango miji na kupima viwanja, kuweka miundombinu ya msingi hususan barabara, maji, shule za msingi na kadhalika. Katika mchanganuo ambao umeanishwa katika jedwali ambalo sitalisoma.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Waziri kiwanda kimekubali kulipa gharama yote inayohitajika kukamilisha zoezi ilimradi Serikali ikubali kwamba, katika muda usiozidi miaka mitatu, kitatumia utaratibu wa kupunguza fedha hizo kwenye kodi itakayolipwa *TRA*. Utaratibu uliopendekezwa na Waziri ambaye ni *Professor* wa uchumi ni kwamba kiwanda kitoa *advance* ya bilioni 60 na kurejesha fedha hizo kupitia *Tax Certificate* ya shilingi bilioni 20 kwa miaka mitatu kutoka mwaka 2013 mpaka 2015.

Mheshimiwa Spika, maswali ya kujiuliza, kama Waziri ameomba kiwanda ambao ni mkopo kwa Serikali, fedha za kulipa fidia shilingi 15,000 kwa *square meter* na kutaka kuwalipa wananchi shilingi 5000 kwa *square meter*, hiyo shilingi 10,000 kwa kila *square meter* inakwenda wapi? *(Makofi)*

Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa, kaya zilizofanyiwa tathmini na hivyo kutakiwa kupewa viwanja mbadala ni Kaya 4,096, iweje viwanja ambavyo Wizara inataka kuvilipia ni viwanja 4500. Viwanja vilivyosalia 404 vya ziada ni mali ya nani? (*Makofi*)

Kama Waziri alikuwa anajua kwamba ardhi siyo ya wananchi na kwamba wananchi hawakustahili fidia zaidi ya kupewa kifuta machozi kama yeye anavyokiita, nini kilichowasababisha yeye pamoja na Mthamini Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ambaye sasa hivi ni Naibu Katibu Mkuu, pamoja na wataalam wa Wizara kuwadanganya wananchi?

Kwa nini walitumia mamia ya mamilioni kujilipa posho na kulipa taasisi ya Waziri ya *TAWLAT* milioni zaidi ya 300 kwa kisingizio cha kufanya tathimini wakati wakijua fika kwamba walikuwa wanafanya kiini macho na usanii?

Nne, ni Serikali gani inayogeuka dalali wa kusaidia mwekezaji wa nje kufukuza raia katika suala ambalo hata hukumu yake imejaa utata mkubwa?

Tano, ni Serikali gani inayokopa kwa mwekezaji kwa ahadi ya makato ya kodi ya hapo baadaye pasipo kuangalia hasara ambayo nchi inaweza kupata hasa ukizingatia kwamba mifumo na viwango vya kodi hubadilika mara kwa mara au siyo *static* na ndiyo sababu kila mwaka kuna Miswada ya fedha?

Mheshimiwa Spika, taasisi yenye mahusiano na Waziri: Katika hali ile ile ya harufu ya ufisadi kama ilivyoanishwa katika ripoti ya tathmini ya ardhi, ambayo nitasoma huko mbele, katika sakata hili, ile taasisi ambayo Waziri ana mahusiano nayo ya TAWLAT nayo imo katika mchakato huu.

Kiambatanisho K1 cha kwanza cha taarifa ya Waziri kinaonesha kwamba Waziri wa Ardhi alikishauri kiwanda kuingia mkataba na taasisi isiyo ya Kiserikali

ya TAWLAT kutoa elimu na kuendesha mazungumzo na viongozi na wananchi wa Chasimba juu ya hali halisi inayowakabili.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Waziri, katika kazi hiyo, taasisi hiyo ililipwa shilingi milioni 300 na katika mchanganuo ambao uko kwenye jedwali ambalo liko kwenye hotuba yenu niliyoanisha hapo awali, wangelipwa shilingi milioni 500 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mbunge wa Jimbo hilo husika, nikuhakikishie kwamba taasisi hiyo haikufanya kazi yoyote yakutoa elimu. Naibu Katibu Mkuu anajua jinsi alivyokuja ofisini kwangu kulia, wananchi hawawaamini, mimi ndiyo nilitoa elimu ya uraia. Na nasema kama Mbunge, kama kuna fedha zilitumika labda zilitumika kuhonga kamati ya wananchi ili wawasiliti wananchi, Diwani wa Bunju na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ambao waliwasaliti wananchi baada ya kukutana na Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fedha kutokupita Wizarani: Katika hali ya kushangaza katika barua ya 8/11/2013, Waziri anamtaarifu Mkurugenzi Mtendaji wa *TPCC* Wazo *Hill*, kwamba fedha husika zilipwe moja kwa moja kwa watoa huduma badala ya kulipwa Wizarani ama Wizara ya Fedha kutokana na vikwazo katika Sheria ya Manunuzi. Fedha ambayo italipwa Wizarani ni fedha tu inayohusiana na uratibu na siyo vinginevyo. Cha kusikitisha zaidi, hata Kamati yako ya Bunge ya Ardhi na Maliasili iko kizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu sana, kwa fedha nyingi kiasi hiki, milioni 69 ambazo ni mkopo utakaolipwa na fedha za walipa kodi, kutokupita katika utaratibu wa kawaida wa Serikali. Hiki ni kiashiria cha mchezo mchafu unaotaka kuchezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji wa haki za binadamu: Katika kile kinachoonekana kupuuza hata amri ya Mahakama ya kuitaka Serikali kuhakikisha imewapatia wananchi makazi mbadala, Waziri katika barua tajwa anamtaarifu mwekezaji kwamba wameshafanya makubaliano na benki za *CRDB*, *NBC* na *NMB* kwamba wananchi hawatalipwa mpaka wathibitike ama wazithibitishie benki kwamba wameshaondoka katika eneo lenye mgogoro na kuvunja makazi yao.

Mheshimiwa Spika, napata tabu kuelewa, ni Serikali ya aina gani ambayo inataka kuchukua hatua za kinyama namna hiyo, wakati ikijua kwamba asilimia 90 ya wananchi wa Chasimba ni wananchi wa kipato cha chini na cha kati, wengi wao hawana makazi mbadala zaidi ya makazi ambayo Serikali inataka

kuwafukuza ili kumpisha mwekezaji. Sasa unapomwambia avunje ndiyo apate pesa, huyu mwananchi anaenda kuishi wapi? Huo muda wa kujenga makazi mapya ili ahamishe makazi yake pasipo kuathiri hali yake ya kiuchumi uko wapi? *(Makazi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka TAKUKURU kufanya uchunguzi wa ushiriki wa taasisi ya *TAWLAT* katika shughuli mbalimbali zinazohusu Wizara ya Ardhi, na wasipofanya hivyo, basi italazimu kuwasilisha hoja binafsi hapa Bungeni kuhusiana na sakata hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathimini ya Wizara juu ya wamiliki wakubwa wa ardhi nchini: Tarehe 5/11/2012, Kambi ya Upinzani kupitia hoja binafsi iliyoletwa Bungeni na mimi, iliitaka Serikali kusitisha zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi mpaka hapo tathmini ya kina itakapofanyika kuweza kubaini ni kiwango gani cha ardhi kilicho mikononi mwa wawekezaji. Hoja hii mahsusi ililetwa kufuatia kukithiri kwa migogoro ya ardhi nchini iliyopelekea umwagaji damu, halikadhalika wimbi kubwa la wawekezaji kutoka nje waliokuwa wakinunua na kumilikishwa ardhi na maeneo makubwa ya ardhi nchini kwa kile kinachoitwa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Je, taarifa ya Wizara imejibu? Wizara ilitoa kazi kwa wataalam washauri wakiwemo Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, na *NGO* inayoitwa *TAWLAT*. Wakati Bunge lilitarajia Wizara ingetupa taarifa ya hali ya umiliki wa ardhi mpaka mwaka 2013, Timu ya Uchunguzi imetumia taarifa za mashamba kwa sensa iliyofanywa na *National Bureau of Statistics* kwa mwaka 2007/2008. Mashamba makubwa 964 yaliyoanishwa na sensa ya mwaka 2007/2008 yaani miaka 7 iliyopita ndiyo yaliyofanyiwa tathimini.

Mheshimiwa Spika, licha ya upungufu, taarifa ya watatifi inaonesha kwamba licha ya Watanzania kumiliki mashamba mengi kwa idadi, linapokuja suala la ukubwa wa ardhi, raia wageni ndiyo waliothibitika kuwa na ardhi kubwa. Kati ya mashamba 901 yaliyochunguzwa umiliki wake, raia wa kigeni wenye mashamba 52 tu, kwa ujumla wao wanamiliki asilimia 19.2 ya ardhi yote iliyopitiwa. Hapa bado sijajumuisha mashamba yanayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania na wageni ambayo mengi Watanzania wana hisa moja hadi kumi. Wakati huo huo makampuni ya Kitanzania, makampuni yanayomilikiwa kwa ubia wa Tanzania na wageni. Taasisi ambazo zina idadi kubwa ya mashamba, yaani 849 kwa ujumla wao wanamiliki asilimia 80 tu ya ardhi yote.

Mheshimiwa Spika, wakati Kampuni za kigeni zinamiliki shamba lenye ukubwa wa wastani wa hekari 5533, Mtanzania anamiliki wastani wa hekari 293. Watafiti wanaendelea mbele na kuonya kwamba tofauti hiyo kubwa ya umiliki siyo ya kupuuza, lazima iangaliwe kwa umakini sana.

Ikumbumkwe kwamba haya ni yale mashamba yaliyotembelewa kwa kutegemea sensa ya mashamba iliyofanyika mwaka 2007. Hali inaweza kuwa mbaya zaidi sasa hivi kufuatia wimbi kubwa la kugawa ardhi linaloendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, harufu ya ufisadi katika utafiti: Taarifa ambazo Kambi ya Upinzani imezipata, gharama ya kufanya utafiti husika uliigharimu Serikali shilingi milioni 700. Ripoti husika inataja watafiti ambao nimeanisha hapa, lakini vilevile taasisi ya mama hapa pia ipo.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa ardhi anatuhumiwa kuingilia huu mchakato, kwa kuingiza jamaa zake na taasisi ambayo ana uhusiano nao kama sehemu ya timu ya kikosi kazi cha kufanya utafiti huu. Waziri anahusishwa kwa karibu sana na taasisi ya *TAWLAT*, anatuhumiwa pia kujaza jamaa zake waliokuja kwa jina la wataalam washauri. Matokeo yake Idara ya Uchumi Chuo Kikuu ilitumika kama chambo tu, huku kiasi kikubwa cha pesa kikimrudia Waziri mwenyewe kwa mlango wa nyuma. Inasemekana ilifikia hatua wataalam wakamsusia kazi Waziri kutokana na kuwa na ujanjaujanja katika suala la fedha, hali iliyomlazimu Waziri kujifungia na wasaidizi wake kukamilisha kazi iliyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubabaishaji ulianza na utaratibu wa kukipata kikosi kazi. Matumizi ya fedha za umma yana utaratibu wake, katika hili hakuna mchakato wowote wa manunuzi uliofanyika ili kuweza kupata wataalam walioshindanishwa wenye uwezo wa kuifanya kazi husika. Ili kuondoa utata huu, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi kwa masuala yafuatayo:-

Moja, utaratibu gani ulitumika kupata kikosi kazi. Mbili, uchambuzi wa kina na kwa vielelezo juu ya mgawanyo wa shilingi milioni 700 zilizotumika, nani alipewa nini na kwa kazi gani. Tatu, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Idara ya Uchumi kitoe maelezo kupitia Kamati yako ya Ardhi na Maliasili jinsi kilivyoshiriki katika utafiti husika. Tena watoe maelezo bila uwoga uwoga, maana wakienda kutishwa tu kidogo wanabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *SAGCOT*, Kilimo Kwanza na Uporaji wa Ardhi: Mkakati huu ulibuniwa na mataifa ya Magharibi. Kama kawaida yetu hatuwezi kufikiri, kila siku nchi za Magharibi zinafikiria kwa niaba yetu, wanatupangia mipango, tukija kushituka imeshakula kwetu! Kwa kile kilichoitwa *The New Alliance for Food Security and Nutrition, w*Watarisha wakuu wakiwa ni G8, mkutano ulifanyika *Camp David USA* mwezi Mei, 2012, kisha kukabidhiwa kwa viongozi wa nchi tano teule za Afrika yaani Tanzania, Ghana, Ethiopia, Burkinafaso na Ivory Coast. Kwa Tanzania mpango huu ulipelekea kuzaliwa kwa *SAGCOT* katika

Mkutano wa Dunia wa masuala ya Uchumi- Afrika yaani *World Economic Forum – Africa)* uliofanyika mwezi Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu unataka kuanzisha kilimo cha biashara kitakachoyahusisha makampuni makubwa kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania. Jukumu la Serikali likiwa ni kuwatengenezea miundombinu ya kilimo sambamba na kutenga 1.3 ya ardhi ya kilimo kwa madhumuni hayo. Ardhi tunayoizungumzia hapa ni ile yenye rutuba, halikadhalika maeneo yenye vyanzo vya maji vya uhakika. Mpaka sasa inasemekana *TIC* imeshatambua hekta 63,000 zitakazotolewa katika mfumo wa *tender*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inataka Serikali itoe majibu ya hoja zifuatazo:-

Kwanza, ni kwa kiwango gani kutakuwa na uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa zabuni? Pili, ni vigezo vitakavyotumika kutoa zabuni na nani anayeweka hivyo vigezo? Tatu, nini nafasi ya wawekezaji wazalendo na wakulimwa wadogo wadogo katika mchakao huu?

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa mashamba makubwa hawalipi kodi: Wakati migogoro ya ardhi ikifukuta nchi nzima kutokana na uhaba wa ardhi kwa matumizi ya shughuli za kilimo na ufugaji, imebainika kwamba, wamiliki wengi wa mashamba makubwa, wamekuwa wakiikosesha Serikali mapatokwa kutolipa kodi.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa hivi karibuni kwa kutembelea mashamba 964 yenye ukubwa wa takriban ekari 3.7 umebainisha kwamba wamiliki wa mashamba 642 kati ya mashamba 964 yaliyotembelewa walishindwa kuthibitisha kama wamelipa kodi kwa katika kipindi cha mwaka 2012 na kwamba kati ya hao, wachache waliosema wamelipa kodi yaani wamiliki wa mashamba 322 zaidi ya asilimia 79 waliishindwa kutoa risiti kuthibitisha hilo, yaani walioweza kutoa risiti ni asilimia 13 tu.

Mheshimwia Spika, kodi inayopotea: Kwa idadi pekee ya mashamba yaliyotembelewa, Serikali inapoteza zaidi ya shilingi bilioni 3.7 kwa mwaka. Wamiliki wa mashamba wanatakiwa kulipa kodi kiasi cha shilingi 1000 tu kwa ekari kwa mwaka. Kwa mwaka 2012 kati ya shilingi bilioni 3.7 zilizotakiwa kulipwa kwenye mashamba, walilipa shilingi milioni 130 tu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Kambi Rasmi ya Upinzani inachelea kusema kuwa, Msimamizi Mkuu wa Sekta ya Ardhi yaani Prof. Tibaijuka ana maslahi makubwa katika ardhi, kwani katika taarifa zilizopo ni kwamba anamiliki kiasi kikubwa cha ardhi maeneo ya Kigamboni, Kagera Wilaya ya Muleba, anamiliki

eneo la hekta 800 alizozipata kiujanjaujanja tu kwa kuwahamisha wamiliki halali kwa nafasi yake ya Ukurugenzi wa *UN-Habitat* na baadaye Waziri wa Ardhi. Siyo hilo tu, inasemekana na Bukoba Mjini anamiliki ekari 100.

Mheshimiwa Spika, linapokuja suala la migogoro ya ardhi, Mheshimiwa Prof. Tibaijuka anakosa *moral authority* katika kuutafuta ufumbuzi wa haki.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia upya suala lolote la ardhi ambalo Prof. Tibaijuka atajiingiza kwani nyuma ya sakata hilo kuna maslahi binafsi yake kama hili la Chasimba na Kigamboni. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuangalia upya mipango ambayo inatarayarishwa na kusimamiwa na Wizara na jinsi gani inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaanza kuamini kile kilichoripotiwa na gazeti la *Daily Nation* la Kenya tarehe 7 Machi, 2009 kuhusiana na kushushwa cheo kwa nafasi yake ya ukurugenzi wa UN-*Habitat*. Japokuwa taarifa husika haikumhusisha moja kwa moja na kashifa ya mabilioni ya shilingi, kinachoelezwa kuwa kiini cha kushushwa kwake cheo ni kushindwa kusimamia majukumu yake kiutendaji, tatizo ambalo inaonekana linamkabili mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Mwanahistoria, Mwanasiasa na Mwanafilosofia wa Kiitaliano Machiavelli aliwahi kusema naomba kunukuu; "*so long as the great majority of men are not deprived of either property or honor, they are satisfied*". Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba kama kundi kubwa la watu halikudhulumiwa mali au utu wao, basi litakuwa limeridhika.

Mheshimiwa Spika, kwa migogoro ya ardhi ambayo Kambi ya Upinzani imekuwa ikieleza tangu Bunge la Tisa hadi sasa, wananchi wetu wataridhika vipi? Na kama ukweli ni kwamba kama hawataridhika, hatua inayofuata itakuwa ni mbaya sana, na majuto ni mjukuu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Hizo *personal attacks* kwa sababu Waziri atapata nafasi ya kujibu ndiyo maana sikumuingilia. Kwa sababu *personal attacks* kwa mujibu wa taratibu zetu haziruhusiwi.

Sasa nitawaita wachangiaji wa asubuhi hii: Kwanza kabisa nitamuita Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari R. Nundu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

Nikiwaita hivi siyo kwamba lazima muongee! Atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Bungara, na Mheshimiwa Naomi Kaihula pia yumo. Nitawaita kadri mtakavyokuwa mnaongea. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE-:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa niaba ya wanchi wa Kigamboni kupata fursa ya kwanza kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwa kutounga mkono hoja hii.

Pili, nataka kutoa pongezi kwa Kamati ya Bunge na Kambi ya Upinzani, kwa kutambua kwamba Jimbo la Kigamboni tuna tatizo kubwa la ardhi na wameweza kuisemea na kuwatetea wananchi wa Kigamboni. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masikitiko ya wananchi wa Kigamboni sasa hivi ni takribani miaka sita na kadri muda unavyokwenda sintofahamu inazidi kuongezeka. Athari kwa wananchi ni kubwa sana, hivi sasa wananchi hawezi kujenga, hawawezi kukopesheka, hawakarabati, hali ambayo inawapelekea unyonge mkubwa sana na umaskini wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hotuba hii haileti matumaini hata kidogo kwa wananchi wa Kigamboni. Hotuba hii imeleta mkanganyiko mkubwa sana. Kwa mujibu wa sheria, kwa sababu zoezi hili liko kwa mujibu wa sheria na sheria ambayo inatawala ni sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007. Wao wenyewe, kwa mujibu wa maelezo yao, ni kwamba, hamuwezi mkaanza mchakato wa mradi wowote pasipo kufanya *public hearing*.

Lakini kwa masikitiko makubwa, Wizara imekuwa inakiuka na sasa hivi imefanya mazoezi ya kufanya tathimini na kuanza kupima baadhi ya maeneo bila kufuata taratibu na kifungu namba 19(c) kinaeleza wazi kabisa kwamba lazima *public hearing* ifanyike, wananchi waukubali au kukataa kabla utekelezaji haujaanza, hivyo kinachofanyika pale Kigamboni ni kinyume kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba wako katika mkakati wa kujenga nyumba za wananchi wa Kigamboni, lakini katika kikao tulichokifanya Desemba mwaka jana na Mheshimiwa Waziri alikuwepo, wananchi wa Vugumba walikataa, walikataa kujengewa nyumba. Sasa huu mradi ambao unaendelea wa kujenga nyumba Wizara inapata *authority* kutoka wapi, wakati wale wadau wenyewe walikataa?

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, wananchi wa Kigamboni, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaongelea suala la hisa. Suala la hisa hatujawahi kukaa na kujadili, hatujawahi kushirikishwa, hatujawahi kuulizwa, Kamati haijawahi kushirikishwa. Sasa mnaposema mnataka kuja kutukata 10% ya fedha zetu, sisi Wandegeleko, Wazaramo, tunapokubaliana tunataka chetu tusepe! Sasa hii 10% inatoka wapi? Suala la hisa ni suala la hiari, suala la hisa siyo suala la lazima. Hili naomba niseme kabisa kwamba hili hatukubaliani nalo. *(Makofi)*!

Mheshimiwa Spika, Serikali inaingia gharama kubwa, wameweka mtaalam mwelekezi, wamemlipa milioni 500 mpaka sasa hivi na lengo ni kumlipa bilioni mbili. Hii ni upotevu wa fedha za Serikali, kwa sababu jambo hili halina ridhaa ya kwetu sisi na sisi hatujaweza kukubaliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Kamati ya Bunge pamoja Kambi Rasmi za Upinzani wamesaidia kutoa suruhisho. Kama Wizara wangekuwa wanatusikiliza, kama Wizara ingekuwa inamsikiliza Mbunge wa Kigamboni, kama Wizara ingekuwa na ushirikiano na Kigamboni, mradi wa Kigamboni siyo mradi mgumu sana, lakini imekuwa na sintofahamu, mambo yanafanyika kwa usiri, ubabe unafanyika, kuna ujanjaujanja mwingi ambayo na sisi yanatupa mashaka makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni haya mapendekezo ambayo tumeyatoa hapa, na mimi naomba sana Serikali wajaribu sana kuyazingatia. Tukifuata haya maelekezo ambayo Kamati ya Bunge imeshauri, tutapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, kuna Kata tatu ambazo zimechukuliwa katika Jimbo letu la Kingamboni. Walipokuja pale awali kuomba zile Kata sita za awali, walikuja kutuomba ridhaa. Mamlaka ya Manispaa ya Temeke iko kisheria, ina mamlaka yake na mipaka yake, lakini sasa hivi mapema mwaka jana Kata hizi zimechuliwa bila ridhaa yetu. Tunaomba hizo Kata zirudishwe katika Manispaa ya Temeke, kwa sababu ni asilimia 75 ya Manispaa ya Temeke, inatuathiri sisi kama Manispaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilikuwa nataka kuomba, kwa sababu tumekuwa na migogoro mingi ya ardhi, na imekuwa inaongezeka kadri siku zinavyokwenda. Kigamboni, tumesikia Chasimba na maeneo mengi mkoani Dar es Salaam, Makongo, kila mahali. Mimi nilikuwa naomba nitoe hoja kwamba iundwe Kamati Teule ya Bunge ifanye kazi ya kuhakiki maeneo haya ili tuweze kufika…

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Siyo utaratibu, wewe unachangia, sasa unachangiaje na kutoa hoja wakati uleule! Anatoa taarifa, lakini siyo hoja, siyo utaratibu. Naomba uendelee na kuchangia, hiyo ni *alarm*, tu siyo hoja.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE-:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa ushauri wako, lakini mchana wakati tutakapokuwa tunasimamia masuala la vifungu, nina mpango wa kutoa hoja hiyo hapo mchana kama hatutakuwa tumepata majibu mazuri kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kengele ya pili inililie, lakini kwa kweli wananchi wa Kigamboni tuna masikitiko makubwa jinsi mchakato huu..., na mimi niseme, hatuna tatizo na mradi huu, lakini tuna tatizo kubwa na jinsi gani mradi huu unavyoanywa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu, mwaka jana wakati tunafanya hitimisho, nilitoa shilingi. Nilitoa shilingi, wewe ukaniomba kwamba Ndugulile rudisha shilingi, mkakae na Waziri, Waziri amekaidi agizo lako na nilikuja ofisini kwako kukueleza hili, siyo mara moja, siyo mara mbili, nilikuandikia barua, lakini Mheshimiwa Waziri anakaidi agizo lako. Sasa na mimi naomba sana mtusaidie, sisi ni Wabunge ambao tunapaswa kuisimamia Serikali, sasa inapokuwa kuna mtu ambaye anakaidi hata agizo la Spika, na sisi tunapata mashaka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, na mimi nilikuwa naomba sana tupate msaada wako ili sasa Bunge lako lichukue hatua ya kuisimamia vizuri Serikali hususan katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba kutoa...

**SPIKA:** Ahsante. Anayefuatia, nilisema Mheshimiwa Mariam Mfaki, yupo? Ee Mheshimiwa Mariam Mfaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani-.

**MHE. MARIAM S. MFAKI-:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimikwa Spika, kwa mara ya kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wa Ta'alla* kwa kutuwezesha sisi sote uzima na kuwepo katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake nzuri anazofanya. Kitabu chake kinaeleza, ingawaje ni kweli kazi zake hazionekani, lakini anajitahidi pamoja na watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dakika ni chache, nitaendelea kusema yale ambayo nilikuwa naona kwamba ni muhimu niyaseme. La kwanza, ni kuhusu upimaji wa viwanja. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 11, unaonesha kwamba kazi ya Wizira hii na kazi ambayo wameiweka mbele kabisa ni kupima viwanja katika eneo lote la nchi hii. Ni kazi nzuri na naamini kazi hiyo ikifanikiwa itapunguza sana migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nije kwa Mkoa wetu wa Dodoma, sisi Dodoma tunayo Mamlaka ya *CDA* ambayo inajitahidi sana toka imeanza kupima viwanja. Mpaka sasa hivi Dodoma nina uhakika wanaohitaji viwanja, vipo, na nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa *CDA* leo asubuhi, kasema vipo.

Mheshimiwa Spika, kubwa kwa kweli katika viwanja hivi ni suala la bei. Kiwanja cha chini kabisa, bei yake ni milioni tatu, wananchi wetu uwezo wao ni mdogo! Hawawezi kununua viwanja hivyo, vinginevyo wataishia katika kupanga. Sasa mimi niiombe Serikali, na naomba itoe jibu, kwamba mpaka sasa hivi, tunaomba, badala ya kuwapa fidia, wale ambao wanakutwa katika maeneo yao na kupimwa viwanja, naomba basi badala ya kuwapa fidia wajengewe nyumba! Tusiwe na watu ambao katika maisha yao wataishia kupanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hilo naomba nipate majibu, kwa nini wasipimiwe viwanja na kama fidia ni kubwa basi kitakachobaki wapewe fidia kwa wale ambao watahitaji utaratibu huo. Kwa hiyo, hilo naomba sana nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la viwanja katika Wilaya mpya. Sisi Dodoma tunayo Wilaya ya Chemba, tunaomba basi tupate majibu kwamba je, Wilaya hizo zimewekewa utaratibu wa kupimwa na kama zimepimwa ramani zake zimetoka, na kama bado, lini ramani za Wilaya hizo zitatoka, ili kuzuia ujezi holela? Vingenevyo tutakuja anza tena kuhamishahamisha watu na kuwasumbua katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba nizungumzie ni juu ya gharama za kubadilisha jina, ni gharama kubwa sana. Sasa kwa wale ambao kwa kweli uwezo wao ni mdogo na wanazo nyumba, ni kweli kabisa, ndiyo maana wengi wamechelewa katika kubadilisha majina, ni kwa sababu ya gharama. Tuiombe Serikali basi, katika gharama hizo, hebu zihuishwe, zipunguzwe, ili wananchi wote waweze kupata uwezekano wa kubadilisha viwanja.

Mheshimiwa Spika, na wakati mwingine kiwanja kimenunuliwa labda na zaidi ya watu wawili/watatu, sasa wale wa kwanza hawalipishwi gharama za kubadilisha na wala hawajaenda kubadilisha. Sasa matokeo wewe uliyenunua

wa tatu au wa pili, inabidi ulipe gharama na zile za yule aliyenunua wa kwanza, na wa pili na wewe unayetaka kiwanja hicho ukibadili ili kiwe na jina lako.

Mheshimiwa Spika, tuiombe Serikali iangalie hilo, iweze kupunguza gharama hizo na ikiwezekana wale waliotangulia kununua, waweze kulipia gharama hizo, na pengine vinginevyo huyu ambaye anakilipia kwa mara ya tatu atapata gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimefurahishwa na suala la kwamba watumishi wa Serikali na mamlaka nyingine watajengewa nyumba, hilo ni jambo zuri, na ikiwezekana basi katika ajira mpya zitakazotoka kwa watumishi wa vitengo mbalimbali na Wizara mbalimbali na idara mbalimbali, basi katika kazi ambayo ni ya kwanza, atashauriwa ni kukubali kujengewa nyumba, ili aweze kukatwa mshahara kuanzia pale anapoanza kazi mpaka atakapokuja kumaliza atakuwa tayari ana nyumba yake. Hili ni jambo zuri sana, na ninaomba Serikali iharakishe jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba vilevile, hii Benki ya Mkopo ya Nyumba, wengi wanahitaji, lakini sasa iko Dar es Salaam peke yake. Ni kwa nini benki hizi zisiwe na matawi katika mikoa ili iweze kuharakisha au kuwarahisishia kwa wale ambao wanahitaji mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa suala la Kigamboni naomba kwa kweli Serikali iseme tu ule ukweli, iko tayari kujenga hizo nyumba Kigamboni? Kwa sababu sasa ni maneno haya mengi, wananchi walio na viwanja, walio na majengo Kigamoboni wanakata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, naomba tu nitoe elimu ya bure, kwa sisi sote Wabunge. Nilikuwa naomba hivi, kwamba Waheshimiwa Wabunge, tujitambue kwamba sisi ni Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tujitambue vilevile, wakati tunatoa kauli zetu, kwa wale wanaotoa kauli nzuri mimi nawapongeza, lakini kwa wale ambao wana mazoea ya kutoa kauli chafu, wajue kwamba, wananchi wao watawapima mwaka 2015 kwa jinsi ya kauli zao ndani ya Bunge. Hawatamchagua mtu kwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imegonga, ingawa ulikuwa unanisaidia mimi kusema kauli chafu hazisaidii. *(Kicheko)*

Haya, Wahehsimiwa tunaendelea, nilisema nitamuita Mheshimiwa Stephen Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa…

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI-:** Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kusema kwamba siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kama Kamati ilivyoamua, na mimi niseme hivyo kwamba siungi mkono hoja. Kwa sababu gani? Nimeona mambo mengi yameongelewa sana Kigamboni hasa Mkoa wa Dar es Salaam, lakini nataka nirudi na mimi upande wa Mkoa wa Tanga, zaidi katika jimbo langu la uchaguzi la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, toka nimekuja Bunge hili lako tukufu, mimi nimelalamikia mashamba ya mkonge, mashamba ya chai, mashamba ya katani, mashamba ya sufi, mpaka leo hii sijapata jibu lolote. Mheshimiwa Waziri anakuja mpaka Tanga, anafika mpaka Muheza, lakini katika Tanzania, Wilaya ambayo inaongoza kwa kuwa na mashamba makubwa sana, ni Wilaya ya Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini kila ninapokuja katika Bunge lako tukufu, nikiomba kwamba wakaangalie wananchi wangu wa Korogwe Vijijini, watalima wapi, lakini inaonekana kama napiga kelele hewani tu, hakuna mtu yeyote anayenisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii kuna shamba la mkonge la kwa Shemshi, wananchi wanajitahidi wanakwenda kwenye mapori ambapo wanavunja msitu wanalima. Wakishakumaliza kulima, wakianza kupanda mahindi, mtu analeta mkonge anapanda, hii ni kunyanyasa wananchi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupima viwanja, kuna sehemu kama Mombo, Mombo ni mji mkubwa unaoendelea, lakini haujapimwa, na ukianza kupimwa ni vurugu, watu hawalipwi haki zao! Leo hii nashangaa kuambiwa kwamba kuna watu wanalipwa, wanalipwa wapi! Kama kweli Serikali ina huruma, kama kweli Serikali inataka maendeleo kwa wananchi wao, hao wananchi wa Korogwe Vijijini wametengwa kwa sababu gani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli hakuna ukabila, Serikali ni moja na watu wote wanatakiwa tugawe usawa wote. Lakini kinachoniuma zaidi, kuna shamba ambalo lilishatolewa enzi hizo na Waziri wa Kilimo, Keenja. Wananchi wa Hale, Mwakinyumbi na CHAVDA lilisemwa litolewe kwa wananchi, lakini kila wananchi wanapokwenda kuingia kwenye shamba lile wanakuja wanavamiwa, wanasukumwa, na kibaya zaidi ni kwamba wanatishiwa na askari.

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii usawa uko wapi mimi nije niunge mkono hoja hii? Sitaunga mkono, na hata jioni ukiniruhusu nitatoa shilingi yangu, mpaka Serikali iende Korogwe ikaone. Nina mashamba 18 katika Tanzania, ndiyo Wilaya pekee ambayo ina mashamba mengi ambayo wananchi wanakaa bila kulima maeneo, sasa leo ninakuja naunga mkono lipi!

Mwaka 2012, nimekuja kwenye Bunge lako, nimekwambia Magoma, Mashewa, nimekwambia Kerenge, Makuyuni, nimekwambia Hale, nimesema mpaka mashamba ya misufi. Serikali inajipanga, tumeambiwa hati ziko kwa Rais, hizo hati zilizoko kwa Rais, kuna miiba huko kwamba hazitoki? *(Makofi)*

Kama hati za mashamba ambayo hayaendelezwi, leo hii ziko kwa Rais, miaka, kila siku hati ziko kwa Rais. Rais huyu mpenda watu, hizo hati haziwekzi kwenda kutoka, kwani kuna miiba?

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali ni wasikivu, hasa Wizara hii, maana Wizara hii ndiyo yenye shida. Kwenye upande wa nyumba bwana Mchechu, hana matatizo yule kijana anachapa kazi kweli kweli, kwanza nampongeza sana yule bwana, Mkurugenzi wa Nyumba, nampongeza mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye upande wa ardhi, Serikali imechemsha. Nataka mniambie leo, kwamba yale mashamba ambayo hayaendelezwi katika Jimbo la Korogwe Vijijini, ambayo wananchi wangu wameomba mpaka Bonde la Mto Mkomazi, kwamba basi kama mashamba hamtaki kuyagawa, eneo la Bonde la Mto Mkomazi ligawiwe kwa wananchi, litengenezwe bwawa ili wananchi walime, pia imeshindikana.

Leo ninakuja hapa naunga mkono, namuungia nani mkono? Itakuwa kila siku sisi ni watu wa kuunga mkono, bajeti zikipita, Wabunge hatuonekani. Wabunge wote tulioko hapa ndani ni Wabunge tu, tumeofautiana kwa vyeo, lakini lazima tuangalie mazingira tunakotoka!

Mheshimiwa Spika, sisi wengine tunakwenda kuhukumiwa, kila siku nikirudi kwenye jimbo, wananchi wananiuliza, wewe tumekutuma kule, au unakwenda kulala usingizi, kwamba Mkoa wa Tanga ni Mkoa wenye mashamba makubwa ya mkonge, Mkoa wa Tanga ni wenye mashamba makubwa ya mawese, lakini mbona ardhi yake haigawiwi, kuna tatizo gani hapa, au nyinyi Wabunge wa Tanga mmenunuliwa?

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, sitaki kuongea mengi sana, ila nataka aniambie Mheshimiwa Waziri, kwani kuna ubaguzi wa ardhi? Kwani kuna ubaguzi wa Mikoa? Kama hakuna ubaguzi wa Mikoa, mbona Tanga walikuja, lakini Korogwe hawakuja kugawa ardhi, hiyo ardhi ya Korogwe iko Kenya?!

Kama iko Tanzania, ni sababu gani zinazuia Korogwe isijewiwa ardhi ile ambayo haiendelezwi? Siungi mkono hoja, naomba nikatishie hapo. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi kwanza ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, kwa hiyo naunga mkono yale tuliyozungumza kwenye Kamati, ni kweli -kabisa bado tuna kizungumkuti. Lakini vile vile, niko kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa hiyo naunga mkono na yale.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kuongezea hapa ni kwamba migogoro ya ardhi na migogoro au upunjwaji, kutolipwa watumishi, yaani wale Wenyeviti wanaofanyakazi kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya nchi nzima, wanafanya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu, na wanapomaliza mkataba wao wanatakiwa walipwe kiinua mgongo, *gratuity* na kusafirisha mizigo yao. Lakini kuna migogoro mikubwa watu hawalipwi, kuna nini? Hebu walipeni hawa watu haki zao, tatizo liko wapi? Au mnataka wale mnaowateua wanapokuwa katika hii migogoro ya ardhi waone wenzao hawajalipwa wao wawe kazi yao iwe ni kupokea rushwa tu wajilipe kabisa kwa sababu Serikali hamuwalipi? Hebu fumbueni matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ninataka kuzungumzia kuhusu waliokuwa wafanyakazi wa mikonge pale Morogoro Mjini, Manispaa. Lile shamba pale jirani kabisa, pale Kata ya Nanenane nilipokwenda pale wakati wa kampeni watu wamelalamika, wanasema wanataka kuwaondoa pale, wengine hawajui, waliachwa pale na marehemu baba zao, babu zao, hawajui waende wapi, lakini ardhi ile inataka kuchukuliwa na Manispaa, wao hawapewi hata nukta ya kipande. Hivi tatizo liko wapi? Kwa nini watu wale msiwaangalie na wao wapewe angalau wapimiwe maeneo, wamiliki maeneo yale na eneo kubwa litabaki, kama mikonge na Manispaa itapata haki? Kwa hiyo mimi naomba mliangalie kwa jicho la karibu.

Mheshimiwa Spika, lakini ukichukulia Mkoa wa Morogoro, kama kuna migogoro ya ardhi nchi hii, kuna mauaji, kuna manyanyaso, ndani ya Mkoa wa Morogoro. Kinachotuponza ni ardhi nzuri yenye rutuba na hali ya hewa ambayo mwaka mzima inavutia. Sasa tumekosa nini?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii sasa ichukue hatua, katika kupata pesa zao za kupima ardhi na kushughulikia migogoro ijikite, kipaumbele iwekwe Mkoa wa Morogoro. Hivi leo ukienda Mkoa wa Morogoro, kuna Wilaya gani ambayo haina mgogoro wa ardhi, hakuna! Kila kona kuna kilio, vifo, ninii. Nenda Wilaya ya Kilombero, kule ndiyo balaa, Bonde Oevu, *Selous*, Chepechepe, huku ukija Udzungwa, huku ukija sijui Mbuga za Mikumi, huku ukija

Jeshi JKT. Leo kuna mgogoro mkubwa wa ardhi kati ya JKT Chita na wananchi wa Kata ya Chita.

Mheshimiwa Spika, hebu naomba mwende kule mkatatue ile migogoro, tatizo liko wapi? Watu wanapigwa, wananyanyaswa kwa sababu ya ardhi yao. Eti wanakwenda wanabadilisha mipaka wanavyotaka wao. Tatizo liko wapi? Hapo Ifakara Mjini wanasema sasa wanaongeza unakuwa Mji Mdogo. Ukienda kule Katindiuka watu walikuwa wanalima mashamba yao, kilimo cha pamba tulilima wakati wa Mwalimu Nyerere, leo ardhi ile watu wanalima mahindi wanalima mpunga wanachukuliwa bila kulipwa fidia, ni ubabaishaji wa hali ya juu, tatizo liko wapi?

Hebu nendeni huko, muunde *task force,* nendeni mkatatue migogoro hiyo, wananchi wabaki na amani katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo migogoro na *Selous* huku ndiyo usipime, tumewapokea Wasukuma na makabila mengine, lakini nendeni mkapime basi ardhi, mtenge ya wafugaji, mtenge ya wakulima, mtenge ya maendeleo, kilimo cha miwa. Shida kubwa shamba la mpira pale Mang'ula, hebu nendeni mkaliangalie.

Leo watu wananyanyaswa pale, shamba la mpira, watu wananyanyaswa, naawambia muende kule, hapo Mang'ula, Serikali nendeni pale haraka. Wanasema wanataka kufufua *General Tyre*, lakini pale kuna mgogoro mkubwa, mpira ule unavunwa hauna mwenyewe, shamba la bibi, lakini wananyanyaswa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuna migogoro mingi. Wilaya ya Ulanga kuna migogoro, kila Wilaya, Mkoa wa Morogoro kuna migogoro. Dada yangu Celina Kombani pale yupo. *Mbanduisoboka*, kuna kazi kubwa kweli ndani ya Wilaya zetu. Naomba sasa nendeni mkatatue hiyo migogoro haraka. Kama hamna uwezo basi mshirikiane na Halmashauri waone ni namna gani mtashirikiana katika kutatua hiyo migogoro ili wananchi walime kwa raha.

Mnasema *SAGCOT*, *SAGCOT* gani eneo ambalo lina migogoro lukuki? Mnasema wawekezaji, wawekezaji hawa wanakuja wanapora ardhi ya wananchi, sisi wenyewe tunabaki na *kibabali* tunaita, ekari moja moja. Tutaendelea vipi? Tutasomeshaje watoto? Hebu mtusaidie. Sisi ni wakulima, tunategemea ardhi, leo ardhi haimilikishwi.

Mheshimiwa Spika, ukienda Wilaya ya Kilombero au Kilosa, unakwenda mahakamani yaani bila aibu unaambiwa, ukitaka kumdhamini huyu lete hati ya nyumba, mlishawahi kupima kule mkatupa hati za nyumba? Nendeni mkapime

hati za nyumba, sheria za Mahakama zinasema mnataka hati imdhamini mtu, lakini ninyi hampimi ardhi, hamtoi hati. Tunanyima watu kudhaminiwa.

Mimi sisemi sana, lakini Waziri lazima ujipime. Kigamboni tulijifunza kule Singapore, Shirika la Nyumba wametupeleka kule kama Kamati kwenda kujifunza. Nasema hivi, nendeni mkaweke miundombinu, nendeni mkachore majengo yenu mnataka yaweje, mshirikishe Shirika la Nyumba, na wale wananchi wapate wawekezaji, kama wanataka ubia haya, kama wanataka kuuza haya, kila mtu afunge chake afe nacho, au vipi? Kwa nini unamlazimisha mtu mpaka hivi hivi, mtu kama anataka kufa nacho? Kama alikuwa anaishi Kigamboni leo anataka kuhamia Morogoro unamkataza wa nini? Unamwambia lazima abaki kigamboni? Kuna uhalali gani wa kumlazimisha mtu abaki mahali? Kwa nini mtu asichague mahali gani pa kuishi wakati Tanzania ni moja. Labda mtu anataka kwenda Zanzibar. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA.** Ahsante. Wale wote walioomba kuchangia Wizara hii watapata nafasi, kwa hiyo msilete tena vibarua, mtapata nafasi. Kwa hiyo anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Nundu. Utaratibu wetu unaruhusu, yaani wote wameorodheshwa hapa.

**MHE. NYAMBALI C. M. NYANGWINE**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami kwa mara ya kwanza nasema kwamba sitaunga mkono hoja hii kwa sababu kubwa zifuatazo:- Kwanza, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, Jambo la kwanza ni kwamba tunajua kabisa kwamba ardhi ni rasilimali ya taifa katika nchi yetu ya Tanzania na ndiyo inayoweza kumkomboa mtu maskini; ni kwa nini isiwekwe katika mpango wa matokeo makubwa sasa, swali la kwanza hilo. *(Makofi)*

La pili, Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nilisisitiza umuhimu wa kuweka hati za kimila katika Wilaya ya Tarime, kwa sababu kuna mambo mengi yanatokea, wananchi wanagombania ardhi na ulitoa ahadi kwamba unaanza kutekeleza.

Halmashauri ya Tarime inakusanya hela nyingi sana kama maduhuli na ina-*supply* hela nyingi sana katika Wizara yako ya Ardhi, hilo nafikiri Mheshimiwa unafahamu, ni kwa nini, ina watumishi wachache na halikadhalika bado hizo hati za kimila hazijatekelezwa kule.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naomba kuongelea jambo kubwa moja, suala la ulipaji wa fidia katika mgodi wa dhahabu wa *North* Mara maaruku kama Nyamongo. Wizara ilituma *task force* kufanya tathmini katika Kata za Kemambo, Matongo, Kibasuka, katika Kijiji cha Nyakunguru, na wakaenda wakafanya tathmini, yapata mwaka mmoja na nusu wananchi wa pale

hawafanyi kazi yoyote, hawalimi, na hata kuyaendeleza majengo katika sehemu ile wamesimama kimya hafanyi chochote kile.

Ukienda kwa mwekezaji anasema kwamba yeye hahusiki, yeye kinachomhusu ni madini tu, akishachukua dhahabu basi, anayetakiwa alipe ni Wizara ya Ardhi. Naomba nifahamu, ni kwa nini Wizara ilituma watu wakaenda wakafanya tathmini na mpka sasa hivi hawajawahi kuwalipa hata shilingi moja wale watu wa Kemambo, Matongo na Nyakunguru.

Hilo naomba nilipate kwa sababu kama sitapata hilo, hatua ambayo nitaichukua ni kali sana, yule mwekezaji tutamwondoa. Na mimi nasema ukweli, kama tatizo ni mwekezaji aondoke. Mwekezaji alipe, kama hatalipa, aondoke. Mengine sitaki kuyasema lakini hatua ambazo tutachukua ni kali sana kwa kweli. Hilo nalisema hadharani na watu wote walisikie na walifuate. *(Kicheko)*

Jambo lingine ambalo ni la muhimu sana, kuna migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Tarime. Kuna watu wamechukua maeneo, nilileta ushahidi hapa, eneo la Ghibaso katika Kijiji cha Mulito na Ghibaso, eneo la Nyandoto na maeneo ya wazi. Kama Wizara haitasaidia Halmashauri kurudisha maeneo yale sisi tutaamua, maana hata tukiamua kubomoa tutabomoa kwa sababu tutahakikisha kwamba maeneo hayo yanakuwa chini ya Halmashauri au yanarudi kwa wananchi ambao ni maskini. Mimi nitakuwa tayari kuwatetea maskini, wala si tayari kuwatetea matajiri ambao wanaweka pingamizi mahakamani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba usadie hilo.

Naomba, katika hili Mheshimiwa Waziri uniambie ni nani mwenye wajibu wa kulipa, ni TAMISEMI au ni Nishati na Madini au ni Wizara ya Ardhi? Kwa sababu, mtu anapofanyiwa tathmini anakaa anasubiri, akienda TAMISEMI wanasema kwamba tunasubiri mwekezaji atafanya au Nishati na Madini watalipa. Tukienda kuwaona wale wanasema kwamba mumuone mama Tibaijuka ndiye anayehusika na kila kitu, ndiye anayehusika na malipo. Sasa mama, wale Wakurya wa Tarime walishakuja mpaka kwako, na nasikia kwamba uliwapokea vizuri ukawapikia. Lakini wananiambia kwamba shida yao siyo kula ugali, shida yao ni kwamba wapate malipo halali. Sasa hayo malipo halali yatapatikana lini? Kwa kweli naomba kwa hilo Mheshimiwa Waziri ulizingatie sana, maana mimi nasema siyo kwamba natishia, lakini hatua ambazo nitazichukua kwa kweli zitakuwa ni maangamizi makubwa mno, na sitaki maangamizi hayo yafike huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine, jirani yangu, rafiki yangu hapa Brandes ameniambia kwamba nimuulizie kuhusu mgogoro uliopo kati ya *Ranch* ya Kitengule iliyoko Karagwe, Vijiji saba havina malisho, na walishaambiwa

kwamba wapewe. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri ufike eneo hilo umsaidie mtani wangu kuondokana na tatizo hilo.

Lingine, Mheshimiwa Waziri, unajua kupanga ni kuchagua. Mimi naamini kwamba maeneo haya ya ardhi ya Tanzania tukiipima, kila mmoja atajua anamiliki eneo kiasi gani, tutaondokana na umaskini. Ndiyo maana siku moja niliwaambia wale watu wa Tume ya Mipango, kila siku mnasema kwamba uchumi wa Tanzania unakua kwa asilimia saba, lakini ukienda kwa Watanzania huko vijijini ni masikini sana, ni kwa nini, tatizo ni moja kwamba, sisi tunategemea kilimo, mkulima hajawezeshwa, mkulima hajapimiwa ardhi yake, ananyang'anywa na matajiri. Hiyo inaelekea kabisa kwamba tutendelea kupiga kelele, lakini tutaendelea kuwa maskini, maskini, maskini na uchumi utakua kwa watu wachache, lakini watu vijijini wataendelea kuwa maskini wa kutupwa. Ukimpimia mkulima ardhi yake atapata dhamana ya kwenda hata kukopa pesa benki na ataweza kuendeleza na atapata rasilimali ambayo atakuwa anajivunia.

Sasa hivi ardhi ya Watanzania iko rehani, mtu mmoja anakuja tu na hela zake, na *briefcase* yake, anaenda anapimiwa, tena ataoneshwa kwamba mpaka kulee! Unaenda unatembea mpaka unachoka. Unatoa milioni moja, mkulima anaanza kufurahi, anafurahi, anafurahi, baada ya siku mbili hiyo milioni moja ikiisha inabaki ni majuto.

Mheshimiwa Spika, mapigano yataendelea miaka na miaka endapo hatutapima ardhi ya Tanzania. Mimi naomba…, Mheshimiwa Ntukamazina ananiambia kwamba ndiyo maana wahamiaji haramu kutoka Rwanda na Burundi wanafika kule Ngara na wanaishi, wanachukua ardhi, kwa sababu haijapimwa. Ni kwa nini tusiamue, kuanzia leo kwamba kipaumbele kikubwa katika Wizara hii ni kupima ardhi. Hiyo itasaidia sana kuondokana na matatizo ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudia kusisitiza kwamba ardhi ya Tarime naomba ipimwe. Ardhi ya Tarime naomba ipimwe. Fidia kwenye ule mgodi wa dhahabu *North* Mara, naomba wale wananchi wote waliofanyiwa tathmini; wengine wanaita tegesha, aliyetegesha ni mzungu aliyekwenda kuwekeza kule, maana ndiye amewakuta wananchi wako pale akaedna kutegesha. Kwa hiyo naomba kabisa, kuanzia leo nipate jibu sahihi na jibu kamili. Na kwa kweli kama majibu hayatakuwa kamili, hatuwezi…

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili. Nilisema Mheshimiwa Omari Nundu atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali.

**MHE. OMARI R. NUNDU-:** Mheshimia Spika, ahsante, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi kuchangia kwenye suala hili zito, ardhi ya nchi.

Mwanzo kabisa nimeona kuwa mwaka wa jana Wizara hii ilitengewa bilioni 108, na mpaka mwezi Aprili tumeelezwa ni asilimia 44.25 tu ya pesa hizo ndizo zimepatikana. Lakini sasa mwaka unaokuja inatengewa bilioni 88.9 ambayo ni asilimia 82, hiyo inanitia wasi wasi kweli. Kama kazi ya mwaka uliopita haikupata pesa za kumaliza, lakini mwaka unaokuja nao tunapata pesa chache. Mheshimiwa Waziri atueleze, majukumu mengi makubwa ambayo ameyaainisha hapa yatatekelezeka vipi wakati tunataka yatekelezeke kwa wakati.

Lakini katika majukumu hayo, kwa mfano suala la mipango miji sikuona Tanga ikatajwa, kuwa Jiji la Tanga nalo litapangwa. Sasa Jiji la Tanga ni Wilaya nzima ya Tanga ambayo ni sehemu kubwa sana, na sasa hivi kuna kitu kinaendelea kinaitwa maboresho. Neno maboresho ni neno zuri, lakini mimi sasa hivi ninalichukia. Nimepita sehemu ambazo maboresho hayo yanafanywa, hasa ukiangalia sehemu kama Masiwanishamba, Usagara, kinachofanyika kule, mtu ambaye amejenga kijumba chake katika sehemu ndogo inapimwa hiyo hiyo anapatiwa hati sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, mji unavurugwa, mji wa Tanga ambao ulipaNgika vizuri tangu zamani barabara zimenyooka, zimekaa vizuri nilitegemea maboresho yangeweza kuuendeleza mji uwe mzuri, mji unavurugwa. Na kinachonisikitisha ni kuwa uvurugaji huo unaletwa Wizarani halafu unathibitishwa. Ni afhadhali mngewaacha wakaishi katika sehemu zile zile tu walizokuwa wakiishi kuliko kufanya hivi. Nimesema Wilaya nzima uya Tanga ina sehemu kubwa, kuna sehemu nyingi ambazo zingeweza kufanyiwa kazi zikapatikana sehemu za watu wale kupangiwa mji vizuri ili waende huko. Waapangiwe *townships* ambazo zina vituo vya mabasi, zina sehemu za watoto kucheza, lakini hilo halitokei.

Mheshimiwa Spika, amesema ndugu yangu Ngonyani hapa, Tanga mjini kuna mashamba mengi ya mkonge ambayo sasa hivi yako ndani ya Jiji la Tanga, na waliomiliki mashamba hayo mpaka leo hawajayatumia. Nilitegemea kuwa mashamba hayo yatarudishwa upesi hasa katika hii dhana mpya ya kusema Wilaya nzima ya Tanga ni Jiji.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria ya kulinda mazingira, na Tanga ina Mwambao kama ilivyo Tanzania nyingine, na ekari 60 zile tangu zamani tuliambiwa watu wasijenge, kwa bahati nzuri, kutofautisha na Dar es Salaam hazijajengwa, lakini hapa karibuni watu wamepewa hati. Wamepewa hati

kwenye sehemu ambazo hawastahili kupewa hati. Naiomba Wizara izinyang'anye hati hizo kabla watu hawajaanza kujenga, mapema sana. Sehemu ya Mwambani kuna viwanja kadha wa kadha ambavyo viko katika hali hiyo na zinaleta mkangamano na ugomvi kati ya wananchi na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ardhi ya Tanga imekuwa kama shamba la bibi, kila mtu anajichukulia tu, hata sehemu ambazo ziliwekwa ziwe ni sehemu za michezo, ziwe ni sehemu za viwanda zimetwaliwa, watu wamezishikilia miaka chungu nzima hawafanyii kazi yoyote pale, lakini wanaweka tu kama njia ya kuweza kuja kupatia pesa huko mbele. Sana wanasisitiza wawe na *title deed* ili waweze kukopa wazidi kututia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, ningeomba masuala haya yafanyiwe kazi, ni pamoja na mashamba hayo ya mkonge, pamoja na kiwanda cha *fertilizer*, pamoja na Uwanja wa Mzalendo ambao pale Mzalendo pana sehemu ya wenzetu waliotoka Bukoba zamani sana, kuna sehemu tunaita Bukoba pale, na wao wamepatiwa hati lakini sasa hati za wale watu waliotoka Bukoba wakakaa Tanga pia sasa zinaingiliwa. Hao ni ndugu zako Mheshimiwa Waziri, na ningekuomba ukipata nafasi baada ya Bunge hili twende pamoja nikupitishe kwa yote haya, kwa sababu Tanga ukifika unapata *snap sheet* ya matatizo ya ardhi yanayotokea ya nchi nzima. Nadhani ukiweza kuyashughulikia yale ya Tanga utapata picha ya kuweza kuyashughulikia sehemu nyingine.

Mimi nisingesema nitazuia shilingi, nataka tu Wizara ijitahidi sana, ifanye yale mambo ambayo yanatikiwa yafanywe. Umefanya kazi kwenye ardhi na unajua thamani ya ardhi ni nini, hatuwezi kuwa Watanzania bila kumiliki ardhi yetu. Na wale ambao ni wageni, wamechukua mwambao wameushika hivyo hivyo kwa nia ya kusema watajenga mahoteli watauendeleza, lakini hakuna kinachotokea.

Mheshimiwa Spika, miaka imepita tusiwe tunasema tu, ninaomba tufanye vitendo. Sehemu ambayo inastahili kurudishwa Serikalini, sehemu ambayo inastahili kurudishwa kwenye Halmashauri, Halmashauri iipangie vizuri, kwa kutumika vizuri, kwa Mipango miji na kwa maendeleo ya wananchi wa Tanga, kiuchumi, kimichezo na kiburudani, yafanyike mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza napenda niwashukuru sana, Ndugu zetu wa CCM kwa msimamo wao mkali ambao wameuonesha asubuhi hii ya leo ya kuwa pamoja nasi, lakini pia nina wasiwasi mkubwa sana kwa sababu, ulishatangaza hapa Tangazo la *Party Caucus* saa saba, yasije yakawa yale yale. Kwa hiyo ninachowaomba Ndugu zangu wa CCM, tuendelee, tuwe pamoja, kwa sababu hiki tunachokifanya ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na jamaa zetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, kuna hii migogoro ya ardhi ambayo kwa kweli ni tatizo sugu na nikienda *specifically* katika mgogoro wa Chasimba, ambao Kambi ya Upinzani iliwahi kuuzungumza mwaka juzi na mwaka jana, lakini pia katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii na leo pia ameizungumzia tena.

Mheshimiwa Spika, huu mgogoro ni wa muda mefu na kwa kweli. Jambo ambalo linasikitisha ni kwamba, pamoja na kwamba kulikuwa na kesi, lakini kesi ikatolewa maamuzi, Mheshimiwa Waziri amefanya ziara mara mbili yeye mwenyewe kwenda pale, amekutana na Kamati inayohusika na mgogoro huo. Pia akarudi, akakutana na wananchi na akawaahidi kwamba kwa yeye kama yeye hatakubali, kwamba wananchi wale wasilipwe fidia za maeneo yao au na nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha ni kwamba hadi hii leo, Mheshimiwa Waziri hilo jambo hajalifanya na badala ya kurudi kwa wananchi, akarudisha mrejesho, sasa anapitia kwa viongozi wa Kata, anafanya haya mambo kisirisiri. Sasa hii kwa kweli wananchi wamekuwa na wasiwasi mkubwa sana kwamba hili jambo lina kitu ambacho si cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa nahisi kwamba au nashauri kwamba au namtaka Waziri atakapokuja, pamoja na kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelisema sana. Kwa hivyo tupate jibu, huu mgogoro wa Chasimba, utakwisha lini? Tathmini imeshafanywa, sasa kama tathimini imeshafanywa wapatiwe haki yao au ijulikane watapata lini, lakini vyovyote vile, Mheshimiwa Waziri nafikiri ni muhimu arudi, taarifa hizo baada ya kumwambia hapa, arudi kwa wananchi, awape hizi taarifa ili wajue msimamo ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia ni kwamba hivi sasa nchi yetu imejikita sana katika kilimo cha biashara na huu ni wito wa kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, lakini pia na Miradi hii ya *BRN.*

Cha kusikitisha ni kwamba, hakujawa na mikakati mahususi ya kuonesha kwamba wakulima wadogo wadogo na wafugaji watanufaika vipi na Miradi hii au watafaidika vipi katika uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, ni vema Waziri atakapokuja, akatueleza au akaeleza wananchi wakasikia kwamba katika Miradi hiyo au uwekezaji huo wananchi watafaidika vipi. Wao watashiriki vipi na haki zao zitakuwa ni zipi. Kwa hivyo, hilo ni jambo muhimu na nafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akijibu hoja zetu atalifafanua kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, hii Miradi ya *BRN,* Mheshimiwa Waziri, kwa kweli inachukua maeneo makubwa. Mfano, mpaka sasa kuna hekta 470,000 ambazo zimekuwa *allocated* kwa ajili ya kilimo cha mpunga, lakini pia kuna hekta 114,000 ambazo zimekuwa *allocated* kwa ajili ya kilimo cha miwa. Sasa hii imefanyika bila kuwashirikisha wakulima.

Mheshimiwa Spika, hii inaleta sintofahamu kwa sababu wakulima ndiyo maeneo hayo hayo wanayoyatumia, wafugaji maeneo hayo hayo wanayotumia. Sasa wakulima na wafugaji wanathirika, hasa wafugaji ambao inabidi watembee masafa marefu kufuata malisho ya mifugo yao. Hili nafikiri atakapokuja kujibu hoja, nalo atatupa ufafanuzi, ili wakulima waweze kuelewa mustakabali wao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwamba kuna hili zoezi la upimaji kwa nchi nzima, ni jambo zuri, ni jambo muhimu, ni jambo la kihistoria katika nchi yetu, lakini Serikali bado, imesema tu. Kwanza hilo la kusema ni jambo moja, lakini pia pesa ni jambo lingine. Sasa upatikanaji wa pesa sijui Waziri atasemaje, lakini nataka nijue kwamba hili zoezi litakamilika kwa muda gani? Maana yake isije ikafanywa kwa mwaka mmoja, halafu likasimama kwa miaka 20, halafu likaja likafanywa tena.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama tumekusudia kulifanya twende nalo mfululizo *or continuously*. Ni vema suala hili pia wakashirikishwa wananchi, zikashiriki Taasisi za Kiserikali, zikashiriki pia Taasisi za kirai ili kupata elimu zaidi na kuepukana na migogoro ambayo inaweza ikatokea. Tunaweza tukafanya vizuri, tukapima ardhi nchi nzima, lakini ikaja ikawa ni migogoro kulikoni hata migogoro iliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri tu kwamba, tunapopima, tuhakikishe kwamba tunatoa *corridors* ndogo baina ya kijiji na kijiji ili kuruhusu zile *free movement* na nini na hii ni kuepukana na migogoro ya badaye ambayo inaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Nimesema namwita Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, atakayefuata ni Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu. Namshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kunisimamisha hapa na kunipa afya njema ili niweze kuchangia Bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, lakini kuna changamoto mbalimbali, ambazo zinaikabili Wizara hii, tunafahamu Wizara hii ni ngumu ina changamoto nyingi ikiwemo migogoro mbalimbali katika masuala yote ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii, kumpa taarifa mchangiaji aliyepita, kwamba Chama cha Mapinduzi kwa maana ya CCM, ni Chama imara, madhubuti ambacho siku zote kinasimamia katika haki na ukweli na ndiyo maana mpaka leo kiko madarakani na kitaendelea kuwepo madarakani. Kule kwetu mimi ni Mganga wa kienyeji na mtabiri mkubwa sana. Sasa hivi natabiri CCM itaendelea miaka 200 mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niingie katika mchango wangu sasa. Nchi yetu imekuwa na migogoro mingi ya ardhi. Tunakabiliana na changamoto kubwa ya matatizo ya ardhi na hasa katika suala zima la upimaji wa ardhi, tungeendelea kwa kasi kubwa ya kupima ardhi ili tuondoe migogoro na changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili sekta hii ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa katika takwimu hizi ukiziangalia hapa, kuna hekta takriban milioni 80 kwa ajili ya kilimo, lakini tunaambiwa asilimia 10 ndiyo ambayo imepimwa kwa ajili ya kilimo. Ili ni tatizo kubwa, tungeendelea na upimaji huu vizuri ingeweza kupunguza matatizo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali tuwe na mkakati maalum wa makusudi wa kuhakikisha kwamba tunajipanga kuondoa migogoro hii ya wakulima na wafugaji kwa maana ya kupima ardhi yetu vizuri ili wananchi wetu waweze kuishi vizuri zaidi, katika maeneo yao. Kwa sababu hii ndiyo inayopelekea kuleta migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, sisi wote tuliopo hapa ni mashahidi. Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yao mbalimbali, migogoro hii ya ardhi inaendelea, mauaji kati ya wakulima na wafugaji sisi wote tunafahamu. Siku mbili, tatu zilizopita kuna maeneo mbalimbali wote tumesikia migogoro hii inaendelea na mauaji haya yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro hiii, ni lazima sasa tuwe na chombo mahususi cha kuhakikisha kwamba tunaondoa matatizo haya ya migogoro ya ardhi na vile vile itapelekea kuondoa kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwangu pale, toka niingie Bunge hili, Kibaha Vijijini, mwaka 2012/2013, 2013/2014 nimezungumzia sana migogoro ya ardhi katika Jimbo langu Kibaha Vijijini. Kuna Kata pale ya Kwala na Ruvu kuna mgogoro mkubwa. Kuna suala zima la Wilaya ya Kibaha Vijijini na Kisarawe, kuna mgogoro wa mipaka hiyo. Kuna Kata ya Magindu, kuna Kata ya Kwala, Dutumi, Mpiji *Station* kule kote kuna migogoro hii ya mipaka kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, miaka yote hii tunazungumzia suala hili hili. Nashangaa mpaka leo sijapata majibu yoyote na nimefuatilia sehemu mbalimbali za ardhi, lakini bado hatujaona mwelekeo mkubwa wa kuondoa tatizo hili la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma kitabu hiki na taarifa ya Mheshimiwa Waziri ya jana, anasema miaka mitatu ijayo Dar es Salaam itakuwa na wakazi takriban 9,000,000. Sasa ushahidi huu unapatika, wakazi takriban 9,000,000 ambao wataongezeka katika Jiji la Dar es Salaam, *obvious* watu hawa sasa hivi watapumulia katika Mkoa wa Pwani, kwa maana ya Kisarawe, Kibaha Mjini, Mlandizi na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuishauri Serikali, ijitahidi kuimarisha upimaji wa ardhi katika maeneo ya Pwani, kwa maana kwamba Kibaha Vijijini, Kibaha Mjini, Kisarawe, na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile niingie kidogo upande wa *National Housing* kwa sababu nimeona na bahati nzuri mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Tumetembelea maeneo mbalimbali, kuna makazi, kuna nyumba ambazo zinaendelea kujengwa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya ongezeko la watu hawa sasa hivi takriban 9,000,000 mahitaji ya nyumba yatakuja kuwa makubwa zaidi. Sasa *National Housing* ingeweza kuangalia sasa upande huo wa Pwani, kujenga

nzuri, kwa maana kwamba kama walivyojenga pale Chalinze, lakini nyumba zile ni chache, waziongeze, pia waweze kujenga nyumba Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Pwani.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze mtaji zaidi, Shirika hili la Nyumba, kwa mfano kuna suala zima la kodi, kwenye Kamati yetu, tumelizungumzia iondoe kodi zote hizi ambazo zinalifanya Shirika hili lishindwe kufanya kazi zake vizuri. Tukiondoa kodi Shirika litafanya kazi zake vizuri. Nyumba nyingi watazijenga na wananchi wetu wengi wataweza kupata nyumba hizo za bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa *National Housing* kwa maana Ndugu yangu Nehemiah Mchechu, kazi zake ni nzuri anazozifanya na sisi wote ni mashahidi. Tumeona hata sasa hivi wamehamia katika jengo lao pale mjini, wamejenga jengo zuri sana. Hii inapelekea kuonesha kwamba wana dhamira nzuri kwa sababu mfano mzuri unaanzia nyumbani kwako, kwa hiyo, leo wameonesha mfano mzuri, wameweza kujenga jengo zuri la *National Housing* pale na Makao Makuu ndipo yalipo pale mjini. Nampongeza sana Ndugu yangu Nehemiah Mchechu kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilisema ataongea Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, atafutiwa na Mheshimiwa Sarah Msafiri.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la matumizi bora ya ardhi, ambalo wenzangu wengine wamezungumza. Tatizo la kutopima ardhi yetu katika nchi hii, hasa kutokufuata Sheria ya Ardhi ya 1999 pamoja na Kanuni zake imesababisha migogoro mingi baina ya wananchi ambao wanafanya shughuli za mifugo, shughuli za kulima na wengine ambao baina yao na Taasisi mbalimbali kama vile wachimbaji, kama vile miji ambayo inapanuka na barabara zinazojengwa. Hii imesababisha mpaka wananchi wameuana, lakini imezidishwa na kukosekana kwa utawala bora. Serikali mara kwa mara hasa Wakuu wa Wilaya wanaangalia maslahi ya wale ambao wana pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika eneo la Wilaya ya Mbulu, kwenye bonde linaloitwa Yaeda chini, kuna makabila mawili yako pale; Watatoga na Wairaq. Hawa Watatogaji ni Wafugaji. Wairaq ni wafugaji pamoja na

wakulima. Kuna mtu amekuja pale mwekezaji anamiliki eka 3,902. Sasa kwa sababu yeye ana pesa, Serikali imemkumbatia na upande mmoja wa Kabila unatetewa na watu wameuana.

Mhesimiwa Spika, sasa tunaiomba Serikali, ili kukwepa mambo kama yaliyotokea kule Kiteto ya Bonde la Murtangos, watu wasizidi kuuana zaidi na Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, aonywe. Sisi suala hili tumeshampelekea Waziri Mkuu, tunategemea kwamba atatusaidia, lakini tunaonya kwamba Serikali ipime ardhi pale na wananchi wafundishwe matumizi bora ya ardhi, wakulima watakuwa wapi na wafugaji watakuwa wapi. Pili, itolewe elimu kwa wananchi kwamba matumizi bora ya ardhi yatakuwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii, kama utaratibu utafuatwa na utawala bora utafuatwa, sheria itafuatwa, kanuni zitafuatwa, haya mauaji yatakoma na hayataendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee eneo la pili ambalo linahusu migogoro mingi iliyotokea ambayo inaamuliwa kisheria na Mabaraza ya Ardhi, tulishukuru wakati fulani kwamba Mabaraza haya yatatusaidia, lakini baadaye tukagundua kwamba, kwa sababu mfumo huu uko nje ya Mahakama na nchi hii Katiba yetu inataka kuwe na mhimili ambao unahusika kuamua haki za watu ambao ni Mahakama. Sasa imekuwa vigumu sana Mabaraza haya kusimamiwa vizuri na Mahakama Kuu, ingawa baadaye mwisho rufaa inakuwa Mahakama Kuu, tunashauri sana masuala yote ya ardhi yawe chini ya Mahakama, yasiwe nje ya mfumo wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naishukuru Serikali kwamba, mlitupa Baraza la Ardhi la Wiilaya ya Mbulu, lakini hamkutupa mpaka leo Mwenyekiti, hamkutupa hata pesa kwa Mwenyekiti wa Babati aweze kutembelea sehemu hiyo na kesi nyingi sasa hivi ambazo kwa mfano, Babati ziko 478, lakini Mbulu, ina kesi zaidi ya 280 kwenye Baraza hilo, angeletwa kule Mbulu, au huyo angekuja angepewa pesa mashauri mengi yangeweza kuamuliwa. Lakini watu wengi wanatoka zaidi ya kilomita 120, wanashindwa kulala, wengine wanatembea kwa ajili ya kufuatilia kesi ya eka tatu au eka nne. Mheshimiwa Waziri, tunaomba ututazame.

Mshimiwa Spika, watazame wajane ambao wanapata shida, wanaonyang'anywa ardhi na ndugu za waume zao, lakini sasa Mahakama ilivyo mbali na ujanja wanaoufanya eka moja ambayo yenye thamani siyo inayofika milioni tatu, wanaandika milioni saba. Kwa hiyo kisheria lazima afungue sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba nizungumzie sasa kuhusu *Value Added Tax (VAT)*, kwenye Nyumba za *National Housing Corporation* na

kwenye bidhaa ambazo zinasababisha nyumba ziwe ghali. Kwa sasa nyumba ya kulala, kupanga kwa kila mwezi, inafika mpaka sh. 4,017,000, *value added* iko wapi?

Mheshimiwa Spika, watu wa *National Housing* wanatuambia kwa sababu walipokuwa wanajenga walikuwa wametozwa *Value Added Tax,* hiyo tunashauri iondolewe. Kama wawekezaji kutoka nje wanauza maandazi wanapewa *exemption,* kwa nini wasipewe *exemption* hawa wawekezaji ambao ni Shirika la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, jambo la mwisho ambalo kama utaniruhusu kulizungumza ni upimaji wa ardhi ambao mpaka leo utekelezaji wake umekuwa ni mdogo, kule mijini sasa miji inajengwa holela, miji inayokua sasa hivi inajengwa holela na mwisho baadaye tunakosa barabara na Mheshimiwa Waziri wa Barabaa naye akija anataka kubomoa nyumba za watu, lakini mwenye kulaumiwa ni wewe kwa sababu uliruhusu kabla ya hapo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwenye Halmashauri zetu Maafisa Ardhi kwa sababu wako chini yao inawapa ruhusa, lakini mwisho na wewe ukija unasema nawakemea. Kwa mfano, mahali kama Mbulu inavyojengwa sasa, wewe hata hujaona Mbulu iko wapi, unawakemea kutoka wapi? Tunakushauri kwamba Sheria itekelezwe la sivyo hali itakuwa ni mbaya sana.

Mheshimwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante na sasa nimwite Mheshimiwa Sara Msafiri Ally atafuatiwa na Mheshimiwa Seleman Said Bungala, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Kaihula na tutamalizia asubuhi hii na Mheshimiwa Esther N. Matiko.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimwa Spika, kwanza kwa masikitiko kabisa nimesikitishwa sana na Serikali kwa kutenga bajeti ndogo sana kwenye Wizara ya Ardhi na hasa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Ardhi kwenye masuala ya maendeleo imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga bilioni 72 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini ni bilioni 15 tu ndiyo zilitolewa. Kwa kweli nimesikitishwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015 badala ya bilioni 72 zilizotengwa mwaka jana kwa ajili ya miradi ya maendeleo wametengewa bilioni 34 kutoka bilioni 72. Sasa kama mwaka jana walitengewa bilioni 72 zikatoka bilioni 15 kwa ajili ya miradi ya maendeleo mwaka huu wametengewa bilioni 34, sijui itatoka shilingi ngapi. Kwa hiyo, kwa kweli nasikitika sana na nimesikitishwa sana na kwa kweli mimi sitaunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Ardhi mpaka Serikali ikae itafakari upya. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, wewe ni shahidi, tumekuwa na migogoro mikubwa ya ardhi, migogoro kati ya wawekezaji na wananchi. Wawekezaji wamepewa maeneo ya uwekezaji, wananchi hawajalipwa fidia, migogoro ya wakulima na wafugaji, ardhi imekuwa ni tatizo kubwa, lakini pamoja na vurugu zote, wananchi wameuana, wakulima na wafugaji sasa hivi ni maadui, lakini Serikali inashindwa kutatua tatizo la ardhi, inatenga fedha kidogo kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimwa Spika, cha kushangaza kwenye hotuba ya Kamati, nimeona kati ya hizo bilioni 34 zilizotengwa, kazi zilizopangwa kufanyika ni nne tu; kujenga mifumo ya kielektroniki katika kuhifadhi kumbukumbu za ardhi, kuboresha maabara na karakana, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miji mipya na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimwa Spika, hakuna kabisa fedha inayotengwa kwa ajili ya kupima ardhi ya Watanzania. Nasema kwamba sasa tufikie hatua, ardhi iwe kipaumbele cha Taifa, ardhi ya Tanzania ipimwe, Watanzania wanataka kujua kama anataka kufuga aende wapi akafuge, kama anataka kulima aende wapi akalime na kama anataka kuwekeza kwenye masuala ya viwanda na biashara aende wapi, lakini nasema huu mchezo unaochezwa na Serikali ufike mwisho sasa.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye fidia zinazodaiwa kupisha miradi ya uwekezaji ni *billions of money,* Kigamboni tu wanadai bilioni 50, lakini wametengewa bilioni saba tu, sasa hapa atafidiwa nani? Hizi fidia ni pesa nyingi na naishangaa Serikali yangu kama kweli ina nia ya dhati ya kupima ardhi hii hizo fedha zinazotengwa *billions of billions* za kulipa fidia wawekezaji, kwa nini hiyo fedha wasiitumie kupima ardhi ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kama ardhi ya Tanzania itapimwa, hakuna haja ya fidia tena, hizi kelele za Kigamboni, Kurasini, kelele za wakulima na wafugaji katika Mkoa wa Morogoro zitakuwa hazipo. Leo Serikali inashindwa hata kulipa fidia, kupisha uwekezaji wa wananchi, wanadaiwa fedha nyingi, lakini Serikali haioneshi nia ya kupima ardhi ili wananchi waamue shughuli ya kufanya. Hili halikubaliki na hili tumelikosea wote yaani Serikali na Wabunge, tumeweka vipaumbele vya Taifa, lakini ardhi siyo kipaumbele. Lakini wote tunajua

kwamba ukitaka uwekezaji wa aina yoyote ardhi ndiyo jambo la kwanza, kwa nini ardhi haiingizwi kwenye kipaumbele? Naomba kabisa Serikali ikae na itafakari upya.

Mheshimiwa Spika, kuna mkakati wa kupima ardhi yaani kila kipande cha ardhi nchini, nawashukuru mmeanza Mvomero mtakuja tena Kilosa na Kilombero. Lakini kasi ni ndogo, bajeti nzima inakwenda kupima Wilaya moja tu ya Mvomero, nashukuru ni Wilaya yangu ninakotoka, lakini hatutaweza kufika kwa hatua hii, lazima kasi ya upimaji wa ardhi ya Watanzania iongezeke, muwashikirishe Viongozi wa Halmashauri, muwaelimishe viongozi wa vijiji kwani viongozi wa vijiji hawaelewi kabisa huko vijijini ukienda. Wanasaini mikataba mibovu, wanaingiza wawekezaji kinyemela, wananchi hawashirikishwi, migogoro kila siku kama siyo ya wakulima na wafugaji basi ni kati ya wananchi na wawekezaji, kama siyo wananchi na wawekezaji ni kati ya wananchi na Serikali, wanadai fidia zao.

Kwa hiyo, naomba kabisa katika utekelezaji wa mpango huu, lazima kuwe na mkakati maalum wa kuwaelimisha viongozi wa vijiji kwa sababu mmewapa mamlaka makubwa ya kusimamia ardhi, lakini hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, ukienda Mkoa wa Morogoro wananchi wanalia, mifugo inaingia shambani kwa wakulima, mazao yao yanaliwa, lakini wakienda kwenye uongozi wa vijiji hawapati nafasi yoyote ya kupata haki zao. Kwa hiyo, naomba kabisa elimu iwepo, lakini msiwaachie hawa viongozi wa vijiji wenyewe kwani hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huku tukiwa tunapima ardhi yetu lazima tuangalie namna ya kusaidia hizi mamlaka tulizowapa, tusiseme tu kwamba tume-*decentralize* mamlaka vijijini kwa wananchi, lakini hawana uwezo, itakuwa ni kazi bure. Matokeo yake Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamekuwa wanashinda maporini kutafuta ng'ombe na kutatua migogoro ambao siyo wajibu wao. Kwa hiyo, naiomba Serikali isikwepe jukumu lake la kuwaelimisha viongozi wa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, mwisho kabisa nataka kusema kwamba migogoro ya ardhi imezidi, ukienda Kilosa, Kilombero, Mvomero, Morogoro Vijijini na maeneo mengi tu wananchi wanapata shida, wanaidai Serikali fedha nyingi sana. Naomba Serikali sasa ikae itafakari upya, kama ardhi inapimwa, basi ipimwe yote isipimwe kwa vipande kwa sababu unapopima ardhi ya eneo moja dogo na eneo kubwa lililobaki watafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba 80% ya wananchi wanaoishi vijijini kazi zao zinategemea kilimo, ni wakulima ambao wanalima na wanafuga. Sasa

mnawachonganisha wakulima na wafugaji bila sababu yoyote, pimeni ardhi ili wananchi wakae kwa amani na wawekeze kwa amani.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, wale wanaoshiriki ibada ya misa ya Katoliki kwenye Jumuiya yao ya St. Homes, ibada ipo leo saa saba.

Nilisema nitamwita Mheshimiwa Suleiman Bungara atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi na pili namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa akili na akili kazi yake kubwa ni kujua ukweli na uongo, haki na batili na kwa kuwa tukiitumia vizuri akili, basi nchi yetu itakuwa nzuri na kwa kuwa akili inajua ukweli na uongo na inasemekana kuna watu wanaamini kabisa kwamba nchi mbili zikiungana zinakuwa ni nchi mbili na Serikali mbili. Watu wenye akili kabisa waliyopewa na Mwenyezi Mungu wanaamini kabisa kwamba nchi zikiwa mbili…

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara unasoma au unafanyaje?

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, sisomi!

**SPIKA:** Nakuona!
**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Njoo uangalia kama nasoma, sisomi!

**SPIKA:** Endelea basi!

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimwa Spika, mimi sisomi isipokuwa hii ni *bobeshi* tu! *(Kicheko)*

Mheshimwa Spika, kwa hiyo, naamini kwa kuwa watu hawa wanaamini kwamba nchi mbili zikiungana zitakuwa ni nchi mbili na Serikali mbili, aah, tutafika tunapotegemea. Naamini akili zetu hatujatumia sawasawa.

Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kwamba Serikali ya CCM itaendelea hata miaka 1,000 kama alivyosema rafiki yangu, lakini itaendelea miaka 1,000 kwa sababu kama watu wanaamini kwamba nchi mbili zikiungana zinakuwa ni Serikali mbili na nchi mbili na wakaamini, aah, wataendelea! Kwa sababu inamaanisha kwamba watu hawaelewi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sana na nawashukuru sana Kambi ya Upinzani kuungana na nilisema zamani sana kuwa tuungane, lakini wenzetu wa CCM wanasema *CUF* kuungana na chama mtakuwa, kwani mna wasiwasi gani? *Wamandharaba nafsi laa yabuki*? *CUF* wakiungana na CHADEMA kwamba *CUF* wajinga kwamba walitukanwa, lakini aliyetukanwa na aliyewaua, ni bora aungane na aliyetukana au aliyewaua?

Mheshimwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Simbachawene, katika Waziri ambaye anaweza kufunga magoli wa CCM, basi Simbachawene anafunga magoli, lakini *defense* hana na nafurahi sana Simbachawene, nilimpa kazi mbili; kazi ya kwanza alipokuwa Madini nikamwambia watu wa Songosongo wana matatizo, ng'ombe wao wamekufa, tangu mwaka 2007, mwanaume yule kafanya kazi wamelipwa hela yao, ahsante sana Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mwezi wa Nne nikampatia barua kwamba, kuna ardhi Mpala yameuzwa, basi kafanya kazi siku tano Mheshimiwa, leo kanipa taarifa kwamba nazuia na kwamba kweli yameuzwa, viwanja 800 alipewa mtu mmoja tu.

Mheshimwa Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri, namheshimu sana. Mheshimiwa Mwanri ni mtu ninayempenda lakini simwamini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni mtu wa porojo, ni msanii. Tarehe 18 Waziri, Mheshimiwa Mwanri alikuja Kilwa na akakutana na Kamati ya Ardhi, Wilaya ya Kilwa wakampa kazi tarehe 18 Februari, 2013 mpaka leo tarehe 28 hajatoa taarifa yoyote. Tukampa *CD* akaweka Kamati ya Mkoa, Mkuu wa Mkoa ukimwendea hakuna kitu, Mheshimiwa Mwanri ukimwendea hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kubwa Kilwa nataka Mheshimiwa Waziri keshokutwa twende Kilwa akaone, Idara ya Ardhi ya Kilwa katika *Block P, TP* kulikuwa na viwanja 194, basi Idara ya Ardhi Kilwa, kazi hiyo tulimpa Mheshimiwa Mwanri lakini kashindwa hiyo, imetengeneza viwanja 600, viwanja 406 inauza Idara ya Ardhi, hiyo Halmashauri hatuijui, wanakula wao tu!

Mheshimiwa Spika, mwaka 1980 *TPDC* ikachukua eneo kubwa sana mpaka leo hii wananchi wangu wa Kilwa Masoko hawajalipwa fedha tangu mwaka 1980. Nakuomba sana Mheshimiwa Messi mimi nakuita Messi wewe kwa kufunga magoli hatari, lakini *defense* hakuna maskini! Uje Kilwa kuangalia matatizo ya Kilwa katika ardhi, hatuwataki Wakuu wa Idara wa Ardhi wa Kilwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, Masoko Pwani wametathminiwa watu, lakini mpaka leo hawajalipwa fedha zao, mpaka leo! Tangu Ubunge kuanzia Bungara, Kingunge, Hasnain na Njalau hawajalipwa mpaka leo! Hili ni tatizo! Serikali ya CCM ni mzigo! Lakini Wabunge wa CCM ndiyo mlioufunga mzigo huo, Wabunge wa CCM ndiyo mlioufunga mzigo huo na hamwezi kuufungua pamoja na maneno yote mnayoyasema hapa, hawezi mtu wa CCM akatoa shilingi hapa, ng'ooo! Kwa sababu mzigo mmeufunga wenyewe! Kama hamkuufungua Wabunge wa CCM, basi Serikali hii mwaka 2015 UKAWA inaichukua. Kama mnataka kuichukua nchi hii, basi ufungueni mzigo mlioufunga, natoa shilingi, natoa shilingi, wakati wa kutoa shilingi hakuna kitu! *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimwa Spika, taarifa!

**WABUNGE FULANI:** Aaa, wewe, kaa chini.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Naomba ukae.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimwa Spika, ombi langu kubwa sana, Waziri wa Ardhi aje Kilwa ili aje kuwachukua watu wake.

Mheshimwa Spika, ahsante sana!

**SPIKA:** Jambo moja napenda niongoze kikao mimi na siyo kila mtu. Tunaendelea!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali, samahani Mwenyekiti, tunahesabu *time*!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimwa Spika, ni kwa kifupi sana!

**SPIKA:** Nimefanya hesabu nahitaji hawa watu wote wazungumze ndiyo maana hata yule nilimkatalia.

Mheshimiwa Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Kaihula! Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia Wizara hii na napenda kujibiwa vizuri na Waziri wakati anajibu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba, Wizara yenu kwa jinsi mlivyo na mipango yenu ya muda mfupi na muda mrefu, mnafikiri mtakuwa mmepima ardhi ya nchi hii na kumaliza lini? Mtakuwa mmepima na mmemaliza au hamfahamu? Kama hamfahamu sisi hatuna shida, lakini mtujibu tu kwamba, kwa mipango ya Wizara yetu mpaka mwaka 2070 na kadhalika, ni lini mnafikiri tukiwaachia hapo mnaweza mkawa mmemaliza kupima ardhi ya nchi hii, lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ni lazima muishi kwa ratiba, tumewakabidhi hiyo Wizara, kwa hiyo, lazima muwe mnafahamu kwa sababu mmetueleza vizuri tu hapa kwenye hotuba yetu mna migogoro huku na kule na kadhalika. Sasa tuambieni mwaka 2050 au 2070 au mwaka gani mtakuwa mmemaliza kupima ardhi ya nchi hii. Jibu hilo ni muhimu mno ili tujue kama mko *serious* au hamko *serious*. Hiyo ni namba moja! *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, namba mbili, tulianzisha Sheria ya Mabaraza ya Ardhi, Sura ya 216 mwaka 2003 na ikaanza kutumika na mpaka leo tuna Mabaraza 42. Kwa hiyo, ni miaka kumi na kitu Mabaraza yanayofanya kazi ni 42. Tukawaambia, ukimchukua mwananchi wa Kibondo pale kwangu kwenda kufuata Baraza Kigoma Mjini, kilomita 240 unamnyima haki yake ya kupata haki, *access to justice*, unamzuia!

Mheshimiwa Spika, mtu amenyang'anywa shamba la sh. 500,000/=, unamwambia afuatilie kesi yake kutoka Kibondo kwenda Kigoma, natoa mfano tu wa Wilaya moja. Kutoka Kibondo kwenda Kigoma ni sh. 30,000/= kwenda na kurudi ni sh. 60,000/=, akienda mara tano ni gharama zaidi ya shamba lake. Tukawashauri kwamba mfumo huu wa Mabaraza hamna uwezo nao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ukaja hapa ukanijibu Profesa, ukaeleza ooh, tutakwenda taratibu, hili jambo limeshashindikana, *you can't*! Lazima haki iwe karibu na watu, watu wa-*access* hivi vitu. Sasa hapa sijui kama kuna Mbunge ambaye hataki Wilaya yake iwe na Baraza.

Mheshimiwa Spika, tukawaambia kwa sababu Mabaraza haya kwanza yame- *perform* vibaya, Baraza la Kigoma lime-*perform* vibaya, linatoa maamuzi, linawanyima watu hukumu ndani ya siku 30, tukawashauri rudisheni hili jambo kwenye mfumo wa Mahakama. Ooh sisi yanafanya vizuri, wapi?

Mheshimiwa Spika, sisi ndiyo tunakaa na wananchi, tunataka Mabaraza yawepo kwenye Wilaya zetu. Tukawaambia tunataka haki hizi zianzie kwenye Mahakama za Mwanzo, tuna Mahakimu kule ambao wana *degree* kama hao Wenyeviti wenu na wengine wanawazidi elimu hao Wenyeviti. Tuna mpaka Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wenye *Masters,* pelekeni watatue kule msitusumbue sisi kutembea kilomita 240, mnazunguka na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikawaeleza tena hapa kwamba, mimi pale Kibondo, nyumba tunazo, maeneo ya kuwapa muweke tu mtu, sisi tunawapa ofisi, nyumba tunazo nimeshamwandikia mara kadhaa Profesa na tumeandika barua, leo akiwa anajibu awaambie watu wa Kibondo ambao ofisi tunampa, hatuhitaji ajenge, tunamwambia jengo hili hapa, awaambie anapeleka lini mtu pale.

Mheshimiwa Spika, sasa anapokuwa anachelewesha vitu vya namna hii, mtu anaomba toka mwaka 2010 kuleta tu Mtumishi inachukua miaka, sasa wale ambao hawana majengo, mtakaa miaka mia mnasubiri haya Mabaraza. Kama mimi nina majengo toka mwaka 2010 ninalalamika, ninyi ambao mnasubiri wajenge sijui watawaletea mwaka gani, labda huko 2070. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo nyingine nijibiwe Baraza la Ardhi ni lini? Tumewaambia tuna majengo pale Kibondo watwambie lini wanaleta?

Mheshimiwa Spika, namba tatu, hii Wizara ina urasimu mno na ambao siyo wa kawaida. Kama huu urasimu hautadhibitiwa, hii Wizara lazima iendelee ku-*perform* vibaya sana. Nchi hii kupata hati tu ya ardhi ni *issue* kubwa sana, yaani mtu kupata hati ni *issue*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya nyingi tu mtu akitaka hati anaambiwa tafuta Afisa Mipango Miji, aje kwanza akupimie, aandae mchoro na nini, maana Wilaya nyingi hazina michoro wala mipango miji. Sasa wewe jiulize Wilaya imeanzishwa mwaka 1920, mpaka leo haifahamiki hapa ni eneo la kuchungia ng'ombe, hapa ni eneo la shule, miaka zaidi ya 80 mnaongoza nchi! Wilaya kadhaa nchi hii, nyingi tu ikiwemo na ya kwangu ya Kibondo haieleweki kwamba, hapa ndiyo hospitali, hapa patakuwa pa kupigia disko na nyie mpo, hivi mnaona ni mambo ya kawaida kweli?

Mheshimiwa Spika, miaka 80, miaka mia ngapi, toka ukoloni hakuna! Sasa mnamwambia mtu anayetaka hati, atafute mchoro, achorewe, akimaliza sijui aende wapi, kwenda huku! Tuone urasimu wa Wizara hii, mtu amenunua ardhi ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante, muda umekwisha. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naomi Kaihula.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na nafasi kuweza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ametuwezesha kufika hapa sisi sote, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala hili muhimu sana la ardhi na makazi. Kwa kweli ni uhai, unapozungumzia ardhi unazungumzia uhai, lakini kitu kinachosikitisha sana ni kwamba, licha ya kwamba tunajua ardhi ni kila kitu, ni uhai wetu sisi na vizazi vijavyo, Wizara hii haijaitendea haki kwa sababu masuala waliyozungumza hapa watu wote ni masuala ambayo hata wahusika wanayafahamu sana kwa kipindi chote kabisa. Jamani inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza niungane na nikubali kabisa taarifa zilizoletwa na Kamati ni kweli kabisa inapaswa muichukulie kwa umakini sana kwamba, ile taarifa ni mwongozo mzuri. Pia niweze kumshukuru Mungu kwa kuwapa ujasiri ile taarifa ya Kambi ya Upinzani, siyo matusi, lakini ni taarifa ambayo unapaswa uambiwe kusimamia. Unapokuwa msimamiaji wa jambo ili liendelee ni lazima uwe mkali kidogo.

Mheshimiwa Spika, nitawaambia kwa nini. Kwa sababu ukichukua kwa mfano katika *National Housing,* nataka nizungumzie kuhusu *National Housing* (Shirika la Nyumba la Taifa) mnalolisifu. Mimi sioni sababu ya kulisifu kwa sababu halijafanya kitu cha maana sana mnachosema, pengine kwa wale wa ngazi za juu kabisa wenye fedha ndio ambao wanaweza wakalisifu, lakini ninachojua ni kwamba, kule kumejaa tu rushwa kubwa kabisa, ubaguzi na kuweka matabaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nimekaa sana katika *National Housing,* hakuna sababu ya *National Housing* kukaa inapandisha bei kila wakati na wanavyotaka kwa sababu tu watu hawawezi kuondoka na waende wapi! Napenda kuwauliza na mnisaidie kuwajibia, kama wao kweli ni watu wanaojali kusimamia shirika lile. Kwa mfano; *National Housing* zile nyumba za Msajili zilikuwa siyo za kuuzwa, lakini ukweli ni kwamba, kutokana na rushwa zao sasa hivi mtaniambia wameuza nyumba nyingi tena kwa bei za kutupwa, lakini wameshirikiana nao na wanakwenda hata kuwashawishi Watumishi wa Serikali ambao walikuwa wanakaa katika nyumba zile wauze kwa Waasia ili waweze kugawiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka mniambie na nashauri zile nyumba muwatafute wote muwarudishe. Kwa nini hao Waasia wenyewe hawapendi kukaa huko pembezoni? Hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba, sasa hivi wanashirikiana nao, wanajenga nyumba na wananunua maghorofa makubwa, lakini hawatengenezi miundombinu, kwa hiyo, unakuta mafuriko, maji machafu, kila kitu hakipo, lakini kodi zinazidi kupaa.

Mheshimiwa Spika, huduma zilizokuwepo kwenye *National Housing* zile za kuhakikisha kwamba, taka, maji machafu, ku-*repair* nyumba kwa nje, hazipo, lakini kodi inazidi kupanda. Hii ni haki jamani? Mnakwenda kusifu, hiyo mnayosifu mnawasifu kitu gani? Kwanza, ukienda kuwakagua wenyewe wengi utawakuta mali wanazomiliki siyo sawa na kazi zao na utumishi wao, hilo ni kweli!

Mheshimiwa Spika, sasa hilo ndilo ambalo Serikali ya CCM hamuwezi kulitambua, acheni ulegevu. Hivi vitu ndiyo ambavyo vinaendeleza rushwa kwa sababu mtu anaingia kwenye kazi anakuta waliopo pale wanafanya mabaya, wanaendelea kama vile *TRA* hawaulizwi. Kwa nini mmeacha maadili mazuri ambayo yalikuwepo wakati ule, ukiona mtu anapanda haraka anapelekewa *paper* ajieleze, tunaishi nao. Mnasema kwamba, mtakaa miaka 100, hamwezi kwa sababu rushwa imezidi na mnaiangalia na hamtaki kuichukulia hatua, mnaibembeleza na nyie pengine ni washiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *okay* semeni pengine mmepewa fungu dogo la fedha, je, kusimamia rushwa nako ni fedha? Siyo fedha kusimamia rushwa. Toka nikiwa mwanaharakati ni migogoro, migogoro, je na migogoro inataka fedha? Inataka ujasiri tu, maarifa, *commitment* na muwe na kitu cha kujali watu. *(Makofi)*

Ninyi Wizara hii ya Ardhi hamjali watu. Moja kwa mfano, mnawaondoa watu hamuwapeleki mahali popote, mnasema kajenge, mkimpa fedha, mtu gani anajenga nyumba kwa siku moja? Sisi tumeona katika safari tunazokwenda za kikazi, tumejifunza kwa wenzetu kwamba, wanapanga mipango toka mwanzo, wanatayarisha, wanakwambia mtu unataka hutaki tunakupeleka *temporarily* hapo, halafu kwenye eneo lako wanajenga nyumba nzuri, wanakuweka pale, unakuwa unalipia baada ya muda fulani unaacha. Ninyi mnasema ooh, tumewajengea nyumba nzuri, watu gani ambao watalipa hata shilingi milioni moja kwa mwaka hawapati jamani?

Mheshimiwa Spika, mbona tunafanya mambo kama vile hatuelewi? Wasomi wazuri, watu mliolelewa, hata kama siyo usomi maana yake tukisema usomi siyo sawa na *education*, *but you are educated*! Ninyi mna maarifa, mmelelewa, *you are socialized, you are well brought up*, mnajua kabisa watu wengi hali halisi kupata milioni moja kwa mwaka hawawezi, mnasema nimemjengea nyumba ya shilingi milioni 20 atapata wapi? Hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nawasikitikia sana na kwa kweli hata Mungu anakataza jambo hilo kwamba, ninyi hampendi watu wenu. Wewe unaanza kumbomolea mtu ndiyo unataka aondoke, kwa vipi jamani? Maafa mliyofanya katika miji, hayo si kuchonganisha watu? Kwa mfano, kama Dar es Salaam watu wamekopa, wamefanya nini, mnasema maboresho, mtu anakula maboresho? Wakati wa mvua, mtu amepigwa na mvua, mtu ana mkopo! Hiyo ndiyo ina-*lead to commit suicide* (watu kujiua) kwa sababu gani? Hamna!

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, jambo langu nililotaka kuwaambia. kwa kweli Serikali ya CCM pamoja na kwamba, nawapenda. mnahitaji Upinzani ambao ni thabiti, uweze kuwasimamia sawasawa. Mnakumbuka niliwaambia zile hadithi tulizokuzwa nazo za Karume Kenge, aliyekataa kwenda shule, ni ninyi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mrema!

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu, la kwanza ni lile la ujenzi wa Mji wa Himo njia panda. Wadau walipeleka kesi Mahakamani mwaka 2002, nimehangaika na wewe hapa Mheshimiwa, hivi anayepanga mji ni Mahakama au ni Wizara ya Ardhi!

Tumehangaika na Wizara ya Katiba na Sheria, lakini nashukuru kwamba ile kesi wiki iliyopita imemalizika na Mahakama ikaamua ule ni mji na utaendelea kujengwa na wale watu wenye ardhi, mtu anayetaka ardhi pale atapewa fidia. Sasa ombi langu kwanza ni kuwaomba wananchi waliohusika na ule mgogoro wasikate rufani, wakikata rufani tena itachukua tena miaka 12, ule mji hautajengwa. Maadam Mahakama imesema wanaweza wakafidiwa mtu akitaka maeneo yao, naomba Watanzania wote wanaotaka kuja njia panda Himo, wanaotaka ile ardhi wasichukue ardhi ya bure, Mahakama imeamua watu wapewe fidia na ndiyo haki, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, nimepiga kelele, nimeonana na Mheshimiwa Simbachawene kuhusu ile ardhi ya Meresini, pale Himo, ina mgogoro mkubwa sana. Katika ardhi ile hapa nina barua ya Wizara ya Ardhi ambayo inasema kwamba: "Kufuatana na maagizo Halmashauri ya Wilaya ilitekeleza wajibu wake wa kupanga matumizi mbalimbali katika eneo hilo.

Baada ya kupanga matumizi taratibu za ugawaji wa ardhi husika zilifanywa kwa kuzingatia kama zilivyoanishwa katika Kanuni *(The Land Allocation Committee Regulations)*."

Mheshimiwa Spika, sasa kilichoamuliwa na ardhi, kule kwangu tatizo siyo wakulima na wafugaji au wafugaji na misitu, tatizo tulilonalo pale ni wananchi na Maafisa wa Ardhi na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Sasa ukiangalia hii barua ni ya juzi, hilo eneo lilikuwa la Mkonge tangu mwaka 2006, wananchi wanaomba waweze kupewa, siyo hata kwa ajili ya matumizi binafsi, ni kwa ajili ya shule, soko na mambo kadha wa kadha. Sasa Wizara ya Ardhi imeandika barua tarehe 11 Machi, 2013 mgogoro haujatatuliwa tangu 2006 Mheshimiwa Waziri, watu wanateseka na hawakushirikishwa (wale wananchi wa Himo).

Mheshimiwa Spika, sasa anasema Kamati ya Ugawaji Ardhi Wilaya ilipaswa kupitia maombi ya ardhi. Haikupitia katika eneo hili. Endapo utaratibu haukuzingatiwa ni muhimu ukazingatiwa. Afisa wa Ardhi wa Kanda anawaambia utaratibu uzingatiwe. Endapo utaratibu haukuzingatiwa ni muhimu ukazingatiwa kwa maana ya kufuatwa upya. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, hawajafuata upya, taratibu, kanuni na sheria zilizopo kwa maeneo yote yaliyopimwa katika shamba lile.

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka 2006 mpaka juzi tarehe 13 bado wanarudia makosa yale yale! Hii barua Mheshimiwa Waziri nimekwishampa Simbachawene, anayo nikamwomba akuletee, wananchi wa Himo wametaja matajiri waliopewa mashamba makubwa na sisi hatuna ardhi, ni eneo dogo. Mimi nitaisoma kama ilivyo; Aloyce Bent Kimaro alipewa heka 11.7 kwa ajili ya kujenga kituo cha redio wakati shule ya Sekondari Meresini yenye watoto 700 imepewa heka tisa. Kitu cha kusikitisha zaidi eneo ambalo wananchi wa Kijiji cha Himo ambalo walikuwa wanalitegemea kwa ajili ya upanuzi wa shule ya Sekondari Meresini - *A Level*, ambalo liko mkabala na shule hiyo ndilo alilopewa huyo tajiri wa kituo hicho. Kutakuwaje na amani jamani? Watu watagombana tu, watapigana.

Mheshimiwa Spika, mwingine ni anayeitwa Minja, alipewa heka saba wakidai ni kwa ajili ya kujenga Kituo cha Watoto wa Mitaani kituo ambacho ni hewa. Wananchi wa Himo waliongezea masikitiko yao pale ambapo Shule ya Msingi Meresini yenye watoto 400 ilipewa heka tano na kuambiwa eneo hilo walilokuwa wanalitegemea kwa ajili ya upanuzi wa shule limepewa tajiri mwingine anayeitwa Edward Shayo mwenye *International School* pale Himo, ambaye anamiliki shule hiyo iliyopo kilomita Tatu (3) kutoka katika eneo hilo. Pia tajiri huyu ndiye anayemiliki asilimia 75 ya ardhi ya Himo.

Mheshimiwa Spika, shamba lililokuwa la Mkonge, kweli mnagawa ile ardhi mnawapa watu wenye fedha, matajiri, wakati pale hakuna soko, hakuna shule ya chekechea, hakuna kiwanja cha mpira! Haya Mheshimiwa inachekesha pale ambapo wanataja eneo la *Super Market* la heka 1.7 kwa ajili ya Halmashauri! Kwa hiyo, naomba hilo Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho ni kile Kiwanda kilicho njia panda cha Kilimanjaro *the Wines and Spirits*. Mliandika barua tarehe 23 Januari, 2013 mmemwandikia Mkurugenzi nyie wenyewe na naomba Wananchi wa Vunjo wasikie kwa sababu inaonekana Mbunge ndiye ana mgogoro au wananchi wa Njia Panda, mkasema eneo hilo ni makazi ya watu. Aliyesema siyo Mbunge au Mrema, barua iko hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza nataka nitoe hiyo barua ya wananchi wa Meresini, pia nitoe hii barua ambayo Mheshimiwa Waziri ameandika na mkasema katika maeneo yale pia kuna maeneo ya kuabudu na kwa ajili ya matumizi ya umma yameongezwa kwenye hilo eneo. Barua iko hapa siyo mimi ninayesema.

Mkaandika kwamba, hicho Kiwanda kwa kuwa kimejengwa kwenye makazi ya watu kibomolewe. Nyie wenyewe mmeandika, sasa mnatuletea mgogoro na wananchi wa kule ili tuonekane labda sisi tuna majungu au ni wazushi, mmeandika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza barua ya kwanza ndiyo hii ya Meresini, naiweka hadharani hapa iwe kumbukumbu ya Bunge hili na pia hizi barua za Kiwanda cha *Spirits and Wines* pale uniambie tunafanyaje.

**SPIKA:** Mheshimiwa hizo barua kama unaziweka juu ya meza basi wanakuja kuchukua.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Haya njoo kijana uchukue hizi umpe Mheshimiwa Spika hapo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukirudi baadaye, nawataja wafuatao, lakini haina maana kwamba ndiyo watakavyochangia, nawataja tu wajue na wawahi kufika.

Yuko Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Khalfan Aeshi na Mheshimiwa Esther Matiko. Naomba Waheshimiwa hao wote wawahi ili tukifika hapa tusiwasubiri.

Waheshimiwa nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi Jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Tukae. Mnawanyanyasa watu mpaka wanasahau kurudi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa nadhani tunaweza kuendelea, namwona Mheshimiwa Chibulunje na Mheshimiwa Mtemvu yupo. Mheshimiwa Chibulunje!

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo iko mbele yetu, naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara hii ni kumilikisha ardhi pamoja na ule utaratibu wa kuwezesha kupatikana kwa hatimiliki za kimila. Mwaka jana nilipokuwa nachangia katika Wizara hii nilitoa malalamiko ya wananchi ambao wanatumia hatimiliki hizi za kimila na wale wengine ambao wamepitia MKURABITA kwamba wanakataliwa na vyombo vya fedha kwamba si hati halali.

Mheshimiwa Spika, sasa inashangazwa wakati Serikali siku zote ikisisitiza ya kwamba hatimiliki hizi ni halali kisheria, lakini vyombo vya fedha nasikitika kusema kweli pamoja na taasisi za Serikali kama *TIB* zimekuwa hazikubaliani na hilo. Sasa sisi linatupa shida kidogo unapokwenda kutoa maelezo kwa wananchi ya kwamba hatimiliki hizi za kimila ni halali, lakini kwa bahati mbaya wanapokwenda kwenye vyombo vya fedha wanagonga ukuta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimwombe Waziri tena, kwamba, maadam msisitizo wa uhalali wa hati hizi uko pale pale, basi angalau angetoa mwongozo rasmi ambao utatambulika kwa vyombo vyote vinavyohusika, vyombo vya fedha, lakini kwa wananchi wenyewe watumie utaratibu gani ili hati hizi ziweze kukubalika, vinginevyo sisi tutakuwa tunaeleza kinyume na wenzetu ambavyo wanatekeleza.

Mheshimiwa Spika, tena katika maeneo mengine ambayo hati hizi zinakataliwa ni vijiji ambavyo ni vikubwa, ambavyo kwenye miji hapa ungeweza kuviita kama ni *prime areas* Vijiji kama vya Haneti, Naibu Waziri anavifahamu, Dabalo, hapo kijijini kwangu mnapopaita Chalinze Nyama, pote hapo

wananchi wana hati hizi lakini wakipeleka kwenye Mabenki hawakubaliwi kwamba ni hati halali. Kwa hiyo, nataka labda msimamo wa Serikali kwa mara nyingine tuone hali ikoje.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nilizungumzie ni juu ya migogoro hii ya mipaka pamoja na kugombania maeneo kati ya wakulima na wafugaji. Wenzangu asubuhi wengi wamelielezea kwa kirefu na nisingekuwa na sababu ya kurejea tena, lakini niombe tu kwamba pengine moja ya suluhu ambayo ingeweza kusaidia katika migogoro hii ni kule kuharakisha kupimwa kwa maeneo haya na hasa katika Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, mimi kwenye maeneo yangu, kuna Kijiji kama cha Haneti na Izava ambavyo tunapakana na Wilaya mpya ya Chemba, lakini Izava kwa upande mwingine tunapakana na Wilaya ya Kiteto na Kongwa. Sasa hizi Wilaya ninazozitaja karibu zote ni mpya pamoja na ya kwangu. Sasa maeneo ya mipaka ya Wilaya hizi bado haijajulikana vizuri. Kwa hiyo watu wengine wanatumia alama za zamani, wengine wanatumia milima.

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara ingetusaidia, ihakikishe kwamba, maeneo haya yanapimwa na kuhakikisha kwamba wananchi wanaeleweshwa kujua kwamba haya ndiyo maeneo halali yanayohusiana na mipaka yao. Katika maeneo mengine unakuta kwenye maeneo ya mipaka hii Wilaya nyingine imetenga eneo hilo la malisho, lakini kwa upande wa pili, Wilaya nyingine imetenga kwamba ni eneo la kilimo. Kwa hiyo, sasa unakuta hapo kuna migongano, lakini kama maeneo yangekuwa yamepimwa mapema yangeweza yakasuluhisha hayo matatizo ambayo yanatupata sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nirudie ombi langu ambalo nililitoa mwaka jana wakati nikichangia Wizara hii kwa *National Housing*. Wilaya yetu ya Chamwino ni mpya, kwanza niwashukuru na kuwapongeza watu wa Shirika la Nyumba kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali nchini. Sasa kwa sisi ambao tunajenga Makao mapya ya Wilaya, Chamwino ikiwa mojawapo, mwaka jana niliomba kwamba pengine Shirika la Nyumba lingeangalia uwezekano wa kuja kwenye eneo letu tuweze tukawapatia viwanja wakatusaidia ujenzi wa nyumba ambao utatatua tatizo la nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kwa mara nyingine tena kwa mwaka huu, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia uwezekano huo na bahati nzuri wiki iliyopita hapa niliuliza swali Bungeni kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuchika alinihakikishia kwamba na yeye alikuwa ameshapeleka ombi hili kwa *National Housing* na walishamkubalia na

sisi tulitakiwa tueleze kama tunavyo viwanja vya kutosha kuweza kuwapa *National Housing* kujenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kupitia kwako Mheshimiwa Waziri leo hii nikuhakikishie tu kwamba tunavyo viwanja vya kutosha pale Chamwino kwenye Makao Makuu yetu ya Wilaya. Kwa hiyo, tuihimize *National Housing Corporation* ije, sisi tutakuwa tayari kuwapatia viwanja ili watusaidie kujenga nyumba kwa ajili ya kupunguza tatizo la nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, Shirika la Nyumba litakuwa limejitanua kwa uzuri, lakini vile vile litakuwa limeleta tija inayotakiwa katika kutatua matatizo ya nyumba za watumishi, lakini wakati huo huo itakuwa inajiwekea kama kitega uchumi katika maeneo haya mapya. Haya sasa nazungumzia tu kwa ujumla wake pamoja na maeneo mengine ya nchi hii ambayo yanahitaji mahitaji kama haya.

Mheshimiwa Spika, nilidhani nielekeze hayo ambayo kwa kweli yote yalikuwa ni kukumbushia tu, kwa sababu yote nilikuwa nimeshayasema kwenye hotuba ya mwaka jana. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri ayakumbuke hayo, watupimie mipaka katika maeneo yetu ya Wilaya mpya, lakini vilevile ahakikishe kwamba hizi hatimiliki za kimila zinaheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba mtoe tamko ambalo wananchi wote watalielewa na mwisho ni ombi langu hili ambalo nimepeleka kwa Shirika la Nyumba, naomba watujengee nyumba pale kwenye Wilaya yetu ya Chamwino ili kupunguza tatizo la nyumba kwa ajili ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Abbas Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini napata kigugumizi labda uniambie kama naruhusiwa maana yake nataka kumwondolea Waziri shilingi, ila simwoni.

**SPIKA:** Wakati wa kuondoa shilingi sio sasa. Wewe zungumza useme mimi nikipata nafasi nitaondoa shilingi.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, nilitaka kuondoa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Niwashukuru kwa hotuba nzuri, nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kumchagua Naibu Waziri, naamini atatusaidia sana. Pia nipongeze sana kwa uchaguzi wa Katibu Mkuu wa sasa wa Wizara hii, Bwana Alphayo Japani Kidata, tunamjua ana uwezo mkubwa katika mipangomiji na akitumika vizuri ataisaidia sana Wizara ile. Pia na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Mayunga, ni mchapakazi sana sana. Niwaombe tu kuna Idara pale ya Mipango yuko Mama Kessi, aidha wamsaidie wampe hiyo nafasi au watafute anayestahili, maana yake bado yuko mwoga mwoga na Wizara ile inataka watu wenye maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wangu sasa wa nane na nusu kwenye Ubunge na miaka yote toka nimeingia lazima katika Wizara hii niongelee suala la Mtaa wa Kurasini na suala la *National Housing*. Sasa nianze na Mtaa wa Kurasini. Mtaa wa Kurasini nimeongelea kwa muda mrefu sana, wananchi wa pale wanateseka kama wanavyoteseka wa Kigamboni. Serikali imekuwa ikiahidi bila utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Serikali ikakubali mawazo yangu, pale atafutwe mwekezaji atakayeendana na ujenzi wa eneo lile na kweli amepatikana. Sasa tatizo liko kwenye mthamini. Nimwombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ndiye namwona basi akaliharakishe.

Mheshimiwa Spika, mvua hizi zilizokwisha wananchi wale wa Mtaa wa Kurasini kwa Mama Komba, walikuwa wanaishi kwenye mazingira magumu sana, ilifikia hata vitanda vyao vya ndani wameweka matofali kuvipandisha juu kwa sababu ya maji. Kwa hiyo, niombe sana suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna suala la Kijiji cha Wavuvi. Wizara ilikubali kwamba kutokana na hali ilivyo eneo lile watalipa fidia wananchi wale waondoke, lakini wananchi wale wanateseka kupita kiasi. Kwa hiyo, naomba Naibu Waziri na hilo alichukue ili aone namna gani atalifanyia kazi. Waziri Mkuu alimshauri Mheshimiwa Waziri aunde Kamati ya Ushauri kwa ajili ya Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri alituandikia barua Wabunge wa eneo lile wote kwa maelekezo ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile akawa na hofu juu ya uteuzi ule, lakini nikamwambia twende tuingie tuone ndani kuna nini. Matokeo yake toka tuchaguliwe, tujibu barua mpaka leo hakuna kikao. Sasa unashindwa kuelewa ni namna gani utekelezaji wa maeneo yale ya watu utafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini nirejee kwenye suala la *National Housing.* Mwaka 2007 ukiwa Naibu Spika, tulipitisha hapa ndani ya Bunge, baadhi ya nyumba ziuzwe kwa wananchi wale wanaoishi pale wa kipato cha chini.

Hatukusema majumba yale makubwa ya Upanga wapi, lakini tulisema maghorofa ya Tandika, Chang'ombe, Keko, tulisema nyumba za *National Housing* za Moshi ambao saa zote wanatuma *message* na tulisema nyumba za Ubungo. Cha kushangaza sijui Kamati walikaa lini maana yake azimio lilitoka hapa, wakati ule Waziri, Mheshimiwa Chiligati. Kwa hiyo, niombe kama mpango ule umekufa azimio lirejee ili tutoe Baraka, utaratibu uendelee, haiwezekani Kamati ikawa inasema.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kunisikitisha *National Housing* naipenda sana na siku zote miaka yangu nane na nusu nimekuwa nikisema hapa juu ya *National Housing* kabla hata uongozi wa sasa wa ndugu yangu Msechu haujaingia, nimekuwa mimi ndio mtetezi wa *National Housing*, walikuwa wanakaa Temeke, juzi Mungu amewajalia wamejenga Upanga wamehama, pamoja na hawakutuaga lakini tunawatakia kila la kheri, safari wanayokwenda. Naamini Bwana Msechu ni mchapakazi mzuri, kijana hodari, wote tunampenda, lakini kwa nini unawaonea wananchi wangu wa Temeke wamekosa nini?

Mheshimiwa Spika, naomba hiki kitabu nitaweka juu ya meza yako uone wananchi wale walioishi pale kwa miaka mingi wanavyoteseka. Niombe kuna ule uongozi wa Nyumba unateseka, kina mzee Gwao, wazee wastaafu wa siku nyingi, kina Kanali Swai wamefanya kazi nzuri pale *Kibaha Education Centre,* hebu msiwakimbie, kaeni nao muwasikilize.

Mheshimiwa Spika, nashangaa sana tumekaa na Waziri Mkuu kuhusu zile Kata tatu, watu wa Ardhi mnazijua na tunaamini Madiwani wa Temeke hivi wako wananisikiliza, wamemsikiliza Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, wananisikiliza mimi na watamsikiliza Dada Maryam.

Mheshimiwa Spika, tunaamini Waziri Mkuu ametoa maelekezo kuhusu zile Kata tatu Pemba Mnazi, Kisarawe *Two* na Kimbiji, lakini mpaka leo sijui kigugumizi kinatoka wapi cha maamuzi. Kata sita zimechukuliwa mara ya kwanza kwenye mradi. Kata tatu zimeongezwa mara ya pili, lakini kinachofanyika hakuna wananchi wa Kigamboni wanateseka, tunashindwa nini kuamua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba leo wakubwa hawa watuambie, kigugumizi cha nini Kata tatu, sita haziwatoshi? Sita zenyewe hamjaanza watu wanateseka kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, nilishapata kukaa na Waziri, nikamshauri vizuri tu, huu mpango anza Kata moja moja, onyesha mfano, baada ya hapo mafanikio yake utaendelea Kata ya pili, Kata ya tatu, lakini nikamwambia shirikisha pia Mashirika ya ndani. Tuna Mashirika hodari yanafanya kazi vizuri; shirikisha

*National Housing, NSSF, PSSF, LAPF* na *PPF,* lakini wenzetu hawa kila ukiwasikia wanakwambia Wakorea, Wajapan, Wachina na hawatuwaoni. Kwa hiyo, tunaomba sana wenzetu hawa waangalie na waone jinsi watu wanavyoteseka.

Mheshimiwa Spika, leo katika mradi ule unatunyang'anya Temeke asilimia 75, kweli Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri *Wallah* sijastarehe leo, kwa sababu Waziri hakuwepo, japo anaingia, lakini ndiyo namalizia, kweli wana huruma, asilimia 75?

Mheshimiwa Spika, nirejee yale mambo ya haraka haraka, nimekaa na mama nimemshauri, Mama Waziri, shirikisha Mashirika ya ndani yatakusaidia. Nina swali langu halijaja hapa linaelezea mambo hayo hayo. Haitoshi Mheshimiwa Waziri amekuja, ile Kamati aliyounda ya nini hajatuita mwaka, hatujui kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, niombe heshima yake kubwa, Profesa, ametoka kwenye Shirika kubwa tu *UN-Habitat*. Nakumbuka Nanjing China tulikutana kule, alitupokea vizuri, aliandaa mkutano mzuri ukapendeza, hebu jambo hili kama analiona zito, atamke jamani...

**SPIKA:** Haya tunashukuru, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mwidau atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nitachangia kwenye mambo manne.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ardhi ni uhai na ni maisha kwa watu na viumbe wote. Hakuna kitu chochote kinachoweza kufanyika popote pale isipokuwa ni juu ya ardhi. Maendeleo ya Taifa letu hili yatatokana na matumizi mazuri ya ardhi yetu nzuri tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Kitendo cha Serikali kutotoa fedha za kutosha na kwa wakati katika Wizara ya Ardhi ili kuweza kutekeleza mipango na miradi ya maendeleo iliyopo katika Wizara hii kwa kweli inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kuanzia asubuhi leo Wabunge wote waliosimama hapa walikuwa wakilalamika juu ya mipaka na upimaji wa ardhi. Hata kule kwetu Tanga yapo matatizo hayo hayo na sisi tuna migogoro hiyo hiyo ya ardhi kwa sababu ya mipaka kwa sababu ardhi yetu imepimwa kwa asilimia ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, pia sisi Tanga, tuna matatizo haya, tunaomba Mheshimiwa Waziri na asikilize ushauri unaotoka kwa Wabunge kuhusu malalamiko yanayotokana na migogoro ya ardhi, ni mengi na kwa kweli inatukera. Kwa sababu ukiangalia katika Mkoa wetu wa Tanga hata kule Pangani wananchi waliishi vizuri sana lakini siku hizi wanagombana vijiji na vijiji.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia leo Kipumbwi na Kijiji cha Kibuyu wanagombea tu msitu uliopo pale kwa sababu inasikitisha sana ni kwa sababu mipaka ni ya enzi na enzi, hata mzee Chibulunje amesema hapa tangu enzi za Nabii Nuhu mpaka leo mipaka ndiyo hiyo hiyo, vizazi vinabadilika, watu wanagombana kwa sababu ya mipaka, tunaomba mliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kitendo cha Serikali kuchukua ardhi na kuifanyia tathimini kwa nia ya kupima uwanja au kuweka shughuli za maendeleo na kuweka uwekezaji na kukaa nao muda mrefu sana bila ya kuwalipa wananchi fidia, na vilevile kuwasimamisha wasifanye shughuli yoyote ya maendeleo katika hayo maeneo, kwa kweli ni kitendo cha kusikitisha kweli kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Tanga katika eneo la Nema, wananchi toka mwaka 2008 mpaka hii leo ni miaka sita, wamechuliwa eneo lao, limefanyiwa tathmini, wameambiwa wasifanye shughuli yoyote ya maendeleo. Miaka sita ni mingi; unazaa mtoto na sasa hivi kwa mwaka huu 2014 anakuwa ni *primary*. Kwa hiyo, kwanza, kisaikolojia inawaumiza, halafu mnawaharibia uchumi wao. Ni kwa nini mnakurupuka? Kama hamjawa tayari kwenye hiyo miradi mnayofikiria, ni kwa nini mnawaondoa watu kwenye maeneo yao? *(Makofi)*

Kwanza, mngekaa chini mkajua kwamba kweli tunataka kufanya uwekezaji huu, pesa tunayo, ndiyo mkawaondoa. Hakuna mwananchi ambaye hataki maendeleo! Lakini kitendo mnachofanya, ninawaomba kwa niaba ya Watanzania wote, maeneo yote mliyochukua Tanzania, kwasababu Wabunge wote wanalalamika hapa, mwarudishie watu maeneo yao! Mkishakuwa tayari sasa mrudi kwa ajili ya huo upimaji, mfanya tena hizo tathmini kuweza kuwalipa fidia na kuweza kuchukua hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, namwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa kujibu, mambo yote yale ambayo aliambiwa ajibu, hili naomba asilisahau, atuambie! Wizara imefikia wapi katika kufuta hati za mashamba ya mkonge Mkoa wa Tanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu pale, Mheshimiwa Ngonyani kaliongelea, Mheshimiwa Nundu kaliongelea!

Mheshimiwa Spika, nashukuru leo Mkoa wa Tanga umetuona, nami natoka Mkoa wa Tanga. Naomba kuweka msisitizo; utuambie kwasababu wananchi wanateseka sana! Mashamba haya wamepewa wawekezaji ambao sio wawekezaji, ni watelekezaji. Ni wawekezaji hewa ambao wamechukua mikopo katika mabenki, wameacha mapori, wananchi wanateseka! Ndugu zangu wa Marungu wanateseka, hawana maeneo! Kuna shamba la *estate* la Marungu, watu sasa hivi wamevamia, wanalima na kujenga. Kesho na kesho kutwa mtakwenda kuwatoa pale kwa mitutu!

Ndugu zangu wa Pangani, *Mwera Estate*, ukiangalia pale kuna eneo la Kilimangwidu, wanateseka! Wananchi wa vijijini wafanye kazi gani? Hakuna viwanda, hakuna shughuli ya uwekezaji, ni kilimo! Mwananchi anapewa nusu heka kulima, atalima nini? Atasomeshaje watoto?

Tunakuomba Mheshimiwa Waziri utuambie, tunajua Mheshimiwa Rais ndio anafuta, lakini sisi tunakulalamikia wewe kwasababu wewe ndio tumekukabidhi hili! Leo wananchi wanaambiwa walime kwenye miraba ile ya mkonge, atalima nini? Sana sana atalima mahindi, mbogamboga, lakini hana uhakika! Kesho mwekezaji kakasirika, anamfukuza. Kwa hiyo, wanateseka ndugu zetu wa vijijini. Vijijini hakuna ajira zaidi ya kilimo! Tunaomba mliangalie kweli kweli suala hili.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Kigamboni. Mheshimiwa Waziri naomba kukuliza, kulikoni Kigamboni? Kwa kweli Kigamboni ni bomu ambalo liko *very hot!* Linaweza kupasuka wakati wowote! Simfichi Mheshimiwa Waziri, tumechoka na hii Kigamboni. Kila bajeti, Kigamboni! Tuna migogoro mingi Tanzania! *(Makofi)*'

Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, kwasababu ya suala hili lilivyo na fumbo, limekaa kama kitendawili, tunaomba ulishughulikie, ufuate ushauri unaotolewa humu ndani.

Ushauri wa Kamati, ushauri uliotoka kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani na ushauri wa Wabunge. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri kwasababu malalamiko yamekuwa mengi. Mwaka 2013 hali ilikuwa hivi hivi na kukatokea mvutano mkubwa sana kati yako wewe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge pale.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwasababu uliweza kutumia maneno ya hekima na busara. Naomba kwa heshima yako nikunukuu ili kuweza kujenga hoja yangu vizuri kumwelewesha Mheshimiwa Waziri aweze kuona umuhimu wa suala hili. Naomba nikunukuu kati ya ule mvutano uliokuwepo

mwaka 2013, tarehe kama ya leo 28, mwezi huu huu wa Mei; tofauti ni mwaka, kati ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge pale.

Mhehimiwa Spika, ulisema maneno ya hekina na busara kwa sababu na wewe lilikugusa suala hili, naomba nikunukuu:

*"Mheshimiwa Waziri, wakati mnajibu mlisema kwamba mko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge. Naomba mshirikiane naye na wako watu walioniandikia barua pamoja na ile barua aliyoitoa Mheshimiwa Wenje, naomba mkae mmalize hili suala; na wala hatuwezi kubishana hapa, naomba mwende mkalimalize."*

Mheshimiwa Spika, naomba kumnukuu Mheshimiwa Mbunge alipopewa nafasi alivyosema:

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa busara zako, maana yake haya mengine aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Waziri hapa kwa kweli hayana usahihi, I am sad to say that. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niko tayari wakati wowote kukaa na Mheshimiwa Waziri na watu wengine ambao wana nia njema na mradi huu ili kutatua hili tatizo tulilonalo.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, naomba nirudie tena kwa faida ya wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge. Hatupingi huu mradi wa Kigamboni, concept yake ni nzuri, lakini tuna matatizo makubwa sana katika utekelezaji na ubabaishaji mkubwa ulioko ndani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hicho ndicho kinachowakera wananchi wa Kigamboni. Mheshimiwa Mwenyekiti niko tayari."*

Mheshimiwa Spika, ukasisitiza, "Mheshimiwa Waziri, *seriously* mkakae pamoja kama ulivyoelekeza katika majibu yako kwamba mnayo tabia ya kusuluhisha, mkazungumze hili suala, litakuwa ni kero kwa sisi hata tunaosikia, ndiyo maana sipendi kuruhusu mjadala."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ulisisitiza hili. Mheshimiwa Waziri uniambie, ni kwa nini mpaka leo hujakaa na watu wa Kigamboni? Tafadhali ukija hapa utumbie Mheshimiwa Waziri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati yako mbaya!

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ulishamaliza kuninukuu, basi inatosha. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Esther Matiko, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza ripoti ya Kamati na ya Kambi Rasmi ya Upinzani na ninaomba Waziri husika ayazingatie yale yote yaliyozungumzwa mle.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia Mabaraza ya Ardhi. Ni dhahiri kabisa tunajua kwamba Mabaraza haya ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanashughulika na usuluhishi wa migogoro, lakini tumekuwa tukishuhudia migogoro mingi sana Tanzania katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ambayo inapelekea kurudisha nyuma maendeleo ya nchi, kwasababu tumeshuhudia mali nyingi zikiharibika na hata vifo.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri anawasilisha hapa kwenye kitabu chake, alisema kwamba ukurasa wa 81, unasema mashauri ya zamani yalikuwa ni 18,328, kwa maana ya yaliyoishia Juni, 2013; na mashauri mapya yaliyosajiliwa mpaka Aprili, 2014, alisema kwamba ni 11,548. Lakini akasema kwamba kwa kipindi hiki, yaliyosikilizwa tu ni mashauri 11,432 na akasema kwamba mashauri yanayoendelea kusikilizwa ni 18,444. Kwa kasi hii kwa kweli ni dhahiri kwamba tutaendelea kuwa na migogoro mingi sana katika nchi yetu.

Kwa hiyo, nilitaka Mheshimiwa Waziri atufafanulie zaidi katika hayo mashauri ambayo yanaendelea kusikilizwa, ni mashauri mangapi ambayo ni ya zamani na ni zamani tangu kipindi gani? Kwa maana hiyo, nataka kujua kuna kasi gani ya mlundikano wa mashauri haya kwa maana ya *backlog?*

Mheshimiwa Spika, ni kwasababu tunajua kabisa, kwa mfano, katika nchi ya *South Africa,* mashauri katika Mahakama za kawaida yakishafika miezi sita katika Mahakama za Wilaya yanakuwa *categorized* kuwa hizo ni *backlog* kwa hiyo zinapewa inapewa *priority.* Kwa Mahakama za Mkoa inakuwa ni miezi tisa na Mahakama Kuu ni miezi 12.

Mheshimiwa Spika, kwa hapa kwetu Tanzania kwa Mahakama za kawaida nafikiri inachukua miaka miwili kuweza kuya-*categorise* hayo mashauri kwamba ni *backlog* sasa kwamba yanatakiwa kupewa *priority*.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nijue vilevile Sera ya Wizara hii katika ufuatiliaji na ukaguzi wa Utendaji wa Mabaraza haya ya Ardhi na Nyumba, kwasabbu tumeshuhudia wananchi wengi sana wanalalamika, licha ya kwamba Mabaraza ni machache na yana changamoto nyingi, na Wizara imegoma kabisa kukubali ile *concept* ya kupeleka kwenye Mahakama hizi nyingine, nilitaka nijue ni Sera ipi ambayo Wizara inayo kuhakikisha inafuatilia utendaji kazi

wa haya Mabaraza; ili kuweza kuhakikisha kwamba maamuzi yanatolewa mapema kutoa haki kwa wadai kama *incase* wanataka kukata rufaa waweze kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi katika migogoro ya ardhi kwenye Wilaya ya Tarime. Katika Kata ya Mwema, Kijiji cha Korotambe, Kitongoji cha Tekoyogera na Kijiji cha Kubiterere Kitongoji cha Nyakangara, hawa wananchi ardhi yao imechukuliwa na JKT lakini hawa wananchi hawajafanyiwa tathmini yoyote ile na mbaya zaidi JKT wamejenga nyumba pale, wanakata miti, na wanalima na zaidi wanang'oa ile miti ya mkonge ambayo inakuwa kama *demarcation* kati ya eneo la mwananchi mmoja na mwingine.

Sasa ninajiuliza, hawa wananchi ina maana hawatafanyiwa tathmini kabisa? Kama watafanya tathmini, wataenda kupima vipi kujua kama hili eneo ni la Esther Matiko, hili eneo ni la Mwita Nyamuhanga na hili eneo ni la Bhoke? Maana tayari hawa JKT wameshang'oa ile alama ya mipaka kati ya mwananchi mmoja na mwingine. Kwa hiyo, ningependa kujua, Wizara inawaambia nini hawa wananchi kuhusu eneo lao lililochukuliwa ambalo walikuwa wanafanya kazi ya kulima na wengine walikuwa wanaishi mle? Maana hawajafanyiwa tathmini, lakini JKT imeendelea kulitumia lile eneo.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa napitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona ameainisha miji ambayo itapimwa, lakini Mji wa Sirari haupo na Silari *is a strategic town* sasa hivi, ni Mji wa kibiashara na ukizingatia uko katika Bonde la Kenya na juzi hapa tulikuwa na *debate* kuhusu *East Africa Community;* ni kwa nini Mheshimiwa Waziri hajaona kama kuna umuhimu wa kupima ule Mji wa Sirari? Upande wa pili kwa wenzetu Wakenya kumepimwa, upande huu haujapimwa na majengo yanajengwa mengi, ikitokea kuna nyumba mojawapo imeungua pale, itakuwa ni *disaster,* kwasababu hakuna gari la *Fire* ambayo itaweza kupita kwenda kuzima moto. Itakuwa ni maafa ambayo hataweza kuzuilika. Kwa hiyo ningependa kujua hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie kuhusu ulipaji fidia kwa wananchi wa Nyamongo na Mgodi wa *North Mara*. Mheshimiwa analifahamu hili na wananchi wameshamfuata mara nyingi, akina Mama Methuselah na wengine, wananchi wa Kipimio, Nyamichele na Mrwambe. Wananchi wale wamekaa pale, hawajafanyiwa tathmini; mbaya zaidi inaenda kinyume na Sheria ya Madini ya 2010, na Mheshimiwa Waziri ameainisha hapa, Ibara ya 97 sehemu ndogo ya (7) ambayo inataka kwamba wale wananchi wahamishwe kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi kabla *operation* haijafanyika.

Sasa Mgodi una-*operate,* unaenda kumwaga uchafu katika nyumba za watu. Hawa watu mmeshindwa kuwalipa tathmini waondoke! Mheshimiwa Waziri unalijua; wamechimba sehemu nyingine kwenye makaburi, Mama

Methuselah kwa mfano, ana makaburi ya watoto wake pale, amemzika Baba Mkwe wake pale na Wajukuu wake, wameenda bila hata kujali wakafukia yale makaburi bila kujua ni nini haki ya wale watu waliozikwa pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba na ninasikitika sana, kwenye ripoti umeainisha kabisa kwamba umesuluhisha mgogoro wa Geita ilhali unafahamu mgogoro wa *North Mara* na ulifutwa nyumbani kwako na ukakiri ungekwenda Tarime, hukwenda. Lakini huku umesuluhisha wa Geita, wa Tarime umeacha. Ni kwa nini? Au unataka uendelee kuona watu wakitaabika na kufa kwa magonjwa ya maambukizi kwa ile *pollution* wanayoipata pale? Wanapigwa kulazimishwa wahame wakati hawajalipwa fidia stahiki Napenda kupata majibu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba wengine wameshaongelea umuhimu wa kupima viwanja mbalimbali, lakini nimejarinu kuangalia pia hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ameainisha kwamba Halmashauri ya Musoma, Rorya na Tarime hawakupewa Hatimiliki ya Kimila.

Mheshimiwa Spika, nataka niulize, ni kwa nini hamkuona kwamba kuna haja hizi Halmashauri kuweza kupata Hatimiliki za Kimila ili wale ndugu zetu na wao wakitaka kujiendeleza au kukopa, waweze kunufaika? Kwa hiyo ningependa kujua ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, niongelee vilevile kwa mkazo kabisa kwamba, nilipokuja hapa niliuliza swali kuhusu wananchi wa Ikoma. Ikoma ilivyo; nusu ni Wilaya ya Rorya na nusu ni Wilaya Tarime.

Kuna Wakenya wamevamia pale. Niliuliza swali humu Bungeni mwaka 2011, Mheshimiwa Waziri akaahidi kwamba watashirikiana na Waziri wa Mambo ya Ndani kuweza kujua kama kweli hawa Wakenya wanaishi pale au la, na wataweza kutoa majibu. Mpaka leo hii hawajafanya lolote lile na wale Wakenya wameendelea kukaa pale.

Sasa mimi ninajiuliza, *are we real serious*? Tunaacha Watanzania maeneo yao yanachukuliwa na Wakenya, tunatoa ripoti huku kuwawakilisha wananchi wetu, *yet* mnasema mtafuatilia, *and then business as usual! Is upset (au upsad)*. Inatia uchungu sana. Mheshimiwa Waziri ningependa uniambie majibu kwa kina kwa haya yote niliyoainisha

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Aeshi, atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia angalau kwa dakika saba hizi ulizotupatia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sitaunga mkono hoja, japokuwa Mheshimiwa Waziri tunaheshimiana sana na ninakuheshimu kama Mama yangu lakini kwenye hotuba yako umeongelea sana kuhusu maeneo yetu, hususan eneo la Sumbawanga ambalo tuna mgogoro nalo mkubwa, shamba letu la Malonje.

Mheshimiwa Waziri, umeongelea suala hili ya kwamba liko Mahakamani, nikapata mshituko sana, kwasababu ninaamini kwamba tutakwenda Mahakamani, ni kwamba tutakwenda hata kama ni miaka kumi, bado wakulima wangu hawa hawatakuwa na uwezo wa kulima ndani ya shamba lile, lakini kwa haraka napata majibu kwamba mwekezaji huyu ataendelea kulima shamba lile mpaka hapo kesi itakapokwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hujafika eneo hili lakini tuna…

**SPIKA:** Ngoja niulize, Mheshimiwa Aeshi, kesi iko Mahakamani au sivyo?

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Waziri amesema iko Mahakamani, lakini ninavyojua mimi, haiko Mahakamani. Sasa nilikuwa nataka kupata maelezo kwasababu hotuba yake ya jana alisema ameshindwa…

**SPIKA:** Naomba Serikali ituambie: Je, kesi iko Mahakamani au haiko Mahakamani?

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Haiwezekani!

**SPIKA:** Naomba uzime *microphone*.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kesi ilikuwa Mahakamani, siku mbili zilizopita ndiyo mchakato umemalizika. Kwa hiyo, sasa hivi haiko Mahakamani.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Aeshi, tunakurudishia dakika zako.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Nashukuru kwa jibu zuri, kwa sababu sasa ilikuwa inanipa shida sana. Naam!

**SPIKA:** Tunarudisha dakika zako.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, naamini sasa suala hili limekwisha na maagizo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba shamba hili lirudi la kwa wananchi. Lakini japokuwa shamba hili Mahakamani limekwisha, kuna fidia ambayo ni lazima tulipe, na fidia hiyo ni takribani Shilingi bilioni tatu, lakini kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri sijaiona. Sasa Mheshimiwa Waziri, hizi pesa zinatoka wapi? Tunawalipa nini hawa?

Naomba nipate majibu kutoka kwako Mheshimiwa Waziri kabla sijazuia Shilingi, maana naona Waheshimiwa Wabunge wengine wanafanya kuzuia Shilingi kama *fashion;* mimi hapana, nitaizuia moja kwa moja mpaka hapo utakaponipa majibu, ni lini sasa; kwasababu mgogoro huu umekwisha na Mahakamani kesi imekwisha, nakuomba uniahidi, ni lini utakuja Sumbawanga na lini utawarudishia wananchi hawa shamba lao?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hujafika eneo hili; watu wanakufa! Watu wanakatwa masikio; watu wananyanyasika; watu hawana pa kulima! Mheshimiwa Waziri ifike wakati sasa hata kauli ya Rais sasa iheshimiwe. Kama Mheshimiwa Rais ameshaagiza, nikuombe sasa na wewe isichukue muda shamba hili kabla hatujawa Wabunge; waliopita walifanya makosa, lakini tunaomba makosa haya yasirudiwe tena, Mheshimiwa Waziri lisimamie na unipe majibu kabla sijaondoa Shilingi. Ninaamini kabisa naweza kupata nafasi nikaweza kushikilia mshahara wako.

La pili, ni ameneo haya ya ndani ya Manispaa ya Jimbo la Sumbawanga Mjini. Mji ule umetanuka sana, lakini mpaka leo hatujapata fungu lolote lile la kuwezesha Wizara iweze kupima ramani na wananchi waweze kupata viwanja na kuweza kujenga nyumba bora.

Matokeo yake sasa, ukienda Eden kule Manispaa ya Sumbawanga utakuta nyumba zimeanza kujengwa kiholela; ukienda njia ya kwenda Kasanga, Mji wetu mpya, unajengwa kiholela. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri, ifike wakati sasa na Manispaa yetu sasa uikumbuke ili na sisi tuweze kupata fedha za kuweza kupanga Mji wetu vizuri. *(Makofi)*

La mwisho, ni kuhusiana na suala la Kigamboni. Mheshimiwa Spika alishatoa maelekezo kila siku kuwa ukutane na Mheshimiwa Mbunge lakini mpaka leo ninaamini juhudi hizo hazijafanyika. Sasa nataka nikuombe tu Mheshimiwa Waziri, hebu hili suala la Kigamboni lifike mwisho. Tumekuwa tukipiga kelele siku hadi siku, kila Mbunge akisimama hapa anaongelea Kigamboni. Sisi wenyewe tuna maeneo Kigamboni, tumeshindwa kujenga. Sasa tunataka kupata jibu moja. Kama kule haiwezekani, mtuambie Mheshimiwa Waziri na kama linawezekana, basi mtoe jibu mapema ili tujipange upya. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naamini kabisa kero yangu kubwa ilikuwa ni shamba le *EFATHA,* nisingependa nipoteza muda mwingi, niwaachie na wenzangu wachangie.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba akija hapa kuongea, basi naomba anipe jibu langu, *EFATHA* lini mtakuja? Sumbawanga ni lini mtakuja na wananchi na wenyewe wategemee, kwa sababu imekuwa ni historia; kila tukifika tunawaambia wananchi Mheshimiwa Waziri atakuja, atakuja, atakuja. Sasa wamekuwa wanakusubiria kama vile Nuhu alivyokuwa anasubiria safina, miaka 40! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tu nimwombe Mheshimiwa Waziri, atuambie ni lini atakuja na lini shamba hili litarudi kwa wananchi kabla ya kilimo kuanza?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Utakumbuka katika hatua za awali Bunge hili wakati wa asubuhi nilikuwa naomba mwongozo, na kwa sababu mwongozo wenyewe ulikuwa unahusiana sana na Wizara hii, naomba niuzungumze tu kwa kidogo ili unisaidie kidogo kupata majibu.

**SPIKA:** Sikupi muda zaidi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, naam ahsante.

Mheshimiwa Spika, tunajadili bajeti ya Serikali, na bajeti ya Serikali ni kujadili mapato na matumizi. Kwa mujibu wa kanuni ya (5) uzoefu wa Mabunge yetu ni kwamba Serikali tunapokuwa tunaanza bajeti inatupatia vitabu vinne, *volume one, two, three* na *four*. Hadi leo tunajadili bajeti, tumefika katikati ya mjadala wa Bunge la bajeti, Serikali mpaka leo haijatoa *volume one* ambayo ni *Financial Statement and Revenue Estimates. (Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea kujadili kama Bunge, Serikali haijatoa kabrasha hatujui mapato ya Serikali. Sasa kwa mfano, leo tunajadili Wizara ya Ardhi ambayo mapato yake kwa mujibu wa kitabu cha bajeti ya mwaka 2013 ni zaidi ya Shilingi bilioni 100. Lakini sasa Waheshimiwa Wabunge hawana fursa yoyote ya kujadili mapato kwa upande wa Wizara, tunajadili zaidi matumizi.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nikuombe uwaambie wahusika ili tuendelee kufanya mjadala wa bajeti uwe endelevu, ni vyema tukapata vitabu kutoka Serikalini vinavyozungumzia *revenue estimates* za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa hiyo ya awali, sasa nirudi kwenye mchango wangu katika Wizara hii. Mji wa Hai katika Mkoa wa Kilimanjaro ulianza mwaka 1975. Wilaya ya Hai ilianza mwaka 1975, ikiwa imekatwa kutoka Wilaya ya Moshi. Wakati huo Wilaya ya Hai inaundwa, maamuzi ya kufanya Vijiji vya Bomang'ombe na Vijiji vya Mungushi katika Halmashauri hiyo ya Wilaya ya Hai kuwa ndiyo Makao Makuu ya Mkoa yalifanyika mwaka 1978 na Serikali ikawataka wanakijiji wanaoishi katika maeneo yale waachie mashamba yao kupisha ujenzi wa Mji wa Hai.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutoa ahadi ile kwa wananchi kwamba ingewapa mashamba mengine ya kufidia ardhi yao, wananchi wale walikubali wakatoa maeneo yao, Mji wa Hai umejengwa, Mji wa Hai umepanuka na sasa hivi unakaribia kuwa na takribani wakazi 50,000; ni Mji ambao umekuwa kwa kasi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro kimsingi hauna ardhi yoyote iliyokuwa tupu. Ukiona kuna ardhi tupu, basi ni ardhi ya Serikali ambayo haitumiki. Serikali ilipohamisha wananchi hawa, iliwapa ahadi ya kuwapa mashamba, haikuwapa mashamba mengine, wakawapa viwanja, wakawaahidi kwamba watawapa mashamba kwa ajili ya kwenda kulima. Leo ni mwaka wa 38 hawajaweza kupewa mashamba yao. Hawa wananchi wametaabika kwa muda mrefu sana, wengine wamekufa wamebaki familia zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeombwa mara nyingi na mara ya mwisho, maombi haya tulimpatia Mheshimiwa Rais Kikwete, mwezi Oktoba, 2012 wakati alipokuja kuzindua barabara ya Kuwasadala – Masama; nilimwomba Rais katika Mkutano ule awaahidi wale wananchi ambao wametaabika kwa muda mrefu kwamba ataweza kuhakikisha kwamba Serikali yake inatoa ardhi kwa ajili ya wananchi hao na Mheshimiwa Rais akaahidi hivyo.

Mheshimiwa Spika, tangu hapo, ahadi haijatekelezwa, huu ni mwaka wa 38. Tumeshaandika kwa Mheshimiwa Waziri mara chungu nzima; Halmashauri ya Wilaya ya Hai iliandikwa kwa Mheshimiwa Waziri; namwona Mheshimiwa Waziri anacheka akifikiri pengine ni uwongo labda nimpe kumbukumbu kwa ajili ya rejea, nitampa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi aliandikiwa barua na wala siyo kipindi chake ni kabla kabisa, mapema kabisa! Mheshimiwa Waziri aliandikiwa barua tarehe 3 Februari, 2007 akiombwa maeneo mawili na ilikuwa ni barua siyo kutoka kwa wale wananchi, ni maombi kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambayo ilitathmini ardhi ya wananchi iliyochukuliwa ikamwandikia Mheshimiwa Waziri ikipendekeza maeneo mawili ambako wananchi wangeweza wakamegemewa ardhi.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza lililopendekezwa kwa Serikali, na haya maeneo yote mawili yako chini ya Serikali. Eneo la kwanza lilikuwa ni kumega kiwango cha heka 2000 za ardhi kutoka eneo lenye jumla ya heka 14,621 ambalo linamilikiwa na Serikali katika eneo linaloitwa *Somali Settlement.* Eneo hili ni la Serikali, halikuwa linatumika kipindi hicho na Serikali vilevile ilimega eneo hili wakatoa kwa Vijiji vya Orkolili katika Wilaya ya Siha lakini wale wananchi wa kutoka Hai hawakuweza kupewa ardhi hiyo hadi leo. *(Makofi)*

Wakati huo huo tulimwandikia Mheshimiwa Waziri katika barua hiyo hiyo, aliombwa, kama awezi kutoa eneo la *Somali settlement,* basi aruhusu utaratibu wa kumega eneo hili kutoka shamba la ranchi ya Taifa *(National Ranching Company)* lililopo katika Kijiji cha Orkolili kule magadini Siha, kuweza kutoa eneo la heka hizo hizo 2000 katika eneo ambalo lina heka 22,256. Kutoa heka 2000 tu kuwasaidia wananchi wale ambao kwa nia njema waliachia ardhi yao, wakaiachia Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mpaka leo Serikali haijatoa majibu. *(Makofi*

Wananchi hawa wamefuatilia kwa Waziri Mkuu, wamekuja kwa Kamishna wa Ardhi, Wameandika Wizarani, na hivi wanataka kuja Dodoma ili waonane na Mheshimiwa Waziri. Nitakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwanza utupatie majibu ya awali, ni kwanini hili jambo ni dogo tu, kwa nia njema wananchi walipisha Makao Makuu ya Wilaya yakafanyika; wapewe ardhi waendeleze familia zao bila sababu yoyote ya kulumbana na Serikali. Hilo ni la pili ambalo nilipenda sana kulizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa nchi hii hatutobaki maskini milele. Kwa sababu hatutabaki masikini milele, ni lazima tujipange kama Taifa tunavyopanga matumizi ya ardhi, tufikirie miaka 100 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea nchi hii katika Miji yetu hususan Jiji Dar es Salaam, Mheshimiwa Waziri jana amezungumza katika hotuba yake kwamba kukua kwa kasi ya Jiji la Dar es Salaam kwa mujibu wa *projections* za Shirika la Umoja wa Mataifa zinazoshughulika na makazi ya watu, wanasema mwaka 2050 Dar es Salaam itakuwa ni mojawapo katika Miji 20 mikubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, kasi ya kukua kwa Jiji la Da es Salaam ni ya kutisha, lakini maandalizi ya Serikali kukabiliana na upanuzi wa Jiji la Dar es Salaam haviendane sambamba kabisa kabisa! Dar es Salaam inageuzwa kuwa *squatter!* Dare es Salaam imekuwa ni *squatter*; na siyo Dar es Salaam tu! Nenda Mwanza, Arusha, Moshi, nchi nzima tunajenga *squatter!* Serikali mnafanya nini? Tufanye nini tuzuie hali hii?

Sasa ukienda katika maeneo haya ya *squatter,* hata kuja kutoa huduma za kawaida za kibinadamu huwezi tena! Kupeleka miundombinu inakuwa ni shida, kupeleka huduma za Zimamoto, majitaka na maji machafu hata njia za umeme wacha barabara, inakuwa ni shida! Sasa hii nchi nzima iko hivyo. Kama vile tutaendelea kuishi kwenye *squatter* kwa miaka 100 ijayo; hatufanyi *plan* tukifikiria kuna miaka 100 au 200 ijayo.

Mheshimiwa Spika, hebu Serikali itueleze katika hoja hii! Hii, Mheshimiwa Waziri kweli kama hakuja na majibu yanayoeleweka, nitapambana naye katika Shilingi yake. Kwa sababu tunageuza nchi hii inakuwa *squatter!* Miji inakua, hatuchukui *action!* Yaani tunakuwa kama sijui tumekuwaje! *(Makofi)*

Sasa nasema Mheshimiwa Waziri siyo kosa lako binafsi, lakini nafikiri ni kosa ambalo lipo kila mahali! Lakini nani aanze sasa hii kazi? Nani aanze kujipanga kwa ajili ya kuokoa hili Taifa siku za mbele? Yaani ukifika Dar es Salaam leo, ukienda Upanga, Oysterbay, Magomeni, Changombe yale maeneo yalipimwa na Wakoloni miaka 50 iliyopita. Leo tunajitawala wenyewe, miaka 50 tunashindwa kupima maeneo yetu. Barabara hakuna, miundombinu hakuna, wananchi wanaishi maeneo ya ajabu! Hii nchi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani ninachosema ni kwamba hili naomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli inayoeleka. Hatuwezi tukaruhusu nchi hii ikaendelea kujenga *squatters*, wananchi hawana huduma na hawawezi wakajengewa huduma. Hata Serikali yetu itakapoingia madarakani tutapata shida kubwa sana kuwahudumia wananchi na tupata shida kwa sababu mmeshindwa kuweka *plan*. Yaani kama vile mnafiki nyie mtatawala milele! Ni lazima mkumbuke kwamba…. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsanteni sana! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwakweli jambo hili nataka nilizungumze kwa umuhimu mkubwa na naomba Wabunge wenzangu wote safari hii wote tukubaliane, kwa sababu hili siyo suala la Chama chochote cha siasa, ni suala la nchi yetu. Tunawaachia watoto nchi gani hii, tumeshindwa kupanga Miji? Ukienda Miji yote utaambiwa huku ni Uhindini, huku kulikuwa ni Uzunguni, huku kulikuwa Uswahilini, hata maeneo waliyokuwa wanakaa wananchi wa kipato

cha chini yalikuwa yanapangwa. Leo tunashindwa kupanga *50 years after independence*!

Mheshimiwa Waziri, unakuja na mkakati gani? Serikali yako inakuja na mkakati gani? Hizi *squatter* katika Miji yetu tunaziondoa vipi? Hili ni suala la dharura na wala siyo suala la kusema tena tunajipanga, tunafikiria……

*(Hapa kengele ililia kukashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, ahsante.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Suleimani Nchambi.

**MHE. SULEIMANI N. NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Muumba wa Mbingu na Nchi na ninawashukuru sana wananchi wa Kishapu kwa kunileta humu ili niendelee kujenga hoja ambazo zitasaidia sana kuboresha maisha ya Wanakishapu na kuchangia kwa kiwango kikubwa kwa wanachi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa ufupi sana umuhimu wa ardhi. Sisi wanadamu wote kwa vitabu vitakatifu vinne vyote, vinakiri kabisa kwamba tumeumbwa kutokana na udongo.

Kwa hiyo, ardhi ina umuhimu wa aina yake. Kwa hiyo, nataka nimweleze ili Mheshimiwa Waziri na katika Wizara zote za Serikali yetu hakuna Wizara ambayo haitegemei Wizara yako ya Ardhi. Kila Wizara inategemea. Iwe ni ya Maji, wakiitaji bwawa, watakuja kwako; Mheshimiwa Magufuli, Mheshimiwa Profesa Muhongo akitaka kuchimba dhahabu na wengine wengi. Kwa hiyo, lipe uzito wa kiwango cha thamani suala hili la adhi.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme nilisikitishwa sana pale ambapo migogoro mikubwa ya ardhi inapoendelea katika Wilaya ya Kishapu na Igunga, nilipoona Mawaziri wa Mifugo wamekimbia haraka sana, Naibu Waziri alikimbia kuja kuliangalia suala lile, lakini nikajiuliza akilini; hivi kama amekuja kuona ng'ombe wamejeruhiwa! Sijui amekuja kuwatibu ng'ombe! Hapa tatizo, watu wanagombea ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri, ndugu yangu, *brother* wangu Mheshimiwa Simbachawene, kwa kweli tangu ameingia amekuwa akichakarika. Naomba nitoe mfano mmoja, japo Bunge siyo sehemu ya hotuba ama mahubiri, lakini naomba uniwie radhi nitoe mfano mmoja.

Yesu Kristo wakati anaitangaza Injili, aliwatuma watu Mashariki, magharibi, Kaskazini na Kusini mwa dunia wakafanye kazi. Lakini miaka ilipopita alipiga tambo na kwenda kuhakiki kazi waliyokuwa wakiifanya wanafunzi wake. Sasa Mheshimiwa Tibaijuka wewe ni mama yangu, *I do respect you* sana. Sasa mimi najiuliza, huyu Profesa ama ni ule msemo unaosema *do not judge a book through its cover!* Napata mashaka! Ndiyo maana sisi Wasukuma tunasema "*pagaga mihayo oto paga shigala,*" yaani usiweke sigara hapa kwenye sikio, weka maneno mazuri yenye busara.

Mimi naomba sana Mheshimiwa Tibaijuka mama yangu, ninakuheshimu lakini watu Kishapu wamepigana, anasema Mkuu wa Mkoa, mpaka wetu ni Mto, hakuna *(GN) Government Note* ya Serikali. Tumetoa taarifa, Naibu Waziri amekuja, amesema kwamba tutatuma watu wa Tume waje wawaonyeshe *GN* ya Mipaka yenu. Hawakufika!

Cha kusikitisha zaidi wakati tunagawa Mpaka wa Igunga na Kishapu, watu wa Wizara yako walipokuja wakakuta Mto Manonga umejaa, hawakuweza kufika wakasema tutarejea. Hawajarejea tena! Watu wamepigana, wameuwana, Wizara ya Ardhi haijafika.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kutoa msisitizo, Wizara yako ya Ardhi inategemewa na Wizara zote za Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Wananchi wana matatizo makubwa, wakulima na wafugaji wanapigana.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kukijibu naomba kabisa, uniweke kwenye kushika ile shilingi yetu! Naomba sana kwa hili, niko chini ya miguu yako mama yangu. Nitainuka, unione kwa jicho la huruma ili anihakikishie Mheshimiwa Tibaijuka atafika Kishapu ili watu wapate matumaini, waonyeshwe migogoro hii inatokana na nini? Watu wetu hawana matatizo, wakiambiwa nyinyi wa kushoto, wa kulia, mbele ama nyuma, *they don't have problem!* Mambo yanakwisha.

Mheshimiwa Spika, suala la hati. Mimi nasikitika sana kwamba inafika mahali Rais wetu; mimi nampenda sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa sababu hata ndugu zetu wa Kambi ya pili, huwa wanarusha maneno makali lakini huwa anawaita, wanakunywa juisi pamoja, wanakubaliana, mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Sasa tusimsingizie kwamba amezuia kusaini hati. Naomba utoe kauli hapa kwamba kama ni uzembe wa watu wako, kama ni uzembe wa aina yoyote katika Wizara yako, tuondelee watu hapa ambao hawakusaidii! Itafika mahali

tutakuwa tunabadisha Mawaziri sawa na kubadilisha tu Sheikh, kanzu na nini, mambo ni yale yale ni yale yale! Unayo mamlaka! Hivi vibodi bodi vya ajabu, Watendaji ukiwaacha wakunyoe mama hapa, mimi nitasikitika! Wararue kwanza tuonyeshe Wabunge wanataka kusaidia wananchi wetu! Usimtie lawama Mheshimiwa Rais wetu, tunampenda sana, ndiyo maana wenzetu huwa wakiitwa wanakubaliana. Busara yake ni kama ya Nabii Suleimani, wanamsikiliza, wanamheshimu, mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Suala jingine la kusikitisha, Mheshimiwa Tibaijuka, Kishapu tuna hati za kimila 45, tuna hati za kawaida 1,445, tuna mashamba yenye hati 52. Matarajio kila mwaka tufanye *registration,* hati za kawaida 1,200, hati za kimila 2,500. Tuko chini kwa asilimia 500. Leo ukienda Pembejeo kukopa trekta wanahitaji hati, ukienda kwenye *SACCOS*, wanahitaji hati, ukienda Benki wanahitaji hati. Huoni unakwamisha kwa kiwango kikubwa uchumi wa wananchi wa Kishapu? *(Makofi)*

Naomba ulitazame hili! Naomba uangalie mfumo utakaosaidia! Kama leo tupo nyuma kwa asilimia 500, *people in Europe They are running, we are still crawing! We are not even walking.* Sijui tunafanya nini? Nikuombe mama, nakuomba sana, sana, sana, suala hili ulipe majibu! Lazima ujue pa kuanzia ni wapi na unawasaidia wapi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lingine hati zenyewe, gharama ni kubwa, na zile za kawaida kodi ni kubwa sana. Wananchi wetu, mbali ya umasikini, lakini usumbufu wanaoupata, wanaogopa. Kodi ya ardhi ni kubwa sana! Lazima uangalie!

Mimi nilidhani ulivyopitisha kodi ziwe kubwa, utaboresha huduma ya ardhi, utatoa hati nyingi, utapima Miji mingi, utafanya kila kitu! *Business as usual!* Naomba urudishe kodi ya zamani, Watanzania waendelee ku-*enjoy* katika nchi yao na wasiwe watumwa katika Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu *Mchechu* wa *National Housing,* mimi nampenda sana kwa sababu amefanya mabadiliko makubwa. Lakini nakuomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mtani wangu Simbachawene, Kishapu tuna tatizo kubwa sana la nyumba. Oneni namna mnaweza kufika; mwaka 2013 niliwaomba kwamba fikieni mtujengee nyumba za *National Housing!*

Mimi nilipiga kelele, mnajenga maghorofa ya Shilingi bilioni 30 Dar es Salaam; wanaoajiriwa ni watu 20 au 30, ndio watu wenye uwezo wanakaa mle. Walimu wetu wana matatizo, watumishi wana matatizo! Angalieni namna mnaweza mkashirikiana. Tumeshawaita mara nyingi. Shinyanga Mjini mmeanza, lakini sasa nawaomba mfike Kishapu.

Kishapu yetu ni shapu, mkifika leo, kesho sisi tunawapa kiwanja. Na nyie muwe shapu keshokutwa muanze kujenga nyuma na mtondogoo watu wetu ni shapu wanaingiza *furniture*, wanaingia katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Waziri tutakupa ushirikiano sana. Naomba uje Kishapu, tena mama mwenyewe, nikupeleke mpaka Itongoitale….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, tunashukuru. Muda wako umekwisha!

**MHE.SULEIMANI N. NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, *oweja* sana, lakini sitaunga mkono hoja mpaka atakapokuja…

**SPIKA:** Sasa naomba uchukue kitabu chako cha kanuni, usome kanuni ya 101(3) na (4). Usiniombe mimi kukataja wakati wa mshahara wa Mheshimiwa Waziri, kuna utaratibu uliowekwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwanri.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara, wafanye maboresho ya kupunguza urasimu uliokithiri katika utoaji wa hatimiliki, muda mrefu sana unatumika katika kutoa hatimiliki za maeneo husika. Hali hii ya urasimu unakwamisha uwekezaji na maendeleo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hatimiliki zinazotolewa na *CDA* ni za muda mfupi sana, hivyo zinakwamisha uwekezaji katika Mji Mkuu wa Dodoma. Kwa sababu ya muda huu mdogo wa miaka 33, wawekezaji wanasita kuja kuwekeza Dodoma. Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na hili?

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi ya ardhi yaliyokwishapimwa na *CDA* Mkoani Dodoma, yana mgogoro mkubwa na wananchi (wakulima) hususani maeneo ya Makulu Dodoma. Mingi ya migogoro hii haijatatuliwa na *CDA* kati yao (kama wapimaji) na wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, wananchi waliopewa viwanja katika maeneo haya wanapambana na madai ya fidia wakidai kwamba maeneo haya yalikuwa ni mashamba yao tangu miaka mingi.

Je, migogoro hii ya ardhi iliyokwishapimwa na *CDA* na kugawanywa kisheria lakini baadhi ya wananchi wanayakatalia itakwisha lini?

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, hii ni nyongeza ya mchango niliotoa kwa maneno.

Naanza kwa kukupongeza wewe, Naibu Waziri Mheshimiwa George Simbachawene kwa kuchaguliwa kwake. Aidha, pole kwa kufiwa na Ami yake. Nawapongeza Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya na shutuma za rushwa zimepungua.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisisitize yafuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro wa Yaeda Chini, Mbulu, hali ni mbaya sana na inasababishwa na Bwana Geso Bajut, Diwani tajiri alijimilikisha ekari 3,902 akijifanya mwekezaji. Mtu huyo akishirikiana na Mkuu wa Wilaya Bwana Anatori Choya na Mwenyekiti wa Halmashauri na baadhi ya Madiwani wa Halmashauri hiyo wamepora ardhi ekari 3,902. Inawezekana amepata hatimiliki kwa njia isiyo halali. Kwa niaba ya wakazi wa Kata za Eskesh, Yaeda na Masieda. Waziri wa Ardhi atueleze uhalali wa umiliki huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi - Wilaya ya Mbulu. Nilichokisema kwenye mchango wangu wa kuongea ni kwamba tulikubali Baraza la Wilaya Babati ifungue *registry* Mbulu na Mwenyekiti atatoka Babati kwenda kuamua mashauri lakini kwa kuokoa gharama na kumaliza mashauri yaliyo mengi kwa muda mfupi bora kuanzisha Baraza la Wilaya Mbulu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia kazi za Wizara kwa mafanikio. Naomba haya yafuatayo yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupima ardhi na kupanga matumizi katika nchi nzima ni kazi kubwa.

Naomba kujua ni lini Serikali itaanzisha vikosi kazi katika kila Wilaya ili kusaidia upimaji wa maeneo yote kila Wilaya?

Mheshimiwa Spika, pili, Manispaa ya Dodoma ina maneno maneno na *CDA* ya muda mrefu. Naomba Serikali iwasikilize Waheshimiwa Madiwani, Mheshimiwa Mbunge ili waelewe tatizo lao na wasaidiwe ili maneno maneno hayo yaishe.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wilaya/Halmashauri zilipe madeni ya fedha walizokopeshwa za kupima viwanja ili na wengine wazikope.

Mheshimiwa Spika, nne, wanaodaiwa na *NHC,* Serikali iwahimize walipe ili waweze kuendelea na kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha mchango wangu katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni migogoro ya ardhi imetawala katika maeneo mengi nchini na kusababisha vifo na mali za mamilioni kupotea. Maeneo yaliyokithiri kwa migogoro hiyo ni Mikoa ya Manyara, Arusha na Morogoro ambako migogoro hiyo ni kati ya wakulima na wafugaji na katika maeneo machache ni kati ya wafugaji na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, binafsi naamini migogoro katika maeneo hayo inazungumzika lakini tatizo limekuwa ni baadhi ya viongozi kutofanya utafiti wa kina katika kutoa uamuzi, kuingiza siasa katika kuitatua pia kutumia nguvu nyingi za dola bila sababu za msingi. Viongozi ngazi za juu Serikalini kwa kujua au kutojua nini chanzo cha migogoro hiyo, wamekuwa wakiwaachia viongozi wa Serikali za Vijiji kutoa uamuzi au kutatua migogoro hiyo hata kama jambo ni zito ambalo linaweza kusababisha athari.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote yenye migogoro, kikubwa zaidi vijiji havijapimwa na ambavyo vimepimwa havina mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyoridhiwa na pande zote na kusababisha baadhi ya makundi kufikiri kwamba yana haki ya kutumia ardhi. Kibaya zaidi ni Serikali kujikita kutatua matatizo kila yanapotokea badala ya kuchunguza chanzo au kiini na kuzuia tatizo.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho naamini kingeweza kutatua migogoro ya ardhi ni sheria kufuatwa na kuwekwe mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa kuzingatia haki za wachache pia. Lakini ikiwa Serikali itaendelea

kutumia nguvu katika kutatua migogoro hii ya ardhi sidhani kama ufumbuzi wa kudumu unaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na migogoro hiyo, naamini kwamba hakuna mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao ni shirikishi na kama upo basi haufuatwi kwa sababu mbalimbali zikiwapo za kisiasa. Ni lazima Waziri atueleze hapa mpaka watu wangapi wauwawe ndio Serikali iweke mfumo bora wa kutatua migogoro ya ardhi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, upimaji wa ardhi eneo la Pugu. Wakazi wote wanaoishi Kata ya Pugu wanakaa katika maeneo ambayo hayajapimwa na hivyo kukosa haki ya msingi ya kupata hati za ardhi na nyumba ili kuwawezesha kukopa. Naomba Serikali iliangalie eneo hili ambapo kwa sasa limekuwa ni mji unaokuwa kwa kasi na kwa hali hii wananchi wanaweza kujikuta wanajenga hata katika maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya shughuli zingine za kijamii. Naishauri Serikali itoe mwongozo ni kwa namna gani wananchi hawa watapimiwa maeneo yao ili wajiandae.

Mheshimiwa Spika, pili, migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya Hifadhi. Kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi hasa kwa wananchi wanaoishi karibu na Hifadhi kutokana na kutokujua mipaka yao halisi au kupewa mipaka ambayo si asili. Wananchi wa Mkoa wa Singida mfano maeneo ya Manyoni/Itigi, Minyughe, Mgori, wanapata usumbufu mkubwa wa kudhalilishwa na Askari wa Wanyamapori pindi wanapochunga mifugo yao katika maeneo yanayodaiwa ni ya Hifadhi. Watu hawa tangu kuzaliwa wamekuwa wakiishi na kufanya shughuli zao katika maeneo yanayoitwa sasa ya Hifadhi. Kukosekana kwa elimu na mipaka halisi kunawafanya wananchi hawa kujiona ni wakimbizi katika nchi yao. Ni busara sasa kwa Serikali kupima maeneo haya upya ili kupunguza migogoro na udhalilishaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, mimi nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya tangu wameteuliwa kushika Wizara hiyo. Pamoja na changamoto nyingi sugu kama migogoro ya ardhi, wameendelea kufanya kazi kwa makini na waledi wa hali ya juu. Binafsi niko nyuma yao, wachape kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba leo nipate maelezo juu ya mgogoro wa ardhi wa kijiji cha Bunene Jimboni Mwibara ambayo ilivamiwa na JWTZ na kukaliwa kwa mabavu katikati ya kijiji. Nimekuwa nikipiga kelele hapa Bungeni lakini hadi leo sioni ufumbuzi au utatuzi wa mgogoro huo. Leo naomba nipate maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeingia katika migogoro mingi ya ardhi iwe Wilaya, Kata na Vijiji kutokana na kuchelewa kufuatilia na kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, UTT ni mwiba na imeleta migogoro mingi ya ardhi kwa kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za uchukuaji wa ardhi. UTT imeanzisha mradi wa upimaji wa ardhi Lindi na kuwadhulumu wananchi na kuchukua ardhi yao kwa bei ya Tshs.400,000/= tu bila hata kuwaonyesha wataenda wapi na bila kufuata *economic value* ya ardhi kwa sasa. Huu ni uonevu mkubwa kwa wananchi hawa. Wananchi hawajatendewa haki na wamepigwa na kudhalilishwa. Wizara ipo wapi juu ya uonevu huu? Nilileta barua ya malalamiko sikupata majibu yoyote. Je, hamuoni wananchi wanaonewa na Wizara wanachukua hatua zipi kutatua tatizo hili? Mgogoro wa ardhi Mitwere dhidi ya UTT ni hatari, naomba Wizara itamke maana hiki ni kilio cha wananchi, wasipuuzie maana inagusa maisha ya watu na amani itapatikana ikiwa haki za binadamu na ardhi yao itapatikana.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa UTT Lindi (Manispaa) ni tatizo kama ifuatavyo:-

(1) Baraza la Madiwani hawakushirikishwa.

(2) Wananchi walidanganywa kuhusu makubaliano ya malipo.

(3) Bei kuwa ndogo kupita kiasi Sh.400,000/= kwa eka.

(4) Malipo hewa kwa wasio na viwanja.

(5) Unyanyasaji, ubabe na dhuluma kutawala mradi nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu sahihi.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ardhi kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, naishukuru Wizara kwa kusikia kilio changu pale nilipoiandikia barua ya kuomba Wizara ya Ardhi kutenga fedha na kupima kila kipande cha ardhi katika Jimbo la Mvomero ili kukabiliana na migogoro ya ardhi ya wakulima na wafugaji. Nashukuru Wizara hii sikivu kwa kutekeleza zoezi la upimaji kuanzia Wilaya ya Mvomero. Kitendo hiki kilinipa amani na nampongeza Naibu Waziri Simbachawene kwa kufika Mvomero na kuzindua zoezi hili Kitaifa na Mvomero ikiwa ya kwanza, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pili, narudia ombi la kuwasaidia wananchi wa kijiji cha Sokoine wanaodai haki yao ya viwanja, wapewe kipaumbele na pia fidia yao sasa ni ya muda mrefu hata thamani imebadilika. Naomba malipo yao yafanywe, huu ni mwaka wa nane bado wanasubiri. Mheshimiwa Waziri, naomba majibu ya madai haya kwa wananchi wangu wa Sokoine ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya. Aidha, nakuomba ufike Sokoine.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba maeneo ya Ranchi za Kipanguni na Mkata na mapori yote yasiyoendelezwa likiwemo Pori la Kuni wapewe wananchi ili kuondoa migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba Wizara ishughulikie mipaka ya Wami Mbiki hasa vijiji vinavyopakana na Hifadhi hii hasa maeneo ya Mapangano (Mziha), Mlumbilo, Maflets (Kumke) na Lukenge. Naomba maeneo haya yaangaliwe kimipaka ili kuondoa unyanyaswaji wa wananchi wa maeneo hayo ili waendelee kufanya kazi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niishukuru Wizara kwa utoaji hati za kimila katika Wilaya yangu na naomba kazi iendelee ili kuwawezesha wananchi kiuchumi waweze kukopa fedha kwa kutumia hatimiliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 na 2012/2013 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haijatekeleza kikamilifu dhima ya kuweka mazingira yatakayoleta ufanisi katika utoaji wa huduma ya ardhi, nyumba na makazi katika muktadha wa masuala niliyohoji Bungeni katika mijadala iliyotangulia. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi haikutekeleza ahadi za Waziri ambaye ameendelea hivi sasa na hata za Naibu Waziri aliyekuwepo za kwenda nami Jimboni tushughulikie masuala niliyoyahoji. Aidha, Waziri hakutekeleza hata ahadi yake

tu ya kutoa majibu ya maandishi juu ya maswali na masuala niliyohoji pamoja na kuahidiwa mara mbili katika majumuisho ya bajeti ya Wizara mwaka 2012 na 2013.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo sioni haja ya kuchangia kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/20155 wakati ambapo majibu ya michango iliyopita hayajatolewa japo kwa maandishi. Hivyo naomba Waziri anipatie kesho tarehe 28 Mei, 2014 katika kipindi cha maswali, nakala ya kitabu cha majibu ya michango iliyotolewa Bungeni.

Kama kitabu/randama ya majibu ya michango hiyo siwezi kupewa nakala basi Wizara ipitie Kumbukumbu Rasmi za Bunge *Hansards* za 2012 na 2013 na kunipa majibu ya maandishi juu ya michango yangu ya masuala niliyohoji na mapendekezo niliyotoa kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kama sitapatiwa majibu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nitalazimika baada ya kipindi cha maswali kabla ya mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2014/2015 kuendelea kuchukua hatua za Kibunge nitakazoona zinafaa. Izingatiwe kwamba Hotuba ya Waziri na randama ya Wizara yote imetoa maelezo ya ujumla pamoja na majibu ya mapendekezo ya Kamati na si hoja za Wabunge mmoja mmoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa jitihada zake na kwa kazi nzuri anazofanya hasa nimshukuru kwa lile shamba letu la *Sisal Estate* Babati japo bado mambo si mazuri ndani ya Halmashaur, lakini nimpongeze kwa kuwa ametimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba anisaidie kuhusiana na Mwanasheria wa Halmashauri ya Mji wa Babati aliyenyang'anya kiwanja cha Bwana Mchana (Mwalimu Mstaafu) ambaye shamba lake lilichukuliwa na Halmashauri bila yeye kulipwa fidia na cha kushangaza Halmashauri ikishirikiana na Mwanasheria Bwana Reginald Mtei na kumruhusu ajenge nyumba bila mmiliki wa awali kulipwa fidia yake. Mwalimu Mchana amekwenda Polisi hakusikilizwa, kwa Mkuu wa Mkoa, Wilaya akapuuzwa. Naomba Mheshimiwa Waziri asitishe ujenzi huo batili maana wengine wote wanamwogopa Mwanasheria huyo na amekuwa tatizo kubwa Babati.

Mheshimiwa Spika, tatu, wale wananchi wengi wa Gijedabuu Ayamengo bado wananyanyaswa na Hifadhi ya Tarangire. Mkuu wa Mkoa aliahidi atamwona Rais tangu Februari, 2014 ili abatilishe mipaka hiyo mipya ya Hifadhi ya Tarangire. Naomba Mheshimiwa Waziri aulize huko kwa Rais kama kapata ombi hilo ili tuwasaidie wananchi wale.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba Waziri afute umiliki wa shamba la *Singu Estate,* Kata ya Sigino Babati kwani mwekezaji yule hana anachofanya zaidi ya kuwakodisha wananchi wakati wananchi hao walishajenga kwenye maeneo hayo tangu miaka 1970. Hivyo leo kuwaondoa ni kuwasumbua tu na kuleta vita na ugomvi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tano, wananchi wa Kata ya Kiru, Babati bado wana ugomvi mkubwa na wawekezaji ni majuzi tu walichoma trekta na mali za mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho nategemea Waziri atanipa majibu yanayoleta matumaini, ahsante.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani na Wilaya ya Korogwe Vijijini kwani katika Tanzania Bara Wilaya ya Korogwe Vijijini imezungukwa na mashamba ya mkonge, chai na sufi. Waziri ameombwa aje aangalie maeneo ya ardhi kwa sababu wakulima hawana mahali pa kulima.

Mheshimiwa Waziri ametembelea Mkoa wa Tanga wote ila Wilaya ya Korogwe hakufika, kwani Wilaya hii haipo Tanzania, wananchi wametengwa sana. Sasa Serikali ina mpango gani na Wilaya hii kwani sehemu nyingine Serikali imeshatoa maamuzi. Naomba Serikali iangalie upya Wilaya ya Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote kwa ujumla kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa viwanja maeneo maalum ya miji ya mipakani kama Tunduma, Isongole, Ileje na kadha wa kadha. Mji wa Isongole ambao ni mpaka wa Malawi na Tanzania unazidi kuharibika kwa ujenzi holela usio na mpangilio, kwa nini Wizara haifanyi juhudi za kunusuru uharibifu huo?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bwawa katika Mto Songwe eneo la Bupigu, Ileje. Bwawa hili liliazimiwa kujengwa kwa lengo la kudhibiti tabia ya Mto Songwe kuhamahama kati ya Tanzania na Malawi.

Kwa kuwa wananchi wa eneo la Bupigu, Ileje wako katika hali ya sintofahamu ya kuhama eneo lile au la kwa kuwa mradi unaonekana kama vile umeahirishwa, naomba kauli ya Serikali ili wananchi waendelee kujenga nyumba za kudumu au waendelee kusubiri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi ni Wizara mama kwa kuwa kila shughuli inayofanywa hufanywa juu ya rasilimali hii. Je, ni kwa nini Wizara ya Ardhi ikipima viwanja Wizara ya Ujenzi ndio *supervisor* kuliko Wizara ya Ardhi na kufanya maamuzi ambayo yanawafanya wananchi wasielewe nani wa kumsikiliza kati ya mamlaka hizo mbili?

Mheshimiwa Spika, gharama za kupima na kulipia viwanja, mara kadhaa wananchi wanalalamikia gharama ambazo zinaonekana kupanda bila wananchi kupata au kuwa na taarifa. Nashauri bei za viwanja na gharama za kulipia viwanja zibandikwe katika mbao za Halmashauri.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi, nichangie hotuba ya Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi. Wizara ya Ardhi inabeba sekta karibu zote zinazowezesha wananchi kuendeleza shughuli za kila siku ikiwemo kuendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Wizara hii ni kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati yake na Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa. Udhaifu katika utawala ngazi hii kwa kiasi kikubwa umechangia ongezeko la migogoro ya ardhi. Uuzaji na uporaji wa ardhi na umilikishaji usiozingatia hali na maslahi ya wananchi wanyonge yamekuwa yakifanyika wakati Mamlaka hizi zikiangalia. Hii inatokana na kuwa ni jambo la makusudi au kwa kutokuwa na mamlaka na uelewa kisheria.

Wananchi katika ngazi za vijiji wamekuwa wakinyanganywa ardhi, sheria zinazosimamia ardhi zinakiukwa na hakuna linalofanyika. Muhimu hapa ni kuwa ngazi hii ya utawala iliyo karibu na wananchi iwezeshwe na kushirikishwa ili iweze kudhibiti ukiukwaji wa sheria katika hatua ya awali. Njia rahisi ya kujaribu kupunguza tatizo hili ni Mamlaka zaidi kama *WDC*, Kamati za Madiwani, Mkurugenzi wa Wilaya na *DC* wanaweza kushirikishwa katika mchakato wa kuuza na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe tena malalamiko ya wananchi wa Kata ya Rutoro juu ya mgogoro wao na *NARCO*. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iliagiza mahasimu katika suala hili watulie wakisubiri uamuzi wa Serikali. Pamoja na agizo hili wafugaji wa wale wanaokodishwa kuchunga katika vitalu kupitia wachungaji wao (Wanyarwanda) wamekuwa wakiwanyanyasa wananchi. Vitendo vya wachungaji kulisha mifugo kwenye mashamba ya wananchi ni jambo la kawaida, wafugaji wanawazuia wananchi kulima na kuwazuia kufuga mbuzi na kuku, hivi ni vitendo vya unyanyasaji hali inayokiuka agizo la Serikali kupitia Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la mahusiano mabaya kati ya Kambi ya Jeshi Kaboya na vijiji vinavyozunguka Kambi hiyo, tatizo hapa ni mipaka na matumizi ya vyanzo vya maji. Naishauri Wizara isaidie kwa kusuluhisha tatizo hili haraka ili wananchi wajue hatima yao. Aidha, wakati Serikali haijabainisha ni maeneo gani itayachukua toka vijiji jirani basi wananchi waruhusiwe kulima mazao ya muda.

Mheshimiwa Spika, katika kutenga mipaka ni busara vyanzo vya maji vibaki wazi kwa wadau wote – Jeshi na wananchi. Endapo Jeshi linazuia wananchi kuingia kwenye vyanzo vya maji basi utaratibu uwekwe ambapo maji yatasukumwa kwa pampu kwenda kwenye sehemu salama kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii nami niweze kuchangia machache katika Wizara hii muhimu sana. Hakika suala la ardhi limekuwa na migogoro mingi sana katika maeneo yetu na kwa vile suala hili ni suala mtambuka linahitaji ushirikishwaji wa dhati wa Wizara nyingine kama vile Maliasili na Utalii, Nishati na Madini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni suala lisiloepukika kuwa wananchi wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki. Lipo wimbi la vijana kuhamia mijini lakini ikumbukwe kuwa hata vijijini idadi ya watu wanaongezeka kila kukicha, bado ufugaji uliokuwa ukifanywa kipindi kile sio wa sasa na hali ya maisha imebadilika.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muhimu sasa kuona kama uhitaji wa kupima viwanja mijini ni muhimu kuona uhitaji wa kuyatambua maeneo ya vijijini yale ambayo yametelekezwa yagawiwe kwa wananchi ili wayatumia kwa matumizi endelevu. Hapa naomba niongelee eneo la pori la Hifadhi la Busigi/Kimisi. Eneo hilo lilikuwa pori la akiba lakini sasa hakuna wanyama wa kutosha. Ningeomba Serikali ione ni jinsi gani ya kumega sehemu ya pori hili na kuligawa kwa wakulima au wafugaji ili kuondoa kero hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la mipaka ya ardhi kati ya Wilaya na Wilaya pia na sehemu zinazopakana na Hifadhi. Jimbo langu limekuwa na mgogoro huo kwa muda mrefu sana hususani katika kijiji cha Nyantimba mpakani na Wilaya ya Chato. Kijiji hiki kimemegwa na kupelekwa Wilaya ya Chato ilhali mipaka na alama zote zimetambuliwa na wataalam kuwa kijiji hiki kipo Jimbo la Bihalamulo Magharibi. Naomba sasa Wizara hii itamke wazi kijiji hiki kipo wapi ili wananchi wajue wanawajibika wapi ili kupata huduma zao za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la mipaka kati ya kijiji cha Kariha na kijiji cha Mpago. Hali hii imeleta kutoelewana kwa wananchi na Serikali yao. Haiwezekani wananchi wameishi kwa muda mrefu lakini leo hii wanaambiwa kuwa wanaishi katika eneo la Hifadhi. Naomba Wizara hii iwahakikishie wananchi hawa utulivu katika maeneo yao ili waweze kuzalisha mali na kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Ni wakati sasa Wizara kuondoa kero hizo ikishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii pia Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba lianzishwe Baraza la Ardhi Wilayani Bihalamulo ili kuwapa nafuu wananchi ambao wanadai haki zao. Baraza lililokuwepo lipo Chato ambalo sasa lipo Mkoa wa Geita na si Kagera tena.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niunge mkono hoja ya Wizara hii. Nianze kwa kuishauri Wizara hii juu ya umuhimu wa kupima ardhi katika nchi hii, kwani Watanzania wakitaka kupata maendeleo ya haraka ni Serikali kutenga *budget* ya kutosha kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi mingi inasababishwa na kutokupima ardhi. Naomba sana Serikali iangalie kupata nafasi ya kipekee ili tuweze kutatua migogoro hasa ya Wakulima na Wafugaji. Suluhu pekee ni kuipima ardhi na kutenganisha maeneo ya Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpanda, 70% ya ardhi imemilikiwa na Serikali kwa maana ya Hifadhi ya Katavi na *Game Reserve* na Hifadhi za Misitu. Wananchi wengi wa Mkoa huu hawana mahali pa kufanyia shughuli za kilimo. Naiomba sana Serikali iweze kuangalia upya juu ya ardhi ya Mkoa wa Katavi kuigawa kwa Wananchi ambao kwa sasa idadi yao ni kubwa kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwaombe sana Wizara wawaangalie Maofisa wa Ardhi waliopo Mpanda, juu ya ugawaji wa ardhi hasa kwenye mashamba ya Kijiji cha Kabage, ambako kulishatokea mauaji ya Wananchi yaliyosabishwa na Maofisa hao kupora ardhi ya Wanakijiji na kujimilikisha. Kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu, naiomba Serikali itafute ufumbuzi wa mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote, kwa Hotuba iliyoletwa mbele ya Bunge letu. Pia napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuteuliwa kuchukua nafasi hii; Mungu akusaidie.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii kulenga kila eneo, bado bajeti wanayopewa ni kidogo kwani naamini hawawezi kutekeleza kwa asilimia mia yote waliyojipangia. Tatizo la kutopatiwa pesa kwa wakati na kutofikia kiwango cha pesa walichoomba kwa bajeti inayoishia mwezi tu inaisha, ni changamoto kubwa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali katika kutatua kero baina ya Wakulima na Wafugaji, Wanakijiji na wachimba madini katika nchi yetu. Matatizo haya kwa asilimia kubwa yamechangiwa na Halmashauri zetu. Kuna baadhi ya sheria ndogo za Halmashauri, ningeomba Wizara iwashauri Viongozi wa Halmashauri zetu, sheria kama ya kufuga mifugo kama ng'ombe watano. Sasa kwa mfugaji anafurahi anaomba eneo la ekari kumi kwa kufuga ng'ombe watano, lakini baada ya miezi analeta mifugo yake toka alikotoka na kuanzisha zogo au ugomvi. Sheria kama hii ndogo ndiyo chanzo kikubwa cha mizozo katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Mashamba ya Mikonge yanayomilikiwa na Halmashauri zetu, ambayo mengi yamekuwa mapori kwa sababu yanamilikiwa na Halmashauri, kama ya Wilaya yangu ya Kilosa. Naomba Wizara iangalie ili Wananchi waweze kunufaika na mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kuhusu kodi ya ardhi ya mashamba; kwa kweli kodi hii ni kubwa sana. Naomba Serikali iangalie kwa makini kwani inawaathiri baadhi ya wamiliki wa mashaba hayo. Naomba Wizara iweke kiwango kwa mafungu kama vile kuanzia ekari mia hadi mia tano kiasi fulani, mia tano hadi elfu moja kiwango chake na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nawatakia kila la kheri.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu maendeleo ya ardhi, nyumba na makazi.

Hata hivyo, bado zipo changamoto mbalimbali katika Sekta ya Ardhi hasa suala la upimaji wa ardhi na matumizi endelevu ya ardhi hiyo na upungufu wa Wataalam wa Ardhi na vifaa katika Halmashauri za Wilaya na hasa kwa Wilaya mpya kama ilivyo Wilaya ya Mbogwe. Suala la mipango miji na ujenzi holela wa majengo mijini na vijijini ni changamoto kubwa kwani nyumba zinajengwa ovyo mijini na kuondoa kabisa dhana ya mipango miji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya Mbogwe imeanzishwa ikiwa na maeneo mengi ya wazi ambayo hayajavunjwa; ni vyema Serikali itupatie Wataalam na vifaa ili Wilaya yetu isije ikavurugika. Tunaomba tupatiwe *Master Plan* ya Mji ili kutoa fursa ya kuwa na mji mzuri uliopimwa.

Mheshimiwa Spika, Shirikila la Nyumba la Taifa lipewe uwezo wa kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Mbogwe. Migogoro ya Wakulima na Wafugaji inayopelekea mauaji kwa raia wasiokuwa na hatia ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, suala la Rushwa katika Vitengo na Watumishi wa Idara za Ardhi maeneo mbalimbali nchini ni jambo la kusikitisha kuona kwamba, maeneo machache yanapimwa halafu Wananchi wanaohitaji viwanja wanakuwa wengi na kuanza kupikuana na kunakuwa na *double allocation* ya viwanja. Ni vyema suala la upimaji ardhi nchini kiwe kipaumbele namba moja. Kwa kutoa kipaumbele kupima ardhi, tutakuwa tumeingia katika historia ya kimapinduzi ya kuwa na miji iliyopimwa, yatakuwa ni mapinduzi ya kipekee.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka na timu yake yote, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha Sekta hii ya Ardhi, Nyumba na Makazi inaleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji na Wakulima na Wawekezaji ni ishara tosha kuwa, nchi yetu sasa inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa ardhi inayotokana na kuongezeka kwa watu na mifugo. Mfano, wakati tunapata Uhuru, Watanzania walikuwa milioni tisa, mwaka 1990 milioni 24, mwaka 2013 watu zaidi ya milioni 45. Kutokana na ongezeko hilo, mtu anahitaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapata Uhuru ng'ombe walikuwa milioni tisa, sasa milioni 25; nusu ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, eneo la ardhi kwa ajili ya uzalishaji limepungua kutokana na tabianchi. Mfano, baadhi ya visiwa vinazama kama kule Pangani na kadhalika, maeneo ya kilimo kama Isimani yamekufa, Kibaigwa eneo la kulima sasa ni zao moja tu la alizeti ndilo linalokubali.

Kwa hiyo, inabidi Wananchi wa maeneo hayo wahamie maeneo mengine kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipime ardhi yote kwa kuwashirikisha Wananchi kwa matumizi mbalimbali ya ardhi. Serikali iongeze fedha kwa ajili ya upimaji kwa ardhi, ipunguze maeneo ya kulishia mifugo, wafugaji wafuge kisasa na elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora itolewe.

Mheshimiwa Spika, rushwa kwa baadhi ya wafanyakazi wa ardhi wakati wa kutoa viwanja na gharama za kupima viwanja ziangaliwe upya ili na wananchi wa kipato cha chini waweze kupima mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafanyakazi wa ardhi wamekuwa wakitoa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja. Wamekuwa wakijigawia viwanja wao wenyewe na jamaa zao.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kutenga maeneo ya ardhi na kuyapima na kuwakabidhi vikundi vya wanawake na vijana kwa matumizi ya kilimo. Baadhi ya Halmashauri nyingi hapa nchini wameshindwa kutekeleza mpango huu kwa tatizo la kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kazi hii.

Ningependa kujua Serikali Kuu inawasaidiaje Halmashauri za Wilaya kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huu wenye nia njema kwa ajili ya kuwakomboa Wanawake na Vijana?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya ya kupima ardhi katika baadhi ya maeneo, bado ipo haja Serikali kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuongeza fedha kwa ajili ya zoezi la upimaji wa ardhi mijini na vijijini kwa sababu fedha ambayo imekuwa inatengwa, haitoshi kupima ardhi maeneo ya mijini na vijijini kwa matumizi mbalimbali.

Pili, kuongeza fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa ardhi na kuajiri wataalam wa sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua wakati Waziri atakapokuwa akihitimisha hoja yake, nipate majibu ya mkakati gani uliowekwa na Serikali kuhakikisha mashambapori yaliyogawiwa kwa wawekezaji au kuuzwa kwa Wananchi kwa matumzi ya uwekezaji wa kilimo na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha yale mashambapori yaliyokaa bila kutumika yanamilikiwa na mtu mmoja mmoja au kampuni yanarudishwa kwa Wananchi ambao hawana maeneo ya kilimo na kwa matumizi mengine?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kufuta hati za wamiliki wa ardhi katika maeneo ya Mkoa wa Arusha, Tanga - Muheza, Morogoro, Kilosa, Mvomero, Kilombero na kadhalika?

Je Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza sera ya kuwezesha Wanawake na Vijana kwa kupimiwa ardhi na kutoa kwa vikundi vya vijana kwa matumizi ya kilimo na kadhalika?

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kupima ardhi kwa ajili ya Wakulima na Wafugaji? Pia ningependa kujua ni shilingi ngapi zimetengwa katika bajeti hii kwa utekelezaji wa zoezi hili?

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inapanga miji vizuri ili kuondoa tatizo la matumizi holela ya ardhi na ujenzi holela hasa katika miji mipya ya Wilaya mpya?

Je, Serikali itapima na kupanga maeneo ya kilimo, miji ya viwanda, miji ya kibiashara, miji ya vyuo na kadhalika?

Je, ni lini Serikali itapima maeneo ya Shule na Taasisi zote za Serikali na kuyapatia hati miliki?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwe na Sera na Sheria ya Tozo ya Kodi ya Nyumba zinazopangishwa kwa wananchi maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. NEEMA MGAYA HAMID:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara hii ni ngumu na ina changamoto nyingi, lakini mnajitahidi na mnafanya vizuri kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, shida ipo kwenye utolewaji wa hati. Kuna shida kubwa sana ya kupata hati kwa wakati. Kuna hivi viwanja vinavyotolewa na Serikali kwenye Manispaa mbalimbali, utakuta kupata hati ya kiwanja inachukua miaka mitatu, minne. Kwa nini hati ya kiwanja kilichotolewa na Serikali ichukue miaka minne? Hili ni tatizo kwenye Ofisi za Ardhi Mawilayani na ninao mfano.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu ina maeneo ambayo kuna mashamba yanamilikiwa na Wazungu kwa hati za muda mrefu. Hata hivyo, kumeibuka mgogoro kati ya Wananchi walio pembezoni mwa maeneo hayo na Wawekezaji au Wazungu hao. Wananchi wamenyanyasika sana, wanatungiwa kesi za uchochezi kisa wanadai haki yao ya kumiliki ardhi na hasa kwa kuwa wamekaa hapo (katika maeneo hayo

takribani miaka 20). Ni aibu kwa nchi ambayo Wananchi wake wananyanyasika ilhali kuna Serikali, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali.

Matatizo haya yapo katika Kata za Daa, Oldeani, Wilayani Karatu. Je, ni lini sasa Wizara itakaa na Wananchi hao ili kutatua matatizo hayo?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwaondoe watu wote waliopimiwa viwanja ndani ya eneo la Msitu wa Kazimzumbwi. Naiomba Serikali ibainishe wazi kwamba, eneo linalojengwa Chuo Kikuu cha Mlonganzila ni eneo la kubwa zaidi ya 80% liko Kisarawe.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze kwa kazi nzuri mnayofanya katika nchi yetu. Ombi langu kule Makambako kuna eneo tulipima na michoro ipo Wizarani toka mwaka jana haijapitishwa, watu wanashindwa kuendelea na ujenzi, tunaomba kuharakisha ili watu wawe wanakopesheka. Nategemea hili litafanyika.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa mipaka katika vijiji vingi vinavyopakana na *Lwangi Game Reserve* vilivyoko Jimbo la Nkasi Kusini. Vijiji hivi ni vya asili, vilikuwepo hata kabla ya kuanza Mbuga yenyewe na wanazo hati katika vijiji hivyo vyote.

Kwa kuvitaja ni Kijiji cha Mtapenda Kata ya Isale, Kijiji cha Kasapa Kata ya Sintali, Kijiji cha King'ombe Kata ya Kala, Kijiji cha Mlambo Kata ya Kala, Kijiji cha Ng'undwe Kata ya Wampembe na Kijiji cha Namansi Kata ya Ninde.

Mheshimiwa Spika, Wananchi hawa wanasumbuliwa na utatuzi ni kupima tu. Naomba ardhi ipimwe Wilaya ya Nkasi.

Pamekuwepo hali ya migogoro ya ardhi katika vijiji vinavyopakana na Shamba la Mwekezaji SAAFI lililopo Kijiji cha Nkundi. Katika vikao mbalimbali vya Mkoa na michango katika Wizara hii, nimekuwa nachangia kuwa, Serikali iongee na Mwekezaji huyu ili kufanya mazungumzo ya kuomba kiasi cha ardhi kitolewe kwa Wananchi wanaozunguka katika Vijiji vya Kalundi, Nkundi na Sintali na Shamba ni kubwa halitumiki lote.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Kalambo Lanchi lina changamoto nyingi ambazo kwa sasa zinarudisha nyuma maendeleo yake; mojawapo, watumishi wachache, tunaomba Serikali ipeleke watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Shamba hili sehemu yake ilibinafsishwa kwa Wafugaji. Serikali iangalie baadhi ya Wafugaji ambao hawajatimiza masharti waliyopewa katika kuendeleza vitalu vyao wanyang'anywe na ardhi igawiwe kwa Wananchi wa Vijiji vya jirani kama Mkomanchindo, Kasapa na Kate.

Mheshimiwa Spika, lengo lake ni jema, lakini inaonekana kwenye ngazi ya Kata ni kichaka cha rushwa hasa wanaopenda kutembelea maeneo yenye migogoro na kesi haziishi bila rushwa. Wananchi wamechoka na rushwa, Serikali itafute namna nzuri ya kudhibiti ubora wake. Mabaraza pia yaanzishwe katika Wilaya au kuruhusu Mahakama za Wilaya na Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni mali ya msingi kwa kila raia. Zipo nchi ambazo suala la ardhi wamefaulu kuliko sisi. Nashauri nchi iboreshe na kila mzawa awe na ardhi yake na mfano wa Dubai katika kuwekeza kwenye ardhi utumike, ambapo kila mtu ana ardhi na Serikali hairuhusu kumpatia mgeni Ardhi kwa maana hakuna ardhi isiyomilikiwa. Kila mwekezaji atashirikiana na mzawa au raia, hakuna ruhusa mwekezaji kuwekeza kwenye ardhi kwani ardhi ndiyo mchango wa raia katika ushiriki wa uwekezaji. Ardhi ipimwe igawiwe kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, hati za ardhi ni gharama ambapo siyo rahisi mtu wa kawaida kupata, ndiyo maana kupimwa ardhi kumekuwa shida. Tafadhali pungezeni urasimu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pamoja na kuwa na bajeti finyu, lakini ina changamoto nyingi sana hususan suala zima la migogoro ya ardhi. Ningependa kupatiwa ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa agizo linalohusiana na maeneo yasiyopimwa, Hati za Makazi zitumike na zitambulike. Ilifanya hayo kwa makusudi ya kusaidia Hati hizo hata katika kusaidia kuwekwa dhamana ya malipo katika Taasisi za Fedha ili Mwananchi aweze kufaidika na rasilimali aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa baadhi ya Taasisi bado hazikubali. Je, Serikali inaweka mkakati gani kukabiliana na hili ili Wananchi waondokane na changamoto hiyo?

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa nini hati hizi zinawekwa muda kidogo wa umiliki; kwa nini zisipatiwe miaka kuanzia kumi ili zile zinazokubali kukopesha kwa dhamana ya hati hizi waweze hata kukopa mikopo ya muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, hapa tatizo kubwa sana na hasa katika Halmashauri zetu, Serikali imekuwa ikiitwa maeneo ya Wananchi kwa ajili ya kuyapima, lakini Wananchi hawafidiwi. Malipo yanachukua muda mrefu sana, kiasi kwamba, yatakapolipwa thamani ya eneo inakuwa imepanda.

Jambo lingine, mtu anachukuliwa ardhi yake anapata mgawo wa kiwanja kimoja wakati familia nyingine wapo watoto zaidi ya kumi, jambo hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa kubadili matumizi ya ardhi hii ni changamoto kubwa sana katika Halmashauri. Tumekuwa tukileta katika vikao na kufanya manunuzi ya kubadili matumizi lakini kunakuwa na urasimu mkubwa sana. Naomba Serikali ijipange kwa changamoto hii, iweze kuangalia njia mwafaka ya kurahisisha ubadilishaji

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba, Mr. Chechu, kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akifanya katika Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya mauzo yanayofanywa ya nyumba zinazojengwa na Shirika; kwa sababu tunategemea nyumba hizo ziwanufaishe Wananchi wote. Kutokana na kipato cha Mwananchi wa kawaida, hataweza kununua nyumba hizo na mbaya sana kuna Wananchi wengine ni wastaafu hawawezi kukopesheka hata kama atalipa kwa zaidi miaka kumi. Nini mkakati wa Serikali wa kushirikisha na kuwasaidia Wananchi wa kawaida waweze kununua pia.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, ni makosa makubwa kwa Serikali kuendelea na tabia ya kuwa na watumishi wachache wa Wizara nyeti kama hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ichukue hatua za lazima kuanzisha mafunzo ya kuwapata Wataalam wengi wa Ardhi kama ilivyoamua katika kuwapata walimu wengi, ilipoamua kuanzisha elimu kwa wote UPE, ikaamua kufungua Vyuo vya Ualimu nje ya Vyuo vya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikichukua hatua kama hizi, tatizo la Watumishi wa Ardhi litatoweka na hivyo Halmashauri, Manispaa na Majiji yetu, yatawapata watumishi wa kutosha, ardhi itapimwa na itatengwa na kugawiwa wahitaji kulingana na mahitaji ya kila Mwananchi.

Mheshimiwa Spika, ardhi ikipimwa na kutengwa kwa ajili ya kila mahitaji, hali ya uvamizi na migogoro itaisha mara moja. Migogoro baina ya Wakulima

na Wafugaji haitatokea kwa kuwa kila hitaji la mtumiaji ardhi litakuwa limetengwa maalumu kwa kila eneo.

Mheshimiwa Spika, ardhi ikitengwa na kugawiwa kwa Wananchi, watapata fursa ya kuimiliki ardhi yao kisheria. Wananchi wataweza kuikopea katika vyombo vya pesa na kuanzisha kilimo kikubwa kitakachochochea upatikanaji wa viwanda vidogo na vikubwa. Umaskini uliotokana na Wananchi kutoitumia ardhi kwa kiwango kinachotakiwa utaondoka ardhi hiyo ikipimwa na kugawiwa kisheria.

Mheshimiwa Waziri alione hili na katika kipindi chake cha kuhitimisha hoja zake, awaambie lini Serikali itaamua kuzitumia mbinu ilizozitumia katika suala zima la kuwapata walimu wengi kwa kufungua UPE hapa nchini. Pamoja na mambo mengine, Wizara iajiri watumishi wengi wa ardhi iliyo moyo wa uchumi. Naomba nipatiwe majibu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii muhimu. Kuhusu mipaka ya ndani ya nchi, kuna migogoro mingi sana imezuka kati ya Wilaya na Wilaya, Vijiji wa Vijiji na kila siku migogoro hii inazidi kupanuka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mgogoro wa mipaka kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge. Serikali ichunguze kwa makini *GN* zilizoibuka kwenye mipaka hiyo, kiasi cha kusababisha maeneo ya Kata za Mitundu na Kata za Mgandu za Wilaya ya Manyoni ziko upande wa Wilaya ya Sikonge, Kata ya Kipili. *GN* ya 1961 wakati tunapata Uhuru ilionesha wazi kuwa, maeneo ya Kijiji cha Makala na Kitongoji chake cha Matagata yako Wilaya ya Manyoni na pia maeneo ya Kijiji cha Kayui na Kata yake ya Mwamatiga yako chini ya Wilaya ya Manyoni. Cha kushangaza ni kwamba, kulizuka *GN* mpya miaka ya 1990 na 2000 ambayo 2009 imeweka Vitongoji vya Matagata na Mwamtiga Wilaya ya Sikonge (Kata ya Kipili).

Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu ya Wizara ni lini marekebisho ya *GN* hizi mpya yatafanyika ili Vitongoji hivi virudi Makale na Kayui? Mgogoro mpaka sasa unafukuta na Wananchi wa maeneo hayo wanaweza kuingia kwenye machafuko ya kupigana wenyewe kwa wenyewe.

Naishukuru Serikali kwa kupima ardhi ya Vijiji vya Sanjaranda na Kitopeni vya Kata ya Sanjaranda. Ninaomba upimaji ufanywe pia kwa Vijiji vya Kata za Ipande, Itigi, Majengo, Kitaraka, Idodyandole, Mgandu, Aghondi, Mitundu, Mwamagembe na Rungwa. Kupimwa kwa vijiji viwili tu vya Kata ya Sanjaranda, imezua malalamiko mengi kutoka Kata zisizopimwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ichukue hatua kwa kutenga fedha za kutosha ili maeneo hayo yapimwe na kuepusha migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kuchangia Wizara hii.

Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kutatua tatizo sugu la mgogoro wa ardhi wa Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto za Wizara hii ni kuongezeka kwa kasi kubwa ya migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi, Serikali na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapotoa majumuisho anisaidie suala hili la Kondoa. Nianze na mgogoro wa Itaswi. Kijiji hiki cha Itaswi kilipimwa na kutengewa maeneo ya matumizi mbalimbali. Kuna mgogoro baina ya Wananchi na eneo lililotengwa kwa malisho ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro umeleta mtafaruku mkubwa pamoja na Tume kufika huko kupokea taarifa ya Mkuu wa Wilaya, bado watu wanateseka na haki ni yao. Viongozi wa Wilaya akiwemo Mkurugenzi na wenzake hadi Mkuu wa Mkoa na Wananchi, walipochoshwa wakachoma vifaa vyao na ndipo wakakamatwa na kufunguliwa shitaka, lakini wao wasingeenda kulima kwenye eneo lililotegwa la malisho, ingetokea hayo. Naomba Wananchi wapatiwe haki zao.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Mkong'onero bado pamoja na Tume kuwepo, Wananchi wanateswa hawatakiwi kufika eneo hilo wakati wao Viongozi hufika huko na madini yanachimbwa. Sasa cha ajabu, kama hilo ni Pori la Akiba mbona linatumika kwa manufaa yao tu si wawape fidia Wananchi wale?

Mheshimiwa Spika, kuna unyanyasaji mkubwa wa kutoa haki za viwanja Kondoa; kwa mfano, kuna bwana moja anaitwa Omolo, alijenga karibu na Polisi, Magereza na Benki, Wilaya ya Kondoa, aliporwa na nyumba yake kuvunjwa na sasa kapewa Mkurugenzi wa Wilaya kajenga eneo hilo. Je, amejenga kwa kigezo gani na huyo katolewa kivipi; kuna uonevu mkubwa mno?

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa Hotuba nzuri na kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kazi inayofanyika, matokeo tunaona, lakini Wizara ina changamoto sana na bajeti finyu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona Wizara kubwa na nyeti kama hii, inapangiwa bajeti kidogo na hata fedha zinazotengwa hazipelekwi. Bajeti ya mwaka 2014/2015 ni ndogo mno, haiwezi kutatua changamoto nyingi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, nashauri bajeti hii irudishwe kwenye Kamati ya Bajeti. Bajeti ya Maendeleo iongezwe na Waziri wa Fedha atakapokuja kusoma Bajeti ya Serikali lazima atueleze ameongeza kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa umaskini na kuwapa watu makazi bora, enzi za Mheshimiwa Chiligati akiwa Waziri, walihamasisha tuanzishe Ushirika wa Nyumba, ili uwasaidie kwa pamoja na kupata misaada kutoka nje (Nje ya Ushirika), wasaidiane kujenga nyumba.

Mheshimiwa Spika, hadi leo hakuna miongozo yoyote iliyotolewa kwa vikundi hivi kuhusu miongozo na mahali pa kupata mikopo ya muda mrefu ya masharti nafuu

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri atueleze hivi vikundi sasa vifanye nini vipate miongozo na fedha?

Mheshimiwa Spika, kwa nini ukiomba hati ya kiwanja inachukua muda mrefu sana hata zaidi ya mwaka? Mna utaratibu gani wa kupunguza huo muda?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza; Mheshimiwa Waziri na Viongozi wa Wizara kwa kujenga mfumo na mwelekeo mpya wa kurejesha hali ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuwa bora na ya kuimarika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuyafanyia kazi mapungufu makubwa na ya muda mrefu ya migogoro ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya kufuta hati za mashamba ya Mkonge yasiendelezwe katika Wilaya ya Muheza. Zaidi ya miaka nane sasa Wilaya ya Muheza ilikamilisha utaratibu wa kuomba hati za mashamba ya Kibaranga, Bwembwera, Kwafungu, Azimio, Songa na Mbambara. Nashauri kwamba yafutiwe hati miliki baada ya kuachwa bila kuendelezwa kwa zaidi ya miaka 36 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2000 Mawaziri wote wa Ardhi wamekuwa wakitoa majibu Bungeni kwamba maombi ya kufutwa hati ya mashamba ya mkonge yasiyoendelezwa yapo mezani kwa Mheshimiwa Rais ili hati hizo zifutwe. Hadi leo tarehe 28 Mei, 2014 zoezi hilo halijakamilika. Mwezi Machi, 2014 wakati Mheshiiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa ziarani Muheza alimpigia simu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi juu ya maombi ya Wilaya ya Muheza na katika Mkutano wa hadhara akawaahidi tena wananchi wa Muheza kuwa hati hizo zitafutwa.

Je, ni lini hatua hiyo itakamilika?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu haki za kisheria kuhusu wananchi waliotumia Ardhi iliyoachwa bila kuendelezwa kwa zaidi ya miaka 36.

Mheshimiwa Spika, kutoendeleza ardhi yenye hati kwa muda mrefu kunatoa nafasi kwa wananchi wanaoishi maeneo jirani na ardhi hiyo kushawishika kutumia ardhi hiyo.

Je, sheria inasema nini juu ya wananchi hao ambao wengi wamepanda mazao ya kudumu kama vile michungwa, miembe na ujenzi wa nyumba ndani ya ardhi hiyo iliyoachwa licha ya kwamba hati ya awali haijafutwa?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kufutwa kwa hati ya shamba la mkonge la Kumburu na kupewa mwekezaji mpya na hati mpya. Niliuliza kuhusu utaratibu uliotumika kufuta hati iliyokuwepo kabla ya hati mpya kati ya mwaka 2002 – 2004. Hadi leo tarehe 28 Mei, 2014 sijapata jibu. Wakati hati mpya ya shamba hilo la Kumburu inatolewa, shamba hili liliachwa bila kuendelezwa kwa muda mrefu na hivyo wananchi kutumia ardhi hiyo kwa kupanda mazao ya muda mfupi na mazao ya kudumu kama michungwa, miembe, minazi na kujenga nyumba.

Bila kujali haki ya kisheria kati ya ardhi kutoendelezwa na kutumiwa, ardhi iliyotelekezwa na hati mpya haikutoa eneo lililotumiwa na wananchi kwa zaidi ya miaka 20 na badala yake kujumuisha maeneo hayo katika hati mpya na hivyo kukaribisha migogoro kati ya mwekezaji mpya na wananchi.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake hivi karibuni katika eneo la shamba hili la mkonge la Kumburu yametokea mauaji kati ya wafanyakazi wa mwekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali haioni ipo haja ya kutumia hekima na busara kuondoa migogoro ya aina hii kati ya wawekezaji na wananchi? Je, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilihusishwa vipi katika kuuzwa na kufutwa hati ya awali na kutolewa hati mpya kwa mwekezaji mpya mwaka 2002 – 2004?

Mheshimiwa Spika, kufutwa kwa hati ya shamba la Kibaranga wakati wa kutaka kuhifadhi eneo la msitu wa Derema – Amani Wilaya ya Muheza, wananchi 1028 waliondolewa na kulipwa mazao yao kwa ahadi ya kupewa ardhi katika shamba la Kibaranga. Tangu fidia ilipwe miaka 10 iliyopita hadi sasa, wananchi hao hawajapatiwa ardhi. Kwa nini hati hiyo isifutwe ili kuwawezesha wananchi hao walioona thamani ya kuhifadhi msitu wa Derema – Amani?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali mbaya iliopo katika kufutwa hati za mashamba ya mkonge, wananchi wana imani kuwa mwaka huu 2014 hati hizo zitafutwa na kipaumbele kitatolewa kwa wananchi kupewa ardhi kwa matumizi yao ya kilimo na makazi.

Mheshimiwa Spika, majibu yatakayotolewa baada ya mchango huu wa maandishi utasaidia kutoa elimu kwa wananchi na kupunguza migogoro na vifo tarajiwa katika maeneo ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi isimamie utekelezaji wa kuondoa migogoro niliyoitaja na pia kuendelea kuboresha Shirika la Nyumba ambalo linaboresha sana nyumba na maendeleo ya makazi kwa ujenzi wa nyumba bora hapa nchini.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika nchi yetu. Wizara hii imekuwa na changamoto nyingi sana. Tumekuwa tukiona kwenye vyombo vya habari matukio mbalimbali ya umwagaji damu na hata vifo vikitokea kwa sababu ya tatizo la ardhi. Hivyo basi, Wizara hii kama hitachukua hatua za haraka kwenye suala zima la upimaji wa ardhi, tatizo hili la mapigano ya wakulima na wafugaji na wananchi wengine wa kawaida litaendelea kuwepo.

Naiomba Serikalli ione umuhimu wa suala hili la ardhi katika nchi yetu. Kama halitawekewa nguvu na kuwa na dhamira ya kweli, jambo hili linaweza kuleta machafuko makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kulipongeza Shirika la Nyumba kwa kazi nzuri wanayoifanya katika baadhi ya maeneo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili ni baadhi ya mashirika machache ya Serikali yanayofanya vizuri sana, lakini kuna mambo ambayo tungependa Serikali itazame.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kuwa nyumba zinazojengwa ni ghali kutokana na manunuzi kulazimika kulipa kodi ya *VAT*. Tunaomba Serikali ione umuhimu wa kuondoa kodi hii ya *VAT* kwa wanunuzi ili lengo la wananchi kuishi kwenye nyumba bora liweze kutimia hasa kwa wananchi wa kipato cha chini na kati.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kupokea ushauri wa Kamati yetu na kuweza kuondoa ushuru wa forodha pamoja na kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vinavyotoka nje ya nchi. Tunaendelea kuishauri Serikali kwamba ni vizuri kuliondolea Shirika hili la Nyumba kodi hii ya *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa maeneo ya ujenzi katika nchi yetu; tunaomba Serikali kupitia Wizara hii na TAMISEMI kuwapatia Shirika la Nyumba maeneo ya ujenzi ili kufanikisha malengo yao. Tukifanya hivyo, itasaidia kupunguza gharama za nyumba kwa sababu yako maeneo mengine wanauziwa aidha kwa bei ya juu na hii inachangia gharama za nyumba kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwanzo nilisema Shirika hili ni Shirika linalofanya vizuri. Kinachonishangaza, ni kwa nini Serikali yenyewe inalikwamisha Shirika hili kwa kutokulipa kodi ya pango kwenye nyumba walizopanga wakati kwenye bajeti zao wanapitishiwa gharama za kodi? Ni kwa nini hawalipi? Shirika hili linaidai Serikali na Taasisi zake zaidi ya Shilingi bilioni nne. Tunaomba Wizara zinazodaiwa walipe madeni yao mara moja ili Shirika hili liweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kigamboni umekuwa Kitendawili kikubwa kwa wananchi wa maeneo yao. Ni mwaka wa saba sasa wananchi wameshindwa kuendeleza maeneo yao pamoja na tathmini kufanyika. Ni kwa nini sasa Serikali isiwe wazi kwa wananchi hawa ili wajue kinachoendelea katika miradi huo kuliko kuwaacha kwenye sintofahamu hiyo ya wasiwasi na kushindwa kujiendeleza wao na familia katika maeneo yao? Ni vizuri leo tukajua ukweli; mradi huu upo au umekufa? Tujue, ili wananchi waweze kuendelea na mambo yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nisema jambo lingine ambalo linasikitisha kama Mjumbe wa Kamati. Mwaka 2013 Kamati yetu ilitembelea jengo la gorofa

lililovunjika katika Manispaa ya Ilala Dar es Salaam na kutoa maelekezo kwa jengo lingine la mmiliki huyo huyo lililo chini ya viwango, Waziri mwenye dhamana ya Ardhi Nyumba na Makazi alitoa tamko la kubomoa jengo hilo kwa kuwa liko kwenye eneo la makazi ya watu na linaweza kuleta athari kubwa za kupoteza maisha ya watu pamoja na mali zao. Wanakamati tuliunga mkono agizo hilo la Waziri, lakini cha kushangaza mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Tunasubiri nini? Au tunataka wafe tena ndiyo tukurupuke na matamko kama tulivyozoea?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa hayo machache.

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, zipo jitihada nzuri zinazofanywa na Wizara na Taasisi zake na hasa Shirika la Nyumba la Taifa. Yangu ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ni shirika muhimu na linafanya kazi vizuri sana. Shirika hili linahitaji kusaidiwa sana na Serikali ili kuboresha makazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tufike mahali ionekane na ieleweke kwamba Serikali inapaswa kutoa makazi bora kwa wananchi wote, sio wa mijini tu. Ni kweli *NHC* wanatembelea duniani kujua wenzetu wanafanya nini. Hivyo, wao au ni vyema kuzingatia mazingira yetu ili nyumba ziwe *affordable* kwa wananchi wengi na vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu na wapo makazini waweze kununua bila kulazimika kufikiria kupata fedha kwa njia zisizo halali ili wanunue nyumba. Njia moja ni kuondoa *VAT* kwa vile *VAT* inakuwa imeshalipwa katika bidhaa zilizotengeneza hiyo nyumba. "*Remove VAT please to make houses affordable,*" hii iende sambamba pia na kuangalia *components* nyingine zinazofanya nyumba kuwa ghali.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu ujenzi wa nyumba za *NHC* Mbinga. Toka Bunge la tisa (2006) nilizungumzia juu ya *NHC* kujengwa nyumba pale Wilayani Mbinga, na ipo ahadi ya Mheshimiwa Waziri wakati huo. Naomba sasa ahadi hii itekelezwe. Viwanja vipo; tatizo ni nini? Naomba maelezo.

Mheshmiwa Spika, lingine ni fidia isiyoridhisha. Mradi wa makaa ya mawe Ngaka, malalamiko bado yapo hasa kwa wananchi wale waliolipwa mwanzoni. Tathmini ile inalalamikiwa kwani viwango vilivyotumika ni vya siku nyingi sana na kusababisha shida hii. Hivi kuna ugumu gani kupeleka wathamini ili kuona uhalali? Hivi mpaka watu wapigane mabomu? Namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hili. Hapa namwalika afike Mbinga na pale kijijini Ntunduwaro. Naomba sana! Nawatakia Baraka tele za Mwenyezi Mungu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, mimi binafsi napinga hoja ya Kamati ya Bunge ya Ardhi ya kupendekeza kufuta *VAT* kwa *NHC* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zake. *NHC* ni Shirika la umma kweli, lakini linafanya kibiashara na linashughulika na kujenga nyumba hasa mijini. Je, wananchi wetu ambao wanajenga nyumba zao binafsi hasa vijijini, hao nao watatolewa hiyo *VAT*?

Mheshimiwa Spika, wanavijiji kote Tanzania wanajenga nyumba kutumia bati, sementi, nondo kama wanavyotumia *NHC*. Sasa ni vipi wafaidike wanaoishi mjini tu? Vilevile mijini kuna idadi kubwa ya wananchi wanaojenga nyumba zao kwa kutumia wakandarasi binafsi: Je, hiyo siyo njia mojawapo wa kupoteza fedha za kodi?

Je, vipi udhibiti wa hiyo *VAT*? Tunataka kupinga misamaha ili pesa isaidie maendeleo ya nchi hii masikini kuliko kufaidi wachache wanaoishi mijini tu. Hiyo ni njia nyingine ya kupoteza mapato ya Serikali. Haikubaliki kabisa, walipe *VAT* tu.

**MHE. MESHACK OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, Ibara ya 62 imeongelea fedha ya ardhi huko Kigamboni kwamba 35,000 sq m *equivalent to* 101,645,000 lakini haijaongelea ni kiasi gani cha fedha kwa eneo ambalo kuna nyumba.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni Shilingi ngapi kwa eneo ambalo kuna nyumba ndani ya kiwanja?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HAMOUD ABUU JUMAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka wa fedha 2014/2015. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mikakati mizuri ya kupambana na changamoto mbalimbali zinazozikabili sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, migororo ya ardhi inayojitokeza kwa sasa katika jamii, imeendelea kuwa tishio la amani ya nchi yetu kutokana na athari mbalimbali zinazodaiwa kuchangiwa na matokeo ya udhaifu wa kimfumo, ongezeko la idadi ya watu, shughuli za uwekezaji, upanuzi wa miji, shughuli za ufugaji na nyinginezo nyingi. Athari hizo zimesababisha watu kupoteza makazi, mifugo na mauaji ya kikatili kutokana na vita kati ya wakulima na wafugaji, wanavijiji na wawekezaji na wengineo wakigombania umiliki wa Ardhi katika eneo moja.

Aidha, takwimu zinaonyesha kwamba kati ya hekta milioni 80 za ardhi ya Kilimo nchini ni asilimi 10 ndiyo iliyopimwa katikati ya ongezeko la Watanzania milioni 45. Hatua hiyo inaweza kuwa sababu ya kuwapo kwa zaidi ya kesi 6,000 za migogoro ya ardhi zinazoendeshwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania kote nchini. Ila utatuzi wa migogoro ya ardhi, ni mojawapo ya mambo ambayo hayana budi kutengenezewa mchakato mahususi katika kupata suluhu ya matatizo ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutungwa kwa sheria mpya za ardhi ya mwaka 1999, yaani Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya ardhi pia umebadilika. Miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanywa na sheria hizi ambazo ni matokeo ya Sera ya Ardhi ya Taifa, ni kutengeneza mfumo wa kipekee wa kutatua matatizo ya Ardhi.

Sehemu ya tano ya Sheria ya Ardhi ya vijiji, Na. 5 ya mwaka 1999, ilihusu utatuzi wa migogoro ya Ardhi ya Kijiji. Kwanza, kabla hatujajua njia hizi za utatuzi wa migogoro ya ardhi, ni vyema tukajua maana ya vitu vifuatavyo, ambayo vina uhusiano wa moja kwa moja na Sheria hii ya Ardhi ya Vijiji na utatuzi wa migogoro kwa ujumla.

Kwanza ni hati ya hakimiliki ya kimila kama ambavyo imeelezea na kifungu cha (2) cha sheria hii ambacho kinafanya rejea katika kifungu cha 25(2) ambacho kinaelezea kwamba hatimiliki ya kimila itatolewa katika fomu maalumu iliyoainishwa na sheria. Itakuwa na sahihi ya Mwenyekiti wa Kijiji na Katibu wake. Pia hati hii itatakiwa kuwekewa sahihi au alama ya dole gumba na mtu atakayepewa hati hii kama mmiliki. Pia itatakiwa kutiwa sahihi na kuwekwa na Ofisa Ardhi wa Wilaya ambayo kijiji husika kipo.

Dhana ya pili ambayo tunatakiwa kuwa nayo akilini wakati wa kutatua migogoro ya ardhi ya kijiji ni ya mwanakijiji aliyepewa sheria hii chini ya kifungu cha (2) kwamba ni mtu ambaye kwa kawaida ni mkazi wa kijiji au ni mtu ambaye anatambuliwa na Halmashauri ya Kijiji husika. Vile vile, ni vizuri tukajua tafsiri ya Halmashauri ya Kijiji kama inavyoelezewa na sheria hii kwamba ni tafsiri iliyotolewa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

Pia Baraza la Ardhi la kijiji pia limepata tafsiri ndani ya sheria hii kwamba ni baraza lililoanzishwa maalum kwa ajili ya kusuluhisha na kusaidia kupatikana kwa muafaka kwa pande mbili zinazopingana katika mgogoro wa ardhi ya Kijiji.

Baada ya kuangalia dhana hizo, basi ni wajibu wetu ni kuangalia taratibu za utatuzi wa migogoro ya ardhi za kijiji. Chini ya kifungu cha 16 cha sheria hii, kila kijijiji kimeamriwa kiunde Baraza lake la Ardhi la Kijiji, ambalo kama

tulivyoona hapo awali, litakuwa na kazi kubwa mbili; kwanza, kusuluhisha migogoro yote inayotokana na ardhi katika kijiji kilichopo; na kazi ya pili, ni kusaidia kusuluhisha pande zinazohusika katika mgogoro wa ardhi za kijiji kufikia muafaka.

Baraza hili kwa mujibu wa sheria hii, linatakiwa kuwa na Wajumbe saba ambao watatu kati yao watakuwa ni wanawake, ambao sheria chini ya kifungu cha 60(2) kifungu kidogo cha (a) na (b) kimeweka taratibu za kuwapata na kwamba watatakiwa kuwa wameteuliwa na Halmashauri ya Kijiji na pia watatakiwa kuafikiwa na Mkutano wa Mijiji. Mkutano huu umetafsiriwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

Kwa mantiki hiyo, mtu anapokuwa anataka kupitia sheria hii, basi anatakiwa kutilia maanani pia sheria hiyo ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 ili kuweza kufanya kazi yake vizuri. Chini ya sheria hii kuna athari pale mtu ambaye kama Mjumbe anatakiwa kuthibitishwa na akashindwa kuthibitishwa, basi mtu mwingine atatakiwa kuteuliwa na kuthibitishwa kuchukua nafasi kama Mjumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji.

Hali hii pia itatokea kama Mjumbe husika atajiuzulu nafasi yake, na kama atafariki dunia, au kama atakosa heshima na sifa nzuri za kuwa na ufahamu wa Sheria za Mila za Ardhi na kama mtu mwenye msimamo.

Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 60(3) cha sheria hii. Hayo niliyoyaeleza hapo juu ni kwa mujibu wa sheria za nchi hii. Kwa kufuata taratibu hizo kwa kuwajengea viongozi wa vijiji wakajua sheria hizo vizuri, ingeepusha sana ama kupunguza migogoro ya ardhi ambayo sasa imekuwa tishio kwa kukosa suluhu.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi inaweza kuepukika kwa kiasi kikubwa kama tu sheria na taratibu zikifuatwa. Kama tujuavyo kuwa ardhi ni rasilimali ya msingi katika uhai wa maendeleo ya binadamu, wanyama, mimea na viumbe vyote. Nchi yetu ya Tanzania ambayo uchumi wake unategemea kilimo kama sekta muhimu kukidhi mahitaji ya wananchi walio wengi, ardhi inakuwa rasilimali muhimu ambayo kila mwananchi hana budi kuipata na kuimiliki, kutumia na kuitunza.

Ardhi ni rasilimali inayohitajika ili kuendeleza sekta nyingine za uchumi, ikiwemo viwanda, biashara, pia makazi ya binadamu ambayo hutegemea ardhi kwa ujenzi wa nyumba, barabara na matumizi mengineyo. Hivyo basi, ardhi ni haki ya kila binadamu. Hivyo, kumnyima mtu yeyote haki ya kuitunza, kutoitumia na kuimiliki ni uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa mila na desturi nyingi katika nchi yetu zimekuwa zinamnyima mwanamke haki. Kabla ya Sheria Mpya ya Ardhi ya mwaka 1999 kutungwa, sheria iliyokuwepo Na. 113 ilionekana kuwa na upungufu mwingi suala hili lililopelekea kuundwa kwa sheria mpya. Kutokana na upungufu uliopo kwenye sheria hiyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mbili kuu za ardhi. Sheria hizo ni Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, na Sheria ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Sheria hizi zimetungwa kuboresha upungufu wa Sheria ya Ardhi ya zamani ikiwa ni pamoja na kuboresha utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya Ardhi.

Mwaka 2002 Bunge lilitunga sheria nyingine iliyoanzisha Mahakama za kutatua migogoro ya ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 Bunge lilitunga sheria nyingine iliyoanzisha Mahakama za kutatua migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002; ni Baraza la Kijiji la Ardhi, Baraza la Kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Mahakama Kuu (Idara ya Ardhi) na Mahakama Kuu ya Rufaa ya Tanzania. Japo kumekuwa na Sheria za Ardhi, lakini migogoro ya ardhi imekuwa ikijitokeza kila kukicha na takwimu zinaonyesha kwamba kwa siku kumekuwa na migogoro ya ardhi isiyozidi 5 – 6. Migogoro mingi ya ardhi inaletwa na sheria mama ambayo inamruhusu Rais kuwa na mamlaka makubwa ya kuchukua, pia inamruhusu Rais kuekeza hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? Uandaaji wa ramani ya mipango miji na matumizi ya ardhi, kuwepo na usimamizi, Sheria za Ardhi zifanyiwe marekebisho, Sheria ya Madini ya mwaka 1999 inatakiwa ifanyiwe marekebisho kwa kuwa kuna kipengele kinatamka kwamba eneo la madini siyo sehemu ya ardhi, kwani hilo ni tatizo. Halmashauri zipunguziwe majukumu kwa kuwa Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 imezipa mamlaka hizo suala zima la upangaji wa Miji.

Pia sheria ya mwaka 1982 inatamka wazi kwamba Serikali ina uwezo wa kuchukua ardhi lakini wananchi kutolipwa fidia, hilo pia ni tatizo. Serikali iangalie ni namna gani itamaliza migogoro ya ardhi? Sera za uwekezaji zifanyiwe marekebisho kwa mujibu wa sheria na taratibu juu ya ulipaji wa fidia. Fidia haiendani na gharama za wakati ujao, wawekezaji wananufaika, Serikali zisimamie, siyo kuachia Halmashauri. Serikali ina wataalamu wengi wa ardhi, lakini haitambui umuhimu wa aArdhi.

Maofisa wa Ardhi waache kufanya kazi mezani pasipo kwenda kuangalia eneo husika pale wanapoombwa vibali vya maeneo na wananchi ndiyo maana wengi wanauza maeneo kiholela tu bila kuwa na uzalendo.

Muda wa umilikishwaji wa ardhi kwa wawekezaji upunguzwe na kuwa miaka 10 badala ya miaka 99 iliyoelekezwa kwenye sheria. Serikali pia ina udhaifu katika kusimamia utawala wa sheria. Kasi ya upimaji wa ardhi iongezwe

ili kupunguza wimbi la watu kuvamia maeneo pasipo viongozi wa vijiji kujua na Serikali za vijiji zipewe madaraka juu ya usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba yatengwe maeneo makubwa ya wafugaji na wakulima pamoja na kuwawekea sheria zitakazowazuia wao kuingiliana kwa kuogopa sheria. Pia ziwepo sheria za kumdhibiti mmiliki wa ardhi. Pia wawekezaji watengewe maeneo yao, siyo lazima wawe sehemu ambazo watu tayari wanaishi. Pamoja na wananchi kushirikishwa katika utaratibu wa ugawaji wa viwanja kwa kuwa ardhi ni maisha ya Mtanzania, haya yote yakifanyiwa marekebisho, basi itapunguza sana migogoro ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wanasiasa wamebainika kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi inayotokea nchini na kusababisha vifo huku waathirika wengine wakibaki na ulemavu kama inavyojitokeza katika migogoro mbalimbali nchini. Mbali na hilo, Serikali imeshindwa kuwajibika huku ikipuuza kuchukua hatua pale mgogoro unapofukuta licha ya kuwa na taarifa za muda mrefu kuhusu mgogoro huo. Wanasiasa wengi wanatoa kauli za uchochezi kwa lengo la kukidhi matakwa na maslahi yao binafsi. Viongozi wanaochangia kuwepo kwa migogoro ni Madiwani, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, sisi Wabunge wenyewe na Mawaziri ambapo katika migogoro mingi ya ardhi katika maeneo mbalimbali, wameshindwa kutafuta ufumbuzi wa kubaki kulumbana katika vyombo vya habari.

Ni vyema sasa wanasiasa wakajiepusha na kauli za kichochezi zenye lengo la kukidhi matakwa yao huku zikiathiri haki na maslahi ya wananchi. Migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali imekuwa ikidumu kwa muda mrefu sasa. Kwa mfano, mara nyingi vyanzo ni maamuzi ya Halmashauri zetu wakati mwingine wa kutaka kuwahamisha wakulima katika maeneo yao waliyokuwa wakitumia kwa kilimo na kuyabadilisha kuwa Hifadhi ya Taifa. Vivyo hivyo na kwa wafugaji kutaka kuwahamisha katika maeneo yao. Migogoro mingi inayotokea imekuwa ikichukua sura mpya baada ya kuwepo kwa madai ya wafugaji kuchangishwa fedha na ama Uongozi wa Halmashauri kwa madai labda ya kusaidia kuendesha operesheni ya kuwaondoa wavamizi katika maeneo hayo.

Licha ya mauaji yanayojitokeza katika migogoro ya ardhi, kuna athari nyingine hujitokeza za nyumba kuchomwa moto na wananchi kukimbia makazi yao na hivyo kupelekea akina mama na watoto kuathirika zaidi. Naitaka Serikali ichukue hatua za dharura kusitisha migogoro ya ardhi popote nchini na kusitisha mapigano yanayoendelea katika maeneo mbalimbali nchini na kuchukua uamuzi wa kupeleka timu ya wataalamu wa mipaka na ramani ili kubaini haki za maeneo yanayogombaniwa.

Mheshimiwa Spika, ipo migogoro inayofukuta na inayoleta maafa ambapo Serikali inapuuza kuchukua hatua na sehemu nyingine nyingi tu, Serikali inakuwa na taarifa mapema kabla ya mapigano kutokea lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa hadi pale vifo vinapotokea ndio Serikali na mamlaka husika hujitokeza. Naishauri Serikali kutokusubiri mpaka hali iwe mbaya, ni heri kuchukua tahadhari mapema ili kuepusha majanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikiri kuwa ufinyu wa bajeti kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ni moja kati ya changamoto inayochangia kuendelea kwa migogoro ya ardhi nchini. Hata ukiangalia katika kipindi cha mwaka 2012 na 2013 watu 58,393 waliopata hati baada ya kupimiwa viwanja vyao nchi nzima na kwamba jukumu la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni kusimamia sera na kuweka miongozo ya matumizi ya ardhi pamoja na kutatua migogoro. Pia hata mwaka 2013 na 2014 hali ni hiyo hiyo! Serikali imekuwa ikichelewa kutoa fedha na hivyo kuzorotesha utendaji wa Wizara. Halmashauri nyingi hazitengewi bajeti na hali hii inasababisha migogoro kutokana na kwamba kiasi kidogo kinachotolewa katika bajeti hakikidhi ulipaji wa fidia kwa wananchi, upimaji wa viwanja na uendelezaji mji hushindwa kufanyika kwa sababu ya uhaba wa fedha. Hatimaye kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kupima na kugawa viwanja linafanywa na mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na majiji, hivyo Wizara imekuwa ikijikita katika kusimamia sera na kuweka miongozo ya matumizi ya ardhi na utatuzi wa migogoro inayoibuka kila mara. Baadhi ya migogoro mikubwa ya ardhi iliyopo nchini huwa ni migogoro kati ya jamiii za wakulima na wafugaji, wanavijiji na wawekezaji, migogoro ya mipaka baina ya mamlaka mbalimbali na wamiliki wawili katika kiwanja kimoja. Haya ni matatizo ambayo yamekuwa yakijirudia na fidia hulipwa wakati wa utwaaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inatokana na elimu duni kwa jamii kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za utawala wa ardhi. Vile vile ukosefu wa udilifu kwa baadhi ya watendaji katika Sekta ya Ardhi, upungufu wa Watendaji na vitendea kazi pamoja na utunzaji hafifu wa kumbukumbu ni moja kati ya sababu inayochangia migogoro ya ardhi nchini kuzidi kushamiri.

Mheshimiwa Spika, ni jinsi gani utatuzi wa migogoro ya ardhi inavyoweza kufanyika? Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya mwaka 2002 imeweka utaratibu wa muundo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Miongoni mwa utatuzi huo ni kuwa na Baraza la Ardhi la Kijiji ambalo jukumu lake ni kusuluhisha migogoro ya ardhi inayotokea hapo kijijini.

Vile vile katika utatuzi huo wa migogoro ya ardhi lazima kuwe na Baraza la Ardhi la Kata na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ambalo limeundwa na Waziri anayehusika na masuala ya Ardhi. Mabaraza haya yanatakiwa kuwepo katika ngazi zote za Wilaya ili kuhakikisha huduma stahiki kwa wananchi inatolewa na kwamba kazi ya Baraza hili ni kusikiliza rufaa kutoka Baraza la Kata, kusikiliza mashauri mbalimbali ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria za Ardhi pamoja na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yake. Nini kifanyike?

Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii ili kuwepo na wataalamu watakaoweza kufikia wananchi wa vijijini na kutatua migogoro pamoja na kuwepo kwa uadilifu kwa baadhi ya Watendaji katika Sekta ya Ardhi na kuongeza watendaji wa vitendea kazi katika maeneo husika. Vile vile kutolewa elimu itakayosaidia kupunguza changamoto hiyo, kwani migogoro mingi ya ardhi inatokana na kutoridhika na fidia inayolipwa wakati wa utwaaji ardhi na hali hiyo inatokana na elimu duni kwa jamii kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za utawala wa ardhi.

Vile vile kwa upande wa ukatili, licha ya kuwepo kwa sheria zinazodhibiti hali hiyo, bado kuna changamoto ya uhaba wa wasaidizi wa kisheria katika maeneo mbalimbali ya nchi ambao wangeweza kutoa elimu ya sheria mbalimbali za ardhi ili kuepusha migogoro hii kuendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro pia baina ya wanakijiji na wawekezaji. Migogoro hii imekuwa ikishamiri sana na hali hiyo imekuwa ikitokana na wanakijiji kutojua taratibu za kisheria zilizowekwa ili mwekezaji aweze kutumia ardhi yao, na taratibu hizo ni kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa hatua za asiye raia wa Tanzania kupata ardhi, taratibu za kupata ardhi kwa mtu asiye raia kwa sababu za uwekezaji zipo wazi katika Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Uwekezaji wa mwaka 1997.

Kwa ujumla mwekezaji anatakiwa kuomba ardhi kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambacho kina wajibu wa kuomba ardhi kutoka Wizara ya Ardhi ambayo itatafuta ardhi hiyo na kuitangaza kwenye gazeti la Serikali na kisha kuimilikisha kwa Kituo cha Uwekezaji.

Kituo cha uwekezaji kitatoa hati mbadala kwa mwekezaji. Hata hivyo, tovuti ya kituo cha uwekezaji inataja njia tano ambazo mwekezaji asiye Mtanzania anaweza kupewa ardhi (i) umiliki mbadala, fungu 20(1) Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999; (iii) kuomba kutoka kwa Kamishna wa Ardhi fungu 25 (1)(h) (iii) kupangisha kutoka sekta binafsi *(sub-lease from private sector);* (iv) Leseni ya Ardhi kutoka Serikalini; na (v) ununuzi kutoka kwa wamiliki wengine.

Muhtasari wa maelezo haya yanamweleza mwanakijiji kuhusu hatua za kufuata kwa ardhi ya kijiji kuuzwa au kupewa kwa wageni kwa lengo la uwekezaji. Kwa kujua na kuelewa hatua hizi, wanakijiji watakuwa katika uelewa mzuri wa ama kulinda ardhi ambayo hawataki ichukuliwe na wageni kutoka kijijini au kuhakikisha wanakijiji wengine wanapata fidia ambayo wanastahili. Elimu hizi ndiyo zinatakiwa kutolewa maeneo ya vijijini ili kuepusha baadhi ya watu wachache kuweza kufanya yale ambayo baadaye yataibua migogoro, hivyo Serikali haina budi kutenga bajeti nzuri ya utoaji wa elimu hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara kuangalia namna ya kutanua Miji yetu kwa kuleta miradi mikubwa ya Shirika la Nyumba kwa ajili ya ujenzi wa majumba, ili miradi hiyo iweze kuja mpaka Kibaha Vijijini kwani tuna maeneo makubwa sana na mazuri kwa ujenzi wa nyumba za kisasa, na ukizingatia Mji wetu sasa hivi unakuwa kwa kasi, maendeleo yanakuja kwa kasi pia. Hivyo watu wengi sasa wanakuja kuwekeza Kibaha.

Kupata nyumba hizo kutasaidia sana kwa wananchi wangu pamoja na watumishi kuweza kuzitumia kwa kupanga na kulipa kodi na hata kununua kama shirika linavyoendelea kufanya mradi huo katika Mikoa mingine kwa kujenga nyumba za kisasa na kuwakopesha watu kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia mgogoro wa ardhi uliopo kati ya mwekezaji na wanakijiji wa Kijiji cha Kipangege na Kitongoji cha Kifuru Kata ya Soga. Mgogoro huu unahusu lililokuwa shamba la mkonge ambalo ameuziwa mwekezaji ambaye ni *Mohamed Enterprises Ltd,* mwekezaji huyu baada ya kuuziwa aliliacha shamba hili kwa muda mrefu bila kuliendeleza na hivyo kugeuka kuwa shamba pori. Kipindi chote hicho wananchi walifanya makazi na hatimaye leo hii wanaambiwa waondoke.

Naomba Serikali kupitia Wizara, iangalie mgogoro huu na kuutafutia ufumbuzi kwani wanakijiji wanataka kuhamishwa katika maeneo yao na kumpisha mwekezaji. Naiomba Wizara kuchukua hatua za haraka kabla mgogoro huu haujawa mkubwa na kuleta shida zaidi. Migogoro kama hii jimboni kwangu iko mingi na bado baadhi haijapatiwa ufumbuzi thabiti. Vile vile lazima sheria ziwekwe wazi kwa wawekezaji wote wanaonunua maeneo na kuyatelekeza wanyang'anywe na kurudishwa kwa wananchi, kwani wananchi wamekuwa wana maeneo haba kwa ajili ya kilimo huku maeneo yamekaa tu na kugeuka kuwa mapori hatarishi bila kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, hata Mheshimiwa Rais aliwahi kutamka kuwa kwa wale watu wote wenye maeneo makubwa na hawajayaendeleza, apelekewe majina yao na kufuta umiliki wao. Kwa kuwa Kibaha Vijijini kumepita njia kuu ya *Morogoro Road*, namwomba Mheshimiwa Waziri anikubalie ombi langu, siku akiwa anatoka Dodoma baada ya vikao vya Bunge aje kutembelea eneo hilo na kuzungumza na wananchi wangu maana kero hii imekuwa ni ya muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naanza na Mradi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyowekwa ni nzuri sana ila nashauri wananchi hawa wa Kigamboni washirikishwe na pia kuwe na uwazi waweze kujua haki na stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, tangazo la mradi huu lilitoka mwaka 2008, wananchi hawa wamekuwa wanateseka sana, hawawezi kujenga, hawawezi kukarabati nyumba zao, hawauzi na wala hawawezi kukopesheka hii imekuwa ni dhuluma kubwa kwa wananchi hawa. Tunaishauri Serikali ifikirie ni namna gani ya kuwaondoshea wananchi tatizo hili. je Serikali iko tayari kutuambia ni nini hatma ya wananchi hawa wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji imezidi kuongezeka, tulifikiria Mheshimiwa Waziri angeweza kuitatua migogoro hii, lakini inaongezeka kila siku. Naishauri Serikali idhibiti migogoro hii kwani itaendelea kuleta majanga makubwa kwa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, dhuluma kwa wananchi dhidi ya wawekezaji imezidi kuongezeka. Wananchi katika baadhi ya vijiji wanahamishwa na wawekezaji na kusema kuwa wao ndio wamiliki halali wa maeneo hayo. Naishauri Serikali wazawa wapewe haki na sio kila mwekezaji aweze kuwa ana nguvu ya kuwanyanyasa wananchi. Jambo hili linawafanya wananchi kukosa imani na uongozi uliopo madarakani.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la wawekezaji kupata ardhi kwa ajili ya shughuli zao. Hii inatokana na kuwa Serikali haina Hazina ya Ardhi *(Land Bank)* ilipokuwa imo katika juhudi ya Serikali kuwa na Hazina ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, wakati utakapofika wa Serikali kupata ardhi ya au kutafuta Hazina ya ardhi iwe na tahadhari kubwa kwani ardhi iliyopo hapa nchini na ukubwa wake ardhi yenyewe sehemu kubwa imeshatengwa kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ardhi iliyopo asilimia 31.3% ni ya vijiji, asilimia 17% ni kwa makazi ya mijini na asilimia 30% ni kwa ajili ya Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo ni asilimia 20% tu ya ardhi ndio iliyobakia ambayo Serikali inaweza ikapata ardhi ikaiweka kwenye Hazina ya Ardhi *(Land Bank)*, pia ardhi hiyo asilimia 20% ndio pia wananchi wengine watahitaji kupata ardhi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mji wa Kigamboni umekuwa ni mjadala wa kila mwaka kwa kupitia bajeti ya Wizara hii. Bado wananchi wa Kigamboni wanalalamika kuwa hawajashirikishwa kwenye mradi huo na pia hawaelewi undani na maslahi ya mradi huo. Pia agizo alilolitoa Spika mwaka jana kwenye bajeti ya Wizara hii ya kutaka pande husika zikutane bado halijatekelezwa. Hapa kuna usiri gani? Nadhani iko haja sasa iundwe Tume ya Bunge ili kulishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kwa wananchi kuwa nyumba za Shirika la Nyumba *(NHC)* ni ghali. Nafahamu miongoni mwa sababu za nyumba hizo ni kununua vifaa vya ujenzi vyenye *VAT*, kuuza nyumba zenye kuingiza *VAT*, shirika huweka miundombinu ya barabara, maji na umeme na fedha inayojengewa nyumba hizi nyingi zao ni mikopo kutoka benki.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza ughali wa nyumba hizo, ipo haja ya Serikali kulisamehe *VAT* Shirika na taasisi husika kama Halmashauri kujenga miundombinu ya barabara, umeme na maji. Je, Serikali imesemaje kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. REV. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo machache tu kuhusu hoja hii:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kupima ardhi yote nchini. Hii itaondoa migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi wake, kwa mfano, migogoro kati ya wafugaji na wakulima, mashamba, vijiji kutoa Hatimiliki za Kimila zitolewe na mpango huu uwe endelevu kwa vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya baadhi ya watu kuvamia maeneo ya wazi, maeneo ya vyanzo vya maji – na hapa kipekee nakuomba wewe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi utembelee Karatu ili kujionea mwenyewe uvamizi unaofanywa na wajanja wachache ilihali wanyonge wakitaabika. Mheshimiwa Waziri anipe jibu kwamba atakwenda lini Karatu?

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa chanzo cha *Qangded* uliosababisha wataalam wa ardhi kushindwa kupima eneo hili, jambo ambalo wahusika wakuu kwa uharibifu huo ni viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa Mabaraza ya Ardhi kwa ngazi zote, Serikali iangalie kwa karibu sana Mabaraza hayo na kwa Karatu mara nyingi Baraza hili halifanyi kazi sawasawa mara Mwenyekiti hayupo au amehamishwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri aingilie suala hili kwa Karatu au jambo lingine ni kesi hizi kuchukua muda mrefu kutolewa maamuzi, jambo linaloashiria mara nyingi harufu ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afike Karatu kuona mashamba yote ya mikataba ya miaka 99 iangaliwe upya. Kuna mashamba mengi sana ambayo mengine hayakuendelezwa, mengine yanaendelezwa nusu ili hali wananchi wengi hawana ardhi kwa kilimo. Malisho na hata makazi.

Mheshimiwa Spika, kwa eneo la Jimbo langu la Karatu, naomba Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa yale mashamba ambayo yanaendelezwa kwa sehemu na kufanya maeneo mengine kuwa *(zoo)* mapori ambayo wanyama wakali huishi humo, Serikali ifanye *Partial Revocation* kwa mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa yale mashamba yote ambayo wamiliki wamebadilisha matumizi ya mashamba hayo bila kupata kibali cha Serikali, naomba Serikali ifanye *full Revocation* na kuwapatia wananchi maeneo ya makazi, kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakuomba wewe Mheshimiwa Waziri utembee na kutatua mgogoro wa muda mrefu wa ardhi Karatu unaofanywa hasa na viongozi wa Serikali na matajiri wakubwa (wakitumiwa na vigogo wa Serikali).

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi hapa nchini ni mingi sana, ingawa Mheshimiwa Waziri amesema katika Hotuba yake

ukurasa wa 54 kwamba, hakuna migogoro ya ardhi bali migogoro hiyo ishughulikiwe ipasavyo kwani wapo watu waliopoteza maisha yao kwa sababu ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingi inasababishwa na Maafisa Ardhi ambao hugawa ardhi kwa wamiliki zaidi ya mmoja. Aidha, ardhi ya wananchi kuchukuliwa na Serikali na kupewa wawekezaji huku wananchi wakiachwa katika usumbufu mkubwa bila kupewa fidia au fidia stahiki. Serikali iharakishe katika kuwalipa fidia wananchi wote waliohamishwa kwa madhumuni ya ardhi yao kupewa wawekezaji. Maafisa Ardhi wanaogawa viwanja kwa wamiliki zaidi ya mmoja wachukuliwe hatua kali, kushtakiwa au kufukuzwa kazi. Wizara isifumbie macho Maafisa hao kwani ni tabia isiyo ya kizalendo na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 57 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kusimamia kupanga matumizi ya ardhi, kupima ardhi, kusajili na kutoa Hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa miliki.

Mheshimiwa Spika, hakuna tatizo kubwa lililo mbele ya Watanzania unapozungumzia ardhi kama kupimiwa ardhi, kuna urasimu uliokithiri, na nia ya dhati ya kupima ardhi haipo.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi ameelezea katika ukurasa wa 57 kwamba, Wizara yake imejipanga kupima ardhi. Nasikitika sana kwamba mwaka ujao kama Mungu akitupa uhai, Mheshimiwa Waziri atatuambia haya haya ya kujipanga kupima ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukulie suala hili la kupima ardhi kwa umuhimu mkubwa. Fedha ya kutosha itengwe kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo. Wananchi wengi waishio vijijini wenye ardhi kubwa ambayo kimsingi ni mali, ni utajiri mkubwa, lakini wamiliki yaani wanavijiji wanaishi katika lindi la umasikini wakati wangeweza kukopa katika taasisi za fedha yakiwemo mabenki na hivyo kuitumia ardhi hiyo kisasa zaidi kwa kulima kwa trekta na hatimaye kujikomboa kutokana na umasikini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wengi wa ardhi vijijini hawawezi kukopa benki kutokana na kwamba karibu wote hawajapimiwa ardhi na hivyo hawana Hati miliki, MKURABITA ilikuja na sera ya kurasimisha mali za wanyonge ikiwa ni pamoja na kurahisisha upimaji wa ardhi, lakini kwa muda mrefu MKURABITA haisikiki, haijulikani inafanya nini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa migogoro kati ya wanavijiji na wamiliki wa migodi inaongezeka, Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 61 amesema migogoro hii inahusiana na wananchi kutotambua haki zao za ardhi.

Sikutegemea kwamba Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba migogoro hiyo sababu yake ni wananchi kutotambua haki zao za ardhi. Je nini kimefanyika? Wananchi/wanavijiji waendelee kunyanyasika?

Mheshimiwa Spika, endapo kinachotakiwa ni mwenye leseni ya kuchimba madini, kuwahamisha na kuwafidia watumiaji wa ardhi hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, je, ni kwa nini elimu haitolewi kwa wanavijiji ili wajue taratibu hizo? Badala yake ukurasa wa 62, Waziri amesema kinachofanyika ni kuwabana wenye migodi kutoa fidia stahiki.

Mheshimiwa Spika, hiyo haitoshi, huo ni mwanya wa rushwa. Kuwabana wenye migodi pekee ina maana wakitoa kitu kidogo kwa Afisa asiye na maadili, wanavijiji wataendelea kuonewa. Nashauri elimu, taarifa ni nguvu, waelimisheni wanavijiji wapate uelewa wa sheria hiyo. Njia ya redio ni rahisi, wengi vijijini wanamiliki redio.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha mchango wangu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa migogoro ya ardhi inatokana na tatizo kubwa la mfumo, kama ambavyo Wabunge wengine wamechangia kuhusu suala la upimaji wa ardhi nchini ambalo limekuwa ni tatizo la muda mrefu, ni lazima leo Waziri atueleze ni ugumu gani ambao unachangia ama unakwamisha upimaji wa ardhi?

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi inayojitokeza kwa sasa katika jamii imeendelea kuwa tishio la amani ya nchi yetu kutokana na athari mbalimbali zinazodaiwa kuchangiwa na matokeo ya udhaifu wa kimfumo, ongezeko la idadi ya watu, shughuli za uwekezaji, upanuzi wa miji, shughuli za ufugaji na nyinginezo nyingi. Haya tuyaone maendeleo mbalimbali ya nchi hapa ikiwemo Mvomero, Kiteto, Arumeru, Handeni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, athari hizo zimesababisha watu kupoteza makazi, mifugo na mauaji ya kikatili kutokana na vita kati ya wakulima na wafugaji, wanavijiji na wawekezaji na wengineo, wakigombania umiliki wa ardhi katika eneo moja. Aidha, takwimu zinaonesha kwamba kati ya hekta milioni 80 za

ardhi ya kilimo nchini, ni asilimia 10 ndiyo iliyopimwa katikati ya ongezeko la Watanzania milioni 45.

Mheshimiwa Spika, lakini wote hapa tunashindwa kusema kuwa, kuna tatizo ambalo tunalisababisha sisi wanasiasa kwa kuwa katika migogoro mingi tu ya ardhi, wanasiasa huwa wanaharibu mchakato mzima wa utatuzi wa migogoro hiyo kutokana na mgongano wa kimaslahi.

Katika hatua za kutatua migogoro kuna mambo yanayoamuliwa kitaalam, wakati mwingine wananchi wanaweza kuwa na makosa, lakini wanasiasa wanaingilia kati kuwalaghai, kuwatia moyo, matokeo yake wananchi wanafikia hatua ya kukosa uvumilivu wakiamini wana haki kumbe sivyo. Ni lazima ifike mahali, wanasiasa tuache kutumia ukosefu wa elimu sahihi ya masuala ya ardhi ili kufanikisha malengo yetu ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa imesababisha vifo vya Watanzania mafukara na hatujawahi kusikia matajiri waliouawa kutokana na migogoro ya ardhi zaidi tu alipouawa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mwanza, Ndugu Mabina hapo ndipo uchungu wa vifo ukaanza kuonekana, lakini leo Waziri atujibu, migogoro ya ardhi mpaka sasa imesababisha vifo vingapi?

Tatizo hili pengine halielezwi ipasavyo na si vizuri kuwaaminisha watu kwamba ili tatizo lishughulikiwe kwa kina, haraka na ufasaha, kwanza waathirike au wauawe vigogo. Kwa nini zipigwe kelele sana alipokufa Mabina, lakini watu walipouawa Kiteto hawakupewa uzito unaostahiki?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anijibu, je tuna Mabaraza ya Ardhi kushughulikia kero hii kila Wilaya? Kuna Mabaraza ya aina hiyo kila Kata? Yanafanya kazi yake inavyotakiwa? Yanasimamiwa vyema na Serikali? Je, yanawezeshwa ili kutenda wajibu wao kwa haki na usawa? Yana watu wenye uwezo au elimu ya Sheria za Ardhi? Majibu ya kila swali hapo juu utajibiwa hapana. Elimu kwa umma juu ya haki na wajibu wa kila mwenye tatizo la ardhi ama alitatueje au aende sehemu gani inatolewa na nani?

Mheshimiwa Spika, tumeunda Tume nyingi tu zisizo na kichwa wala miguu, leo vifo vinavyoendelea kutokea havistahili Tume? Kuna wenye dhamana juu ya hili, wamewajibika au kuwajibishwa na nani? Au bado hawajapoteza sifa za kiasi cha kuwajibishwa? Roho za marehemu wote wa migogoro ya ardhi zimlilie nani?

Mheshimiwa Spika, ninachokiona mbele ni sawa na methali ya asiyeziba ufa atajenga ukuta. Tatizo tunaliona dogo, wanauana wakulima na wafugaji kesho tutasikia tunaanza kuuana kwa makabila ili kugombania ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anitatulie matatizo mawili. Naomba arejee barua yangu Kumb. Vunjo/*KNCU*/121/2014 ya tarehe 10/5/2014. Pale Meresini Himo Vunjo tuna tatizo kubwa la ugawaji wa ardhi usiokuwa na haki na usiozingatia mahitaji ya jamii na wananchi wa Himo.

Mheshmiwa Spika, pale Himo kulikuwa na Shamba la Mkonge. Serikali ikaamua mwaka 2006 shamba hili lirudishwe kwa wananchi.

Wananchi wa Himo wakaomba ugawaji huo utakapofanyika wapewe kipaumbele kwenye shughuli zao za kijamii. Tangu wakati huo wamekuwa wapewe:

(1) Eneo kwa ajili ya shule ya Meresini *(A Level)*.

(2) Eneo la upanuzi wa shule ya msingi Meresini.

(3) Eneo kwa ajili ya soko dogo.

(4) Eneo kwa ajili ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, lakini Halmashauri ya Moshi haikutakiwa kuwashirikisha wadau ambao ni wananchi wa Himo. Badala yake ikaamua kugawa sehemu kubwa ya eneo hilo kwa mambo kama yafuatayo:-

(1) *Super Market;* na

(2) Watu ambao walikwisha kufa kama Mariam Mfinanga na kadhalika.

Matajiri waliopewa ardhi katika eneo hilo ni:-

(1) Aloyce Kimaro – eka 11.7.
(2) Edward Shayo eka tatu.

(3) Anselm William Minja – Eka saba

Wananchi walimlalamikia Afisa Ardhi, Kanda ya Kaskazini, alikiri kwamba, kumekuwa na ukiukwaji wa kanuni ziiitwazo *The Land Allocation Committee Regulations*, 2010 hazikufuatwa. Hivyo, akaiandikia Kamati ya Ugawaji wa Ardhi Wilaya ilipaswa kupitisha maombi ya Ardhi katika eneo hili na endapo utaratibu huo haukuzingatiwa ni muhimu ukazingatiwa kwa maana ya kufuata upya taratibu na kanuni za sheria zilizopo kwa maeneo yote yaliyopimwa katika shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamishna wa Ardhi wa kanda alimwandikia tajiri mmoja barua Kumb. Na. *LD.NZ*/383/129 alimwambia:-

"Ofisi inakushauri uwasiliane na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi aweze kutekeleza agizo la barua yenye Kumb Na. *LD*/*NZ*/383/22/*DW* ya tarehe 13/3/2013 ili kuzipa nguvu sheria miliki zilizotolewa katika maeneo hayo kwa sababu utaratibu uliotumika kugawa eneo hilo ndicho kiini cha mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kilimanjaro *Spirit and Wine* kinachojengwa na wawekezaji kutoka Kenya. Wizara iliandika barua Kumb. Na. C/91/329/01/A.86 ya tarehe 23 Januari, 2013. Barua inasema kiwanda kimejengwa

(a) Kwenye makazi ya watu;

(b) Kinajengwa katika kiwanja katika makazi ya watu;

(c) Maeneo ya jirani yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za kuabudia na matumizi ya umma yaliongezwa kwenye kiwanja hicho;

(d) Mkurugenzi kuhakikisha kiwanda hakijengwi; na

(e) Kama kimeanza kibomolewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa maelekezo yake hayatekelezwi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hotuba hii ya Wizara. Kwanza kabisa kwa kuanza na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza haya ndiyo yanayosuluhisha migogoro ya Ardhi, ni dhahiri kabisa migogoro ya Ardhi katika nchi yetu imekuwa ikikua siku hadi siku na inapelekea kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi kwani tumeshuhudia mali zikiharibiwa na vifo vingi vinavyotokana na migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 81, Waziri ameainisha mashauri ya zamani kuwa ni 18,328 (kwa maana hadi Juni, 2013) na mashauri yaliyosajiliwa Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 ni 11,548 na kwamba mashauri yaliyokamilishwa ni 11,432 na kuna mashauri yanayoendelea ni 18,444. Kwa maana nyingine ambayo si lazima mashauri ya zamani bado 6,896 hajakamilika.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua katika haya mashauri yanayoendelea ni mangapi ya zamani na mangapi ya sasa. Vile vile ili tuweze kujua kasi ya mrundikano wa mashauri haya *(blocklog)*. Ningependa kujua hayo mashauri ya zamani ni ya tangu mwaka gani au yana muda gani? Mfano Afrika Kusini kwa Mahakama za Wilaya kesi/mashauri yakikaa miezi sita hiyo ni *backlog*, kwa Mahakama za Mikoani ni miezi tisa na mashauri ya Mahakama Kuu ni mwaka mmoja. Kwa hapa Tanzania kuna Mahakama za kawaida, mashauri yakifikia miaka miwili inakuwa *backlog*. Je, katika mashauri ya Mabaraza inachukua muda gani kuwa *backlog* na nini mpango mkakati wa Wizara ili kuhakikisha mashauri hayachukui muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo baadhi ya Wenyeviti wa Mabaraza wasiofuata maadili ya kazi zao na hii inapelekea mashauri kuchukua muda mrefu na hii inapelekea usumbufu kwa wadai na hata kupelekea kukosa haki hata ya kukata rufaa kwa muda muafaka. Kwa mantiki hiyo, nataka kujua sera za Wizara katika kukagua na kufuatilia utendaji wa Mabaraza haya ili kugundua Wenyeviti wanaokiuka maadili ya kazi na kama Wizara ina hii sera, niambiwe ni Wenyeviti wangapi wamechukuliwa hatua na ni hatua gani zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi Tarime, kuna ardhi ya wananchi wa Kata ya Mwema kwa maana wananchi wa Kitongoji cha Kokeregeya, Kijiji cha Korotambe na Nyakangara Kijiji cha Kubiterere ambayo imechukuliwa na JKT bila ya wananchi kufanyika tathmini.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa nini wananchi hawa hajafanyiwa tathmini ilihali JKT wanajenga nyumba, wanakata miti ya wananchi kwa ajili ya kuni, wamelima lakini mbaya zaidi wanang'oa mikonge ambayo ni alama za kuainisha maeneo ya wananchi, baina yao yaani (wananchi kwa wananchi). Nataka kujua kwa nini JKT wanang'oa mikonge bila kutambua wamiliki kwa ajili ya fidia au ni njia gani Wizara itatumia kuwatambua wamiliki katika ulipaji wa fidia. Naomba kujua kweli kuhusu utata huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ni mgogoro wa wananchi wa Kipimio, Mrambwe na Nyamichele na mgodi wa *North* Mara kwani kinyume kabisa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010, sehemu ndogo ya (7) Ibara ya 97 inayotamka mchimbaji Madini asi-*operate* kabla hajawalipa watumiaji wa ardhi kwa mujibu wa sheria. Mbaya zaidi wananchi hawa wamefika hadi kwa Waziri na analitambua tatizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tibaijuka alisema atakuja kusuluhisha hiyo migogoro na kutafuta suluhu, lakini hajaja badala yake kwenye hotuba yake anaainisha kuwa anasuluhisha migogoro ya Geita. Je, hii ni ya Nyamongo (*North* Mara) havina maana au ni fahari wananchi wale kuendelea kumwagiwa kifusi, makaburi yao kufunikwa, Polisi kuwapiga na nyumba zao kuwa magofu. Naomba majibu juu ya wananchi hawa akinamama Methuselah, mzee Maswi na wengine wengi. Maana ule umegeuka kuwa mradi wa vigogo na hasa *DC* wa Tarime na wananchi hatumtaki.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya baadhi ya majedwali, mfano, jedwali 5B linaonesha Wilaya ya Tarime hakufanyiwa tathmini kwa mwaka huu wa fedha kwa nini? Jedwali Na. 2 linaonesha Wilaya ya Tarime Musoma (W) (pg 68) na Rorya hakukuwepo na utoaji wa hati miliki ya kimila, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na uhamisho wa Milki za Ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya kina.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, watendaji wa Ardhi katika baadhi ya mikoa ni majambazi waliohitimu katika Vyuo vya Shetani. hawana huruma, kazi yao kubwa ni kupora urithi wa wanyonge waliopewa na Mwenyezi Mungu hasa sehemu za mijini.

Mheshimiwa Spika, wana uchu wa pesa karibu kila kona, Wizara iweke utaratibu mzuri ambao utawaweka Watanzania kuwa huru kwa mfano mtu anapokuwa na eneo lake apimiwe yeye mwenyewe na auze yeye mwenyewe, badala watu wa Ardhi kuuza viwanja hivyo na endapo mtaona mtu analalamikia ardhi yake, viongozi wahusika wawajibishwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, imeandikwa mashamba yenu na mazao yenu mtanyanganywa na hata kuuawa mtauawa, lakini tukae kimya? Lazima tuseme, Wizara iwaelimishe kumwogopa Mungu kama watu watakaohukumiwa na Mungu. Wajue chini ya jua hakuna zaidi ya kula, kunywa, kuvaa na kulala hata kama wangepewa dunia yote wangefaidika nini?

Mheshimiwa Spika, mtu anapojenga nyumba yake katika mipaka ya kiwanja chake bila kuvuka vile vipimo vinavyotakikana aelekezwe utaratibu wa ramani, alipe, wamchoree ramani kufuatana na alivyojenga, si kumvunjia nyumba yake kwani huu ni unyama uliokithiri, naamini kuwa katika Wizara zenye mateso makubwa kwa wananchi ni Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, uporaji wa ardhi ni mkubwa mno katika nchi hii, watu wamekosa imani na viongozi wao wa Serikali, wamekata tamaa, wamefedheheshwa, wamedhoofika katika nchi yao kuliko miaka yote. Ni kweli imeandikwa wenye akili, akili zao zitapotea na ufahamu wa wenye busara utafichwa, hawatajua wakati wa amani wa kujiliwa kwao. Mtu apimiwe eneo lake na kupewa yeye mwenyewe sio watendaji kuuza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, historia itajirudia, sasa inajirudia kwa kupitia wawekezaji na mateso ya kutisha yanakuja kupitia wawekezaji nawaambia kama Biblia haisemi uongo hamtapata mlango wa kutokea wala pa kukimbilia, eleweni watendaji wenu ni wanyama wa kutisha wasio na kipimo; mikoani ni mateso. Ni watu wa kupenda fedha wenye kiburi, wazushi, wenye majivuno, wanaopenda anasa kuliko kumpenda Mungu.

Mheshimiwa Spika, ombi, wakuu kemeeni, karipieni, onyeni tena mkawe kitisho kwa Wakurugenzi wanaopanga safu zao za ujambazi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake ya wataalam hasa Katibu Mkuu, ndugu Kidata kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara katika mazingira magumu ya bajeti finyu. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa uamuzi wa Waziri wa kuipatia Wilaya ya Ngara, Baraza la Ardhi katika bajeti ya 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, mchakato ulishaanza kwa Wilaya kuleta majina ya wazee wa Baraza ambao hawajateuliwa mpaka sasa. Wizara iliipatia Wilaya *computer* ambayo niliibeba mimi mwenyewe. Wilaya ilitoa jengo kwa ajili ya Baraza hilo. Namshukuru sana Msajili wa Mabaraza mama Bahati Mlole kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipatia.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Baraza haujaanza naambiwa bado wataalam hawajapatikana pamoja na samani, lakini pia wazee wa Baraza hawajateuliwa ingawa majina yalishapendekezwa. Wananchi wa Ngara wenye kesi za ardhi bado wanasumbuliwa kwenda Chato, kilomita zaidi ya 200 kusikiliza kesi. Wakifika huko inabidi wakae kwenye gesti na mara nyingi kesi zao zinapigwa *date*.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana iwapo mchakato huu wa Baraza la Ardhi la Ngara utakamilika. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngara yuko tayari kutoa samani ya muda iwapo atapewa wataalam, jengo liko tayari.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa MKURABITA, mpango au mradi huu wa MKURABITA ni ukombozi wa wananchi wa kawaida MKURABITA ambao ni Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge unahitaji ushiriki wa Wizara ya Ardhi kupima mashamba ya wananchi ili wapate hati miliki za kimila ambazo zitawasaidia kama *collateral* au mdhamana wakati wakitaka kukopa benki.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngara inapakana na nchi za Rwanda na Burundi ina tatizo kubwa la kuporwa ardhi yake na wahamiaji haramu ambao hupitia kwa Wenyeviti na Vitongoji na Vijiji na kujichukulia ardhi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, iwapo Wizara ya Ardhi itashirikiana na MKURABITA kupima mashamba ya kaya zote za Vijiji 72 vya Wilaya ya Ngara na kaya mbalimbali kupewa hati miliki za kimila, tatizo la wahamiaji haramu kupora Ardhi yetu litakwisha. Mradi wa MKURABITA umeshakubali kuanza na Wilaya ya Ngara kutokana na tatizo hilo la wahamiaji haramu.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kuandika sitaunga mkono hoja kwa sababu nataka kupata maelezo ya kina kuhusu jengo la ghorofa lililoanguka na lingine linaweza kuanguka wakati wowote mtaa wa Indira Gandhi, kiwanja namba 2032/73 mali ya Ladha *Construction Limited*. Nitatoa shilingi kama nisipoelezwa ni kwa nini ghorofa dhaifu la Ladha *Construction Limited* ambalo linatakiwa kuvunjwa, lakini hadi leo jengo bado lipo na linatishia maisha ya majirani na wapita njia. Nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka baina ya Kijiji na Wilaya, naomba nipatiwe ufumbuzi wa mgogoro uliodumu kwa takriban miaka 14 sasa katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini, Kata ya Maboma, Kijiji cha Katunda ina mgogoro mkubwa na Wilaya ya Urambo kuna wakati wataalam kutoka Mkoani Tabora walipita na kubainisha mpaka, lakini mpaka huo hauendani kabisa na mpaka wa asili ambao unatambulika na wazee waliopo kuwekwa kwa alama feki za mpaka inaashiria rushwa imetumika kuwanyang'anya wananchi eneo lao la kijiji, hili halikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata yangu ya Isikizya na Ibelamilundi kuna eneo la hifadhi na mipaka ipo imebainishwa, wananchi kwa miaka mingi

wamekuwa wakiheshimu mpaka, lakini cha kusikitisha ni kwamba, mwaka jana wataalam kutoka Wizarani walikuja na kuweka mipaka upya ambayo imemega eneo kubwa la kijiji ambalo limeendelezwa. Ni kwa nini mipaka iliyopo ya zamani haiheshimiwi na kumega eneo la kijiji ambalo limeendelezwa, hii haikubaliki na nisipopata majibu, nitatoa shilingi.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, ngaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba na *Management* yote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hata hivyo naishauri Serikali sambamba na kuliondolea shirika *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi wanavyonunua nje ya nchi ifanye hivyo kwenye vifaa inayonunua hapa nchini ili shirika liweze kufikia azma yake ya kujenga nyumba 15,000 ifikapo 2015. Halikadhalika nashauri shirika liendelee kujenga nyumba Wilayani kama inavyofanya Monduli na hata vijijini ili Watanzania walio wengi waweze kuishi katika makazi bora.

Mheshimiwa Spika, ubomoaji ya majengo ya zamani: Kila nchi, kila familia, kila mtu ana historia toka alipotoka hadi hivi sasa, lakini jambo la kusikitisha hapa kwetu tunataka kufuta historia ya nchi yetu kwa kubomoa majengo ya zamani katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni jengo la Salamander. Jengo hili lilijengwa mwaka 1901, hadi linabomolewa lilikuwa tayari lina miaka 112. Je ni kwa nini Wizara yako inaruhusu uharibifu wa historia ya nchi yetu? Kama tatizo ni umri wa majengo mbona yapo majengo yaliyojengwa miaka ya 2007 na yameporomoka na kusababisha vifo? Majengo haya ni muhimu kwa historia ya nchi. Ni muhimu kwa utalii lakini pia ni muhimu kwa kuwasaidia wajenzi wa sasa ambao wengi wamekuwa wakijenga majengo na kubomoka ni vizuri wakaangalia ili wajiulize hawa wenzetu wanawezaje kujenga majengo yakudumu kwa muda mrefu na ya sasa yanabomoka.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wazanzibar wameweza kuhifadhi historia yao pale *Stone Town*. Kilwa Kivinje, Kilwa Masoko, Bagamoyo hizi zote ni historia ambazo tunahitaji kubaki nazo.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hotuba yake, tunaomba atoe tamko la kusimamisha ubomoaji wa nyumba hizo za zamani ambazo ni historia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya mipaka: Lipo tatizo la migogoro la mipaka katika Wilaya ya Monduli, Wilaya ya Arumeru na Longido na tatizo hili limedumu kwa muda mrefu sana. Mwaka juzi katika mchango wangu nilieleza

lakini hadi hivi sasa mgogoro huu haujaisha na umesababisha hadi vifo. Naomba Mheshimiwa Spika mara baada ya bajeti hii Mheshimiwa Waziri na wataalam na Wabunge tuongozane tukamalize mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali yanayotokana na ardhi ni madogo sana ikilinganishwa na makadirio yanayowekwa kila mwaka, moja ya sababu ni mawakala wa ukusanyaji kodi ya ardhi yaani Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa au kukataa kutimiza wajibu wao, kwa vile hawathamini sana fedha zitokanazo na kodi ya ardhi kwa vile Serikali Kuu huwapa fedha yaani ruzuku kwa kuzingatia hali ilivyo. Kwa nini Serikali isiajiri wakala wa kujitegemea *(tax collector)* atakayekusanya kodi ya ardhi badala ya Serikali za Mitaa?

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa afya, na sasa nachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna suala la migogoro nchini inayotokana na ardhi baina ya wakulima na wafugaji. Mheshimiwa Spika, haya makundi yote yana haki sawa na kutumia ardhi kwa usawa. Hivyo Serikali itenge maeneo kwa shughuli za wafugaji na wakulima ili wasiingiliane katika shughuli zao na maeneo yao. Baada ya kufanya hivyo ndipo sasa sheria ifuate mkondo wake kwa atakayeingilia eneo la mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wakulima kuna baadhi ya wakulima ambao wanamiliki ardhi zaidi ya hekta 100 hadi 200 wakati hawana uwezo wa kulima zote bali hekta 5 tu. Sasa kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuhakikisha kila mkulima mdogo apate hekta zisizozidi 10 ili maeneo mengine yabakie kwa wafugaji?

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna maeneo mengi tatizo ni matumizi mabaya yaliyojaa tama, hivyo kukuza na kuendeleza migogoro ya ardhi naiomba Serikali ifanye marekebisho makubwa ili kila upande ufaidike na ardhi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, migogoro kati ya hifadhi na maeneo ya Vijiji: Naiomba Serikali kupitia maeneo haya upya ili kuleta amani kati ya wananchi wa Vijiji na maeneo ya hifadhi. Mfano, eneo la Hifadhi katika Kijiji cha Luhafwe kilichopo Kata ya Mpanda Ndogo, Kitongoji cha Misanga Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Spika kitongoji hicho cha Misanga kinahati zenye baraka zote za viongozi waasisi wa Wilaya ya Mpanda, lakini tarehe 18/10/2013 Askari wa Maliasili na Polisi walikwenda kuwataka wananchi kuhama maeneo haya ya Misanga kwa kuwapiga na kuwapora mali zao kama mpunga, mbuzi, kuku

na bidhaa za madukani, na kibaya zaidi wanawake kubakwa. Hii ni aibu kwa Serikali kushindwa kuhakiki maeneo yaliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa kupitia upya maeneo hayo ili wakulima waelewe mipaka yao na hifadhi ibaki na maeneo yake na amani ya wananchi maskini ndani ya nchi yao ibaki palepale.

Mheshimiwa Spika, katika upimaji wa viwanja mijini kuna viwanja ambavyo vilipimwa muda mrefu bila kujengwa na wamiliki na kusababisha vichaka katikati ya miji kwa muda mrefu. Je, Serikali kupitia Wizara naomba itueleze ina mpango gani kwa wamiliki wanaoweka viwanja bila kuvijenga kwa muda mrefu?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na changamoto nyingi zinazowakabili.

Pamoja na pongezi hizi ninayo machache ya kuchangia ili kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Ranch* ya Kitengule (Kata Kihanga) Wilaya ya Karagwe: Mheshimiwa Spika, *Ranch* ya Kitengule iligawanywa katika vitalu *(blocks)* vya ufugaji. Vipo vitalu 13 na sehemu nyingine alipewa mwekezaji Kagera *Sugar* hekta 45,000. Kwenye Kata ya Kihanga kuna Vijiji saba ambavyo ni Mushabaigune, Kibwera, Katanda, Kihanga, Kishoju, Nyamwele na Mlamba. Vijiji vyote hivi vinaizunguka *Ranch* ya Kitengule na ni wafugaji, lakini kwa makusudi mazima wananchi hawa hawajapewa hata ekari moja kwa ajili ya mifugo yao. Wao watafugia wapi? Mifugo yao ikiingia kwenye *block* za waliopewa ardhi wanapigwa risasi. Serikali iliahidi kuwapa wananchi hawa ekari elfu mbili (2,000) tu.

Hekari 2000 si chochote kwa Vijiji saba! Ekali 2000 inatosha ng'ombe 100 tu ili hali wananchi wa Vijiji hivi wana mifugo zaidi ya 1000. Hata hivyo hizo ekari 2,000 Serikali ilizoahidi hadi sasa hazijakabidhiwa kwa wananchi wa Vijiji hivi. Je, ni lini basi hata hizi ekari 2,000 zitakabidhiwa? Pia, nataka kujua ni lini Serikali itapima upya Kitengule *Ranch* ili kuwapatia maeneo ya malisho wananchi wa Vijiji hivi na wengineo.

Je, ni kwa nini Serikali imempatia Kagera *Sugar* eneo kubwa la ufugaji wakati yeye ni mkulima na eneo hilo la hekta 45,000 hajalilima? Tunaitaka Serikali ipunguze eneo hili na wananchi wetu wapatiwe eneo la ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Baraza la Ardhi na Nyumba Wilayani Karagwe: Mwaka jana tuliambiwa kuwa Baraza la Ardhi na Nyumba litaanza kazi Wilayani Karagwe. Jengo liko tayari lakini hatuoni Baraza kuanza kazi. Je sababu ni zipi? Bado ahadi iko palepale? Na kama jibu ni ndiyo, je, ni lini Baraza hilo litaanza kazi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji umepelekea vifo vya wananchi kadhaa, lakini imebainika baadhi ya viongozi wa Serikali ngazi za Wilaya wanachangia kuendeleza migogoro hasa kwa kauli zao. Naishauri Serikali kuwaondoa katika nafasi viongozi wa Serikali walioshindwa kuzuia migogoro katika maeneo yao, hasa kuhakikisha ardhi inapimwa na kupatikana hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuuzwa kwa ardhi na mikataba mibovu ya muda mrefu inachangia mgogoro katika maeneo mbalimbali, hivyo naishauri Serikali kuangalia upya umililikishwaji wa ardhi kwa wawekezaji na mikataba mibovu ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani juu ya mashamba yasiyoendelezwa huko Korogwe na tatizo la mashamba ya Mkonge na wananchi huko Korogwe – Tanga?

Mheshimiwa Spika, tatizo la Mji Mpya wa Kigamboni limekuwa ni jambo la muda mrefu linalolalamikiwa na wananchi hasa fidia stahiki inayostahili ya kulipwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika tatizo la kuzuia wananchi wa Kigamboni kukarabati halikubaliki hivyo kama mchakato utachukua muda mrefu ni vyema Serikali mkaangalia utaratibu mpya.

Mheshimiwa Spika, pango za nyumba za Msajili ziangaliwe upya kwani wapangaji hawa ni maskini, hivyo uwezo wa kulipa umekuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Shirika la Nyumba kujenga nyumba na kuziuza ni jambo jema, lakini bei ya nyumba hizo zimekuwa kubwa, hivyo nashauri Serikali kuangalia upya mpango mkakati wa shirika la nyumba namna ya kiwango cha mabadiliko ya bei ili maisha bora kwa kila Mtanzania iweze kutekelezeka na siyo maneno.

Mheshimiwa Spika, mpango wa upimaji wa ardhi, upewe nafasi ya pekee na ushikishwaji wa wananchi ngazi mbalimbali upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya ardhi ina umuhimu wa kipekee katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Kwa vile Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa na kinategemea ardhi, pia ufugaji, viwanda na hata nyumba za kuishi zinategemea sana ardhi, ardhi ikitumiwa vizuri, uchumi wa nchi utaimarika na pia kinyume chake!

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeshindwa kabisa kusimamia kabisa matumizi bora ya ardhi. Wizara hii ya ardhi imegubikwa sana na rushwa, kiburi, uvivu, uzembe, umangimeza na kila aina ya ufisadi.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda Wizara ya Ardhi kwa shida ndogo tu kama ya kutaka kuoneshwa tu mipaka ya kiwanja au nyumba ambayo ipo Jijini Dar Es Salaam iwe Ilala, Buguruni, Magomeni au Tandika, utadaiwa rushwa ya shilingi milioni mbili (2,000,000/=).

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki na halivumiliki. Jambo la fedheha na aibu zaidi ni hawa viongozi wa juu wa Wizara hii hawawezi hata kuwapa onyo/karipio la mdomo tu seuze kuwaadabisha kinidhamu wafanyakazi wala rushwa walio chini yao! Katika Wizara hii kila mfanyakazi ana jeuri ya ajabu! Imekuwa kama Wizara ya kambare wote wana ndevu, hajulikani mdogo wala mkubwa!

Mheshimiwa Spika, msiba zaidi ni malalamiko ya wananchi juu ya kushutumiwa hata Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa Kamati imefumbwa mdomo na uongozi wa *NHC* ili wafanye wapendavyo!

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kuna ubadhilifu mkubwa ndani yake. Nyumba za Shirika la Nyumba zinapandishwa kodi sana kwa kisingizio cha kuendana na soko. Iweje nyumba za umma zilizojengwa zamani kwa misaada ya wahisani na wengine zilizotaifishwa ziwe sawa na nyumba za kisasa *(mpya)*?

Mheshimiwa Spika, ujanja wa wizi wanaofanya *NHC* ni kuzipaka rangi nyumba za *NHC* na kuzibadilisha madirisha bora yaliyokuwemo na kuweka madirisha hafifu ya *alminium* ili ukipita nje zionekane na mvuto, lakini ukiingia ndani nyumba hizo ni mbovu na zinavuja kwenye *roof* na hata kwenye hayo madirisha mapya ya *alluminium* mvua zikinyesha maji yanapita madirishani kama vile hakuna dirisha kabisa, hii ni kwa sababu *NHC* wanafanya ubabaishaji mkubwa katika kuzikarabati nyumba hizi ili wapate kisingizio tu cha kupandisha kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani kabisa na kuondolewa *VAT* vifaa vya ujenzi kwa *NHC* pamoja na kuonekana kuwa hii ni dhana nzuri, lakini kutokana na ufisadi ulioko *NHC* tija haitapatikana, vifaa hivyo vitauzwa kwa wafanyabiashara na nyumba zinazojengwa hazitoshuka bei bali watatoa visingizio vingine kama vile ukosefu wa miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Mfano mzuri wa hoja yangu hii ni nyumba zinazojengwa Mchikichini Dar es Salaam, ambazo gharama halisi ya ujenzi si zaidi ya milioni sitini (60,000) kwa *apartment*, lakini inauzwa milioni mia mbili (200,000,000/=), 200% *profit*! Huu ni wizi na jambo hili halikubaliki!

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana ni kuwa Serikali imeshindwa kabisa kurekebisha Wizara hii ya Ardhi. Bila shaka sababu ni hizo nilizozieleza, na kwa mantiki hiyo tusubiri mizozo na migogoro zaidi kati ya wananchi na wapangaji wa *NHC*, kati wakulima na wafugaji, kati ya wananchi na Serikali na kuendelea kuporomoka kwa maghorofa yanayojengwa kwa vibali *fake*.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu nataka ufafanuzi juu ya shamba la Malonje.

Mheshimiwa Spika, swali: Wapi fedha iliyotengwa katika bajeti hii kumfidia mwekezaji kama ulivyoeleza katika hotuba yako ukurasa wa 64 ili tuamini maelezo yako?

Mheshimiwa Spika, swali je, wananchi waendelee kuteseka mpaka lini? Kama kweli kesi ipo Mahakamani kama ulivyosema katika hotuba yako ukurasa 64, umesema sasa unaweza kwenda Sumbawanga kwa kuwa una majibu ya utatuzi wa shamba hilo la Malonje. Naomba utamke utaenda lini? Kwa nini usiwaambie wananchi kuanzia msimu huu waruhusiwe kulima mashamba hayo?

Mheshimiwa Spika, unasema wazi kuwa shamba hilo halijaendelezwa kama mkataba unavyoeleza, Je, kwa nini umeshindwa kuwa wazi kuisaidia Serikali kulichukua shamba hilo kuwapatia wananchi bila Serikali kutoa fidia yoyote maana mwekezaji amevunja masharti ya mkataba? Bila kupata maelezo ya kutosha natarajia kushika shilingi katika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi ya kuelezea juu ya dhuluma na unyanyasaji uliowapata wananchi hao, nategemea kufumuka kama sintapata maelezo ya kutosha.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika sana nilidhani Wizara hii ingekuwa mkombozi wa wananchi, lakini imekuwa kinyume kabisa na matarajio hayo.Wananchi wamekuwa wanadhulumiwa haki zao, wanatapeliwa, lakini Wizara iko kimya tu.  Wananchi wamiliki wa ardhi wamekuwa wanatupwa kwenye dimbwi la umaskini.

Katika Vijiji vingi sana wananchi wanakuwa wanavamiwa na watu wengine kutoka aidha Manispaa au Wizara ya Ardhi kwa kisingizio kuwa ni upanuzi wa miji na hivyo sehemu hizo siyo tena maeneo ya mashamba. Kwa kisingizio hicho wamekuwa wakilipwa hela ndogo sana na baadaye wale wanaochukua maeneo hayo kuyauza kwa bei mara kumi ya pesa walizopewa wananchi.

Wananchi hao wenye ardhi wanaachwa bila ardhi kwao na vizazi vyao na pia bila ardhi ya kilimo na ufugaji na hivyo kushindwa kuhudumia familia.

Maeneo hayo ni pamoja na Kigamboni - Dar es Salaam, Kisura - Pwani, Ikwiri/Mpalange, Rufiji, Mabwepande na maeneo mengi mengineyo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, suala la Mji wa Kigamboni ni unyanyasaji mkubwa sana ambapo sijui ni kwa sababu gani watu hawa wa Kigamboni wanapewa adhabu hii!

Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya miaka minne toka tuingie kwenye Bunge hili wananchi wa Kigamboni hawaruhisiwi kujenga, kulima wala kuendeleza kwa namna yoyote eti kwa sababu kuna mji mpya unakuja. Matokeo yake wananchi hao hawawezi kuendeleza kwa vyovyote maeneo yao, lakini wananchi kwa kuwa wengi wao ni wa kipato cha chini wamekuwa wanarubuniwa na watu wenye fedha ili wauze maeneo yao. Na kwa kuwa hawana uwezo, wamekuwa wakiuza maeneo hayo kwa bei ndogo sana. Na sasa watu hao wamekuwa wanauza hata nyumba zao ambazo zimefanyiwa tathimini.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa Serikali isiwachie wananchi hao waamue wenyewe anayetaka kubaki abaki na kama kuna mwekezaji azungumze nao yeye mwenyewe?

Mheshimiwa Spika, Kariakoo kulikuwa na wananchi wengi tu wadogo lakini kuna maghorofa yamejengwa bila wananchi hao kulazimishwa na imesaidia wananchi hao kupata kipato cha uhakika cha kuweka ubia na

mwekezaji, lakini pia wamepata majumba mbadala na kubaki na fedha za kutosha kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Bunge liingilie kati Serikali isiendelee kuwanyayasa na kuwadidimiza wananchi kwenye dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipime na kutoa hati za ardhi kwa wanakijiji ikiwa ni pamoja na hati za mashamba. Hii itawasaidia wananchi hao kutumia hati hizo kuweza kukopa na kuboresha mashamba, mifugo na biashara zao. Wananchi wako kwenye mzunguko wa umaskini ambao wamechoka kuendelea na maisha ya namna hiyo.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na Makatibu wake Wakuu kwa kazi nzuri na ngumu wanazozifanya kwa Watanzania. Malipo yako kwa Mungu, msikate tamaa na Mungu atawasimamia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kigamboni: Naomba mpango huu sasa utekelezeke. Wananchi wamesubiri kwa muda mrefu hawakopesheki hawakarabati wala hawana la kufanya. Naomba ushauri wa Kamati uzingatiwe, Serikali iangalie njia mbadala ya kutatua tatizo kwa njia nyingine. Je, tulijipanga? *Plan A* ikishindikana, *plan B* itumike.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kurasini: Walipwe fidia zao waondoke. Hali ni ileile kama Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Keko Bora: Wananchi wanataka kuvunjiwa nyumba zao na *NHC* ili wajenge nyumba kubwa, ni wazo jema. Lakini wale wananchi waliopo pale wanaenda wapi? Kwa nini wasinunue maeneo yasiyopimwa yakaboreshwa.

Mgogoro mwingine unatengenezwa Kinondoni, itajengwa lini? Wananchi wamekubali wakabomolewa nyumba zao, lakini mpaka leo ujenzi bado kama hadithi, wanaenda kuchokoza mambo mengine Temeke. *Why NHC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ardhi Plan. Je wana kibali cha *KDA*? Tunatengeneza migogoro mingine mingi, wananchi wanachukuliwa maeneo yao na yanapimwa kwa mkataba wa kugawana viwanja na mwenye shamba. Huu ni wizi wa mchana, naomba Serikali yangu ichukue hatua haraka kusimamisha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%

Mheshimiwa Spika, Ushauri: Tuunde chombo cha kupitia migogoro ya ardhi nchi nzima, kazi hii ni kubwa Wizara peke yake itakuwa ngumu watazidiwa na majukumu.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi ni Wizara yenye migogoro lukuki kiasi fulani, hii inatokana na Serikali kwa muda mrefu kutokuwa na mpango mkakati wa kupima ardhi yote nchini na kubainisha au kutenga maeneo ya ardhi kulingana na matumizi yake.

Hivi sasa kama inavyooneshwa katika hotuba ya Waziri Prof. Anna Tibaijuka, Serikali ina mipango mizuri, lakini tatizo ni utekezaji. Migogoro sugu ni mingi lakini ile iliyosambaa nchi nzima ni ile inayohusu mipaka ya vijiji na hifadhi na mgogoro baina ya wakulima na wafugaji kutokana na Serikali kushindwa kutenga maeneo ya malisho katika maeneo mengi. Swali, Serikali ina mpango mkakati gani kutatua matatizo hayo, na mpango huo utatekelezwa kwa muda gani?

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waziri anaposema kuwa miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta yake ni pamoja na (i) uelewa usiotosheleza wa wananchi kuhusu sekta yenyewe hasa sheria zake, taratibu na miongozo iliyopo, haki zao na wajibu wao, (ukurasa wa 6). Nakubaliana naye kwa sababu ni kweli kuwa wananchi wengi, wa mijini na vijijini, hawana uelewa wowote wa sheria na kanuni za ardhi. Je Serikali ina mpango gani wa kuwapa elimu wananchi ili matatizo yatokanayo na utovu wa uelewa yaishe?

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la mapato yanayotokana na sekta hii. Mapato hutokana na pango la ardhi, ada na tozo nyingine kwa mujibu wa sheria zilizopo. Wizara ililenga kukusanya bilioni 100, lakini hadi Aprill, 2014 ilikuwa imekusanya bilioni 37.03 tu. Na mapato ya Shirika la Nyumba linalosimamiwa na Wizara yalikuwa shilingi bilioni 55.63 hadi kufikia April 2014. Mapato haya ni kidogo sana kwa sekta hii. Kwa uzoefu wa nchi nyingine, mfano, Japan, China, Urusi na kadhalika, mapato haya yanaweza kuongezeka mara nyingi sana iwapo Wizara ingechukua hatua za haraka kuwekeza fedha za kutosha katika urasimishaji wa ardhi yote ya vijiji, upimaji wa miji midogo yote, na urasimishaji wa makazi holela katika mijiji na majiji. Kwa nini Wizara isikope fedha ya kutosha ili zoezi la urasimishaji wa ardhi yote ya vijiji, upimaji wa miji midogo yote na kadhalika likamilike mapema na Wizara ipate mapato ya uhakika zaidi?

Mheshimiwa Spika, nitaongelea Mpango wa Kina wa Makongo ambao Waziri amekuwa akiuzungumzia kwa muda wa miaka mitatu. Katika hotuba yake ya sasa ameugusia ukurasa wa 30. Waziri alipoanza kuulezea mpango huu

miaka michache iliyopita, wakazi wa Makongo waliupokea kwa hisia tofauti, kuna waliounga mkono na wapo waliopinga. Tatizo kubwa linahusu tozo ya maboresho *(beterment fee)* ambayo inapaswa kulipwa na wakazi.

Katika hotuba yake amesema zoezi la kuhuisha mpango huo limeanza tena na kwamba awamu ya kwanza ya utekelezaji wa zoezi hili itahusisha upimaji wa barabara kuu. Barabara inayotajwa hapa tayari imepangwa kujengwa na Wizara ya Ujenzi (tazama Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mei 2014), ukurasa wa 207 ambayo imetengewa shilingi 1,500,000,000,000 (trilioni 1.5). Cha kushangaza ni kwamba katika hotuba ya Waziri hakuna mahali popote ambapo watu wamejengewa barabara kisha wakalipa tozo ya maboresho.

Mheshimiwa Spika, Waziri aeleze kinaganaga kama utaratibu wa tozo ya aina hii unaihusu Makongo Juu tu. Kwa mtazamo wa kawaida, kama maboresho yatahusu mambo mengine (soko, shule, na kadhalika) inawezekana ikawa halali kulipa tozo ya maboresho, lakini si ujenzi wa barabara kuu. Tafsiri ya mwongozo wa upangaji na usimamizi shirikishi wa matumzi ya ardhi ya vijiji inasubiriwa kwa hamu (ukurasa wa 38 wa hotuba) baada ya mwongozo huu kutafsiriwa usambazwe ili wadau wote wafahamu haki zao na wajibu wao.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa hotuba nzuri. Baada ya pongezi napenda kuchangia kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa mradi wa kupima viwanja, lakini niombe Serikali iangalie namna ya kupunguza bei za hivyo viwanja. Naamini upimaji unafanyika kwa nia njema, lakini Halmashauri nyingine zinafanya biashara badala ya kutoa huduma kwa wananchi. Naomba leo Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusu gharama (bei) za viwanja.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Shirika la Nyumba wasaidie kuijengea Halmashauri ya Morogoro nyumba za wafanyakazi katika Makao Makuu ya Mvuha, Halmashauri iko tayari kuwapatia eneo la kujengea.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri leo hii atoe tamko kuhusu shamba namba 217 lililoko Mkulazi ambalo niliomba wananchi wanaohama kupisha bwawa la Kidunda wapewe angalau ekari 3,000 ili wajenge makazi na wapate mashamba. Aidha shamba namba 362 katika kijiji cha Pangawe hatimiliki yake ilikwisha na shamba linarudishwa Halmashauri ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza ni Wizara kuamua kumrudishia mwekezaji ambaye sasa anadiriki kuiambia Halmashauri inunue ardhi kwake.

Hivi sasa hili shamba ni la nani? Ni lini Wizara ilifuta barua waliyoiandika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Mheshimiwa Waziri awatamkie wananchi wa Kidogo kuhusu hatma ya mgogoro wa shamba la Kidogo ambalo lilimilikishwa kwa mwekezaji wakati kesi ikiwa Mahakamani pamoja na kuwekewa zuiyo (*stop/caveate*) na wananchi wa eneo hilo. Suala hili Mheshimiwa Waziri analijua na aliahidi kulishughulikia lakini mpaka sasa hajasema lolote. Kuchelewa kwa Waziri kumesababisha athari ya wananchi kubomolewa nyumba zao na kuharibiwa mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, naomba hatua za haraka zichukuliwe ili kusijetokea athari mbaya zaidi kwani pande zote za mgogoro zimekasirika.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kama Mheshimiwa Waziri atatoa matamko kuhusu mashamba niliyoyatamka hapo juu. Nawatakia utekezaji mwema wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Msajili wa Ardhi kwa kazi nzuri pamoja na uadilifu wake kwa Watanzania. Mama huyu ni mfano wa kuigwa katika Wizara hii. Naomba mamlaka husika itambue uzalendo wake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijatoa mchango wangu, naomba nitamke hapa kwamba na mimi naunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, humu ndani yamesemwa mambo mengi na ndiYo maana tumeona kuna haja ya kuchangia kwa sababu sisi na wizara hii ambayo inatoa hotuba yake na inatoa mapendekezo ya bajeti, tunafanya kazi kwa karibu sana. Ndiyo maana tunafikiri kwamba kuna haja ya kusema angalau kujaribu kufafanua yale ambayo yamesemwa.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo limezungumzwa hapa la kutoa elimu kwa ajili ya Watendaji waliopo katika Halmashauri na kujaribu kuwaelekeza Wenyeviti wetu wa Vijiji pamoja na Watendaji wetu. Sisi kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hatuna tatizo kabisa na suala la kutoa elimu kwa ajili ya watu wetu. Nani hapa duniani anaweza akasema usitoe elimu? Elimu ni afya ya ubongo. Kama watu wakipata elimu, wataelewa vizuri na watafanya vizuri zaidi. Kuishi ni kujifunza na kujifunza ni kuishi vizuri zaidi.

Kwa hiyo, hili sisi tunalipokea, ni wazo zuri, limetolewa na Waheshimiwa Wabunge na tutakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa pia hapa habari ya migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Niliwahi kujibu swali hapa na ninaomba kurudia tena. Waziri Mkuu aliagiza Wizara zinazohusika na masuala haya ya maendeleo ya ardhi tukae kwa pamoja; na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka utakumbuka tuliwahi kukaa wote kwa pamoja tukazungumzia masuala haya kwa karibu, lakini bado kuna maelekezo ya Serikali kwamba tuendelee kukaa na kufikiri vizuri kwamba tunaondoaje matatizo haya. Ni pamoja na yale mapendekezo ambayo yataletwa na Waziri wa Mifugo kuzungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini tumewahi kurudia tena hapa, tukasema kwamba ukitaka kuondokana na tatizo hili; na bahati nzuri tunashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia; hapa kinachozungumzwa ni kuhusu matumizi bora ya ardhi ambayo ni lazima useme eneo hili tutatumia kwa ajili ya mifugo na litumike kwa ajili ya mifugo tu. Ni lazima useme eneo hili litumike kwa ajili ya kilimo, na litumike kwa ajili ya kilimo tu. Ni lazima useme eneo hili litatumika kwa ajili ya watoto kubembea, watumie watoto! Ukisema hii ni *open space,* basi iwe ni *open space!*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwa niaba ya Waziri Mkuu na kwa niaba ya Waziri wa Ardhi. Tutachukua hatua kali sana, na tunaendelea kuchukua hatua. Haiwezekani eneo hapa Halmashauri imetoa na imejulikana kabisa eneo hili ni kwa ajili ya kazi hii *and yet* unakuta linatumika. Habari ya *double allocations* limezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka, kwa sababu muda wetu ni mdogo na mfupi, niseme kwamba, Mheshimiwa Bwege amezengumzia kuhusu migogoro ya ardhi iliyopo katika Halmashauri ya Kilwa na katika Mkoa wa Lindi. Amesema unajua, Mwanri nampenda sana, lakini msanii!

Mheshimiwa Spika, tukisema mambo *serious* ya nchi hapa, tuongee tuseme maneno *serious* hapa. *Equally* Bwege namheshimu sana! Tumeondoka hapa, tumekwenda Lindi nzima tumefuatana na Mwenyekiti wa CCM, Mzee Mtopa na Mbunge mwenzake yupo hapa. Tumefika kule, tumemaliza, tumetoka pale nimetoa *booklet* nzima, tukaagiza kwamba Mkuu wa Mkoa aunde Kamati ya kufuatilia mambo haya!

Mheshimiwa Spika, eneo la *TPDC* tunalozungumza hapa, limekubalika kwamba nusu ya eneo hilo lirudishwe kwa wananchi pale. Huo ni usanii huo! Unarudisha nusu ya eneo lote la *TPDC!* Ndani kule kuna mapendekezo hawa wananchi 26 wanaozungumzwa hapa, imetamkwa kwamba hao nao kuna

mapendekezo ya kuwafanyia fidia ambapo Mheshimiwa Bwege pia ana *interest* kule ndani, ningetegemea angesema hilo jambo hapa.

Mheshimiwa Spika, tumeondoka hapa, hawa Viongozi tunaowasikiliza hapa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana! Wanachohitaji hapa ni kutiwa moyo na kuwaambia, jamani tuna-*appreciate* kazi yenu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Profesa wakati watu walikuwa wanazungumza habari zake, wapo waliokuwa wanasema tunafurahi Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri inayofanyika. Haya maneno siyasemi kwa sababu eti kwamba nimekuwa-*offended*; nataka kusema kwamba nimekaa katika vikao mbalimbali na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ninaelewa mazingira magumu ambayo anafanyia kazi. Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake tumpe! Tusifike mahali tukamkatisha tamaa akaanza kusema, liwalo na liwe, akaenda akakaa.

Mheshimiwa Spika, huyu ni Mwanamama ni shupavu, amekwenda mpaka Umoja wa Mataifa, amefanya mambo makubwa, Mataifa yanamheshimu. Akirudi hapa, kama kuna mambo mazuri ameyafanya, tuseme amefanya kazi nzuri. *It is my judgment as a member of Parliament.* Yapo mambo ambayo Kiongozi huyu amefanya ambayo tunahitaji kumsifu na kusema kwamba amefanya kazi nzuri. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hilo.

Mheshimiwa Spika, hili lingine lililosemwa hapa, Mheshimiwa Nundu amezungumza kuhusu vile viwanja sita kule Tanga. Tumezungumza na Halmashauri ya Jiji na tumekubaliana. Tumekwenda kukagua na tumekubaliana; tumeagiza Halmashauri na wamesema watakwenda kuangalia, na *notice* imetolewa ya siku 90 ili wakaangalie tena upya kuhusu eneo hili linalolalamikiwa na ikionekana kwamba kwa kweli limekinzana na mazingira, basi tutafuta.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limesemwa hapa ni kuhusu ndugu yangu *home boy* wangu, Mheshimiwa Freeman Mbowe. Ni kweli jambo hili limezungumzwa; na Mheshimiwa Rais alipokuja, *once up on a time*, Siha ilikuwa ni sehemu ya Wilaya ya Hai na yapo haya malalamiko hapa. Kilichoagizwa hapa, kilikuwa kwamba Mkuu wa Mkoa aunde Tume Maalum, Kamati ambayo itashughulikia jambo hili na imefanya kazi hiyo. Sasa kilichoagizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai ni kwenda kufanya uchambuzi wa kina na kuangalia jambo hili na kuangalia hizo fidia zinazozungumzwa zipo katika sura gani. Ndiyo tumejaribu kuulizia! Kwa hiyo, sisi tutaendelea kufuatilia; na yeye mwenyewe ni Mjumbe katika Halmashauri ya Wilaya kujua kwamba wamefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na chochote kitakachoamuliwa kwa sababu nimesikia barua imesomwa hapa katika hotuba yake kwamba ilikwenda kwa Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, lakini yale maeneo yanayotamkwa hapa kwamba yanaombwa yafidiwe, yapo Siha. Yale ni maeneo ya Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, tukizungumza, ajue anazungumza habari ya Wilaya ya Siha. Sina matatizo na madai anayosema na hizo fidia ni kweli kama anavyosema hapa. Mkuu wa Mkoa ameagizwa kwamba afanye kazi hiyo. Kwa hiyo, tutamsikiliza Profesa kwamba yeye anaona ni sehemu gani itakayotolewa, lakini nilitaka nijibu hapa kwa upande wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nafikiri nimemaliza, la Tanga nimelimaliza, *TPDC* nimemaliza na suala la elimu nimelimaliza. Majengo pacha haya yaliyozungumzwa hapa. Tuliitwa hapa na nilijua Waheshimiwa Wabunge wana-*interest* sana. Wale viongozi wote waliohusika na jambo lile pale Ilala, wote wamewekwa ndani na kesi ile imekuwa ni *murder case*. Kwa hiyo Fuime na wenzake wote na wale wengine wote waliwekwa ndani.

Kuhusu suala la jengo lile la pili kwamba livunjwe, halikuweza kuvunjwa kwa sababu yule bwana alikwenda akaweka pingamizi na ile kesi ikaenda Mahakamani. Ilipofika pale na *notice* zilikuwa zimeshatolewa ili liende likavunjwe.

Mheshimiwa Spika, kuvunja jingo, huvunji wewe, unamwambia yule mwenye jengo, vunja jengo. Asipovunja jingo, unamwambia nakupelekea *notice*, sasa nakuja kulivunja na nikivunja utalipia gharama zote. Ndicho kilichotokea, kesi hii ikaenda Mahakamani. Baada ya hapo, hatukuwa tena na jinsi nyingine. Lakini wale watumishi *administratively* wote waliohusika na jambo hili wamechukuliwa hatua na hivi tunavyozungumza wako ndani kwa sababu hii imekuwa ni *murder case*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa natamwita Mheshimiwa Mtoa hoja wa kwanza, Naibu Waziri. Kutokana na uzito wa maneno mliyoyasema atapata dakika thelathini.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya dakika thelathini ili niweze kutumia kwa ajili ya kupitia angalau kwa yale ambayo tutaweza kuyasema kwa sababu kwa kweli kwa hoja zilizosemwa na uzito wake ni nyingi na zingehitaji muda zaidi pengine hata ya huo, lakini hata huo tunashukuru.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya kufanya hivyo, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Ubunge, lakini na sasa ambapo nafanya kazi hii ya Unaibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nawashukuru sana na ninaomba waendelee kunipa ushirikiano huo.

Pili, namshukuru sana mke wangu Mariana kwa namna anavyonipa ushirikiano na kufanya kazi yangu iwe nyepesi zaidi.

**SPIKA:** Sema, hatushukuru tena wadada hao siku hizi. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hoja zilizosemwa hapa ni nyingi na pengine siyo rahisi kuweza kumjibu Mbunge mmoja mmoja, lakini nimejaribu kuchukua zile za jumla na baadaye nikipata muda nitaendelea na zile zinazomgusa Mbunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa jambo kuhusu upimaji wa ardhi nchi nzima na Wabunge wote wamechangia vizuri na wamesifia kwamba mpango huu ni mzuri ingawa kwa kweli walionesha wasiwasi kwamba: Je, uwezekano huo upo? Maana wanaamini kwamba kunatakiwa uwekezaji mkubwa wa fedha, lakini je, na muda tulionao na changamoto zilizopo, tunaweza?

Mheshimiwa Spika, sisi tumeanza kujaribu; tumeanza Mvomero, tukitoka hapo tutaenda Kilosa na ikiwezekana Wilaya nyingine za nchi hii. Dhamira yetu ni kwenda nchi nzima. Lakini tunadhani pengine kasi hii na rasilimali zinazohitajika ni nyingi mno. Kwa mfano, kwa Mvomero tu kwa asilimia 20 ambayo tumeipima na tumepima mashamba 1900 na kitu na maeneo mbalimbali ya makazi katika vijiji kadhaa tu, kwa asilimia 20 ya Wilaya ya Mvomero tumetumia zaidi ya Shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona mpaka tumalize Mvomero nzima inaweza kuwa zaidi ya Shilingi bilioni moja na kiasi fulani. Fedha hizi ni nyingi, lakini tumejaribu kuongea na watalaam, wanasema, kama tulivyokuwa tumekubaliana mwaka jana, 2013 kwamba tungenunua mtambo wa *satellite receiving station* tuliokuwa tunataka kuuweka Dodoma, tukinunua mtambo huu ambao gharama yake wanasema ni kama Shilingi bilioni 20, tungeweza kupima nchi nzima kwa kasi kubwa, kwa gharama ndogo, lakini kwa faida nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge ninyi ni wajibu wenu kutushauri na leo mmefanya kazi kubwa sana ya kuishauri Wizara yetu. Kazi hii mnayoifanya

mnatekeleza wajibu wenu, lakini na hili nalo tunadhani tukishauriana vizuri, tukalifanya, itatusaidia kupata mtambo ambao utatusaidia sana kuweza kupima nchi nzima, lakini pia utakuwa una faida nyingi katika Sekta nyingine za Maliasili, Kilimo, Madini, Sensa, Miundombinu, Ulinzi na Usalama na mambo mengine. Mtambo huu utatusaidia, lakini pia utaingiza fedha nyingi kwa sababu hata majirani zetu wanaweza wakautumia.

Kwa hiyo, mimi nadhani hii ni fursa ya pekee, tuwahi, tufanye hivyo na Wizara tunataka tujipange, tunaomba *support* yenu ili tuweze kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limezungumzwa ni suala la migogoro ya ardhi; imezungumzwa kwa kiasi kikubwa sana, karibu na kila Mbunge amesema na wale waliosema wameweza kusema hivyo, na ambao hawakusema, naamini wanayo migogoro mingi wangeweza kusema. Jamani, migogoro ya ardhi ipo, hata tukipima itaendelea kuwepo. Kwa sababu ushahidi uliopo ni kwamba hata maeneo yenye mipaka na yanayojulikana na yenyewe bado yana migogoro. Kwa hiyo, hapa ni suala la sisi sote kuwajibika kama Taifa, kwanza kufuata sheria, lakini pili mamlaka zote za utawala lazima ziwajibike na masuala haya.

Mheshimiwa Spika, nasema mbele ya Waziri Mkuu kwamba mahali ambapo kumetokea mgogoro, wapo watu waliofanya uzembe, lazima! Ni lazima kuna watu wamefanya uzembe kwenye ngazi za chini. Kama hivyo ndivyo, basi kama kumetokea mgogoro, huyo Mkuu wa Mkoa na Mikoa ya jirani waulizwe kwanza; Wakuu wa Wilaya zilizopo pale, waulizwe kwanza; Afisa Tarafa, Mtendaji wa Kata; ukishuka mpaka chini utajua chanzo cha migogoro ni nini. Migogoro mingine hii inasababishwa na utawala wa watu wa chini ambao wanaisababisha kwa mambo ambayo pengine kama mtakaa hapa mtasema Wizara, Wizara kazi yake ni *approval* tu.

Sisi tunasema, una eneo hili, ukishapima sisi tunakupa hati. Tukishakupa hati, ni juu yako wewe na jirani yako kuishi vizuri. Sasa kama wewe unamwingilia jirani yako, halafu unauita mgogoro, ndiyo maana Waziri wangu anasema, na ninamshukuru sana kwa namna ninavyofanya naye kazi, anasema hakuna migogoro ya ardhi ila kuna migogoro ya watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwamba katika hii migogoro, ni lazima sote kama viongozi tushirikiane. Watu wanauana, rasilimali watu inapotea. Amani inapopotea, watu wetu wanakuwa masikini. Tukikaa hapa ukasema Simbachawene na Waziri wake, Mheshimiwa Tibaijuka watamaliza migogoro hii, kwa kweli haiwezekani. Tushirikiane wote, sheria zipo na vyombo vyote vitekeleze wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, mashamba yaliyokuwa ya Serikali ambayo hayajaendelezwa na wananchi sasa wanateseka; mashamba hayo ndiyo yaliyokuwa yamechukua ardhi nzuri, ardhi ambayo ndiyo yenye rutuba leo, na sasa mashamba haya hayaendelezwi na hata walioyanunua hawatekelezi mikataba kadri walivyokubaliana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la mashamba kwa kweli nikubaliane na Wabunge wengi walivyosema. Haiwezekani mtu akachukua shamba asiliendeleze, halafu wananchi wanapolitamani kwenda kutaka kuzalisha pale anawakodisha. Huo ni ukabaila ulikwishapita, Nyarubanja ilikwishafutwa na Sheria ya Ardhi inakataza. Hii haikubaliki! Ni lazima tuchukue hatua kali na za haraka kuhakikisha kwamba wale wote waliokiuka mikataba, tunafuta umiliki wao. Hili ni lazima litanyike, na litafanyika kwa kuanzia na wadau mlioko chini. Mapendekezo yakija, mkatoa mapendekezo, huko kwenye Wilaya na Mikoa ndiko mliko na mashamba hayo. Mkishaleta mapendekezo yenu, sisi hatutasita kuchukua hatua na nikubaliane kwamba baadhi ya Halmashauri zimeleta mapendekezo na yapo katika mchakato wa ufutwaji.

Mheshimiwa Spika, ufutwaji siyo jambo la haraka haraka; hata anayefuta ni lazima ajiridhishe kwanza anachofuta kinafutwa katika uhalali namna gani. Maana wakati mwingine unaweza ukafuta halafu ukaleta mgogoro mwingine.

Katika mchakato huo, ndiyo maana pengine kuna uchelewaji, lakini hatua na maamuzi ya Serikali ni kwamba tumechukua, tumefanya *evaluation* ya mashamba yote na sasa tumeamua kwamba yale ambayo yatakuwa hayakidhi mikataba iliyokuwepo tunayafuta na kuwamilikisha wananchi ili waweze kuyatumia katika kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; yapo maoni yametolewa kwamba Mabaraza haya hayafanyi kazi vizuri, yapo maoni yametolewa kwamba tuyaboreshe, lakini pia yapo maoni yametolewa kwamba Mabaraza haya ni bora tuyarudishe kwenye muhimili wa Mahakama. Tumesikia, Serikali inaendelea kufanya tathmini na Tume ya Kurekebisha Sheria imeleta mapendekezo yake juu ya Mabaraza haya. Bado katika Serikali tunaendelea kutafakari tuone njia ipi ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba wananchi wanateseka kwa sababu mabaraza ni machache na tulikusudia na malengo yale tuliyotaka hatujafikia. Ni kwamba baadhi ya Mabaraza ambayo tulikuwa tumeyapitishia bajeti yake kwa mwaka 2013, nataka niwahakikishie, yale matano ambayo tulikuwa tumepitisha, hadi Julai mwaka huu, 2014 tutahakikisha kwamba Mabaraza hayo yameanza.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu uporaji wa ardhi unaofanywa na makampuni ya upimaji kwa kushirikiana na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni jambo linalosikitisha. Ni kweli Sheria ya Upimaji inaruhusu Makampuni binafsi kufanya kazi hiyo. Lakini sheria ile hairuhusu makampuni binafsi kupora ardhi ya wananchi. Ndiyo maana rafiki yangu Mheshimiwa Bungara alisema kwamba kuna shamba lililokuwa linajulikana ni la Sumry, lilitelekezwa mwaka 1958, umiliki wake ulikuwa haujulikani mpaka baadaye. Imeibuka kampuni moja tu, imekwenda, imepima, imemtengeneza mmiliki pale, akajiita yeye ni wa familia ile, wamechukua ile ardhi na wananchi waliokuwa wanaishi mle, wakasema hamna fidia, mlikuwa mnaishi ndani ya shamba. Hii haikubaliki!

Mheshimiwa Spika, kutakapotokea mazingira ya namna hiyo ambayo hayashirikishi wananchi, lakini wananchi wamevamiwa katika maeneo yao kwa visingizio vyovyote vile kutokana na Makampuni hayo, upimaji huo sisi kama Wizara hatutaukubali na hatutaupitisha na hatutautambua. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kueleza mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba upimaji wa shamba la Mpara, la Lindi, Kilwa, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na umilikishaji wake, ninaufuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mengine yote ambayo yataonekana na mazingira hayo, tutayafuta. Katika Sheria ya Mipango Miji, hata kama ni Mji unatanuka, wewe ni Mamlaka ya Ardhi, huwezi ukafanya bila kushirikisha wananchi wanaoishi maeneo yale. Ushirikishwaji ni jambo la lazima na kama hukushirikisha, basi mchakato huo wote ulioufanya siyo halali kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, nizionye na kuzitaka Halmashauri zote nchini na mamlaka zote za ardhi nchini kuhakikisha kwamba zinafuata sheria bila kuweka ubabaishaji. Vinginevyo kazi hiyo wanayoifanya na umilikishaji wa watu hawa watakaokwenda kujimilikisha kwa kutumia kazi ambayo haikufanywa kihalali katika mipango ile, hautatambulika na hivyo watakuwa wamepata hasara bure.

Lingine ni suala la *National Housing. National Housing* imepongezwa sana, wengine wanasema inafanya kazi nzuri na mmeipongeza sana.Ni kweli inafanya kazi nzuri na mmejaribu kuisemea hapa kwamba waondolewe *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi, lakini waondolewe *VAT* kwenye nyumba zilizokamilika. Hoja ya *National Housing* ambayo tunaifahamu ni kwamba *National Housing* wanaomba kuondolewa *VAT* kwenye nyumba zilizokwishakamilika, lakini siyo kwenye vifaa. Nyumba hizi zilizokamilika ni zile ambazo thamani yake ni chini ya Shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Mtu anayeweza kununua nyumba ya Shilingi milioni zaidi ya 100, huyo ni tajiri. Sisi tunataka nyumba za masikini

ndizo ziondolewe *VAT* ili masikini waweze kununua nyumba. Hawa watu wa kipato cha chini ndiyo wanaotakiwa na ndiyo lengo la Serikali. Hili Serikali tunajaribu kulijadili tuone namna gani tunaweza tukaiondoa *VAT* hiyo katika wigo huo wa watu wenye uwezo wa kununua nyumba ya chini ya thamani ya milioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limesemwa ni kwamba nyumba za *National Housing* ziuzwe. Hili limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Yako maeneo yanadiwa kwamba yalikuwa yamesemwa yauzwe na kwamba kulipitwa Azimio la Bunge na hapa Mheshimiwa Mtemvu amesema. Kwa mujibu wa Sera ya *National Housing* ya sasa iliyopitishwa na Bodi yake, sasa hawauzi tena nyumba zao za zamani kwa sababu zile nyumba za zamani ndiyo *land bank* yao wanayobakia nayo, na ile ndiyo nguvu yao. Maeneo hayo yanayodaiwa kuuzwa hizo nyumba, ni maeneo ambayo leo hii ni *prime areas* ambayo wanaweza waka-*demolish,* wakaweka *investment* kubwa na Shirika likaendelea kustawi na ndiyo maana leo mnalisifia.

Mnalisifia kwa sababu ya uwekezaji uliofanywa kwenye maeneo ambayo ni *prime* iliyokuwa inayamiliki. Sasa kama litakuwa linaanza kuyauza, kesho tutabaki na nini? Haitakuwepo *National Housing* tunayoisema hii na malengo ya nyumba 15,000 hayatafikiwa. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, jambo hili ni vizuri tukalikubali kwamba *National Housing* inaendelea leo kwa sababu ya mazingira yaliyokuwepo na mazingira iliyoachiwa na Serikali.

Pia *National Housing* imeombwa kwamba wajenge nyumba katika maeneo mbalimbali. Maombi yako mengi, lakini pamoja na kasi ya uwekezaji wa *National Housing,* hawataweza kufanya kwa mara moja. Sisi tuko tayari kushirikiana na Halmashauri zote nchini, siyo tu kuwajengea nyumba kwa fedha zetu, hata pale wanapokuwa na fedha zao. *National Housing* wako tayari. Kwa hiyo, tunawakaribisha.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa hapa ni ardhi. Tukishafika huko, tukitaka kuweka huo uwekezaji wa *National Housing,* ardhi inaruka bei tayari kwamba *National Housing* wamekuja, sasa muwauzie kwa bei kubwa. Ni dhahiri kwamba watashindwa na hawataweza kufanya kile ambacho mlikiomba au kukusudia. Kwa hiyo, tutafutilieni ardhi. Ukileta mpango wako, tafuta na ardhi kabisa, tuonyeshe na ardhi uone sisi tutafanya jambo gani.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa jambo lingine kuhusu *squatter.* Mheshimiwa Mbowe kalizungumza kwa nguvu sana kwamba *everywhere squatter. Dar es Salaam squatter, Moshi squatter,* wapi *squatter,* kila mahali *squatter.* Lakini sisi ni viongozi, hizi *squatter* tunazijua chanzo chake.

*Land Authority* na *Land Planning Authority* ziko chini. Halmashauri zetu, Miji yetu ndiyo *Land Authorities*, ndiyo *Planning Authority,* sisi Wizara ni *approval.* Tuwaulize huko nyinyi, kwa sababu Wabunge mko kule na hakuna mabadiliko ya matumizi ya ardhi, hakuna chochote kinachoweza kufanyika Wizarani kama hakijatoka na hakijapitishwa na Baraza la Madiwani. *(Makofi)*

Hii mikanganyiko yote, hizi *squatters* unazozisema, leo unasema jamani tulieni hapa tunataka tupapime, unashangaa wanakwambia, mimi nimeruhusiwa, najenga. Ameruhusiwa na Mamlaka! Hilo eneo wewe huja-*declare* kuwa *planning.*

Sasa mimi nasema, hapa tushirikiane wote, ni wadau katika hili. Kama tunataka *squatter* nchi hii zisiwepo, sote tushirikiane; Madiwani na Serikali tushirikiane. Leo hii unashangaa; tusizungumze *squatter.* Tukitaka kupanga hata Miji tu kwamba hii barabara imewekwa kwa ajili ya kupita watu, hii barabara imewekwa kwa ajili ya kupita watu gani; inashindikana kwa sababu leo hii ukisema jamani sasa Wamachinga tuwaweke hapa, msije huku. Hapo inageuka siasa! Nani anayependa kupoteza? Hao Wamachinga kura zao wote tunazitaka! Kwa hiyo, tunabakia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusilaumiane. Leo unasema, msiwaguse, mnawaonea, watu masikini! Leo mkija mnasema *everywhere is squatter, no!* Tukubaliane wote! Siku moja hoja ya Kambi ya Upinzani iseme, tuwaondoe watu wafuate sheria, wasikae hovyo; iseme hivyo! Tutaona kweli mko *serious!* Lakini siyo kutulaumu tu kwamba kila mahali *squatter*, kila mahali *squatter. Squatter* ni kwa sababu ya Mamlaka ziko nyingi huko, lakini sote sisi ni viongozi. Tushirikiane tuhakikishe kwamba *squatters* zinapungua na kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu utoaji wa Hatimiliki zile kubwa na zile za kimila. Hatimiliki hizi zinatolewa; kasi ya kutolewa ni ndogo. Tumeweka utaratibu, sasa tumeweka kwenye Kanda Mamlaka za Upimaji na utoaji wa Hati. Tunadhani tumeongeza kasi kwa kiasi fulani, lakini tunaweza kuongeza zaidi kama tutaingia kwenye mfumo wa kielektroniki zaidi na uwekezaji huo na mtaona hata kwenye vitabu vyetu tumeonyesha kwamba tutaendelea kuwekeza katika mpango wa kisasa wa ku-*manage land system,* kwamba angalau mtu akiomba aweze kupatiwa hati haraka na isiwe anapitia kwa watu. Maana ile ndiyo inayosababisha ku-*tempt* hata vijana wetu kuweza kujishirikisha kwenye rushwa na mambo mengine. Tunadhani tukiingia kwenye *system* ya elekroniki itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, limesemwa hapa na Mheshimiwa Chibulunje alisema kwamba hati za kimila hazitambuliki kwenye Taasisi za fedha. Kwa tafsiri ya kisheria ninayoifahamu, hati za kimila ni nzuri tu na zinafaa kama zilivyo hati

nyingine za umiliki wa ardhi. Sasa katika *practice* inaonekana baadhi ya mabenki yanakataa. Hii ni changamoto, lakini mimi nasema tukitafsiri vizuri Sheria na hata haya mabenki yakitafsiri vizuri Sheria ya Ardhi, Sheria Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999, hati hizi ni hati zinazoweza kuweka dhamana isipokuwa tu itategemeana na kiwango cha dhamana ambazo zinaweka. Hati kubwa itaweka dhamana kubwa zaidi, lakini hati ya kimila itaweka dhamana ndogo zaidi. Nami nafikiri lengo la watu wetu wa kijijini siyo kukopa mabilioni ya pesa lakini kukopa fedha kiasi cha kuweza kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa hapa mambo mengi. Hili la Kigamboni niliache, litazungumzwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini Mheshimiwa Mfaki alisema Wilaya ya Chemba upangaji wa Miji na mambo mengine na Waheshimiwa abunge wengi wamesema hili kwamba maeneo yao wangependa yapimwe. Tunaweza tu kupima endapo tutakubaliana na kushirikiana katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono. Sasa hivi tuko katika mchakato wa Kiserikali wa kuhakikisha kwamba wale ma-*Land Officer* wa kwenye kila Wilaya wanawajibika kwenye Wizara ya Ardhi. Hii itatusaidia ili tuweze kuwawajibisha pale wanapokwenda kinyume. Mtuunge mkono hili wakati wowote na mahali popote mtakapoliona. Itatusaidia sana! Lakini hawa wakiwajibika kwetu, tutaweza kuwatuma vizuri na hivyo upimaji wa kila Wilaya unaweza ukafanyika na kila mahali unaweza ukafanyika.

Pia Halmashauri zetu ziwekeze kwenye ikama ya watumishi, lakini vile vile ziwekeze katika kutenga fedha kwa ajili ya hata maandalizi ya huo upimaji. Tukingojea *program* ya Wizara *program* ya Serikali nzima pengine inaweza ikachelewa na hivyo kwa hatua za haraka tunaweza tukaanza hata kupima baadhi yetu kwa maeneo tunayoishi katika Wilaya zetu. Zimezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wengine, Mheshimiwa Ngonyani na yamezungumzwa mashamba ya mkonge, alizungumza Mheshimiwa Ngonyani na Waheshimiwa wa Tanga kama kaka yangu Mheshimiwa Omari Nundu na wengi wamesema.

Mheshimiwa Spika, lakini masuala ya mashamba haya ambayo yalikuwa ni ya Serikali, sasa wananchi wanaongezeka, *seriously in a serious note* ni lazima tufikie maamuzi. Kama nilivyosema, baadhi tunataka kuyafuta, lakini na ninyi leteni maoni yenu kwa uwazi yaliyopitia katika ngazi zote kwa sababu ninyi ndio mnaojua na kuona hayo mashamba na sisi hatutasita kuchukua hatua.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, amezungumzia masuala ya maeneo ya wazi na hapa niliunganishe

maeneo ya wazi ambayo yalisemwa pia na Kamati. Maeneo ya wazi kwa mfano kama ya Dar es Salaam, ni kweli yamevamiwa. Katika muda mchache ambao tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri, tumejaribu kupambana, tumeweza kuyakomboa machache. Ukombozi huo wa machache, unatokana na maamuzi yaliyofanywa na Mamlaka za Halmashauri, hususan Halmashauri ya Kinondoni ambayo nayo Sheria inairuhusu kufanya baadhi ya maamuzi kwenye ardhi iliyoko katika eneo lake. Vivyo hivyo katika Wilaya nyingine. Kwa hiyo, ninaposema masuala ya matumizi bora ya ardhi, masuala ya mipango ya Miji yetu ni lazima Halmashauri na Miji yetu na yenyewe wajitahidi kufuata sheria. Hili ndiyo jibu kwa hoja inayohusu eneo hili.

Masuala mengine ya Nyamongo na fidia, haya tutajaribu kuona, tukutane na Mheshimiwa Nyambari tuweze kuona maelezo zaidi tuyapate kwamba limekwama wapi kwa sababu fidia ilikuwa imekubalika. Inayolipa fidia siyo Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi tusimamia tu *evaluation,* lakini hatulipi fidia.

Mheshimiwa Hamoud Jumaa amesema tupime nchi nzima, hili nimeshalisema; lakini akaomba *National Housing* na migogoro kwenye maeneo yake kwamba *National Housing* waweze kuendelea kujenga maeneo yale kwa sababu Dar es Salaam sasa inapumua; ni kweli. Nakubaliana naye, tutaendelea kuwashauri *National Housing* waone umuhimu wa kuendelea kusogea pembeni ili waweze kujenga maeneo.

Mheshmiwa Mustapha Akunaay amesema upimaji wa ardhi ni kwamba mtu mmoja anachukua heka 3,000 mwekezaji mmoja. Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Akunaay kwamba ni kweli kwamba kama mtu mmoja anaweza akachukua ekari 3,000 mahali ambapo pana shida ya ardhi, ni dhahiri ni ugomvi toka siku ya kwanza. Hata anayechukua hiyo ardhi, hajitakii mema kwa sababu hutaitumia hiyo ardhi yako kwa raha kwa sababu unachukua ardhi wakati unajua watu wanaitamani, huwezi kufanya kitu.

Kwa hiyo, tukubaliane tu kwamba ifike mahali wanaochukua na hata wanatoa na tujitahidi utoaji wetu uwe wa makini kuhakikisha kwamba tunaangalia maslahi ya wananchi walio wengi na siyo maslahi ya mtu mmoja mmoja, ingawa hii haifuti Sera ya Serikali ya kuhakikisha kwamba kama kuna ardhi ambayo mtu mmoja ana mtaji mkubwa na anapenda kuanzisha kilimo ambacho kitawafanya na watu wanaomzuka wakanufaika, hili ni jambo zuri. Lakini ushirikishwaji tu hapa nadhani ndiyo tatizo, tutajaribu kuona namna gani tunawashirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sara Msafiri amesema kuhusu bajeti hii ndogo. Ni kweli bajeti hii ni ndogo na kwamba fedha zilizotolewa zilitolewa

asilimia. Lakini nasema tu, pamoja na hii fedha ndogo tuliyonayo, kama tutaipata yote, tunaweza tukapiga hatua fulani. Lakini ni kweli kwamba ni fedha ndogo lakini ndiyo *ceiling* yenyewe ilivyokuwa na mnapopanga bajeti mnagawana kwa *ratios.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msafikri ameshukuru sana kuhusu Mvomero, Mvomero mmefanya mfano mzuri wa kupima, nimeusema, lakini tunaendelea.

Mheshimiwa Mkosamali amezungumzia suala la Baraza na Urasimu! Hilo la Baraza nimelijibu, lakini urasimu wa watumishi wa kutoa hati na Mipango Miji. Ni kweli urasimu huu watumishi wanasikia. Nichukue nafasi hii kuwaagiza watumishi wote wa Sekta ya Ardhi kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jamani tunaonekana. Yote tunayoyafanya tunaonekana! Tubadilike, tu-*change attitude,* tuhudumie watu. Ardhi imekuwa ni rasilimali muhimu kwa kila mtu na kila shughuli yoyote mnayoisikia inafanyika juu ya ardhi. Kwa hiyo, jamani, tusiwe Miungu watu, ni lazima tubadilike.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hatutasita kama Wizara kumchukulia hatua yeyote yule atakayeonekana kama ni tatizo. Tunachoomba tu ni kwamba tupate habari na tupate ushirikiano kwa wateja wetu tunaowahudumia.

Mheshimiwa Kaihula umeizungumzia *National Housing,* lakini ukatoa changamoto kwamba bado kuna matatizo mle ndani. Tutajaribu kuzamia ndani tuweze tuyachunguza tuone ukweli wake na kama kuna hatua za kuchukua, basi tutachukua na tunakushukuru sana kwa tahadhari uliyotupa na umesema unatupenda sana.

Mheshimiwa Mrema alizungumzia masuala ya njia panda ya Himo na upangaji wa Miji.

Mheshimiwa Mrema mimi na wewe tumezungumza sana. Nami nataka niseme hapa kwamba, kama utaratibu wowote wa Mipango Miji, umefanyika bila kuwashirikisha wananchi wale vilivyo, vizuri, upangaji huo unakosa uhalali. Kwa maana hiyo basi, tutachunguza tuweze kuona utaratibu gani na sheria gani ilikiukwa ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, nimesema yamesemwa mengi na mengi wachangiaji waliosema kwa mdogo ni karibu 26. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia. Nawaomba tu kwamba jamani, Bajeti hii mnayotupitishia hapa ni ili tukafanye kazi hii kwa upungufu huo mnaouona. Mkitushikia Shilingi hapa mkatuzuia tusipate hata hicho kidogo, maana yake basi hamna malengo

mazuri na hicho tunachotaka kwenda kukifanya hata kama ni kidogo. Kutuzuilia hapa bajeti yetu isipite, hautusaidii ila unatuongezea matatizo.

Kwa hiyo, niwaombe sana, pamoja na changamoto zote ambazo tuko nazo, pamoja na upungufu wote mliousema, nakubaliana na wote kabisa mliosema. Mengi mliyoyasema yapo, wenzangu wamezungumza Shamba la Malonje, yamezungumzwa masuala mbalimbali kule Kigamboni; jamani, haya yote ni katika mchakato wa kuhangaika, lakini tatizo ni ukosefu wa fedha. Kama fedha ingelikuwepo, matatizo haya yasingekuwa makubwa kiasi hicho.

Nawaomba sana pande zote mbili za Bunge mtusaidie Bajeti yetu ipite kwa sababu mkizuia, ndiyo mnatukwamisha kabisa. Kwa hiyo, kama mnatupenda kweli na mmetusifia hapa kwa baadhi ya maeneo, lakini mmetuelekeza kama sehemu ya kutekeleza wajibu wenu, tumekubali, tumesikia, tutakwenda kuona namna bora ya kufanya. Mawazo ya Bunge ndiyo yanayoisaidia Serikali kutekeleza kazi yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, namshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ananielekeza vizuri, ananisimamia vizuri na ninasikia raha kufanya naye kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa mtoa hoja! Muda wako ni dakika 60. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na muda kuwa mfupi, sitaweza kuwataja wachangiaji kwa majina kwa kuokoa muda na ninakushukuru kwa kunipa saa moja niweze kuyajibu yale ambayo nitaweza kufanya, lakini yalikuwa mengi. Hapa nina bango kitita la wachangiaji wa maandishi 154.

Kwa hiyo, katika hali hiyo, nadhani tutakubaliana kwamba kwa wale ambao nitashindwa kwa namna fulani kuwafikia, itabidi niende kama ambavyo huwa nafanya kwa kuangalia hasa ni swali gani linazungumziwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kwa ruhusa yako nianze kuomba mwongozo wako kwa sababu Kanuni za Bunge zinaelekeza kwamba hapa

Bungeni kwa namna yoyote ile tutatoa taarifa sahihi. Sasa yamesemwa mambo hapa ambayo ni uongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kanuni ya 64 inasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, hili nalikabidhi kwako. Anaposimama Mbunge hasa Waziri Kivuli; nadhani vile vivuli vifupi vile nilivyosikia jana vilikuwa vinafafanuliwa hapa. Sasa Kivuli kinapokuwa kifupi Mbunge akaanza kusema uongo, tunafanyaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba hilo nilikabidhi kwako uweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze nijikite kwa wachangiaji ambao wamesaidia kazi yetu hii ngumu. Nimshukuru kabisa na kumpongeza Naibu Waziri ambaye tayari ameshajibu masuala kadhaa na hoja kadhaa ambazo sasa kwa kuokoa muda sitazirudia.

Sasa sina budi kushukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa mawazo yao mazuri; na maelekezo, maoni, ushauri ambao wametoa. Niseme kwamba kimsingi nakubaliana na mawazo yao na ushauri wao kama ulivyoainishwa katika ukurasa wa 39 hadi wanapohitimisha ripoti yao.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wangu, Kamati hii nimefanyanayo kazi sasa hivi hii ni bajeti ya tatu, imenisaidia sana, wamenielekeza na sekta kama mnavyoona ni mtambuka, ni ngumu. Naomba nichukue nafasi hii kwa kurudia kusema kwamba, shughuli za ardhi *(land administration)* duniani kote kwanza hazina kusema kwa kuwa nchi imeendelea migogoro itakwisha au *challenge* zitakwisha, changamoto zinakuwepo, zinaweza zikageuza sura tu. Jana nilizungumzia kwamba sekta hii inalinganishwa na figo. Sisi tukitoa hatimiliki hata laki moja, wale ambao hawajapata hatimiliki wana habari gani na kazi yetu sisi lakini kuna sekta nyingine ambazo zinafanya mambo yanayoonekana waziwazi. Naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba, ni lazima pia na sisi wenyewe, hasa kama wawakilishi wa wananchi, kuboresha pia uelewa wetu wa sekta hii kusudi kazi nyingine zinazofanyika ambazo hazina muonekano wa moja kwa moja ziweze kutambuliwa kwamba zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kamati imeelekeza mambo muhimu hapa ambayo nakubaliana nayo na nitayapitia moja moja kadiri hoja zilivyotoka. Nianze kabisa na kwa nini panaonekana kama kuna tumezorota katika utekelezaji? Suala la ufinyu wa bajeti kwa sekta hii wote mnalifahamu na nataka kusema kwamba na huwa nasema na narudia tena kama nilivyosema

mwaka jana kwamba mimi nafanya kazi ambayo iko mbele yangu. Nikikaa na kuanza kulia bajeti haitoshi, haitoshi, hata na kile kidogo ambacho ningefanya tutashindwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bajeti inapokuwa finyu vitu vingi vinasimama. Ni kweli kwamba, hata na wale Waheshimiwa ambao mmenishikia shilingi yangu naomba muirudishe kwa sababu msiporudisha tutakwama kabisa.

**SPIKA:** Hakuna aliyeshika shilingi yako mpaka sasa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na kwa nguvu zako wale waliotishia labda watafikiria tena.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema hivi, fedha ambazo tunaomba hapa hazina bajeti ya vitu vingi. Hapa hakuna bajeti ya kutatua migogoro, hakuna kabisa ndani ya bajeti hii. Hakuna bajeti ya kupima ardhi labda Morogoro. Hakuna bajeti ya kupanga mji hata mmoja, labda ile miji ambayo nimeitaja na kadhalika. Kwa hiyo, hili naomba nalo tunapojadili Wizara hii tuelewe *realistically* nini kinawezekana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, pamoja na udhaifu wa Waziri, labda na wasaidizi wangu na watendaji wangu lakini hata ungekuwa wewe kama huna fedha za kupima ardhi huwezi kupima ardhi. Nianzie na upimaji wa ardhi na nimetangaza programu kwamba tungependa kupima ardhi Tanzania nzima. Tanzania nzima ni takribani 10% ya ardhi ndiyo imepimwa 90% haijapimwa.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa hapa, nadhani alikuwa ni Mheshimiwa Mkosamali, aliuliza tunamaliza lini upimaji? Nitoe mfano, nchi ya Uingereza, 12% ya Uingereza haijapimwa; hili ni zoezi endelevu, linatokana na hali halisi. Kuna nchi ambazo kila kipande kimepimwa hususan Sweden na sehemu nyingine, kuna wengine kufuatana na *customary land tenure* ilivyo, sasa wale Waingereza wale hata na Katiba ya nchi hawana, wenyewe wana mila zao ndio zinaendesha mambo, lakini zinaheshimiwa kiasi kwamba hawahitaji Katiba iliyoandikwa na vitu kama hivyo. Kama wewe hujazaliwa na Malkia huwezi kwenda ukasema mimi ni *Prince Charles,* haiendi namna hiyo Uingereza, kila mtu anajua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba suala la kupima ardhi kwa kweli ni kilio cha kila Mbunge na mimi nikiwepo. Waheshimiwa Madiwani kutoka Muleba wako hapa wananisikia, hata na kule kwangu Muleba hakujapimwa. Kwa kweli kutopima ardhi kidogo ni upungufu lakini ni zoezi ambalo litachukua muda.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Serikali imedhamiria kabisa kwa uwezo ilionao sasa hivi kuharakisha zoezi hili lakini nataka nijibu hoja zote kuhusu upimaji. Fedha za kupima ardhi zenu Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge haziko kwenye bajeti hii ambayo iko mbele yenu. Hata na Waheshimiwa Madiwani kutoka Muleba mnasikia wenyewe, fedha za Muleba hazimo humo kwa hiyo, mtu asiniulize. Kwa nini nasema hivi? Nasema hivi ili kusudi tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa tunafanyaje? Tukienda kwenye Halmashauri zetu na hilo huwa nalisema kila mwaka, kwenye Halmashauri zetu tafadhali sisi wenyewe tusibweteke, tusisubiri Serikali Kuu kuja kufanya kila kitu. Serikali Kuu uwezo wake ni mdogo sana; awe nani amesimama kwenye nafasi yangu hataweza kufanya kitu chochote kwa sababu ni vigumu sana kupata bajeti ya kupima. Kwa mfano, pale Mvomero kwa sababu ya matatizo yaliyojitokeza, Kijiji kimoja cha Lukenge ambacho kimefanyiwa *detailed design* ambacho kabla ya kuja hapa nilikabidhi Hatimiliki za Kimila. Katika Kijiji kimoja zoezi lilipofika hapa tumetumia shilingi milioni 460 kufanya *detailed design* na imebidi kwanza kukarabati Masijala. Watu wengi najua mmejitahidi kupima lakini Sheria hairuhusu kutoa Hatimiliki za Kimila kama hakuna Masijala kwenye Kijiji na ndio maana benki nyingine zimekwama kukubali Hatimiliki za Kimila kwa sababu ni *documents* ambazo baadaye zinaweza zikapotea hivihivi. Kwa sababu haziandikwi na *Registrer of Tittles and Documents,* Msajili wa Hati na Nyaraka wa Wizara ya Ardhi hashughulikii nyaraka zile. Kwa hiyo, unakuta kwamba vyombo vingine vya fedha wanasita kidogo.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema Lukenge juzi nilipokuwa nakuja hapa, nimekuta kwamba tayari wataalam wangu wako pale wanafanya kazi nzuri, wanafanya kazi ya ziada, Wazungu wanasema *beyond a call of duty*. Hata hivyo, unahitaji barabara, maana tunapopima ardhi tunaweka na barabara ya kuifikia ardhi hiyo, tunaita *access;* hatimiliki ambapo mtu shamba lake haliwezi kufikiwa ni benki gani itaikubali? Kimsingi ni kwamba hiyo ni ardhi ambayo haiuziki, haiko-*marketable*. Niliwaomba wananchi wa Lukenge na Mheshimiwa Amos Makalla naomba unisaidie katika hili utakapokwenda wajenge barabara za kufikia mashamba yao kama tulivyofanya mara baada ya uhuru, wanasema Bulungibwansi, Mwalimu alifanyaje na ulikuwa ni mfumo wa Wajerumani. Kama una shamba, shamba moja linafikisha barabara shamba la pili, la pili linapeleka la tatu, la tatu, la nne mwisho wa siku barabara inakuwepo. Hapo hatimiliki inakuwa na maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme suala la upimaji ni kitu ambacho mimi mwenyewe natambua umuhimu wake lakini mpaka sasa hivi tumefikia tulipofikia. Bajeti hii ambayo iko mbele yenu na yenyewe ina upungufu huo kwa sababu haina bajeti ya kutosha ya kuweza kupima ardhi. Sasa tunapima ardhi

katika sehemu ambazo zina kipaumbele na imekuwa ni sehemu zenye migogoro.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kweli iko sehemu nyingi na katika bajeti yangu nimejaribu kuifafanua. Waheshimiwa nimewawekea kiambatisho *(appendix)* pale inayojaribu kufafanua migogoro hii. Ili kuitatua ni lazima tuelewe ni ya aina gani. Maana tusipoelewa ni aina gani *that means* hatujui kiini chake ni nini, maana tutakuwa tunashughulikia tu ishara za migogoro *(symptoms)* lakini hatuelewi sababu zake.

Mheshimiwa Spika, nifafanue tu kwamba kupima na kupanga ardhi ni muhimu. Naomba nirudie na nadhani nilisema tena mwaka jana, migogoro kati ya wakulima na wafugaji sio migogoro ya ardhi ni migogoro ya teknolojia. Pale kinachokosekana ni ule utaalam wa ufugaji na ukulima wa kisasa ambao unahitaji ardhi kidogo. Kwa hiyo, watumiaji wa ardhi hawa wote tuboreshe tija yao *(productivity)*, wanagombania ardhi kwa sababu watu wanazidi kuwa wengi ardhi yenyewe inazidi kuwa kidogo, sasa kama teknolojia haiendi mbele hata ungepima na kupima tutapima na Mvomero tuko kule tunapima, lakini nataka niwahakikishie kwamba kuna vitu vingine sisi Wachumi tunasema ni *predictable,* kuna mambo mengine yanatabirika. Mimi nikipima na tunapima na tutapima ni kazi yetu, lakini wakati wa kiangazi kama hakuna maji, mifugo itahama, kama hakuna malisho bora mifugo itahama na kama kuna kupe au magonjwa mifugo itahama. Kwa hiyo, ni lazima tuelewe kwa nini mifugo inahama, *what is the basis of pastoralism?* Kwa nini watu wanakuwa wachungaji? Hakuna mtu anayependa kutoka huku na kwenda kule, lakini inakuwa utamaduni kwa sababu ya hali halisi.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, bila maji, bila malisho bora kwa kupanda nyasi, nimekuta Wataalam wangu wa Ardhi, sina budi hapa kumtambua Afisa wangu Mama Suma ambaye yuko kule Mvomero, nimekuta amepanda nyasi. Baada ya kupima maeneo ya wafugaji, anajua kwamba eneo ni dogo, ikabidi sasa afanye kazi ya ukulima na kwenda kuwapandia nyasi, kwenda Kibaha kutafuta nyasi bora, kwenda Mpwapwa kuwaonesha namna ya kupanda nyasi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba suala hili la wafugaji na wakulima ni tatizo la teknolojia na naomba lieleweke hivyo. Sisi tutafanya kazi yetu lakini tukishafanya kazi yetu ya kupima, sio muarobaini wa kumaliza migogoro. Nadhani wengine wanaamini kwamba kupima ni muarobaini wa migogoro ya wafugaji na wakulima, haitawezekana kwa sababu wale wanahitaji *technological revolution,* kwa hiyo, lazima hiyo nayo ipatikane, nimeisema sana naomba nirudie tena kusudi ieleweke.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna migogoro kati ya wafugaji na hifadhi. Naomba radhi kwa wale ambao sijawafikia, Mheshimiwa Suleiman huko Kishapu nitakuja, lakini najitahidi ninakwenda ila sehemu ni nyingi na migogoro inaibuka kila kukicha. Nikitoka Ngorongoro wanasema urudi Loliondo, nikitoka Loliondo wanasema urudi Magu, nikitoka Magu wanasema nenda Ngara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, kuna migogoro kati ya wafugaji na hifadhi. Migogoro hii nimeifafanua sana katika Hotuba yangu, naomba muiangalie mkipata nafasi na hii suluhu yake pia naomba nizungumze na ninawasiliana na mwenzangu Dokta Kamani katika Wizara ya Mifugo, hapa tunataka wafugaji wetu lazima waundwe upya, ni *organization* ya ufugaji. Hapa tunataka *small scale ranching companies,* ufugaji wa ushirika; mifugo ikusanywe sehemu moja, wapewe *ranch,* wakishapewa *ranch* nini kitatokea? Wakishapewa *ranch* watafanya *fencing,* watafanya *demarcation,* wataweka maji, wataboresha nyasi na wataweka majosho. Naamini kabisa kwamba wenzetu Wizara ya Viwanda watakuwa tayari wameshaweka *abattoirs* yaani machinjio ya kuweza kuvuna wale wanyama. Ukiingia kwenye ufugaji wa kisasa ni lazima pia uwe na mbinu za kuvuna wanyama. Kwa sababu ukishakuwa na ng'ombe ambao wanalishwa vizuri wakanenepa ina gharama zake lakini sasa ile *off take,* kama una ng'ombe 100 inatakiwa uuze ng'ombe 25 kwa mwaka, *off take* ni 25% kama uko kwenye ufugaji wa kisasa. Sasa unakuta kwamba hapa tunazungumzia mgogoro wa ardhi kwa kweli ninaitwa lakini nikiitwa huwa nachukua pia utaalam wangu kuzungumza haya nayoyazungumza. Hapa nimwambie Mheshimiwa Waziri Kivuli kwamba kule kuwa Waziri wa Ardhi hakuniondolei mimi Utaalam wangu, bado mimi nabaki Mtaalam tu na unapokuwa unajua kitu, unajua *substance,* kuna watu hapa huzama kwenye *process, procedure. It is not about what you do but how you do it,* lazima pia pawe na unavyofanya kazi. Sasa unapokuwa na maarifa ya kitu fulani, unakishughulikia pia kwa namna hiyo, hiyo haimaanishi kwamba unaingilia kazi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa mfano, nikiandika andiko, bosi wangu hapa ni Waziri Mkuu yuko hapa, nimetumwa kazi, kazi ambayo imeshindikana kwa muda mrefu, natakiwa nitatue mgogoro wa Chasimba na ni mgogoro mkubwa lakini ule mgogoro unataka tafakuri, unataka mkakati, lazima uelewe tatizo ni nini pale. Huwezi tu kwenda pale uka-*sympathise* na wananchi bila kuelewa tatizo hasa ni nini. Baada ya agizo la Waziri Mkuu kutoka kwamba Wizara ya Ardhi tusimamie ule mgogoro, nikajipanga kwenda kutatua mgogoro ule, nilijipangaje?

Mheshimiwa Spika, kwanza unajipanga kurejesha amani katika eneo. Walio wengi mnaweza kuwa mnafahamu kwamba lile eneo lilikuwa limeshageuka *a no go area.* Hii miji inapokua huwa inaleta matatizo,

mmeyaona nchi za Uarabuni, zote nazifahamu Cairo, Libya, nimefanya kazi kule nikiwa *UN*. Kwa sababu kinachotokea kwenye *urban communities* nikiwa kwenye *slum settlements, squarters* ambazo Mheshimiwa Mbowe amezungumzia kwamba tuondokane nazo na mimi nakubaliana naye. Kwa kumsikiliza Mheshimiwa Mbowe, kama yeye kweli tunayejua ndiye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, sasa nikashangaa kama anazungumza miji hii *squarters* kila mahali, huyo ndiye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na amezungumza vizuri nakubaliana na kila kitu alichokisema lakini sasa haiendani na Ripoti ya Kambi ya Upinzani kama nilivyoisikia mimi. Maana pale inatetea Chasimba ibaki kama ilivyo, Chasimba ni *squarter*. Unasema kwamba Kigamboni tusirekebishe, kupanga mji ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, tuachane na ndoto, kupanga mji ni kazi ina usumbufu, inamaanisha kupangua kizazi cha sasa hivi uende na kizazi kinachokuja ili mahali pawe bora kwa hiyo, hakuna *illusion* yoyote kama unajua unazungumzia nini, kama sio tu kuzungumza. Unajua Mwenyezi Mungu ametujalia kila mtu ana mdomo, anaweza akazungumza lakini kinachotoka mdomoni sasa ndicho kinasaidia… *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Aliongelea nje ya kipaza sauti)*

**SPIKA:** Sasa mnaleta fujo. Waziri anajibu na mnampa nafasi ajibu. Mheshimiwa Halima naomba utulie, endelea Waziri?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba unilinde dakika zangu pia zisipotee.

**SPIKA:** Endelea Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Watu hamna utulivu na uvumilivu jamani? Waziri anajibu, mtulie.
**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Aliongelea nje ya kipaza sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima! Kila wakati tunabishana bila sababu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, najibu hoja kama ulivyozileta. Chasimba ni *squarter*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri na wewe tulia. Tumeweza kusikiliza Hotuba zenu wote na yeye ajibu sasa. Tumewasikiliza kimya na yeye muacheni ajibu na sitaki

kubishana na mtu sasa. Mheshimiwa Waziri, endelea. Naomba uendelee kujibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Aliongelea nje ya kipaza sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, nani kakuita?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, inategemea na uwezo wangu maana sio lazima niangalie karatasi kujibu hoja.

**SPIKA:** Waziri naomba ujibu Hoja? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Hoja umeitoa, nimeisikia, najibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri endelea kujibu sio kubishana na hawa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kitu kimoja kwa Waheshimiwa Wabunge. Wakati *speech* ya Mheshimiwa Waziri Kivuli inasomwa mimi nilipaza sauti? Kwani mimi sina sauti?

**WABUNGE FULANI:** Unayo!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, lakini tofauti ni ule ustaarabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba unisikilize. Endelea kujibu hoja zako, achana na maneno yasiyokuwa na busara hapa ndani na ninyi wote hamuongozi kikao naongoza mimi. Kwa hiyo, naomba mumsikilize na Mheshimiwa ujibu, usiendelee na hivyo vituvitu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kusema hivi, nilipomsikiliza Mheshimiwa Mbowe alivyochangia hapa na *Hansard* ipo na kusikiliza Hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani yaani kulikuwa hakuna *alignment* yoyote kwa sababuhuwezi kupanga mji kama huna ujasiri, kama huna ukweli, kama huna uelewa wa kujua kwamba utakwenda kupangua watu. *It is as simple as that* yaani ndivyo ilivyo, tuache ubabaishaji kwa sababu ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa pale Chasimba kuna kama familia zaidi ya 4,096 ambazo zimethaminiwa, wanaweza hata wakawa zaidi. Wale wanahamishwa kusudi tutekeleze amri ya Mahakama na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameniagiza na kazi hii naifanya kiufundi, baada ya kazi hii kuwa imeshindikana. Hapa tulipofika sio pabaya. Tumeshafanya *progress,* pale kuna wananchi; sasa wale wananchi kuwadanganya kwamba watakaa kwenye eneo ambalo wanatakiwa, kama tukitaka Sheria, kama sio hii Serikali sikivu ya CCM wananchi pale wanaondoka hawana haki yoyote kwa sababu ni *squarters* lakini Serikali kupitia Waziri Mkuu akasema tutafute namna ya kuwahamisha hawa wananchi kwa njia ya kibinadamu, kwa hiyo, fidia ni hisani, pale hakuna fidia ya kisheria yoyote inayowezekana kwa sababu pale kuna *ruling* ya *Court of Appeal* (Mahakama ya Rufaa). Kwa hiyo, inashangaza kuona kwamba mwakilishi wao anaingia pale kuwaambia uwongo mweupe na isitoshe anaiba nyaraka za siri za Serikali. Hili nalikabidhi kwako mtu anapoiba nyaraka za siri za Serikali unafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unakuta kwamba nusu ya hotuba hii imeiba barua yangu… *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikabidhi, ni kweli, hapa kuna barua yangu niliyomwandikia Waziri Mkuu ambayo ndiyo hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili naomba nilikabidhi kwako, naomba mwongozo wako kama kujipatia barua iliyokuwa imeelekezwa kwa Waziri Mkuu bila kunakiliwa kwa mtu yeyote ni kosa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47, Toleo la 202. Naomba niwasilishe suala hili kwako ili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali muangalie kama ni sahihi. Naomba kusema kwamba Mheshimiwa Mdee amekuwa na tabia hii kwani katika *speech* iliyopita aliiba andiko la Chuo Kikuu, akaliwakilisha hapa, mimi nikakubali nikayaacha kama yalivyo sikujua kwamba itakuwa tabia. Sasa kwa kuwa ni tabia naomba niwakilishe kwa Spika atajua la kufanya lakini ni hoja naiweka hapa mezani, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa wananchi wa Chasimba naomba niwaambie hivi, mimi mnavyoniona hapa nimefanya mambo mengi nchini lakini pia na nje ya nchi na nimejifunza na naendelea kujifunza kwa sababu ni mpumbavu tu ndiyo anafikiri anajua kila kitu, kwa hiyo na mimi kuna mambo mengine ambayo najifunza. Kwa mfano, kujifunza kwamba kuna watu wengine unaweza kufikia kwamba mpo *at per,* mnaweza mkaelewana kumbe unatwanga maji kwenye kinu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika hali hiyo, nataka kusema kwamba wananchi wa Chasimba wakiendelea kumsikiliza Mheshimiwa Mbunge wao kama nilivyomuona hapa itakula kwao kwa sababu pale mimi najitahidi na

Mheshimiwa Waziri Mkuu anajitahidi kwa nguvu zake zote tuweze kuwapa fidia hisani waweze kupata makazi mbadala. Sasa anakuja mtu ambaye wamemkabidhi dhamana hii ndiyo anakuwa mlaghai. Unajua *problem* ya Mheshimiwa hapa ni *opportunism,* miradi yote ambayo najaribu kuitekeleza ukiwepo mradi wa Makongo, maana yake yeye anakuja anavizia kuangalia mambo yatakwendaje, yakienda vizuri sasa hivi Serikali hii ya CCM imeweka fedha katika Wizara ya Ujenzi, kwa hiyo ninapofanya kikao kwa sababu bajeti iko kwenye ujenzi siyo lazima bajeti za Wizara zote ziko hapa, kwa mfano barabara ziko ujenzi hapa anakuja mtu anasema unajua wananchi tupo pamoja, *the same person* ambaye alikuwa anasema msiwasikilize, mkae kama mlivyo. Ndugu wananchi wanaonisikiliza kama huo ndiyo, Mheshimiwa Mbowe uliniuliza mbona nacheka wakati anaongea na nilikujibu nikasema nacheka kwa sababu huu siyo upinzani hii ni kelele, hakuna hoja, ukiangalia hiki kitabu najibu nini?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa*
*Wabunge walikuwa wakiongea)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba ujielekeze kwenye hoja tafadhali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naendelea. Sasa tunakuja kwenye suala la uadilifu, hapa kuna tuhuma binafsi, ule mradi wa Chasimba, ulivyo, *concept* yake ambayo tayari kwa kuwa umeshaiba *document* ya Waziri Mkuu umeshaiona, ile *concept* watu wanaofanya kazi pale ni wengi, pale kuna bajeti ya watu wa Usalama ambayo wala haikuandikwa humu, pale kuna bajeti ya watu wa Wizara, pale kuna bajeti ya watu *social interlocutors* kama hiyo *TAWLAT* tunayoisema, sasa hizi tuhuma za rejareja naomba nizijibu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TAWLAT* limeundwa nikiwa *UN-Habitat* kusaidia wanawake kuweza kupata ardhi za mijini. Kwa hiyo, ni Shirika ambalo nalilea ni *fact* na najivunia. Ukienda Kenya utakuta *KEWLAT (Kenya Women Land Access Trust)* nimeiunda tena iko Kibela inafanya kaz, ukienda Uganda Kampala utaikuta inaitwa *UWLAT*, ukienda Mozambique utaikuta *MOZWLAT*, ukienda Ghana utaikuta *GHAWLAT*. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa*
*Wabunge walikuwa wakiongea)*

**SPIKA:** Jamani naomba tusikilizane mnavyofanya wala siyo heshima.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, mimi nimefanya kazi kama Mtanzania nilikuwa nawawakilisheni nyinyi

wengine ni vijana na wewe ukiwepo hapa mkienda kule muweze kupata kazi kwa sifa tunazoziacha kule msibaki kushangaa. Sasa mtu unapokuwa unajua kwa mfano unapokuja kusema kwamba mtu ana maslahi binafsi, unapoandika hapa kwamba kuna dili imechongwa, unajua wakati mwingine unatuhumu mtu kwa kile kitu ambacho wewe ungepata nafasi ungefanya, hilo ndiyo tatizo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeh!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Ukisikia mtu anakimbilia kusema dili, dili, sasa kumbe wewe ukiwa Waziri halisi kama una ndoto za dili utaanguka, huwezi kupiga *round,* kwa hiyo hapa unaona kwamba mtu yupo kwenye ndoto za dili, hapa hakuna dili yoyote, hapa kuna kazi ngumu ambayo ni *multisectoral,* ni *interdisciplinary* na inataka uwe na uwezo wa kuitekeleza siyo kubabaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani katika hili, amenitumia simu mtazamaji kutoka Chasimba, naomba nisome, mwananchi wa Chasimba ameniletea *message* wakati tumekaa hapa, naomba noisome. Mheshimiwa Mbunge anachofanya ni sawa na fadhila ya punda na mateke. Tumemuona mara nyingi akiomba Serikali itatue mgogoro leo hatua zinachukuliwa anatia dosari na uchochezi lakini sisi wananchi tunajua hapo ndipo CHADEMA ilipofikia. Tunachoshukuru ni kuwa hata Kamati ya Bunge inahimiza utatuzi wa mgogoro, mwisho wa kunukuu. Sasa mambo yasije yakaenda kombo ukasema Mama Tibaijuka umeyataka mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba mimi mnavyoniona hapa, nilijipanga kuja kufanya kazi ya wananchi hapa, kweli sikukurupuka, nilihakikisha kwamba najiandaa, nikahakikisha kwamba naenda kutafuta angalau maslahi kidogo, kwa hiyo, mimi nafanya kazi kwa uadilifu, sina haja ya dili yoyote hapa mimi, sasa kama wewe una ndoto za dili hizo ni ndoto zako siyo unakuja kuzileta hapa kuja kunibambikizia mimi kwamba nina dili, sina *any personal interest,* nimevifanya na ninavifahamu na ni lazima nitumikie Taifa langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, muda unaisha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**SPIKA:** Naomba mnyamaze tuendelee kufanya kazi. Waziri muda unaisha masuala mengine kama ya Kigamboni hujasema.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka kusema kwamba vitu vya uwongo vingi nimesema nitakabidhi kwako, kwa sababu hapa kuna uwongo mweupe ambao sasa Kanuni zetu za Bunge itabidi uje ulete ushahidi kwa Spika, hiyo nakabidhi kwa Spika kwa sababu muda ni mfupi. Nataka kusema kwamba lakini pia ni vizuri sasa kama mtu umejipanga kwa uwongo utasaidiaje watu ukipata madaraka…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Sikilizeni kupiga kelele ni dalili ya utoto. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea kujibu. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, tunaomba mwongozo wako, Waziri ajibu hoja zetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul kwanza hujaitwa na mtu.
**MBUNGE FULANI:** Ajibu hoja zetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba ujibu hoja, endelea kujibu muda umekwisha achana nao.

**MBUNGE FULANI:** Kigamboni!

**SPIKA:** Naomba mnyamaze tuendelee na kazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 41 imeongelewa kazi, yeye mwenyewe katika kikao chetu cha Novemba hapa Mheshimiwa huyohuyo Waziri wetu Kivuli hapo, alikuja na *sensation* zake, *excessive sensation* ambayo ni *sense* ya *immaturity* alikuja nayo hapa, akasema kwamba tusitishe shughuli zote za ardhi, Hoja Binafsi ilikuwa ni *crisis* na nakumbuka aliyemaliza hiyo *crisis* ni Mheshimiwa huyuhuyu Mbowe alisimama akasema hapana, hatuwezi kusitisha ilikuwa ni Novemba lakini katika kikao cha mwezi Aprili ilikuwa inabidi tuje na tathmini ya mashamba.

Mheshimiwa Spika, tukaondoka hapa na *crisis,* Azimio la Bunge linataka tathmini ya mashamba, mchakato wa manunuzi ukaanza. Kwa hiyo, *under emergence procurement, under single source method* ilibidi itumike na ununuzi huo unawezeshwa chini ya Sheria ya Ununuzi wa Umma 2004, Ibara ya 59 na Kanuni ya 95 na 98. Sababu za ununuzi wa dhararu kama nilivyosema ilikuwa ni

kuweza kufanya andiko la tahmini na kulileta Bungeni mwezi wa nne. Kazi hiyo ilifanyika kwa kufuata Sheria na taratibu na aliyepewa kazi hiyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliingia mkataba, Kitivo cha Uchumi ndicho kilipewa tenda hiyo. Sasa mtu anakuja na porojo, kuna ndugu zake Waziri, hii ni porojo, *please, please,* unajua hapa najibu hoja lakini pia lazima niwe *serious* katika kujibu hoja. Hizo ndiyo zinaitwa porojo, *University* of Dar es Salaam ndiye ana *contract.*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa huyu anasema kwamba, sasa angalia *cut and paste*, tatizo la hii *document* ni *simple cut and paste,* ndiyo tatizo lake, *the left arm is not the right arm is doing* hakuna *coherence*. Inasema hivi, ukurasa wa 41, hakuna jipya lililoletwa na hilo andiko zaidi ya kutegemea taarifa za sensa zilizofanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2007 lakini ukisoma hii *document* hususan kwa mfano ukurasa wa 49 anaendelea kunukuu matokeo ya Utafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo, unaona hapa kwamba huyu mtu ni *cut and paste product* yaani unaona kwamba kimsingi haelewi kitu anachotakiwa kufanya lakini kwa kuwa atapata *audience* ya kuzungumza atazungumza na *in the process* ata-*mis lead* umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo wameombwa wafanye kazi ambayo imeombwa na Bunge kwa dharura. Sasa wanapoweka watu wa kufanya kazi, hiyo siyo juu yangu, ni juu yako sasa kwa sababu nimemuomba Mheshimiwa Spika wewe kuja kuonyesha nilivyofaidika, nilivyopata maana tatizo lako hapa Mheshimiwa Mdee unajaribu kuleta ndoto za yale ambayo unataka kuyafanya ukipata madaraka, hilo ndiyo tatizo lako, kwenye ndoto tu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea kujibu hoja tafadhali muda umeisha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tumpe nafasi Mheshimiwa ajibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nimejielekeza kwa tuhuma binafsi na ya mwisho kabisa, naomba nifafanue kwa sababu kama nilivyosema hoja ambazo ni za kufanyia kazi tutazifanyia kazi, tutajitahidi, tutafanya kazi na Halmashauri lakini hoja za propaganda lazima zikabiliwe kama inavyostahili. Maana yake mtu anayepiga propaganda, hoja za propaganda lazima zikabiliwe ki-propaganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kujua kwa nini mtu analeta propaganda ya namna hii, kama unafikiria kwamba huyu mtu ni mtu *smart*, ni mtu ambaye anaelewa, sasa anapofanya vitu ambavyo vinaonekana kama anababaisha unashangaa…

**WABUNGE FULANI:** Jibu hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Najibu hoja na ninyi sikilizeni mimi siyo mtu wa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba endelea kujibu hoja, Mheshimiwa Waziri endelea kuji-*address* kwenye hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho kabisa kwa upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 63, Mheshimiwa Mdee anazungumzia *demotion* yangu, anazungumzia yaliyotokea *UN-Habitat,* anazungumzia kama nilivyosema kwa mtindo wa *cut and paste*. Mimi nimefanya kazi Umoja wa Mataifa miaka kumi na mbili na nimeingia Umoja wa Mataifa kwa ushindani, nimechukua kalamu nikiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nikaomba kazi nikaipata. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Jibu hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, najibu ukurasa wa 63.

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Kama hoja haikuwa ya ardhi basi msikilize maana hiki ni kitabu chenu au mnakinana ninyi wapinzani, kama ni chenu *you better listen. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisome ukurasa wa 63 wa hoja ya Upinzani kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inaanza kuamini kile kilichoripotiwa katika gazeti la *Daily Nation* la Kenya la tarehe hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nifafanue hivi, kule *United Nations* ni lazima uelewe tunafanyaje kazi uweze kuelewa haya mambo siyo kama nilivyosema unafanya *cut and paste* unaandika kitu ambacho hakina *context* yaani mazingira ya kwamba ni kitu gani kilikuwa kinaendelea kule. Kilichoendelea ni kwamba baada ya kazi yangu iliyotukuka… *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafanya haraka, baada ya kazi yangu iliyotukuka, Umoja wa Mataifa mimi nilikuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa *UN-Habitat,* kazi ile kuipata unapigiwa kura na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, nchi zote

zinakupigia kura, walinipigia kura nikashinda, nikawa Mkurugenzi, nikamaliza kipindi cha miaka minne, nikapigiwa kura mara ya pili nikashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Koffi Anan akaniteua, maana kuna kazi aina mbili Umoja wa Mataifa, kuna kazi ya kuchaguliwa, kuna kazi ya kuteuliwa…

**MBUNGE FULANI:** Jibu ya ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Niko kwenye ardhi, hii ni ripoti yenu sikilizeni ninyi.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo ni hoja, wanakupotezea muda.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hawanipotezei muda, hii ni propaganda naijibu propaganda ya Halima Mdee, unajua *we are beating you at your own game* kwa sababu ni propaganda, *the art of* propaganda mtu anataka aweke neno uliache hivi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba uingie kwenye hoja zile *substantive* na nasema hivi kwa sababu unapom-*personalize* mtu kwa kweli matokeo yake ni hayo.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Naomba uhame sasa uingie kwenye hoja *substantive* tafadhali, naomba achana na hawa endelea na hoja *substantive*.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, muache Mheshimiwa Waziri ajibu mapigo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mwongozo wako imetosha…

**MBUNGE FULANI:** Usihame jibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Lakini watu wasifikirie kwamba wana-*monopoly* ya propaganda, hakuna mtu ana *monopoly* ya propaganda. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwa wachangiaji ambao kama nilivyosema upimaji wa ardhi

utaendelea, unahitaji bajeti za kutosha na hapa nitoe rai kwa Halmashauri, ndiyo njia pekee kwamba twende Halmashauri kwa Halmashauri. Nikubaliane na hoja kabisa ya kupima miji yetu lakini pia tukubaliane kupima miji kuna gharama zake, gharama zake ndizo hizo ni kwamba ni lazima tuwe na nidhamu.

Mheshimiwa Spika, napokuja kwenye upimaji wa miji nifike kwenye suala la Kigamboni. Mji mpya wa Kigamboni kama nilivyosema kwenye hotuba yangu umeainishwa katika Ilani ya CCM, Ibara ya 60(c), imeandikwa kabisa kwamba tunakwenda kujenga mji mpya wa Kigamboni. Kujenga mji mpya wa Kigamboni ni msalaba mkubwa sana kwa wananchi wa Kigamboni, hii wala haina mjadala kwa sababu popote pale mnapotaka *master plan* inamaanisha kwamba tutapanga watu upya, hakuna njia nyingine ya kupanga mji. Kama kuna mtu atafikiria watu watakaa kama walivyo na utapanga mji *then you don't know what you are talking about.*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kusema kwa wananchi wa Kigamboni, jana nilizungumza kwa kirefu leo sitazungumza sana, nashukuru kwamba Kamati imeona kwamba labda tuongezewe bajeti kama itapatikana lakini pia mkakati tuliojipangia hakuna kisichojadilika, kwanza ndiyo elimu yenyewe kwa sababu tunaweza tukafanya *review*, ikionekana kwamba tufanye *review*. Hata hivyo, mji mpya wa Kigamboni hatua tuliyopiga sasa hivi tumeshaunda *KDA* nimesema jana, tumeshaweka mtu wa kutafuta fedha, sasa watu wameshaanza atalipwa, sasa Mtaalam Mwelekezi lazima alipwe na anapolipwa wenye ndoto za dili wanafikiria ni dili na wanaosema nina ardhi, mimi sina ardhi Kigamboni. Kwa hiyo, narudi Kigamboni nasema kwamba Mji Mpya wa Kigamboni ni *challenge* kwa watu wote, ni kazi ambayo tumejipangia sisi kama Taifa na wananchi wa Kigamboni wana kila haki ya kutoa wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kwa wachangiaji wengine kwa maandishi, wengine kwa maneno, tatizo ni kwamba tunataka mji wa kisasa, wa viwango. Kwa hiyo, namna za watu kuingia ubia kubaki kwenye ardhi yao, nimefafanua jana, naomba nirudie tena, wanabaki pale kwa kutumia soko. Sasa kutumia soko ndizo hisa na ukitaka kulinda maslahi ya wananchi kama unataka kupigana na ufisadi lazima uwaombe wananchi wafungue benki akaunti ndiyo njia pekee pia ya kuhakikisha kwamba hakuna malipo hewa yataingia.

Mheshimiwa Spika, sasa nasikia hoja hapa watu wanataka kuwa na keki yao na kuila hapo hapo, haiwezekani hizi ndizo njia za kisasa. Sasa mtu anapokuja na mawazo, upo *knowledgeable*, unajua kitu kinachotakiwa kufanya, watu wanabaki kushangaa na kupinga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahusiano na kuzungumza, mimi niko kuzungumza na mtu yeyote na kama unavyosema natulia mimi, sina haja ya kupiga kelele *heckling*, *I can't follow to that level,* hakuna haja ya kupiga kelele na *to follow to the level* ya kuanza kupiga kelele hasa kwenye Bunge. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba Mji Mpya wa Kigamboni ni *challenge*, tumeyasikia maoni ya Kamati na wachangiaji wengine wameweka mawazo ambayo ni mazuri, tutakaa tutaangalia, lakini wanasimama watu wanasema kwamba miradi ya *National Housing* imekwama kule Kigamboni kwa sababu Wizara inakwamisha. Mimi niliyesimama hapa ndiye Waziri mwenye dhamana na *National Housing, National Housing* ikifeli nafeli nayo. Kwa hiyo, mimi ndiyo mdau wa kwanza kuona kwamba *National Housing* inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo mdau wa kwanza katika *National Housing* lakini sasa inapokuja Kigamboni kama eneo lake liko kwenye njia za *master plan,* hapo sasa ndiyo nidhamu inaanza, tunaanzia kwetu.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Hatuwezi kuharibu *plan* za mji kwa sababu ya maendelezo mbalimbali. Kwa hiyo, *National Housing* na wengine wote ambao wanaadhirika, kila mtu pale anapewa fidia na ile fidia nimeisimamia mimi katika kazi zangu, ni fidia endelevu. Hela zilizopangwa nimezisema jana, sina haja ya kurudia ni fidia endelevu. Kwa hiyo, suala hili tuamue, kama tunataka *squatter* ambazo Mheshimiwa Mbowe alikuwa anazizungumzia tunaweza tukaenda nazo. Kama tunataka miji iliyopongwa tuwe na nidhamu, tuwe na *sophistication*, tuwe na *discipline* ya kwenda mbele lakini pia na ustaarabu wa kwenda kwa hoja siyo kwa propaganda and *cheap* propaganda, twende vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Mji Mpya wa Kigamboni, niseme kwamba niko *committed*. Uamuzi wa Serikali tunatafuta fedha za Mji Mpya wa Kigamboni. Serikali haitajenga Mji wa Kigamboni, Serikali inawezesha kupanga Mji Mpya wa Kigamboni. Ujenzi utatokana na *equity*, sisi wenyewe Watanzania kwa ujumla na watu wa kwanza kuchangia hisa pale ni wananchi wa Kigamboni wenye maeneo. Kweli kuna wananchi wengine kule wana maeneo makubwa na ni kweli kwamba katika hii fidia ya awamu ya kwanza shilingi bilioni 30 zinakwenda kwa watu wachache, wana maeneo makubwa. Sasa unaweza ukajadiliana na wale watu tunakwendaje, hilo linajadilika lakini haimaanishi kwamba Anna Tibaijuka kwa kuwa eneo ni kubwa ameingia kwenye dili, huo ndiyo uwongo, ni upotoshaji ambao unaweza ukaangamiza Taifa hili usiposimamiwa tena kwa ujasiri. Hakuna mtu atakayeogopa, kama mtu anasimama ana-*distort fact,* sasa eti mtu usijaribu, ukijaribu sasa kumkosoa

anasema huna hoja, hiyo ndiyo inaitwa *cheap* propaganda na ni hatari sana ikiruhusiwa inaweza ikasabaratisha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba watu wengine wana maeneo, sasa kwa yale ambayo Mheshimiwa amedai ninayo, hayo yako mikononi mwako utaelewa maana yake nitakuja kuidhihirisha vitu vyote ambavyo ni uwongo na itabidi viletewe ushahidi kwa yule anayevisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye suala la uthamini, watu wengi wamezungumzia uthamini na mimi nakubali na katika hotuba yangu jana tayari nilishawaambia na huwa nasema kila mwaka, uthamini kwa kweli unaleta matatizo. Kwa sababu sisi Ardhi hatufugi, hatuhifadhi, hatuchungi, hatuna shule, hatuna *dispensary,* kazi yetu sisi tu ni *land administration*. Kwa hiyo, kama wanajenga chuo, mfano MUHAS kule Mloganzira, sisi tunapimia wenzetu wa Wizara ya Elimu. Sasa nitoe tu rai kwamba, wale ambao wana miradi yao pale ambapo hawana fedha za kutosha kusema kweli mpira mwisho wa siku unarudi kwa wathamini maana sisi ndiyo tunaonekana wakati wa kuthamini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lazima niseme mambo ambayo nimeyakamilisha ni kuweka viwango vya uthamini endelevu. Kwa mfano, Kurasini Mheshimiwa Mtemvu nimekusikia, Kurasini bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara waliyokuwa wameweka haikutosha kwa sababu ya viwango vipya vya uthamini, pale ni Sh.80,000 kwa mita moja ya mraba, kwa hiyo heka moja ni milioni 300, fedha hazikutosha wanaendelea kujipanga. Natoa tu rai kwa wale ambao wana miradi yao kwamba ni vizuri kabisa fedha ziwe tayari. Kama unavyoona kwenye zoezi ambalo nimesimamia la Chasimba ndiyo maana nimekwenda kwa Waziri Mkuu kwa mfano kuweka utaratibu kwamba tupate pesa tutakapothamini tunakwenda kama *operation*. Huwezi kuwa na *incremental* yaani unamlipa huyu, kesho huyu, kesho yule inaleta bughudha na inaleta kutoelewana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mashamba makubwa. Waheshimiwa kutoka Tanga nimewasikieni na nina habari nzuri, mashamba saba ya mkonge ambayo yanatakiwa kutwaliwa, tayari Mheshimiwa Rais ameshaHridhia, tuko kwenye mchakato wa kutwaa mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kapunga, nilikwenda Kapunga kwa sababu tuko kwenye mchakato wa kutwaa lile eneo kusudi tumege hekta 1,870 zirudi kwa wananchi. Mheshimiwa Rais ameshaHridhia kwamba hilo eneo itabidi litwaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nifafanue kitu kimoja, hata ukiamua kutwaa eneo bado kuna mchakato, kwa sababu Sheria ya Ardhi, inasema kwamba kama kuna *encumbrance* mfano kuna mkopo, labda shamba limetumiwa kuchukua mkopo huwezi tena kumfutia yule mtu mwenye shamba. Sasa hapo sheria ambayo tunatumia ni Sheria ya mwaka 1967 ya Utwaaji Ardhi na ardhi haiwezi kutwaliwa bila ridhaa ya Mheshimiwa Rais na ardhi inatwaliwa kwa fidia inayotosha. Kwa hiyo, kwa Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Malocha na wengine, Sumbawanga kwa mfano, Sumbawanga ule ulikuwa mchakato, mlinikaribisha, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amenikaribisha sana tena ni rafiki yangu Mheshimiwa Stella, nilishindwa kwenda kwa sababu nilikuwa najua kwamba kulikuwa na mgogoro wa Mahakama unaendelea. Sasa Waziri wa Ardhi unakwenda kujitupa kwenye mgogoro wa Mahakama itasaidia kitu gani. Sasa hivi nitafurahi sana kufika kule kwa sababu nina habari za kuwaambia wananchi. Nilipokwenda Kapunga, nilikuwa tayari nina habari za kuwaambia wananchi. Kwenye migogoro mikubwa ya ardhi ukienda pale huna kitu cha kuwaambia wananchi unakwenda tu na wewe kuchochea vurugu, unaondoka watu wanaanza kupiga. Kwa hiyo, ni kazi ambayo pia inahitaji mtu uwe na uvumilivu, hakuna jazba, hakuna *sensation* na hakuna *cheap popularity* katika hili, ni lazima unafanya kazi hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kafulila amenikaribisha kwa muda mrefu, ziara yangu nimeshaipanga ndiyo nakuja Kigoma sasa.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Hayupo, lakini amenikaribisha sana, atapata habari hata kama hayupo. Kwa sababu kule Kigoma kuna wawekezaji wakubwa wanatafuta maeneo makubwa na nitakuja kuangalia hali ilivyo. Sasa hivi Waheshimiwa Wabunge mkae chonjo, naomba nitakapokuja kwenye maeneo yenu niwakute, wakati mwingine hata pamoja na kutoa taarifa unapoingia kwenye eneo unakuta wahusika hawapo, hiyo nayo inakuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba migogoro ya ardhi tunaweza tukaondoka nayo, ile ya hifadhi tunafanya kazi kama Wizara shiriki chini ya uongozi wa Waziri Mkuu. Mimi kwa upande wangu migogoro ya hifadhi, ile unaiondoaje, ile huwezi kuiondoa bila kujua mifugo itakwenda wapi. Pamoja na kuzungumzia teknolojia ni lazima tutafute ardhi mbadala kwa ajili ya mifugo. Zoezi hilo pia linahitaji nidhamu. Nilipokwenda Lukenge juzi wataalam wangu wakanionyesha mpango wa matumizi bora ya ardhi, sikuona kwamba walikuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya mifugo iliyo ndani ya kijiji kile. Kwa hiyo, moja kwa moja inabidi niwasiliane na Waziri wa Kilimo na wa Mifugo kwamba tutafanyeje kuhusu mifugo hii. Sheria zetu zinaruhusu, Waziri wa Mifugo

ana mamlaka ya kumwambia mtu kupunguza mifugo lakini, je, hiyo inatekelezeka kwa urahisi? Kwa hiyo, unakuta kwamba kazi hizi tunazifanya kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka sana nashukuru sana Kamati imesema watu ambao wana hela zetu tunaowadai wazirudishe, wakizirudisha *revolving fund* yetu itafufuka, tutafurahi.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Ndugulile inabidi tukutane kama unavyojua mimi niko *ready*, wala kule kutokutana siyo kwamba siko *ready*, niko tayari kabisa tukutane kwa sababu tunajenga nyumba moja, hakuna haja ya kugombania fito. Mheshimiwa Spika agizo lako siyo kama nililikiuka, nilishakutana na Mheshimiwa Ndugulile mara tatu tangu tulipotoka pale.

**MBUNGE FULANI:** Sio kweli.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Tumekutana Dodoma, tukakutana Dar es Salaam, tukakutana kwa Waziri Mkuu, kwa hiyo tumekutana lakini labda hiyo haijatosha.

**MBUNGE FULANI:** Aaaaah!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Kata tatu za Kigamboni, ni kweli kwamba Kata tatu zimeongezwa kwenye eneo. Hapa naomba nirudi kwenye kupanga mji, mji wa Dar es Salaam kama tunataka *silver spring revolution* kama zile Cairo tucheze na mji wa Dar es Salaam. Mji wa Dar es Salaam nimesema na naomba nirudie unakuwa kwa asilimia 5.6 kwa mwaka. Kwa hiyo, *population* ya Dar es Salaam baada ya miaka 13 itaongezeka. Sasa kule Kigambani Serikali ilikaa ikaamua kwamba basi lile eneo lote lipangwe kwa mpangilio wa kisasa kwa sababu bahati nzuri jiografia yake ni eneo ambalo bado lilikuwa halijajengwa sana kiholela.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtemvu amezungumzia kwamba Halmashauri ya Temeke ina hekta 22,000 bado inaizidi Halmashauri ya Ilala lakini Halmashauri ya Ilala inaendesha shughuli zake. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kama tunataka kupanga mji ni uamuzi pia siyo lazima uwe uamuzi wangu, kwa sababu mimi natekeleza Ilani ya Chama Tawala kama tunataka kukaa zagalabagala tuendelee lakini sasa hivi zile Kata zimeunganishwa pale na Serikali, ni uamuzi wa Baraza la Mawaziri, siyo uamuzi wa mtu wa binafsi na kama unavyosema kurekebishwa inaweza ikarebishwa, itarekebishwa na Serikali kwa ujumla. Kwa hiyo, asije akafikiria kwamba unaweza ukapanga mji peke yako, hiki ni kitu cha Kiserikali kwa ujumla wetu kwamba zile Kata zipangwe vizuri kusudi na sisi tuwe na mahali pa kujivunia na wote mliokuwa mnanikaribisha tuje kupanga miji yenu ndiyo hayo mnayoyataka.

Mheshimiwa Spika, nifafanue kwamba Mheshimiwa Rais ameomba msaada na tumeupata, watakuja wataalam kutoka China. Walipokuwa wanazungumza na Mheshimiwa Rais kule Zanzibar, yule Waziri wa Makazi wa China alimuuliza upangaji wa miji hapa ukoje, alisema katika nchi ya China, unajua wenyewe unajua wana watu wengi, Uchina mji wowote ambao una zaidi ya watu milioni 20 unapangwa na Serikali Kuu Beijing. Nimeomba na nafurahi kwamba wengi wameunga mkono wataalam wa Ardhi wamesambaa. Kwa hiyo, sina *mobile teams* na wengine wanapokaa kule kwenye maeneo yenu na wenyewe wanakuwa ni watu wa Halmashauri wanakaa na Madiwani na wenyewe wanakuwa *local*, wakipima viwanja na wenyewe wanajigawia 20 mambo yanakuwa kama kawaida. Tunaamini kwamba katika utaratibu mpya, wengine mmekubaliana na hili likipita tunawarudisha katika *central command* kusudi wawe ni *mobile teams* wanaingia mahali, wanafanya kazi yetu ya utaalam wanaondoka hawa *local stake,* ndivyo inavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Susan Kiwanga alizungumzia watumishi wa Mabaraza. Suala hili nirudie kusema kwamba Mabaraza kwa kweli yanatakiwa yawe kila Wilaya na sasa hivi hayapo kila Wilaya. Kusema kwamba ni usumbufu mimi sibishi najua kwamba ni usumbufu lakini sasa kwa hali halisi, utaratibu ule wa Mabaraza, unajua Mabaraza kweli kama alivyosema hapa kwenye hotuba, wengine wako TAMISEMI, Mabaraza yako chini ya Wizara ya Ardhi, halafu unapopanda ngazi za juu ndiyo unakwenda kwenye Mahakama ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ngazi ya Kata na ngazi ya Vijiji zile ni *mediation*, kwa kweli pale ni usuluhishi, migogoro ya ardhi iliyo mingi humalizika kwa usuluhishi na ndiyo maana utaratibu wa Mabaraza kwa ngazi ya Wilaya unakwenda kwa usuluhishi. Hata Mabaraza yetu ya Wilaya yana wazee wale *(assessors),* wanatakiwa waelewe ni kitu gani kinaendelea, wafike mahali pa tukio, wazungumze na wananchi wajiridhishe. Sasa kama huo utaratibu ukipelekwa kwenye Mahakama zetu za kawaida ambazo kwa kawaida ushahidi unakuwakuta mezani ilionekana kwamba watu wataumia. Kusema kwamba ukosefu wa Mabaraza katika kila Wilaya ni dosari kubwa na mimi nakubaliana kwamba ni dosari kubwa lakini nguvu zangu katika bajeti hii zimefika hapo zilipofikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Nundu, nadhani mashamba yenu huko Tanga yatarudishwa, tuko njiani ila sasa yakirudishwa ndugu zangu naomba tuelewane, yaende kwa walengwa ambao ni wananchi. Kwa hiyo, hapo naomba ninyi Wabunge msimamie kuhakikisha kwamba yanakwenda

kwa walengwa. Siyo tunarudisha mashamba tena yanakwenda kwa watu ambao hawakuwa walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abood nakushukuru kwa pongezi chache zilizopatikana hapa leo. Wewe ngoja siku moja figo ikikorofisha ndiyo utajua figo leo imeleta matatizo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini upimaji wa ardhi uliuzungumzia na umewakilisha pia kimaandishi, mawazo yako tunayachukua, mengi yatatusaidia huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, Kibaha kweli hampati majibu kuhusu vijiji na migogoro iliyopo. Niseme kwamba Kibaha kwanza tumeunda Kanda mpya sasa ya Ardhi ambayo itakuwa inashughulikia Pwani na Morogoro na naamini kwamba italeta majibu ya haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nifafanue kwamba na hizi ziara zangu za kuja Mikoani pia zinaathiriwa na bajeti finyu tuliyonayo kwa sababu kama mnavyofahamu kutatua mgogoro ni kitu ambacho kinahitaji fedha za kutosha na kama huna fedha za kutosha huwezi kutatua migogoro, kwa hiyo, wengine mtanivumilia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda umekwisha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa hayo marefu na machache, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**KAMATI YA MATUMIZI**
**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi**
**Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Bado natudia kusema anapokuja *Serjeant-at-Arms* kuondoa hii siwa hapa tunatulia, maana tusipofanya hivyo tunataanza kuwa na kitu ambacho hakieleweki. Kuna *rules* zetu ndogo ndogo naomba zifuatwe ili Bunge lionekane liko *neat,* tunaendelea!

Kif. 1001 - *Administration and*
*HR Management* .........................Tshs.6,976,011,652/=

**MWENYEKITI:** Sawa, ni Mshahara wa Waziri, kwa mujibu wa kifungu cha 101(3) na (4), ninayo majina yaliyoletwa na vyama. Sasa namuita Mheshimiwa Amina Mwidau. Waliochaguliwa na chama sina haja ya kuwataja kwa maana wamechaguliwa hukohuko!

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Leo kwa kweli ilikuwa niondoke na shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri lakini angalau kidogo amesema Tanga mashamba ya mkonge yatarudishwa, namshukuru kwa hilo ila sasa msikae miaka miwili tena ikapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa kuongea, mbali ya mashamba ya mkonge pia niligusia kitendo cha Serikali kuchukua maeneo ya wananchi na kuyafanyia tathmini kwa ajili ya kupima viwanja na kukaa nayo kwa muda mrefu sana, miaka sita kama ambavyo nilitoa mfano wa Neema bila kufanya kitu chochote na kuwazuia wananchi kuwafanya shughuli zozote za maendeleo kwa muda mrefu. Nikaomba Wizara kama Wizara ituambie itawasaidiaje wananchi hao, kubwa nililiomba waweze kurudishiwa maeneo kwa sababu ni kilio karibu cha Tanzania nzima, warudishiwe maeneo yao mpaka Serikali itakapokuwa tayari. Waziri na Naibu Waziri nadhani hawakugusia lolote kwenye suala hili. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe *commitment* ya Serikali watawasaidiaje wananchi hawa ambao maeneo yao yamechukuliwa na yameshafanyiwa tathmini lakini hawajalipwa chochote, ni muda mrefu, wameathirika kisaikolojia, wamekaa hawajui nini kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri, maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Amina Mwidau kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli imekuwa ikitokeatokea mara kadhaa malengo fulani ya kuchukua eneo fulani yanakuwa yamekusudiwa. Malengo haya yanatofautiana na wakati mwingine yanaweza yakawa ni kwa maslahi ya Serikali kwa maana ya kwamba Serikali inalihitaji eneo hilo lakini wakati mwingine ni kwa ajili ya uwekezaji wenye faida chanya kwa maana ya

kwamba tunatarajia mtu fulani anaweza akafidia na sisi kazi yetu pale kama Wizara ni kuhakikisha kwamba waliothaminiwa wanathaminiwa vizuri maana kazi ya kuthamini ni kazi ya Wizara yetu lakini pia kuhakikisha kwamba wanalipwa kitu sahihi. Hata hivyo, wakati mwingine miradi hii au malengo yale hayakamiliki, tutajaribu kuona kwa sababu jambo hili linaenda kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu *scenario* zinatofautiana, pale ambapo tutakuta *evaluation* imefanyika na imekaa muda mrefu, maana *evaluation* ina muda wake, kama muda ule ukipita tena inakuwa si ile tena. Tunajaribu kuona namna tutakavyoweza kuyapitia yote na ku-*evaluate* tuone maeneo gani ambayo kwa kweli kama imekaa muda mrefu basi tutakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge yaachiwe au shughuli nyingine ziendelee kwa sababu kimsingi inawakwaza sana wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Namelok  Sokoine!

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia tatizo la mgogoro ya mipaka kati ya Wilaya ya Monduli, Longido na Arumeru. Nilikuwa naomba kusikia majibu ya Mheshimiwa Waziri, je, ana majibu gani ya kutupa kwa sababu tayari kuna mauaji yametokea katika maeneo hayo na mgogoro ni wa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Naibu au Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Namelok Sokoine alileta mchango wake wa maandishi na nadhani jambo hili ni la kwenda *site*, kwa sababu masuala ya migogoro hasa yanapohusisha Wilaya tatu, kuna hatua zilizokuwa zimefikiwa lakini bado juzi tumesikia tena watu wameuwana. Tulikubaliana na Mheshimiwa na tulikwishaongea naye kwamba tutakwenda, hata kabla ya Bunge hili kuisha tujaribu kwenda kuona chanzo na pengine *scenario* imebadilikaje maana kulikuwa kuna hatua fulani zilikuwa zimefikia ili tuweze kumaliza jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Blandes.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia kwa uchungu sana mgogoro wa ardhi ya Ranchi ya *NARCO* ya Kitengule ambapo Serikali iliamua kugawia wawekezaji wachache na zaidi ya nusu ya *ranch* hiyo ikagawiwa kwa kampuni ya Kagera *Sugar* wakati wananchi wanaoishi jirani na ranchi hiyo wa vijiji karibu saba, ikiwemo Kibwera, Katanda, Mshabaiguru, Kishoju, Mramba na Nyarwere hawana sehemu ya kufugia hata ng'ombe mmoja. Serikali ilishaji-*commit* kwa kusema kwamba inawagawiwa wananchi wale hekta 2000 ambazo kimsingi na

zenyewe hazitoshi. Pia, Serikali pamoja na kuzigawa bado haijawapatia hata hekta moja na mgogoro huo unaendelea kufukuta. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwa sababu ndiye jirani yangu, Muleba Kusini na Jimbo la Karagwe tunapakana. Sasa nimechangia hapa na sijapata majibu na mgogoro wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Simbachawene, tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu na nimemtaka aende pale akatatue mgogoro huo, yeye akiambatana na Waziri wa Mifugo na Naibu Waziri pamoja na wa TAMISEMI. Kwa masikitiko makubwa sana sijapata jibu wala hata hawajagusia mgogoro huu ambao ni mkubwa sana. Ningetaka nipate majibu!

**MWENYEKITI:** Umepata tatizo la kilimo au la ardhi au la nini? Kama mna majibu jibuni!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nifafanue tu kwamba katika migogoro hii kati ya mashamba makubwa hususan *Kagera Sugar,* wananchi na vijiji, Serikali tayari tumeshaanzisha zoezi na tunaanzia Mkoa wa Kagera kwa kuangalia *viability* yaani uwepo wa vijiji ambavyo viko jirani na mashamba haya ya *NARCO* yaliyotaifishwa na pia Ranchi kama Kitengule lakini pia Ranchi kama Kagoma ile ya Muleba. Nataka kusema kwamba migogoro ni mikubwa na naifahamu, Mheshimiwa Blandes kama unavyofahamu sina haja ya kusimuliwa migogoro hii, Mheshimiwa Mwijage amekuwa akizungumzia sana. Kwa hiyo, tutafanya zoezi la kutathmini vijiji ambavyo viko karibu na Ranchi ya Kitengule kuangalia sasa matumizi bora ya ardhi na kupanga upya.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili tunakwenda hatua kwa hatua, kwa mfano, tunapoangalia ranchi nyingi wale wenye *blocks* tayari wana mikataba na *NARCO*. Sasa ile mikataba inazuia Sheria ya Ardhi kufanya kazi, unakuta sheria tuliyobaki nayo pale ni Sheria ya Utwaaji wa Ardhi. Tunapotwaa ardhi lazima pia tujipange kutoa fidia lakini mchakato huu unaendelea na Serikali ina taarifa nao na tunaanzia Mkoa wa Kagera kwa sababu kama tunavyofahamu migogoro ni mikubwa kama vile tulivyokwenda Morogoro. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tunalishughulikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lulida, hukuondoa shilingi, ulitaka ufafanuzi tu, Mheshimiwa Lulida!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru lakini nipende kusema kitu kimoja Lindi tuna maeneo makubwa ya mashamba ya katani hayakuguswa vilevile kuna mgogoro mkubwa ambao sasa hivi

unaleta hatari katika Mkoa wa Lindi, mradi wa UTT ambao umeingia Mkoa wa Lindi kwa Wilaya ya Kilwa na Lindi na tathmini yao imekuwa ni ya chini. *Square meter* moja ni shilingi mia moja ukilinganisha na wenzetu kama Dar es Salaam, *square meter* moja ni shilingi 80,000/- mpaka 35, 000/- hii inawafanya wananchi kutaka kuchukuliwa maeneo yao kwa shilingi laki nne tu na ni maeneo ambayo ni ya baharini na kuwafanya wananchi wa kule kunyanyasika sasa hivi, wanapigwa na kutiwa ndani na imekuwa ni tatizo kubwa. Waziri anasema nini maana Waziri wa TAMISEMI amezuia lakini katika hotuba yake humu amesema kwamba wanaendelea kupima katika eneo la Lindi. Naomba tamko la Waziri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waziri majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimwia Mwenyekiti, nifafanue tu kwamba hapa ni wananchi kujua haki zao kwa sababu Sheria ya Fidia ni kwamba mimi mwenyewe kama Waziri wa Ardhi lazima niridhike na fidia inayotolewa. Hiyo, fidia ya shilingi mia moja kwa mita ya mraba ya Lindi haijafika Ofisini kwangu. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba ni sisi tu wenyewe kusimamia haki za wananchi kwa kujua haki zetu. Kwa hiyo, kama kuna Halmashauri au kama kuna watu wengine ambao wanatoa fidia ambazo siyo stahiki ni kutafuta ufafanuzi kwa *Chief Valuer,* tuko pale tutaangalia hali ya soko, maana fidia inaendana na bei ya soko. Kama ni shilingi mia moja kwa mita mraba kwa Lindi, kama nilivyosema mwezi ujao wataalam wangu watakuja Lindi kuangalia namna tunavyopanga Lindi na Mheshimiwa Lulinda hapo nakutegemea sana kutukaribisha kusudi kazi yetu ngumu kama unavyoina iweze kwenda vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitika sana. Katika mchango wangu wa maandishi na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 62, 63 na 64 ameeleza utatuzi wa migogoro ya mashamba kati ya wananchi na wawekezaji. Nachotaka kusema ni kwamba ameelezea namna ambavyo baadhi ya wawekezaji hawaendelezi yale mashamba na akaeleza vizuri kwamba Serikali inakusudia kuyatwaa yale mashamba. Akatolea mfano wa Shamba la Malonje kwamba litatwaliwa na Serikali lakini akasema inabidi lifidiwe. Sasa mimi nimeshindwa kuelewa, kama mashamba yale hayakuendelezwa, fidia hiyo inatokana na nini na katika fidia hiyo katika bajeti yake hakuna mahali ambapo ametenga hiyo fidia. Nimepata wasiwasi kwamba jambo hili haliwezi kuisha na jambo hili ni kubwa sana, lina mateso kwa wananchi, wananchi wanakatwa masikio, wanakatwa miguu, wanakufa na sisi wawakilishi tunatishiwa vifo. Sasa sijajua jambo hili Serikali inaliweka katika mazingira gani.

Mheshimiwa Spika, nahitaji maelezo ya kutosha vinginevyo nashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Shamba la Malonje limefikia tamati yake, mwenye shamba alikopa fedha, sasa fedha alizokopa ameshindwa kulipa, sasa hivi shamba lile kimsingi linaelekea mnadani, unakuta na Serikali hapo na sisi tunajipanga kwenda kuokoa shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba, mtu anapokiuka masharti ya miliki, hiyo inaitwa *revocation,* sasa hapo anafutiwa, unapotwa shamba unatwaa *in public interest* kwa manufaa ya umma, ni lazima utoe fidia kwa mwenye shamba. Kama mtu amekiuka masharti ya miliki, sasa hiyo ndiyo inaitwa *revocation*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shamba hili la Malonje, sasa hivi tulipofikia ni kwamba sisi tunajitayarisha kuhakikisha kwamba shamba hilo linarudi mikononi mwa Serikali. Niseme kweli bajeti, kama nilivyosema ndiyo maana tuko huko Chasimba na bajeti kubwakubwa mnavyoziona, katika bajeti yangu hakuna hata shilingi moja ya kufidia shamba lolote tutakalochukua. Hiyo ndiyo hali halisi, huo na ukweli niuseme kama ulivyo kwamba hakuna hata shilingi moja. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba fidia zinapatikana, huwa nakwenda kwa Waziri Mkuu tunahangaika, itabidi zitafutwe kama *emergence* maana huwezi kujua mchakato wa kufidia utakuwa lini, lakini hizo bilioni tatu ambazo tutazihitaji na zenyewe ni kama zikipatikana haraka, tukawahi sasa kwenda kule Mahakamani kulikomboa lile shamba ili turudishe kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maelezo hayajatosheleza kwa sababu shamba hili limeanza kuzungumzwa karibu miaka mitano iliyopita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha fuata utaratibu!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua shilingi!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa*
*Wabunge walikuwa wakiongea)*

**MWENYEKITI:** Mimi nasimamia shughuli hapa, najua, hakusema nitatoa siyo hujatoa, mbona mnajitia mafundi sana hapo katikati!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa huo ndiyo utaratibu!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ninyi mmesimama kwa ajili ya nini?

**WABUNGE FULANI:** Tunamuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Shilingi haiungwi mkono, yeye ametoa hoja ya kuondoa shilingi ili apate maelezo vizuri, sasa ndiyo nampa nafasi aendelee kueleza, sasa wengine mtachangia, siyo mnaunga mkono.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Shamba hili ni mgogoro wa muda mrefu ilipelekea hata mwaka jana kumuambia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais akatoa maelezo kwamba siwezi nikakubali wananchi wakateseka kwa sababu hawana mahali pa kulima. Akamuagiza Mheshimiwa Waziri, kwamba nakuagiza unileteee tatizo la shamba hilo, ukiniletea saa tatu, saa tano nitakuwa nimelimaliza. Sasa nashanga Mheshimiwa Rais alitoa agizo mwaka jana tarehe 17 Juni na sasa hivi ni miezi kumi na moja, nashindwa kuelewa nchi hii, nani kiongozi wa kuheshimika, naomba maelezo ya kutosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Keissy, nitafanya *randomly* kwa sababu…

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua…*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza! Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Keissy sasa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Inahusianaje, shamba lenyewe ukienda kuliona huyo mwenye shamba alikuwa na ng'ombe zaidi ya 300 kauza zote, hajaendeleza lolote, leo kaenda kukopa Kenya mabilioni ya hela, bilioni 300, Serikali mlipe fidia bilioni 300. Hii Serikali ya kuchukuliwa hela kienyejienyeji tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatuhusu nini sisi, kuweka dhamana hilo shamba bilioni tatu kaenda kuchukua Benki ya Kenya wakati shamba halifikii hata bilioni moja, yeye alinunua shamba kwa milioni mia sita na kulikuwa na ng'ombe zaidi ya 300. Kwa hiyo, mimi napinga kabisa wazo la kulipwa fidia, yule bwana lichukuliwe shamba lirudishwe kwa wananchi mara moja, zile ng'ombe zinamtosha kwa shamba lake. Hii siyo Serikali ya kuchezea, kodi ya wananchi kuchezewa kuchezewa hatukubali sisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi *seriousness* ya Serikali ingeonyeshwa kama jambo hili lingekuwa limewekwa kwenye bajeti na sisi wananchi wa Rukwa tungekuwa na uhakika kwamba wananchi wale wanaenda kupata shamba. Hata hivyo, inapokuwa kwamba hakuna pesa yoyote ambayo imetengwa kwenye bajeti halafu Serikali inakuja inasema kwamba wananchi watapata shamba lile na wakati wanatuambia kwamba ni lazima mmiliki apewe fidia, maana yake ni kwamba Serikali wanataka kutudanganya, hawana uhakika na hiki wanachokisema kwa sababu wangekuwa na uhakika wangeweka kwenye bajeti. Naomba tupate maelezo ya uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwanza linaifedhehesha Serikali na inaonesha dhahiri kabisa ni namna gani mnafanya maamuzi yasiyokuwa na tija. Kuna vijiji ambavyo vinazunguka shamba hilo, kuna vijana ambao hawana ajira wangeweza kuliendeleza eneo hilo lakini Serikali ikaona ni bora kumuuzia mwekezaji ambaye ameshindwa kuliendeleza na vijana wanahangaika hawana mahali pa kufanyia kazi zao na majibu yanayotolewa pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais lakini hakuna utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kwamba sasa mnasema nini kurudisha ardhi hii kwa wananchi hawa ili waweze kuiendeleza. Ni aibu na ni fedheha kabisa vijana wetu leo wamekuwa ni manamba katika shamba hilo na mtu huyo ambaye amekuja kwa *umbrella* ya dini badala ya kufanya kazi ya kuhubiri na kuingiza watu katika dini ananunua ardhi na anaendeleza mashamba sehemu nyingi za nchi hii. Hii biashara ni lazima tuiangalie, ni nani wana maslahi na Efatha? Ni waumini wa Efatha au kuna watu nyuma ya Efatha, tunataka kujua hilo pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nijue kitu kimoja kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Muda wa kilimo umeshakaribia na yeye ametujibu vizuri tu, mimi nashukuru kwa majibu yake. Kwamba, lengo letu sisi ni kupata shamba, haya maneno mengi, mwisho wa siku nikuombe tu Mheshimiwa Waziri, tuahidi hapa lini utakuja Sumbawanga?

Mimi nakuunga mkono tena hoja yako, lakini naomba utuahidi hapa, lini utakuja Sumbawanga, kwa sababu umefika wakati wa kuanza kulima na Wananchi wanasubiria? Sasa ndiyo maana nimesema toka mwanzo, tumekuwa tukiwaahidi sana hawa Wananchi. Lini utakuja Sumbawanga na kurudisha shamba hili kwa Wananchi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa uchungu, shamba liliuzwa na hapo lazima nikiri kwamba, liliuzwa kwa Viongozi wa Mkoa. Serikali ilirudisha shamba mkoani na mkoa ndiyo ukaliuza kwa mmiliki wa sasa. Pamoja na hayo, mimi kwa upande wangu, suala hili nalishughulikia na wiki iliyopita nimekaa na Mheshimiwa Rais, tukawa tunazungumzia shamba hili hili. Kwa hiyo, sasa hivi kama mnavyofahamu, ni kwamba tunakwenda na mchakato wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi ambazo tunazizungumza, zinazonifunga, mimi ningependa tukitoka hapa twende Sumbawanga nikakabidhi shamba, lakini sasa mchakato wa kisheria. Kwa sababu kesi moja haiwezi kufuta kesi nyingine, maana kesi iliyopo sasa hivi imewekwa na Wakenya, kwa sababu huyu mtu alikopa Kenya Shilingi bilioni tatu. Kwa hiyo, unakuta kwa mfano, Shamba la Kapunga, mwekezaji amekopa dola milioni 15, Hon Kong, ndiyo maana nimechelewa. Kama nilivyowaambia Figo, hamuelewi kwamba huku nyuma tunahangaika na hii kazi. maana yake hizi hati miliki, ukishapata hati miliki, unakwenda kwenye benki yoyote Duniani unakopa.

Sasa Sheria yetu ya Ardhi tuliyonayo, kwa mfano, Shamba la Kapunga au hili, hili nilisubiri, la Shinyanga nilikuwa nimekaa kimya na mimi nikimwomba Mungu kwamba, huyu atashindwa kesi, tulipate angalau kwa bei hiyo. Kwa hiyo, *Alhamdulillahi* kesi imemshinda, kwa hiyo, tunakazana sasa hivi kwenda na Mheshimiwa *PM* yuko hapa anasikia. Kwa hiyo, mimi mara moja nikipata zile bilioni tatu, nakimbia, tunakomboa lile shamba, nakuja hoi hoi vifijo, tunakabidhi Wananchi shamba lao.

Shamba la Kapunga kwa mfano, mchakato wa kisheria unaendelea, kwa sababu pia Tanzania inaweza ikashtakiwa ngazi za Kimataifa kwa kukiuka mikataba. Kwa hiyo, unakuta tunakweda polepole, hilo ndiyo tatizo. Sasa kama kuna *encumbrance*, Sheria ya Ardhi haitusaidii, maana yake Kamishna

amezuiwa na sheria ile kutwaa shamba, kufanya *revocation* kama kuna *encumbrance*. Kwa hiyo, hapo tunategemea Sheria ya Mwaka 1967 ya Utwaaji Ardhi na hapo utwaaji ardhi unatwaliwa kwa fidia.

Sasa kama mtu amekiuka masharti ya miliki, kwa mfano, mtu hajalima, yuko pale, tunamfutia. Sasa kama unafahamu, huo nao ni mchakato mwingine wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labla mimi nitoe mfano, katika *frustrations* zangu kubwa nilizonazo, ni mahakama inavyoweza kuingilia kazi ya ardhi. Kama mahakama inalinda jengo ambalo tunajua ni *condemned building,* lakini linalindwa na mahakama lipo; sasa inatoka kwenye mashamba inaingia kwenye nyumba na kadhalika na kadhalika.

Kwa hiyo, mara Serikali itakapoweza kukamilisha tukapata lile shamba, tunakuja kulikabidhi kwa Wananchi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Sijaridhika kabisa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza, suala hili ni kashfa kwa Serikali. Kwa sababu Shamba hili linazungukwa na vijiji zaidi ya kumi na ni kashfa kwa Serikali, Viongozi wote Wakuu wameenda kule wamelalamikiwa na wametamka mbele ya Wananchi kwamba, lazima Shamba hili lirejeshwe, lakini muda ambao Serikali inachukua katika kutatua matatizo ni muda mrefu.

Mimi nitakubali endapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa tamko namna ya kurejesha lile Shamba la Wananchi. Kwa sababu labda nitoe maelezo, Serikali haiko *serious*, wale watu waliokopwa fedha kule Kenya, walikuja na baada ya kuja walifika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakasema kwamba, tumekuja na hati ya shamba letu tunataka kuliuza, lakini tunatoa *priority* kwa Serikali kwanza.

Shamba lile limekaa miezi miwili, Serikali haijatamka chochote, ikabidi yule dalali aende mahakamani kuomba kibali cha kutangaza kuliuza shamba, akapewa kibali. Alipotangaza kuliuza lile shamba, ndiyo mwekezaji akaenda kuomba mahakama iwakutanishe ili yule bwana a-*withdraw*, waanze kuelewana kienyeji. Kwa hiyo, Serikali ingekuwa *serious*, shamba lile lingerejeshwa tena kwa gharama ndogo. Kwa hiyo, mimi nataka Serikali iji-*commit* katika suala hili, Wananchi waweze kurejeshewa shamba, mwaka huu waweze kulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu utataka kusema? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimenyamaza kwa sababu natoka huko, kwa hiyo, nikasema pengine nisije nikaonekana na mimi nina upande gani. Mgogoro ule tunauelewa na ni wa siku nyingi. Baada ya kuwa tumefikia katika hatua za mwisho, kwa kweli kilichotokea ni *technicalities* tu, ni masuala ya kitaalam tu. Kwa hiyo, hivi sasa tulichokuwa tunajaribu kuona ni namna ya kuondoa hiyo hali ambayo ndiyo imekwamisha utekelezaji wa utwaaji wa ile ardhi.

Sasa ukifika hapo, hakuna namna nyingine isipokuwa kutafuta tu mchakato mwingine wa namna ya kutoka nje ya hilo tatizo. Kwa hiyo, pengine mimi nimwombe tu ndugu yangu Malocha na wenzake wote ambao walisimama, watuvumilie tutatue huu mgogoro kwanza. Siwezi nikasema ndani ya muda gani, laini ndiyo tatizo lililokwamisha upatikanaji wa ile ardhi. Kwa hiyo, tutajitahidi tuone kama tunaweza tukafanya hilo jambo mapema na yeye ana shauku kubwa, kwamba labda mwezi wa tisa au wa kumi, kabla msimu haujaanza, tuone kama tunaweza kuwa tumepata hiyo ardhi. Hicho ndiyo tunachoweza kukuahidi kwa sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha tumalize hili.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa imani niliyonayo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, narudisha shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Jafo. Nafauata maeneo, watu waliozungumza wa maeneo fulani nawaacha. Mheshimiwa Said Jofo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi hoja yangu ipo katika suala zima la ujenzi wa Chuo Kikuu cha Muhimbili katika eneo la Mloganzila. Nilipeleka mchango wangu wa maandishi katika Wizara husika. Hapa hoja kubwa ni kwamba, eneo lile karibu asilimia 84 liko katika Wilaya ya Kisarawe na asilimia 16 iko katika Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa maelekezo kwamba, Waziri mwenye dhamana afanye utaratibu eneo hilo sasa liwe katika Halmashauri mojawapo kati ya hizo. Kwa uzito wa jambo hilo, ina maana kwamba, eneo hilo kwa sababu Kisarawe tunatoa asilimia 84, ni wazi kwamba, irekebishwe mipaka basi eneo lile lije Kisarawe.

Kwa hiyo, sasa nataka *commitment* ya Mheshimiwa Waziri; ni lini hilo jambo litakamilika, sambamba na kuhakikisha kwamba, fidia za watu ambao

wanadai pale za ardhi ambapo Mheshimiwa Rais naye alipokuja kuweka Jiwe la Msingi, watu walilalamika na *documents* zote ziko kule Serikalini? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Mheshimiwa Saidi Jafo, nimwambie kwamba, tunazungumza na wadau kuhusu shamba kubadilisha mipaka. Kama unavyojua ni mchakato ambao unazihusu Halmashauri husika, kusudi wakubaliane namna tutakavyoweza kurekebisha mipaka hii na hivi sasa mchakato unaendelea, kwa hiyo, hiyo *process* ni kutoa taarifa kwamba unaendelea.

Kuhusu fidia za ardhi, kama ulivyosema, suala la fedha zenyewe za ardhi. Pale Mloganzila eneo lilidhihirika kwamba, lilikuwa ni eneo la *Tanganyika Packers*; kwa hiyo, fidia haikutolewa kwa ajili ya ardhi, ilitolewa kwa ajili ya maendelezo. Unaona kadiri tunavyojitahidi kwa mfano tunapotaka kutoa fidia hisani kama inayotolewa Chasimba, kama fedha zikipatikana, 15,000 kwa mfano inakuja 5,000, sasa ukibadilisha kidogo inaonekana zimeingia mfukoni mwa Waziri, kitu ambacho siyo kweli.

Sasa kule Mloganzila, mchakato nilipoukuta, fidia ya ardhi haikutoka Mloganzila, pametoka fidia ya maendelezo. Wananchi wa Mloganzila wamekuwa wakiomba, wameshalipwa tayari fidia ya maendelezo. Sasa hili suala la fidia ya ardhi, kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais imempendeza kwamba, tutoe fidia ya ardhi, sasa mchakato huo unaanza upya. Kwa sababu kabla ya hapo, bajeti hiyo haikuwepo na kimsingi kwa Wizara ya Ardhi, tulikuwa tumeshafunga mjadala wa Mloganzila, lakini sasa kama fidia hisani itapatikana, itakuwa ni fidia hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili nalo lieleweke, kwa sababu lile eneo walikuwa ni *squatter,* hiyo ni sehemu ya *squatter,* walikuwa hawawezi kupata fidia halali. Kwa hiyo, nitafuatilia kuangalia kama bajeti itapatikana, eneo ni kubwa. Naona Mheshimiwa Saada anasema, aaah, lakini kwa sasa hivi kwa bajeti iliyo mbele yenu, hakuna hata shilingi moja kwa ajili ya Mloganzila.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Naibu Waziri kuhusu mgogoro nilioufikisha mbele yake kutokana na barua ya Wananchi wa Himo. Sasa nieleze tu kwamba, hilo Shamba pale Meresini linalogombaniwa, siyo la ukoo, ni shamba lililokuwa la mkonge la Serikali *(General Land)*. Mgogoro ulianza mwaka 2006, Wananchi wakasema jamani kwa kuwa hatuna ardhi hapa, eneo hili tulitumie kwa manufaa ya jamii. Viongozi hawakuchukua hatua zozote, wakaanza kujigawia.

Sasa kilichojitokeza kwenye hii barua naomba nirudie tena kwamba, matajiri wamepewa mashamba makubwa katika eneo hilo la umma na umma kupewa maeneo madogo na wametaja kwa majina. Hizi ni hujuma, wanaohujumu nchi hii ni Viongozi. Aloyce Bent Kimaro amepewa eka 11.7, kwa ajili ya kujenga kituo cha redio, wakati Shule ya Sekondari Meresini yenye watoto 700, imepewa eka tisa! Cha kusikitisha zaidi, eneo ambalo Wananchi wa Kijiji cha Himo, walikuwa wanategemea kwa ajili ya upanuzi wa Shule ya Sekondari Meresini *(A Level)*, ambalo liko mkabala na shule ndiyo alilopewa tajiri huyu. Redio iko hapa, shule iko hapa na tunataka kuendeleza shule ile.

Tajiri mwingine wa Arusha anaitwa Minja, kapewa eka saba wakidai kwamba ni kwa ajili ya kituo cha kulea watoto wa mitaani. Shule ya Msingi, ambayo ina wanafunzi 400 wamepewa eka tano. Sasa hakuna Mwananchi wa pale anayesema apewe yeye, lakini tunachoshangaa, hii *general land,* hii ardhi ya umma, kwa nini imegawanywa bila kuzingatia mahitaji ya watu wa pale; wanataka soko, wanataka vituo vya watoto, wanataka mahali pa kuchezea, viwanja na kadhalika.

Sasa nilikusomea nikakwambia Afisa Ardhi wa Kanda, kwa barua ya mwaka jana, ameandika wazi na iko hapa, anaonesha kwamba ardhi ile imegawanywa visivyo. Sasa nani kawapa tena madaraka ya kuwamilikisha hao watu ambao tunawalalamikia? Nimemwonesha Mheshimiwa Naibu Waziri pale na wewe Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachotaka, sishiki shilingi, naomba utufafanulie wale wadau pale, wale Wananchi maskini, wenye watoto, vita viko pale kati ya Wananchi na Maafisa wa Ardhi na Mkuu wa Wilaya na Halmashauri, siyo Wafugaji na Wakulima.

Kwa hiyo, naomba utuepushe na huu mgogoro.  Unawaambia nini Mheshimiwa, hebu rudia yale maneno uliyosema?  *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante.  Rudia yale maneno sijui yapi!

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mrema alishanionesha hizo *documents* zote. Msingi wa tatizo hili ni kwamba, kwanza, ardhi ni ya kwao pale, lilikuwa shamba.  Ninaamini walipewa kama Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na wakaweka mchakato wa kugawiana walivyoona inafaa. Kinachoelezwa hapa ni kwamba, wako baadhi wamegaiwa waeneo makubwa na kwamba, masilahi ya jamii hayajaangaliwa, ila ubinafsi umezidi sana.

Kama umilikishaji bado, tutakuwa na fursa ya kupitia na kuliangalia na kama ni tayari, tutajaribu kutafuta tuone tunaweza tukafanyaje na kurekebisha. Kwa sababu ninachotaka kusema hapa, anayesema hapa ni Mbunge na mimi siwezi kudharau. Mbunge anawakilisha watu, anayoyasema siamini kama ni yake binafsi. Basi tujaribu kuona kama muda unaturuhusu tuweze kupitia upya, namna walivyoligawa lile eneo, tuone uhalali wake na kama jamii, wadau wote walishirikishwa inavyotakiwa na kwa mujibu wa sheria.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama kupata maelezo kuhusu Mabaraza ya Ardhi, kwa sababu migogoro ya ardhi inaongezeka na ni wazi kwamba, majibu yaliyotolewa hapa ya upimaji, *squatters* zinazidi kuwa nyingi mjini na nini na vijijini, kwa hiyo, migogoro itazidi kuwa mingi.

Sasa mimi nilisema kwamba, Mabaraza haya yarudishwe kwenye Mahakama. Hili nililihoji tangu mwaka jana, nikasema mwaka jana peke yake kwa bajeti ilikuwa Mabaraza matano yaanzishwe, ambayo hayo Mabaraza ya mwaka jana mpaka mwaka huu ndiyo hayo hayo tunaendelea nayo. Nikatoa mfano, Mwananchi wa Kibondo, kutoka Kibondo kwenda kwenye Baraza Kigoma, ni zaidi ya kilomita 240 na maeneo mengi.

Kutoka Kibakwe kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kuja kufuata Baraza Dodoma, ni kilomita nyingi sana, ni mateso, ni usumbufu. Mtu hawezi kuwa na mgogoro wa shamba la laki tano, aanze kuhangaika kulifuata hilo Baraza huko liliko kwa zaidi ya gharama hata ya shamba lake. Nikasema, sasa Mheshimiwa Waziri amejibu, kwamba, kuna utaratibu wa Mabaraza, haya yana Wazee wa Mabaraza. Ninataka nimwambie hata kwenye Mahakama za Mwanzo, huu utaratibu wa Mabaraza upo. Hawa Mahakimu ambao tunawaajiri kwenye Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, wamesoma mambo haya ya *mediation*, mambo haya ya utatuzi na vitu vingine. Wanayafahamu vizuri, tena wengine wana ujuzi kuliko hata Wenyeviti hawa wa Mabaraza.

Sasa tukiendelea na utaratibu huu wa miaka miwili tunahangaika na Mabaraza matano, toka mwaka 2003 tumeanza kutumia Sheria hii, ni Mabaraza 42. Wananchi wanahangaika nchi nzima. Nataka majibu ya Serikali na nisipojibiwa nitatoa shilingi kwenye jambo hili. Lini mambo haya yanarudishwa kwenye Mahakama, kwa sababu Wizara haina fedha za kuanzisha Mabaraza nchi yote? Nikaeleza hata kwangu Kibondo, tuna jengo tumetoa, lakini wameshindwa kuleta watumishi.

Kwa hiyo, kuendelea na mchezo huu ni kutaka Wananchi wahangaike kutafuta haki zao. Nitaondoa shilingi endapo sitapewa majibu kwenye jambo hili, ili jambo hili liweze kujadiliwa. Naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mabaraza ya Ardhi kama linavyosemwa na Mheshimiwa Mkosamali, ni sahihi kabisa kwamba, Wananchi wanapata shida kwa ajili ya kwenda umbali mkubwa na kwamba Mabaraza ni machache na utekelezaji wa Sheria ile haukwenda kwa kasi kama tulivyotarajia na sababu ni rasilimali fedha, hii inaeleweka.

Hoja ya Mheshimiwa Mkosamali, ambapo ninasema, kusudio lake la kuondoa shilingi aliache na mimi ninaongea na yeye kama Mwanasheria na mimi pia hapa ni Mwanasheria; Mabaraza haya yalianzishwa kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo, kusema ni lini, maana yake sasa tunabadilika kutoka kwenye Sheria ya sasa, sasa sijui tunai-*repeal*, sijui tuna maana ya kuifuta; maana sheria ile kwa ujumla wake ilizungumzia zaidi Muundo wa Mabaraza na uendeshaji wake.

Tume ya Kurekebisha Sheria, haikusema Mabaraza haya hayana faida kabisa. Imekiri kwamba, pamoja na hayo yote, lakini Mabaraza haya angalau yanakwenda kwa haraka na kesi nyingi sana za ardhi zimeamuliwa. Sasa, ndani ya Serikali tunaendelea kulijadili hili, tukizingatia maoni ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Tupewe muda, kwa sababu Mabaraza yameanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, huwezi ukasema kama ilivyo hoja ya Mheshimiwa Mkosamali kwamba ni siku fulani tutafanya. Nimwombe sana Mheshimiwa Mkosamali, mchakato huu tunaufahamu na hayo unayoyasema yote ni sahihi, tuachie tupewe muda Serikali tuone namna ya kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, kwa hiyo, unaondoa shilingi sasa?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa shilingi ndiyo. Jambo hili lazima tulitazame sana. Wewe fikiria Wabunge wangapi hapa wamejadili kuhusu hali ya migogoro ambayo itatokea kutokana na *squatters* silizoko mijini. Serikali imekiri hapa kwamba, haina uwezo wa kupima maeneo. Kwa hiyo, ni wazi kutakuwa na migogoro mingi kila mahala, migogoro itakuwa inaongezeka kila siku. Mmesikia Wabunge wengi sana wamesema hili.

Sasa mimi nimezungumza hoja hii kwamba, lazima Mabaraza haya yawe kwenye Wilaya na tukasema uwezo wa Wizara haupo, kujenga ofisi, nyumba za Mabaraza haya ili yawepo kila Wilaya haiwezekani. Tumeliona hili kwenye bajeti zote zilizopita miaka minne, mitano nyuma na tukasema Sheria inataka Mabaraza yawepo kwenye kila Wilaya, mpaka leo tuna Mabaraza 42. Sasa

tunachosema hapa, hoja ni kwamba, Katiba ya nchi inatambua kwamba, chombo kikuu cha kutoa haki ni Mahakama, Ibara ya 107.

Kwa hiyo, Sheria hiyo kwanza ipo kinyume na Katiba, ndiyo maana nikawaambia mnang'ang'ania ya nini kwa sababu hata kesi zikitoka kwenye Mabaraza hayo zinakwenda Mahakama ya Rufaa? Huku chini hayo Mabaraza wanayosema yako *efficient,* yako TAMISEMI, haya-*perform* wala watu hawa hawana ujuzi wa *mediation* wala *arbitration*, hawajui chochote! Mimi naomba Wabunge wenzangu muisikilize hoja hii na mniunge mkono; nchi hii imejaa *squatters*, migogoro ni mingi, Wananchi hawawezi kuwa wanakwenda mikoani kufuata haki za mashamba yao madogo madogo, kutembea kutoka huko Kibakwe, sijui wapi, kwenda mikoani kufuata haya Mabaraza.

Naomba Serikali iji-*commit*, inaanzisha haya matano hayatoshi, kama wanayang'ang'ania watuambie mwaka gani watakuwa wamemaliza, kwa sababu hatuko tayari kuvumilia. Tukienda na utaratibu huu miaka mitatu, minne, mitano, ni Mabaraza mawili, tutakaa miaka mingapi mpaka Wilaya zote ziwe na Mabaraza na sisi tunataka kesi za ardhi zianze kutatuliwa kuanzia kwenye Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii ijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, hoja yenyewe hasa ni nini, watafanyaje kuanzisha Mabaraza kila Kata au hoja ni ipi sasa?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba, kwa sababu Mabaraza haya ni machache na hayawezi kutatua migogoro kwa kuwa karibu na Wananchi, basi yarudishwe kwenye Mhimili wa Mahakama na kwa sababu Katiba ndiyo inautambua. Mahakama za Mwanzo ziwe zinasikiliza kesi ndogo ndogo Mahakama za Wilaya ziwe zinasikiliza, kwa sababu kule kuna Wataalam, Mahakimu hawa wamesoma Sheria za Ardhi, wamesoma mambo ya *arbitration* na *mediation.* Kwa hiyo, hatuna haja ya kuhangaika kufuata Mabaraza haya mikoani ambayo yameshindwa kufanya kazi yake.

**MWENYEKITI:** Hatufuti hata Sheria tunaendelea tu?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria itafutwa, wala haina tatizo ni kuileta tu tunabadilisha tunaendelea.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hoja hapa ni kufuta Sheria ya Baraza wala si chochote, vinginevyo haifanyiki hapo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Sawa, nadhani imeeleweka katika kufafanua.

**MWENYEKITI:** Niwaite wale ambao hawajasema sana, Mheshimiwa Salim. Wanasheria hawa wakubwa wanataka kutuchanganya, wenyewe wanajua sheria, ndiyo maana siwaiti. Haya endelea bwana, Mheshimiwa Salim kwanza. Endelea tu, nimewaandika, nawajua. Kwa hiyo, ni hayo tu tuendelee. *(Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni kupunguza mateso kwa Wananchi kama alivyosema mtoa hoja. Kwanza, naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Mkosamali. Hali ya migogoro imekuwa ikiongezeka na hoja inakuja kwamba, Mabaraza haya yerudishwe kwenye Mahakama kutokana na umbali ambapo wanapata usumbufu Wananchi wetu. Kwa msingi huo, mateso ambayo wanayapata Wananchi wetu na uchache wa Mabaraza haya na hali inaonekana kwamba, kila miaka mitatu, minne, Mabaraza yanayopatikana ni mawili, matatu au manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mateso kwa Wananchi, lazima kuwe na mkakati mahususi. Kukiwa na mkakati mahususi, Mabaraza haya kufutwa au kurudishwa kwenye ngazi za chini za Mahakama, itaweza kutoa haki kwa Wananchi na watajua haki zao na haki inaweza kutolewa kwa sababu Mahakama ndiyo chombo pekee kinachoweza kutoa haki za Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja aliyoita Mheshimiwa Mkosamali. Nashukuru sana.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mkosamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi zote, umetengeneza balaa kubwa katika nchi hii ambalo linatishia kusababisha maafa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mabaraza ya Kata hayana Wanasheria, hayana Wataalam, ni rushwa tupu, ni balaa.

Mabaraza ya Wilaya yanaitwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; lakini ukweli ni kwamba, Mabaraza haya hayajawahi kuwa ya Wilaya, kwa sababu linaloitwa Baraza la Wilaya unakuta linasikiliza kesi za Mkoa mzima. Zamani kesi za ardhi zilipokuwa chini ya utaratibu wa kimahakama, zilikuwa zinaanzia Mahakama ya Mwanzo. Karibu kila Wilaya katika kila Tarafa kuna Mahakama ya Mwanzo yenye Wanasheria. Zilikuwa zikitoka Mahakama ya Mwanzo zinakwenda Mahakama ya Wilaya, karibu kila Wilaya ina Mahakama ya Wilaya yenye Wanasheria. Zikitoka huko zinaenda hata Mahakama ya Hakimu Mkazi iliyoko kila Mkoa, ina Wanasheria, zikienda hapo zinaenda juu Mahakama Kuu. Kwa hiyo, utaratibu wa kimahakama ulikuwa uko *manned* na

watu wenye utaalamu wa sheria. Leo hii Mabaraza yote chini ya Mabaraza ya Wilaya ni ya watu baki, ni balaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili linahitaji kushughulikiwa; na namna ya kulishughulikia ni kuleta Muswada wa Sheria kuvunja Mabaraza, utaratibu wa utatuaji wa kesi za ardhi wa kutumia Mabaraza ya Ardhi, turudishe mamlaka haya katika mfumo wa kimahakama. Bahati nzuri na hiki ni kitu muhimu, tumetengeneza sheria mwaka wa jana au mwaka wa juzi, ambayo imeruhusu wanaofuzu sheria katika vyuo vikuu na siku hizi ni wengi, tuna vyuo vikuu 15, waweze kuajiriwa katika Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, tuna idadi kubwa ya Wanasheria katika hizo ngazi za chini wanaoweza kuajiriwa na kushughulikia kesi hizi kwa namna ambayo ni ya kisheria zaidi na suala hili ni *urgent* sana. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kimsingi, nasimama kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mkosamali. Ninaunga mkono hoja kwa sababu moja tu kubwa ya msingi; Tume ya Kurekebisha Sheria ni chombo kilichoundwa na Serikail. Kama Tume ya Kurekebisha Sheria imeona kuna matatizo kuhusiana na haya Mabaraza ya Ardhi, halafu bado Serikali inakuwa na uzito katika kuona umuhimu kwamba, Mabaraza haya yanapaswa kuundwa pasipo kuchanganywa. Baadhi yanaonekana kwamba, yapo kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni tatizo la kwanza. Wakati huo huo, *High Court* pia inakuja kuingia ndani yake na *Court of Appeal,* tayari kunakuwa kuna mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninafikiri Wizara ya Ardhi watuambie tu kwamba hapa ili kuhakikisha tunaondokana na matatizo haya na kwa sababu malalamiko ni makubwa ukienda kwenye kila kona; haya Mabaraza kama ambavyo Waheshimiwa wengine wametangulia kusema, kwa kweli haki ni kidogo, malalamiko ni makubwa sana. Tuamue tu kwamba, pengine Bunge lako liseme, kesi zote za ardhi ziende zikashughulikiwe kwenye mkondo wa kimahakama, ambapo tunaamini kuna watu wengi wamebobea kwenye masuala ya kisheria wanaelewa.

Huu utaratibu na ahadi ambazo zimekuwa zinaendelea za Wizara kwamba kila mwaka, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, muda umekwisha. Mheshimiwa Mbowe!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nitaongea kwa kifupi sana. Napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mkosamali, hasa tukiangalia tatizo hili ambalo nililizungumza mapema kwamba, *squatter* ambazo zinasambaa nchi hii kwa kasi ni hatari kubwa kweli kweli kwa usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la *rural urban migration*, watu kuhama maeneo ya vijijini kuhamia maeneo ya mijini. Lazima kama Taifa tujue kwamba, hili ni tatizo kubwa na lisipowekewa *mechanism* ya kuli-*control,* litaweza kusababisha maafa makubwa sana siku za usoni.

Sasa hoja ya Mheshimiwa Mkosamali kwamba, turudishe mfumo huu wa migogoro ya ardhi kwenye Mahakama ni hoja ya msingi sana, kwa sababu ya mtandao mkubwa sana wa kimahakama ambao tunao katika nchi yetu. Ukweli kwamba, Naibu Waziri amesema hapa kwamba, tatizo lipo kwenye Halmashauri za Wilaya, Waziri vilevile baadaye akatoa majibu mengine kwamba, hawana fedha. Ina maana hatuna mkakati, hatuna *strategy* yoyote ya kukabiliana na migogoro ya ardhi kwa kasi na kwa upana ambao unatokea. Kwa hiyo, naomba niunge mkono hoja hii na niwaombe Wabunge wengine wote waunge mkono hoja hii, kwa sababu ina masilahi mapana si kwa mtu yeyote lakini kwa Taifa kwa ujumla, kwa sababu matatizo ya ardhi yatatuletea ugomvi wenyewe kwa wenyewe na si jambo ambalo tunastahili tulifumbie macho. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza, niseme kwamba, siiungi mkono hoja hiyo, kwa sababu zifuatazo:-

Hakuna Wizara ambayo inatengeneza fedha kwa maana ya kwamba, inajitengenezea mafungu haya na hivyo kugawa kadiri ya mahitaji yake. Fungu kuu la Serikali ni moja, kila Wizara inagaiwa na haigaiwi kwa kuzingatia vipaumbele ilivyo navyo. Mwaka jana wakati Waziri wa Ardhi akihitimisha hoja yake, alieleza hapa kwamba, ili aweze kuendesha Mabaraza ya Ardhi nchi nzima, kwenye Wilaya zote, anahitaji Shilingi 22,000,000,000 kwa mwaka, kwenye Mabaraza hayo. Kiasi alichopewa hapo ni kiasi gani kwa ajili ya Mabaraza? Kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja hapa, ni kweli kwamba, tuna migogoro ya ardhi na nyumba. Tutatatua vipi? Kwanza, tushirikiane kuhakikisha kwamba, eneo hili la Mabaraza ya Ardhi linatengewa fungu la kutosha. Hiyo moja.

Jambo la pili, tuangalie pengine labda kurekebisha sheria, kuona kwamba, pale ambapo Baraza la Ardhi bado halijaanza, basi Mahakama ya

Wilaya iliyoko pale ipewe *jurisdiction* ya kusikiliza mashauri hadi hapo Baraza la Ardhi litakapokuwa limeanzishwa. Ukisema kwamba, tuondoe Mabaraza ya Ardhi, *spirit* ya kuanzishwa kwa Mabaraza haya sasa inaondoka na ilitokana na uwezo mdogo wa mahakama za kawaida kushindwa kutatua migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi mtazamo wangu, ninaenda kwa uzoefu. Wilaya yangu ya Kisarawe pale kuna Wananchi wangu wa kawaida, wana migogoro ya ardhi ambayo mpaka waende Kibaha, kuna watu wanatoka Mkuranga mpaka waende Kibaha. Inaonekana kuna changamoto kubwa kwa Wananchi wetu wa kawaida kuweza kutatua matatizo yao ya kiardhi, hata Bagamoyo. Nini maana yake? Kwa sababu tuna rasilimali hizo hizo chache tulizokuwa nazo, kwa sababu tuna Mahakama zetu zipo, mimi kwa mtaji huo hoja ya Mkosamali naona ina mantiki kubwa sana, kwa masilahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu kuna kuna haki zao zinapotea, uwezo wa kusafiri kwenda mbali ni mdogo, tuangalie ni jinsi gani tutafanya ilimradi huyu Mwananchi wa kawaida tuweze kumsaidia aweze kupata huduma iliyokuwa bora zaidi. Kwa hiyo, mantiki ya hoja hiyo mimi naona ina masilahi kidogo kwa Wananchi wetu wa Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi juzi tulijibu swali hapa kuhusu haya Mabaraza ambayo yanazungumzwa. Nia na shabaha ya - Mabaraza haya ya Kata ambayo yanasemwa hapa, ilikuwa ni kutafuta tu maridhiano katika *level* hiyo. Moja hilo. Sheria ile na hii tunataka tuiweke vizuri ili watu waelewe kwamba, ni kitu gani tunachozungumza. Pale hakuna *lawyer*, kama wewe ni *lawyer,* huna sifa ya kuingia pale.

Kwenye Baraza, ile Sheria ukiisoma, kama wewe ni Mbunge au ni Diwani, huwezi kuingia pale kwenye Baraza la Kata ukazungumza. Pale wanatafutwa watu wa kawaida tu, ambao wanaridhiana wanazungumza mambo. Pale kama una *degree* au una diploma ya sheria, huingii kwenye haya Mabaraza. *Spirit* yake ilikuwa ni nini? *Spirit* yake ilikuwa ni kuondoa migogoro midogo midogo ambayo inatokea mingi katika jamii pale, wakae kwa pamoja wazungumze waridhiane.

Leo ukija hapa ukasema unataka uondoshe haya Mabaraza; yana matatizo yake na labda niseme ili niweze kuwa *objective* zaidi. Ni kweli, unakwenda kwenye Mahakama ile pale, unakwenda kwenye lile Baraza pale,

halafu unasema hivi, ili kuendesha kesi hii hapa tunataka wale ambao wana kesi hiyo watoe hela kwa ajili ya kuliendesha Baraza. *That is wrong*.

Mimi nikienda pale nikatoa shilingi laki mbili, laki tatu, *definitely, obviously,* wakati watakapofanya maamuzi wata-*consider* aliyekuja na dau kubwa. *This is the problem* ambalo tunajaribu kuli-*address* sasa, kwa sababu moja ambalo tumelifanya sasa tumeagiza kwamba, Halmashauri zetu zote zihakikishe zinatenga hela kwa ajili ya kuendeshea haya Mabaraza ambayo tunayazungumzia hapa.

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ni muhimu na hoja yenyewe ni kweli inashikika. Kwa maana ya kwamba, kwa uzoefu tulionao ni kweli, kama alivyosema Mheshimiwa Mkosamali kwamba, Mabaraza ni machache, *efficiency* haijawa nzuri sana, tunajua tuna uzoefu, tunaishi kwenye Wilaya huko, kesi haziendi kwa kasi kutokana na sababu nyingi ikiwemo bajeti. Kwa hiyo, uendeshaji wa Mabaraza haya ni kweli tunajua na hoja ni ya msingi kwamba, hata hayo 45 uendeshaji wake ni wa mashaka.

Kwa hiyo, nafikiri kama Serikali tunaweza tukasema hoja hii ina mshiko, ni hoja ya maana. Mheshimiwa Mkosamali, atusaidie ili angalau *think tanks* ya Serikali tukakae pamoja tuangalie *the way forward*. Hoja tumeipata na uzoefu tunao, tuone namna ya kufanya na hata hili pendekezo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi Mstaafu, linaweza kuwa ni *alternative*. Kwamba, pale ambapo hakuna Mabaraza kama kuna Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Kawaida, zifanye hiyo kazi. Haya ni mambo ya ku-*consider* wakati tunaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Mheshimiwa Mkosamali, mjadala huu umekuwa na afya, umetupanua mawazo kama Serikali, tupo wote hapa, Serikali ni moja maana hawezi kuamua Waziri wa Ardhi peke yake, tuko wote hapa tumelisikia, ngoja tukalitafakari kwa sababu ni hoja ya msingi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawashukuru wote waliochangia. Hoja hii, neno lolote litakalosemwa ni sahihi. Lolote likisemwa na hakuna aliyesema uongo na wote tunakubaliana kimsingi. Sheria hii ni Sheria ya Bunge, ilitungwa kutokana na mazingira ya wakati huo na *concept* hii ni ushauri uliotokana na Ripoti Shivji juu ya migogoro mingi ilipokuwa iko *subjected* kwenye Mahakama zetu za Kawaida na ikatufikisha mahali ikawa kidogo ni ngumu. Kwa sababu aina ya migogoro ya ardhi si kama kesi za kawaida, ina *speciality* yake, haiwi-

*solved* kwa *degree* wala haihitaji sheria. Jamii za zamani zilizokuwa hazina Wanasheria, walilima pamoja, walichunga pamoja, hawakupigana kama leo.

Leo tunapigana na *degree* tunazo na ni Wanasheria. Sheria hapa siyo msingi wa kumaliza migogoro. Hapa kinachotakiwa ni kukubaliana tu kwamba, hoja hii inayoletwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali, inachokihitaji hakiwezi kupatikana kwa haraka kama anavyotaka, lakini tunatakiwa kufikiria namna gani tunaweza tukafanya. Hilo mimi ninakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi tumesema, Ripoti ya Tume ya Marekebisho ya Sheria, imeshauri ikasema, haisemi kabisa kwamba, Mabaraza haya hayana maana. Inasema yana *fast truck,* lakini hata wanaohusika katika migogoro hii ni jamii za kawaida sana. Ukimpeleka kwenye utaratibu wa kawaida wa Kimahakama, unawatisha, pale Hakimu yuko na nini. Hii migogoro ukienda kwenye Mabaraza ni ya kirafiki, unafika pale unaulizwa enhe mama, kuna akina mama wazee kabisa vibibi vimekamatiwa mkongojo wanafika mpaka pale anaulizwa mama unasemaje, anabembelezwa. Kwenye Mahakama ya Kawaida huikuti hiyo. Kwa hiyo, ninasema tujaribu kuiangalia kwa umakini mkubwa kwa kuzingatia pia ushauri uliotolewa na Tume kama alivyosema Mheshimiwa Ole-Medeye kwamba, Tume imesema pale ambapo hakuna Baraza basi tunaweza tukatumia Mahakama ya Kawaida. Hayo yote na msingi wote wa ushauri wowote, ama kufuta au kwenda kwa njia yoyote mbadala tutakayoiona, jamani inahitaji mchakato. Mchakato huo hauwezi ukawa wa jibu la lini tutamke hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Felix Mkosamali, kwa maneno haya utusaidie kuturudishia shilingi, kwa sababu jambo hili haliwezi kujibiwa kwa jibu moja, linahijaji mchakato fulani. Ingawa tunakubaliana na hoja kwamba, kweli Wananchi wanateseka, umbali ni mkubwa na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mkosamali, mimi naamini, wewe ni rafiki yangu utarudisha shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali mwenye hoja. Mmh, kuna watu wana midomo imechongoka wakati wote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Mkosamali, tafadhali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni kweli kwamba, waliochangia wamechangia vizuri na hoja hii ni ya msingi.

Nikubaliane na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kwamba, jambo hili tulitazame. Serikali ikubali kuleta Muswada na ione kama ni jambo sasa siyo la kuchelewa kwa sababu tuliomba toka miaka iliyopita. Kwa hiyo, mimi niiache hoja hii, lakini Serikali sasa iwe na *commitment*. Kwa sababu Tume ya Kurekebisha Sheria imeshatumia fedha, imeshatafiti jambo hili, kwa hiyo, Serikali ni kwenda tu kwenye kutekeleza na kuleta Muswada hapa, kwa sababu kazi imeshafanyika. Haya mambo ya kutazama kwamba, Mabaraza yatakuwaje na nini, tutayajadili wakati Muswada wenyewe uko hapa. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ilichukulie jambo hili kama la msingi, kwa sababu watu wanaumia sana kwenye Mabaraza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwarudishie shilingi yao. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Unajua hili swali lilikuwa la msingi sana, maana linavuruga Sheria tulizotunga sisi wenyewe. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri sana, uamuzi ni kwamba, tulifanyie kazi. Waheshimiwa Wabunge, mkileta hoja zenu zikiwa na mshiko namna hiyo msiwe mnaishia humu, endeleeni kusaidia huko nje tupate kitu ambacho ni cha kuangalia sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mkosamali. Kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (5), nitaongeza dakika zangu 30, ikifikia kasoro dakika kumi tutaingia kwenye utaratibu wa *Guillotine*.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na niseme tu kwamba, ninakusudia kutoa shilingi, iwapo maelezo ambayo nitayapata hayataniridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda katika hoja mahususi, nilitaka nitoe ufafanuzi katika majibu ya hoja ya Mheshimiwa Waziri, kurejea agizo lako la mwaka 2013, uliagiza kwamba, Mheshimiwa Waziri na imesomwa hapa na Mheshimiwa Mwidau, kwamba, akutane na Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni kuweza kujadili masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme kabisa kwamba, hatujawahi kukutana na Mheshimiwa Waziri. Hatujawahi kuonana barabarani, kuonana kwenye *corridor,* hiyo ninakiri kwamba imefanyika. Kikao cha mwisho na ninaweza nikakisema kwa tarehe, ilikuwa tarehe 7 Februari, 2013 na huo ulikuwa ni mkutano wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam na Waziri Mkuu. Mara nyingine ambayo huwezi ukasema yalikuwa ni mazungumzo, ilikuwa Desemba, 2013 wakati alipokuwa akionana na Wananchi wa Uvumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maagizo yako, hatujawahi na ninaweza nikasema kwamba, agizo lako limepuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mradi wa Mji Mpya wa Kigamboni bado ni changamoto kwetu sisi. Maelezo ambayo tunayapata mpaka sasa hivi hayatupi matumaini, nina hakika kabisa na Wananchi wote wa Kigamboni ambao wanafuatilia kwa sasa hivi, kwa kweli bado inawatia unyonge mkubwa sana, ninapata *message* nyingi sana, kusema kwamba, hadi hivi sasa tunavyoongea, hawaoni matumaini ya Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ambazo zinatufanya sisi tusikubaliane na utaratibu mzima wa huu Mradi; Mradi ni mzuri, *concept* ni nzuri, lakini ni jinsi gani unavyotekelezwa. Suala zima hapa, ni masuala ya jinsi gani Sheria ambazo zinasimamia mchakato huu zinakiukwa na hiyo ndiyo hoja ya Wananchi wa Kigamboni.

Pili, Wananchi jinsi gani wanashirikishwa katika suala hili la mradi wa mji mpya wa Kigamboni.

Suala la tatu, ni suala la haki stahili na hatima za Wananchi wa Kigamboni. Mpaka sasa hivi bado tuna giza nene na huu ni mwaka wa sita na haya ndiyo malalamiko ya Wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013, limeongelewa suala la hisa, kwamba, Wananchi wa Kigamboni watalazimishwa kukatwa asilimia kumi ya mapato yao, kuingiza katika huo Mfuko ambao ni wa kuendeleza Kigamboni. Litakuwa ni jambo jema kama tungelikuwa tumeshirikishwa sisi Wananchi wa Kigamboni tukaulizwa, tukaridhia na ingeliwezekana kabisa tukatoa hata asilimia 20 hata 30, lakini suala hili hatujashirikishwa. Halijawahi kuletwa kwetu na sisi tukaulizwa. Sasa tunasikia kwamba, kuna Wataalam waelekezi wameshachukuliwa wanafanya moja, mbili, tatu; lakini suala hili la hisa siyo suala la lazima. Hisa ni suala la hiari. Kwa hiyo, ni lazima niseme wazi katika hili suala la hisa, tutafikishana pabaya na mimi niko tayari kuwa Mbunge wa kwanza wa Chama cha Mapinduzi kuipeleka Serikali yake Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne, ni suala la hizi Kata tatu. Manispaa ya Temeke ipo kisheria, ina mamlaka yake, ina mipaka yake. Sasa hivi katika hilo agizo ambalo limetolewa katika Gazeti la Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, dakika zako tano zimeisha.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate majibu, kama sitaridhika nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika, unaonaje tukimaliza hili halafu mkakaa na Waziri Mkuu, kwa sababu *the big issue here, when I need his support. Thank you. (Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Ndungulile, niseme kilio chake na hoja zake kwa niaba ya Wananchi wake wa Kigamboni zinaeleweka. Kimsingi, ni changamoto, kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba, tangu 2008, Mradi unaendelea; ni Mradi mkubwa sana, unaboreshwa, lakini bado haujafikia tamati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kuhusu kukutana, ninaomba tukitoka tu hapa mimi na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tukutane, tukubali yaishe. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa suala la kukutana ninaomba nikusahihishe. Mimi pale Ofisini kwangu sasa kuna faili zima la barua, ndiyo maana nikasema, wale watu ambao wanaandika hizi barua wanajulikana, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wewe na Wataalam wako, mkakae, tena kama hilo mnalolizungumzia lingine jipya hilo ndiyo ingelikuwa vizuri zaidi, siyo wewe na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tu.

Ninaomba kabisa, kwa sababu ninazo barua nyingi na wewe mwenyewe unajua nimekurudishia barua nyingi sana. Kwa hiyo, ninaomba hili ndivyo hivyo ninavyosema mimi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekusikia, lakini kama mwenyewe alivyosema, Desemba pale Chuo Kikuu cha Nyerere, tukiwa na Wananchi tulifanya mkutano mzuri, ambao nilifikiria kwamba ulikuwa ni mkutano, sasa kama kuna barua hyingine tutaendelea tu. Tutakutana, sasa hivi ni tarehe zake tutakutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo tayari wakati wowote kukutana na Wananchi wowote. Kama nilivyosema, kusudi tuweze kwenda mbele zaidi na suala hili, ila sasa tutakapokutana na Wananchi mchakato unaendelea. Maana sitakutana na Wananchi kuwaambia sasa leo ninalipa fidia. Siwezi kulipa fidia ambayo mimi sina. Huo ndiyo ukweli wenyewe. Huu ni Mradi wa Serikali, ni Mradi wa Chama cha Mapinduzi, *it is not a personal issue.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika *point* ninaomba niseme kabisa kwamba, tutakapokutana na Wananchi wanaonisikiliza sasa hivi, ninaomba niseme, sekta yangu ni ngumu, hii siyo sekta ambayo utakutana na Wananchi na kuwaambia uongo, kwa sababu una-*raise expectation.* Sasa una-*solve* tatizo lako unalihamishia kwao. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, tukikutana tutaangalia namna ya kwenda, sawa kabisa.

Mheshimiwia Mwenyekiti, sasa kuhusu sheria kukiukwa, majibu tunayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumejibu. Mheshimiwa Makamu wa Rais umejibu, Mheshimiwa Spika umeyaandikia barua. Tunajibu kwamba, sheria tumezifuata ila mgogoro ni mrefu. Hilo ninaomba niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hisa, kazi hii, huwezi kuifanya kama huna ubunifu. Ndugu zangu tunapokwenda hapa pia Serikali imejipanga kuboresha maisha ya Mtanzania. Sasa huko nilikotoka, kwa utaalam nilionao na vitu nilivyojifunza, mojawapo ni hili kwamba, unapowapa watu fidia, ufanye pia kazi ya wenzangu ambao wako Wizara ya Fedha, watu ambao wako wanapambana na umaskini. *Saving,* ni wakati mzuri kumhamasisha Mwananchi kufanya *saving.* Siyo suala la kwamba, utalazimisha mpelekane Mahakamani, siyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mfano; Mheshimiwa Waziri Mkuu, alinituma kumaliza mgogoro wa *Geita Gold Mine*. Mgogoro ule ulianza mwaka 2004 na sasa hivi ndiyo nimeumaliza. Nimeumaliza vipi? Kwa sababu ninajua *skills* za kumaliza mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi ule unachimba, kama nilivyosikia kwa upande wa Tarime kule *North Mara* ambako sijafika, lakini ninajitayarisha kwenda. Mgodi unachimba lakini haujawahi kuwafidia Wananchi ambao wana maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hiyo, unakaa kwenye *mediation* na hapo ilikuwa wazi wazi kwamba, baada ya vuta nikuvute na Mgodi na hapa lazima nikiri kwamba, Waziri mwenzangu wa Nishati na Madini, tukakubaliana kwamba, kwa kuwa yeye ameshatoa leseni ya kuchimba, mimi ni lazima nitoe *surface right*. Haki za ardhi ziko wapi. Kwa hiyo, ilibidi kuukodolea macho mgodi na kusema kwamba sikilizeni ninyi watu wa Mgodi, fungeni huu Mgodi, kwa sababu hamjawahi kuwafidia Wananchi ambao wana eneo lao, kama Sheria inavyosema.

Mheshimiwa Spika, sasa matokeo kwa Kigamboni; hisa, ninatoa mfano, nataka kujibu kuhusu hisa. Kule Geita sasa hivi kuna *SACCOS* ya Wananchi wa Geita waliofidiwa, ina shilingi milioni 680. Kwa sababu Wananchi baada ya kukaa nao kwenye *Town Hall Meeting,* hiki kitu huwezi kulazimisha, tutafanya

vikao kama nilivyokaa na Wananchi wa Chasimba na Mheshimiwa Ndugulile tulikuwa wote. Wananchi baada ya kuelewa maana ya hisa, tulikaa Kigamboni, pale kwenye Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere. Wananchi wakanisikiliza nikatoa somo la hisa. Zile hisa ni kwamba, ni *savings.* Sasa kwa upande wa Kigamboni, Wananchi wanalilia na ni haki yao na mimi ninawaunga mkono asilimia 100 kwamba, wanataka kubakia kwenye ardhi yao. Sasa kule Kigamboni siyo *SACCOS,* wenyewe ni kubaki kwenye ardhi yao. Watabaki vipi kwenye ardhi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watabaki kwa kununua hisa au niseme *shares* katika hiyo *trust* ambayo ndiyo inaundwa. Kwa hiyo, Mwananchi anayepata kwa mfano kama una ekari moja, unachukua shilingi milioni 141, kwa fidia ya Kigamboni ya Mradi. Sasa shilingi milioni 14, huyo Mwananchi ananunua hisa, anaweza kuamua kurudi Mkuranga kuendelea na maisha yake, lakini anabakia kwenye ardhi kwa kupitia zile karatasi. Ataweza kuzirithisha kwa vizazi vijavyo. Kwa sababu ile ardhi, baada ya muda itakuja kupanda thamani kuliko tunavyoweza kufikiria sasa hivi kama kweli tutaweza kuwa na uvumilivu na tutaweza kuwa na nia. Wanasema penye nia pana njia, tujenge mji wa kisasa kama miji ya wenzetu mnavyoiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mambo ya *faster faster,* basi tutabakia kwenye *squatter* zetu. Sasa ninachotaka kusema ni kwamba, kwa pale zile hisa, hii ni mbinu mpya. Kwa hiyo, huwezi kufungua mawazo tu, kusikia namna ya kufanya *modern business.* Siyo kwamba kila mtu anasema nitaingia ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kigamboni, kwa mfano, kule Uvumba, tumeshaanza kufanya tathmini. Wananchi walio wengi wana maeneo madogo, kwa hiyo, inabidi ukusanye ardhi pamoja kusudi uweze kupata eneo kubwa kutoa kwa mfano kwa wekezaji wa nje na wa ndani, ambao wataweza kuleta viwango tunavyovitaka. Hiyo haitawezekana kwa sababu Wananchi walio wengi wana maeneo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wananchi wengine ambao wana maeneo makubwa na Kamati yangu ilishaelekeza na ushauri mzuri ninaufanyia kazi. Kusema kwamba, labda wenye maeneo makubwa wale wanaweza wakanunua hisa zaidi au wengine wanasema waingie kwenye ubia wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalokuja ni *Master Plan* ile. Wewe unaweza ukawa na mwekezaji wako wa Hoteli, wakati sisi tunataka Chuo kwenye eneo lako. Ninaomba mnielewe, kwa hiyo, ninataka kusema kwamba, suala la hisa ni suala la elimu. Mimi ninaona kazi yangu ni ushawishi na kama unavyosema ninafikiri kikao tutakachofanya na Mheshimiwa Mbunge, ni lazima

nitoe hii elimu ieleweke tunafanya nini. Hizi ndiyo njia za kisasa za kufanya kazi, siyo mtu unabaki kwenye sehemu yangu eti ni sehemu yako, unabaki kwa kutumia hisa, unakuwepo unakuwa *shareholder*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niki-*digress* lakini hapo hapo ku-*make point;* kwa mfano, Kiwanda cha *Wazo Hill* cha *Cement,* wengi mna hisa mle. Si ajabu kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wana hisa kwenye Kiwanda cha *Cement*. Kwa hiyo, unaposema mwekezaji, unazungumzia wawekezaji Watanzania wenye hisa ndogo ndogo, kwa sababu hiyo ni *public company*.

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, katika hili tuwe wote, kama kuna kitu ambacho hakijaeleweka nieleze, ndiyo kazi yangu. Bila ushiriki wake na kuunga mkono, kwa vyovyote vile itakuwa vigumu, kwa sababu yeye ndiye mwenye eneo na ndiye mwenye Wananchi. Kama ninavyosema, Madiwani wangu wa Muleba wako pale. Bidii ninayoiweka Kigamboni, ningelikuwa nimeiweka Muleba mambo yangu yangekuwa kidedea. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ujue kwamba, mimi niko kule, ninafanya kazi ambayo hata kwenye Jimbo langu mwenyewe sina muda wa kufanya. Ahsante.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Menyekiti, mimi ninaomba nitoe shilingi, kwa sababu maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli hayajitoshelezi. Hapa tunaongelea haki za Wananchi wa Kigamboni. Katika suala la hisa, Wananchi wa Kigamboni hawajatoa ridhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anasema kwamba, wataishi Kigamboni kwa kupitia hisa; aniambie hisa ina vyumba vingapi; hisa ina sebule ngapi; hisa ina vyoo vingapi ili na mimi nitoe maelezo haya kwa Wananchi wangu wa Kigamboni niwaeleze kwamba unabaki kuishi Kigamboni kwa kupitia hisa hiyo hisa ina vyumba vingapi na sisi tuweze kuelewa inakuwaje.

Pili, Mheshimiwa Waziri anaongelea suala la ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni, ni kwamba, hauwezi ukaanza mchakato wowote bila kufanya *Public Hearing,* kwa mujibu wa kifungu Namba 19 (c). Hapa Mheshimiwa Waziri anasema ameshaanza kufanya tathmini na kupima miundombinu; ni kinyume na haya ndiyo mambo ambayo na sisi Wananchi wa Kigamboni tunayalalamikia!

Mheshimwa Mwenyekiti, mimi ninaomba nitoe fursa kwa Wajumbe wengine nao wapate fursa ya kuchangia kabla sijahitimisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tatizo kubwa lililopo Kigamboni kwa namna ninavyolitazama mimi, toka Mheshimiwa Dkt. Ndugulile amelileta hapa miaka mitatu iliyopita, imekuwa kwa kweli ni ukosefu tu wa ushirikishwaji wa Wananchi, lakini pia hata Viongozi wa kuchaguliwa wa kisiasa; kwa mfano, Mbunge mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani Mradi huu ni mzuri na hakuna anayepinga kwamba, Mradi huu ni mzuri na utekelezwe na Serikali yetu. Sasa tatizo linakuja namna unavyotekelezwa. Kama Serikali kweli ina nia ya dhati ya kutaka kutekeleza Mradi huu kwa mafanikio, ni lazima ishirikiane na Mbunge wa Jimbo hilo, lakini pia ishirikiane na Wananchi wa eneo lile. Hata mimi ni Mwananchi wa Kigamboni, kwa hiyo, yanayosemwa na Mbunge hapa ninayafahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeliweza kushirikishwa sisi Wananchi wa Kigamboni, kwa kiasi kikubwa tungeliweza kutoa mawazo yetu, ni namna gani wazo hilo la hisa lingeweza kutekelezwa kwa ufanisi na tija kubwa bila migogoro hii inayojitokeza hapa. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ni msomi mzuri, Profesa ni Profesa ni msomi mzuri. Mimi ninaamini hili wazo ni la kizalendo na lina nia njema ndani yake, lakini namna ambavyo mahusiano yanapotea hata Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema hapa kwamba, una malalamiko mengi na Mbunge hajakutana na Waziri wakazungumza jambo hili, pamoja na wadau wengine, inaonesha wazi kabisa ni namna tu wanavyoenda katika kulitekeleza jambo hili, ndiyo inayoleta utata katika kupata ufumbuzi wa suala hili.

Hivyo basi, mimi napendekeza kwamba, Serikali ikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wanahitaji kushirikishwa zaidi ili waweze kupata suluhu ya Kigamboni na sasa iwe mwisho, tumechoka kusikia hadithi sijui kuna hisa, sijui kuna hili, hatuna pesa, hatuna nini na kadhalika. Wakae waamue Wananchi wa Kigamboni waambiwe ukweli waweze kujua wanafanya nini na ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Esther Bulaya, maana naona mmefanya kazi sana hapo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa moyo wa dhati kabisa, mimi ni miongoni mwa watu waliokuwa wakimuunga sana mkono Mama yangu Mama Tibaijuka na mpaka kesho ninamheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niseme wazi kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati. Kamati ilikwenda Kigamboni kuongea na Wananchi, tulipokelewa na mabango na malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwambia kabisa Mheshimiwa Waziri, hilo suala la hisa kwenye Kamati tulikwambia usili-*introduce* kwanza, nenda ukawashirikishe Wananchi wa Kigamboni. Tulikwambia kwenye Kamati na kama naongopa, Wajumbe wa Kamati wenzangu wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, amesema hapa kwamba, hawezi kuongelea masuala ya fidia kwani hana pesa, ni aibu kule Wananchi wameshafanyiwa tathmini na ndiyo maana kwenye Kamati tumemwambia a-*deal* na *infrastructure,* hilo sijasikia akilisema.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala ingilia kati, litaitia aibu Serikali. Kwa mkakati uliopo anaoung'ang'ania Waziri hautekelezeki. Mheshimiwa Waziri Mkuu, okoa Serikali yako katika suala la Kigamboni, tumechoka na migogoro, mambo mengine yanaendelea Kamati hatuna taarifa. Kigamboni hili ni cha mtoto, bado Chasimba, bado Makongo. Mheshimiwa Serukamba ni Mkazi wa Makongo, yule pale anajua. Hatuwezi kukubali, Kamati tunataka majibu sahihi, tumechoka na historia ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Ndugulile. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwanza, ilitakiwa wasemaji wote wa-*declare* wanaishi wapi. Mheshimiwa Madabida! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nasikitika sana, kwa sababu nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri kutoka mwanzo mpaka mwisho, mimi bado ninaona ni giza nene sana kwa Wakazi wa Kigamboni. Miaka sita unaambiwa usitengeneze wala usifanye kitu chochote!

Leo yule mtu maskini ya Mungu ambaye ndiyo mahali pake pa kukaa umemkataza asijenge, hawezi kuuza, hawezi kufanya kitu chochote, unazidi kumtumbukiza katika dimbwi la umaskini; kwa nini? Mbona sehemu nyingine zimeendelea bila kuwa na huo mpango? Wawekezaji wanakuja, kitu ambacho walipaswa kufanya tengenezeni ramani ya kitu gani mnataka kitengenezwe Kigamboni, halafu waachieni watu. Kama mtu ana uwezo atengeneze, kama hana uwezo, mwekezaji atakapokuja ataongea naye yeye, kuliko hivi ambavyo wanaambiwa wanadanganywa, wanawekwa katika dimbwi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba sana wawahurumie Wananchi wa Kigamboni, watu wameteseka kwa miaka sita hawajui hatima yao! Sasa hivi kinachosemwa sikielewi mpaka sasa hivi ukiniuliza kwamba imejibiwa nini, Watu wa Kigamboni wameambiwa nini, mimi sijaelewa hata kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali tuseme mwisho. Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi alikuja Kigamboni, wameonana na watu, wamezungumza nao, wamemlilia, wamemwambia tunaomba Serikali ifikie mwisho. Kwani kikubwa mno ni kitu gani kwamba lazima iwe Kigamboni si kuna sehemu nyingine? Kama ni bahari twende Masaki au Oysterbay, kule watu wanaelewa watakwenda. Watu wa Kigamboni hawakatai, lakini *the concept,* watu hawashirikishwi, hawajui, wako kwenye giza, hawajui wanakotoka wala wanakokwenda. Ifike mahali tufike mwisho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, tufike mahali tufike mwisho Wananchi wa Kigamboni wajue kama wamekaa, wamelala au wamesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*
**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Rukia!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ndugulile. Siku alipotangazwa Mheshimiwa Waziri kuwa ni Waziri wa Wizara hii, nilitegemea kuwa tatizo hili litamalizika.

Zile sifa alizotutajia hapa …

**MWENYEKITI:** Acheni habari za watu, hebu semeni.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Na hekima zake tuliona zitatumika, lakini kwa kweli suala hili linaitia aibu hii nchi na Serikali kwa ujumla. Inakuwaje Watu wa Kigamboni wanateseka na sisi tunajua watu hawa hawakopesheki, hawawezi kuuza, hawawezi kununua, hawawezi kujenga, ile dhana ya MKUKUTA ya kukuza uchumi pamoja na kupunguza umaskini iko wapi? Kwa kweli hii ni aibu na inakitia aibu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Kigamboni wamechoka, tatizo hili litatuliwe mara moja. Wananchi washirikishwe, wewe tayari unajua kwamba hili unalolidai wewe Wananchi hawalielewi. Hivi Mwananchi wa kawaida atajuwaje mambo ya hisa? Washirikishwe Wananchi pamoja na Mbunge wao,

wajue stahiki zao na haki zao na hatima ya Watu wa Kigamboni ipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu!

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimepata meseji, Madiwani wa Temeke ambao tulikwenda kwa Waziri Mkuu, wameniambia ukipata nafasi ya kuzungumza, hebu mwombe Waziri Mkuu, asimame azungumzie zile Kata tatu, lakini pia azungumzie hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sita suala la Kigamboni linazungumzwa tu! Hali ya Kigamboni ni mbaya sana, hata kama ndiyo Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi, lakini kama limetushinda tunafanyaje si tunaliacha? Haitoshi, Mheshimiwa Waziri umesema, hili jambo ungelifanya Muleba wangefurahi sana. Mimi nakuomba, kama Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, lipeleke Muleba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, nilipochangia nilikwambia kwamba, tuna Mashirika mazuri, tumeona *National Housing* ana eka 200 kule. Uliposimama kuzungumza unasema eneo la *National Housing* ni njia; hivi eka 200 zote ni njia?

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa!

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Tuna Mashirika ya *NSSF, LAPF* na *PPF, wana uwezo* hutaki kuwashirikisha; unataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mradi umetuchosha, hatuutaki! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri! *Repetition, repetition!*

**WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nawashukuru wachangiaji kwa sababu na sisi ndiyo tunaboresha mawazo yetu namna ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba, hoja tumezisikia, ushirikishwaji ni wazi kwamba, itabidi tujipange upya kwa suala hili, tuhakikishe kwamba, wale ambao watataka taarifa zaidi, tutakwenda nao. Niseme tu kwamba, kwa pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge wengine ambao pia ni Wakazi wa Kigamboni, nanyi mtasaidia zoezi hili tuwe pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyosema, mimi ninatekeleza kazi yangu ambayo tunajaribu kwenda mbele na ni mawazo, yanaweza yakawa mapya, kitu kipya kina matatizo maana kinakuwa bado hakijaeleweka. Kikishaeleweka kila mtu anasema mimi ndiyo nilifanya hivyo, lakini hiyo siyo hoja. Mimi naamini kabisa kwamba, utaratibu wa hisa ni mzuri lakini ni lazima ueleweke kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwamba, tumesikia hoja, nazikubali, sasa basi tupewe muda tuzifanyie kazi. Tutajipanga katika bajeti yetu ndogo tuliyonayo, itabidi karibu nusu itumike katika kuendesha hizi elimu ili twende na Wananchi.

Mheshimiwa Mheshimiwa, Saada kama una zaidi utanisaidia lakini hali ndiyo ilivyo. Nami niamini kwamba, Wananchi wa Kigamboni wanaonisikiliza na mimi wanielewe, ninajua kwamba, tangu mwaka 2008 mpaka sasa hivi ni muda mrefu. Sasa sitaki kuingia kwenye Hotuba ya Msahafu na kugeuka nyuma tunaweza tukageuka tukawa chumvi; kwamba, muda umepita tunajaribu kusonga mbele, lakini nisiseme mengi, niseme kwamba, suala la elimu tumelisikia na Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Dar es Salaam tuwe wote.

Kuhusu Kata hizi tatu, Mheshimiwa Mtemvu tupo wote na mimi nitumie nafasi hii kusema kwamba, Mheshimiwa Mwenyekiti umezungumzia malalamiko na mimi nina malalamiko ninayafaili. Kwa mfano, nina malalamiko kutoka kwa Wananchi kwamba Halmashauri ya Temeke imeendelea kwenda kwenye maeneo yao na kukata viwanja na kuuza na kuwapa fidia kidogo ambayo iko chini ya ile iliyotangazwa na Wizara kwa mfano, ni malalamiko!

Vitu vingine ni kwa sababu labda wengine siyo wazuri sana katika kusema na kusema, lakini ni kwamba, malalamiko yanatoka pande zote. Watu wanasema baada ya fidia ya Serikali kutangazwa, Wananchi hawataki kupimiwa viwanja wanataka wasubiri fidia ya Serikali, ambayo sasa ndiyo mchakato unaendelea. Kwa hiyo, hayo malalamiko ninayo dhidi ya Halmashauri ya Temeke.

Nami nikasema itawezekanaje kwa sababu sasa hivi kwa mujibu wa Sheria, Tarafa ya Kigamboni iko chini ya *KDA*. Kwa hiyo, Halmashauri ya Temeke haina tena idhini ya kuingia pale na kukata viwanja. Ila tulikubaliana katika kikao cha pamoja kwamba, kwa vile viwanja vilivyokuwa vimepiwa awali, waendelee wamalize kuvigawa waweze kulipa deni walilokuwa wamechukua benki.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, katika hili Wabunge wa Dar es Salaam na Wabunge wengine ambao ni wakazi wa Kigamboni, tujipange. Kamati tulikuwa pamoja, kweli mlitembelea, watu wanalalamika na ni kweli kwamba Katibu Mkuu wa CCM alitembelea kule na mimi ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM. Nami nitapata nafasi ya kwenda kuelezea kama unavyosema ni maamuzi ya ngazi za juu kabisa, kwa sababu huu Mradi upo kwenye Ilani. Mimi nafanya kazi yangu kama Waziri kutekeleza, kama maamuzi yakiwa mengine kuachana nao, nayo inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba tumalizie hili suala!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ambazo zimekuwa ngumu na hii ni mojawapo, sijawahi kusimama zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, niliposikiliza Taarifa ya Kamati na kama mtaona ukurasa wa 22 na 23 na zile kurasa za mwisho kwenye hitimisho, yapo mawazo ambayo nafikiri ni mazuri sana. Kinacholeta tatizo hapa inaonekana pengine Serikali hatujafanya kazi ya kutosha katika kuelimisha jamii juu ya Mradi wenyewe, namna utakavyosimamiwa, utakavyoendeshwa na kubwa zaidi dhana hizi mpya za hisa, unajua ni dhana ambazo zinahitaji elimu ya kutosha. Hata haya mambo mengine ambayo yanadaiwa hapa ya kutokushirikishwa na kadhalika, kwa sababu yamesemwa hapa ndani ya Bunge, mimi nadhani jibu sahihi tukubali.

Tukubaliane na aliyoyasema Mheshimiwa Ndugulile pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, acha Serikali jambo hili tulichukue upya, tupitie maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema, tutashirikisha Wabunge wenyewe na zile Wizara zote ambazo zinahusika. Kubwa ni Baraza la Madiwani katika Manispaa ya Temeke, maana eneo hili mpende msipende, ni eneo ambalo lipo chini ya Manispaa hiyo. Tulichofanya ni kuchukua eneo kwa madhumuni ya uendelezaji, lakini hatuwezi kuacha lile Baraza bila kulielimisha kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie na niwaombe wenzangu kwamba, Serikali acha ilipe uzito unaotakiwa, naamini tutafikia mahali pazuri tu bila tatizo kubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ingekuwa ni majibu yale ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli tusingeweza kukubaliana.

Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa busara zake kwamba, katika suala hili, kwa kurudia maneno yake, suala hili litaenda kutazamwa upya mchakato mzima jinsi ulivyokuwa, suala la hisa zile Kata tatu na ushirikishwaji wa Wananchi na Baraza la Manispaa ya Temeke.

Kwa hoja hizi, narudisha shilingi ili hayo yaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa tunaingia kwenye *guillotine* dakika zimebaki kumi tu. Someni Kanuni.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*...........Tshs.13,822,867,400/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*..............Tshs. 1,017,520,600/=
Kif. 1004 - *Management Information System*......................................................Tshs. 783,329,120/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* ....................Tshs. 489,823,760/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* ..........................................................Tshs. 602,931,948/=
Kif. 1007 - *Government Communication Unit* ..........................................................Tshs. 413,413,840/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ....................Tshs. 502,812,384/=
Kif. 2001 - *Land Administration Division*..................................................Tshs. 2,751,830,816/=
Kif. 2002 - *Surveys and Mapping Division*................................................Tshs. 4,702,364,000/=
Kif. 2003 - *Registration of Titles Unit*........Tshs. 1,427,366,800/=
Kif. 2004 - *Valuation Unit*....................Tshs. 1,092,067,456/=
Kif. 3001 - *Rural and Town Planning Division* ..............................................Tshs. 11,272,354,424/=
Kif. 3002 - *Housing Division*..................Tshs. 2,382,904,000/=
Kif. 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*............................................Tshs. 6,233,154,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*…. .................................. Tshs. 4,000,000,000/=
Kif. 2001 - *Land Administration Division* ................................................Tshs. 13,779,977,000/=
Kif. 2002 - *Surveys and Mapping Division* ................................................Tshs. 13,600,000,000/=
Kif. 3001 - *Rural and Town Planning Division* ……………..........................................Tshs. 2,500,000,000/=
Kif. 3002 - *Housing Division*…….……………..Tshs. 500,000,000/=

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 bila mabadiliko yoyote. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kupitisha Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba, katika maisha yangu ndani ya Bunge hili, Wizara kama hii huwa

inakuwa ngumu kila mwaka. Yapo mambo ya msingi ambayo nafikiri Wizara myazingatie.

Katika *innovations* hizi mpya, ushirikishwaji wa Wananchi ni muhimu sana na kwa sababu ya hali halisi ya Wananchi kutambua maana ya matumizi ya ardhi, ndiyo maana tunapata migogoro kwa sababu watu wanajua matumizi. Kwa hiyo, ninyi wenzetu mlioko kwenye *center* ni vizuri mkashirikisha watu na msikie maoni yao kabla ili mnapotunga Sera zenu zinakuwa pamoja na Wananchi wenyewe. Mimi nadhani tatizo kubwa lilikuwa ni hilo. *(Makofi)*

Tatizo lingine ambalo ni kubwa, nadhani juzi mlimbana Waziri wa Mifugo kuhusu Kamati tuliyoiunda sisi kuangalia migogoro ya ardhi. Kwa mujibu wa kanuni zetu, wakati wa Bunge la Bajeti hatuingizi kitu kingine zaidi ya kumaliza mambo ya bajeti, lakini tunaangalia uwezekano wa kuongeza muda baada ya kumaliza bajeti, kuongeza siku chache, kwa sababu kuna mambo ambayo nadhani yanatakiwa kufanyika. Moja, ambalo linatakiwa kufanyika naambiwa, Serikali inataka kuleta Sheria inayohusiana na *VAT*.

Nasikia jana Mheshimiwa Mbunge mmoja kanirarua Spika nafanyaje, eeh, someni Kanuni. Spika haleti Muswada Bungeni, tunaambiwa tu kwamba wanaleta na kama hawajaleta *officially* siwezi, lakini ukweli mimi ninayo taarifa hiyo ya migogoro ya ardhi. Kamati tuliyoiunda wenyewe hapa itabidi tuizungumze kabla hatujaondoka. Kwa hiyo, itabidi tuongeze siku baada ya Bajeti. Kwa hiyo, hilo nalo litapewa sura kubwa sana, kwa sababu Kamati ile imekwenda mbali sana na imeona vitu vingi, kimfumo kuna matatizo na mengineyo. Nadhani tutajadili na tutaweza kuishauri Serikali kadiri itakavyofaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, haya ni mambo ambayo inabidi tuwapongeze Wizara wamejitahidi. Ucheleweshaji katika ofisi zenu mjaribu, mlianza zamani ku-*computerise* vitu, mka-*computerise* lakini inafika mahali wengine wanakuwa wajanja hawafanyi vizuri. Yapo mambo ya namna hiyo, ambayo mnaweza kuyarekebisha na hali ikawa nzuri zaidi.

Naomba niwatambue baadhi ya wageni kama wapo na wengine tumekuwa nao toka asubuhi hapa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri wa Fedha ambao ni Diwani wa Kata ya Mtowa, Mheshimiwa Athuman Idd Kaliki. Yupo na Mwenyekiti wa CCM Tawi, sijui Tawi lipi; Ndugu Lucas Bundu. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, ambao ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Lugoba, Bi Rehema. Yupo Mwenyekiti wa Kijiji

cha Lugoba, Ndugu Zaituni Omar na yupo Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ya kwao, Ndugu Yussuf Bandula. *(Makofi)*

Wageni tunawakaribisha na tunawashukuru sana kwa kufanya kazi pamoja na sisi. Ilikuwa ni siku ngumu, lakini tumeimaliza vizuri, nadhani masomo tumepata wote.

Naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.21 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 29 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*